Ujumbe – Sehemu Ya Pili

Ujumbe - Sehemu Ya Pili

Ja'far Subhani

Kimetafsiriwa na
Dhikiri U M Kiondo

Al-Islam.org

Author(s):

Ja'far Subhani [1]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [2]

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The Message, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, Ujumbe. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Pili.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

Translator(s):

Dhikiri U M Kiondo [6]

Topic Tags:

Qur'an [7]
History [8]
Mi'raj [9]
Battles [10]
Quraysh [11]

Person Tags:

Bwana Abu Talib [12]
Prophet Muhammad [13]
Imam Ali [14]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The *Message,*

kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, *Ujumbe.* Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Pili. Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Haya ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na mwanachuoni mwandishi wa kitabu hiki juu ya maudhui haya yaliyotaja hapo juu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imea- mua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Maalim Dhikiri Kiondo (Allah *'Azza wa Jalla* amkubalie amali zake na amweke karibu na Maasumina 14 [a.s.]-Amin) kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Kuhusiana Nasi

(Inawahusu watoaji wa toleo la Kiingereza ambalo kitabu hiki ni tafsiri yake)

Leo hii, akili iliyo macho huyaona mabadiliko kwenye maisha ya kiakili ya mwanaadamu.

Sayansi na teknolojia, vikiwa kwenye ustawi wake wa juu zaidi, vyaelekea kukifikia kipeo chake cha mwisho. Mahitaji ya kimwili pamoja na tamaa ya mamlaka na tawala vimemwongoza mwanaadamu kwenye ufisadi wa dhahiri wa maadili yake. Katika hali hii ya kukatisha tamaa, mtu alazimika kutulia na kuitathmini hatari iliyojificha na inayowatishia wanaadamu wote kwa ujumla. Mwanaadamu, tayari kaisha mkodolea macho tena Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu, kwa kuwa, sasa kaishatambua ya kwamba ufumbuzi wa matatizo yake na wokovu wake umo kwenye kuzifuata Amri za Allah.

Mgeuko huu, wa kutoka kwenye fikara za kimwili na kuja kwenye fikara za kiroho unaafikiana kabisa na malengo na shabaha za hii Seminari ya kiislamu. Mafundisho ya dini yanakwenda sambamba na maendeleo ya huu wakati wetu, yakitoa kimbilio lihitajiwalo mno na akili yenye kusum- buka na mashaka. Haya ni matokeo ya mtanabahisho, ya kwamba sasa inatambulikana ya kwamba siri ya kuishi maisha ya kiuchamungu kwenye ulimwengu huu huongoza kwenye baraka ya milele ya maisha ya Ahera. Huu ndio ujumbe wa UISLAMU kwa ulimwengu mzima.

Hii Seminari ya kiislamu inadhamiria kuinua juu kurunzi ya mwongozo wa kiroho na kusaidia kwa juhudi zote katika kuukuza urithi wa mwanaadamu. Inaionyesha njia ya maisha ifundishwayo na Qur'ani kati- ka utukufu wake wa asili. Inayaonyesha yale yenye nguvu na yaliyo ya kweli tu. Vitabu vyake vimekusudiwa kufaa katika kuyafikia mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi. Vitatumika kama kijito kitiririkacho maji daima, kwa wale walio na kiu ya elimu.

Hii Seminari ya kiislamu ni taasisi ya ulimwengu mzima yenye kujitahidi katika kudumisha udugu wa kiislamu. Inafurahia mchango wa akili zilizo bora zaidi, zaidi ya kuwa na msaada wa kimataifa kwa ajili ya kuyafikia malengo yake makuu. Inavyo vituo Canada, na Mashariki ya Mbali.

Orodha ya anwani iko kwenye kurasa za mwisho za kitabu hiki. Msomaji (wa Kiingereza) anaweza kukiandikia barua chochote miongoni mwa vituo hivi ili kuvipata vitabu vyetu.

Islamic Seminary Publications

Kwa Ndugu Msomaji

Asalaam Alaykum

Kitabu hiki kinatolewa na Seminari ya kiislamu (S.L.B. 5425, Karachi, Pakistan). Vitabu vyake vimelengwa kuyatimiza mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi, na msisitizo maalum juu ya kuzisafisha akili na fikara. Juhudi nyingi zimefanywa na Seminari hii kuweka kwenye vitabu vyake yale yaliyo na nguvu na yaliyo ukweli halisi kwenye Uislamu.

Unaombwa kukisoma kitabu hiki katika hali iliyodhamiriwa. Vilevile unaombwa kuwasiliana nasi, kuhusu maoni yaliyo huru kuhusu vitabu vyetu, jambo tutakalolipenda mno.

Kuubalighisha ujumbe wa Uislamu ni jukumu lihitajilo ushirikiano wa watu wote. Seminari hii inakukaribisha ushiriki kwenye jukumu hili ukiuitika mwito wa aya ya Qur'ani Tukufu isemayo:

{قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۖ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۚ 46}

"...Sema: Mimi ninakuahidini jambo moja tu, ya kwamba msimame kwa ajili ya Allah, wawili-wawili na mmoja-mmoja..." (***As-Saba, 34:46***).

Allah na Akubariki.
Nduguyo katika Uislamu,
Katibu wa Uchapishaji.

Utangulizi

Kwa Jina La Allah, Mwingi Wa Rehema, Rahimu.

Tangu zamani za kale, mwanadamu amekuwa akiitafuta elimu kupitia milango yake ya fahamu. Hivyo basi, kwa kuvitambua vitu, hujaribu kulitatua tatizo lake. Katika mchakato huu, amekuwa akifanya majaribio, na hatimaye kwa kubahatisha alifikie kwenye ufumbuzi uwezekanao wa matatizo yake. Ikiwa imetegemea juu ya dhana na utendaji huu, sayansi ilistawi kwa ukubwa mno kwenye maeneo na nyanja mbali mbali za matu- mizi yake.

Kwenye zama hizi mpya za sayansi, mamia na maelfu ya maabara ya utafiti yanavutia nadharia ya wanasayansi ambao hufanya ugunduzi na ubunifu mkubwa mno wa kiwango cha kutoaminika cha usahihi wa ala na zana. Vivyo, kitu pekee ambacho hadi sasa sayansi imeshindwa kukikamata ni tatizo la kijamii. Ni dhahiri kwamba matatizo ya kijamii ni matatizo ya wanadamu. Na matatizo ya wanadamu ni ya hali ambayo haiwezi kuingizwa kwenye neli ya majaribio /testityubu (test-tube). Ili kuisadiki habari hii, mtu yuatambua vizuri mno kwa mfano, ya kwamba bado sayansi hai- jatoa jibu la kutoafikiana na chuki iliyomo miongoni mwa watu au tofauti za kimatabaka zinazokithiri kwenye matabaka ya jamii za wanaadamu.

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu, zilizochakaa. Hakuna shaka kwamba sayansi inagundua habari za maisha kwa njia ya ufukuaji wa mashimo yanayodhaniwa kuwa na vitu vya kale kwa ajili ya uchunguzi, na kwa kujifunza masalio ya vitu visivyo na uhai (relics) na (vikisukuku) vile vyenye uhai vilivyogeuka kuwa mawe (fossilis), vilivyogandamana na miamba ya ardhi. Lakini tukiyaachilia mbali yote hayo, hakuna matokeo ya dhahiri yaliyopatikana kuhusiana na matatizo mengi ya wanaadamu.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikara zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema:

“Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao, kwa juhudu nyingi niliyapitia matendo yao, nilizifikiria fikara na matendo yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu; na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika, historia imeandika habari zote, zile zenye kupendeza na zenye kuchukiza, lakini lile lisikitishalo ni kwamba hakuna yeyote aliyejali kuza- ma ndani ya kina cha sababu za habari hizo. Ama kuhusu ufumbuzi halisi wa tatizo, liwe kubwa au dogo, hakuna juhudi katika upande wa mwanaadamu uonekanao kwenye historia. Ni yale mambo yasiyo muhimu ndiyo yaliyoshughulikiwa kwa maelezo marefu yaogofyayo.

Kwa kuwa historia ni masimulizi ya matukio ya kale yaliyoandikwa, yana- pata kuwepo kwake kutoka kwa mwandishi wake. Watu walioiandika historia hawakuwa huru kutokana na kiburi cha ubinafsi, rangi au sehemu atokayo mtu, na hivyo basi, lengo lake hasa laonekana kushindwa. Mbele ya tafsiri mbaya na uzushi wa habari za kihistoria, msomaji wa kawaida wa historia yumo kwenye hasara ya kuuelewa ukweli wa jambo hilo. Ni kama daktari ambaye, kama hana taarifa sahihi kuhusu maradhi ya mgonjwa wake anayemwuguza, hataweza kuchunguza maradhi halisi ya mgonjwa wake huyo.

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taar- ifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote, wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kujifunza maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w), mkuu zaidi miongoni mwa wanaadamu wote, kunachukuliwa kuwa ni kwenye kuleta hofu na kujierevusha. Nyororo ya matukio ya kabla na ya baada ya kuza- liwa kwa huyu mtu mkuu kunatoa mawazo kwa ajili ya kila mtu aliye na japo punje ndogo tu ya akili na hisia za ulinganifu.

Kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akiwa yu mtoto aliyezaliwa baada ya baba yake kufariki dunia, na kifo cha mama yake, Bibi Amina (a.s.), alipokuwa na umri wa miaka sita tu, na kulelewa kwake, kwanza na babu yake na kisha na ami yake ni mambo yasiyo kifani.

Baada ya kuyapitisha maisha yenye mambo mengi, kujitenga kwake kwenye Pango la Mlima Hira na Ufunuo wa Allah uliofuatia, kuwaitia watu kwenye dini ya Allah, upinzani wa makafiri na wenye kuabudu

masanamu, maonevu na mateso yao, umadhubuti wake uliodumu katika kuimarisha ujumbe wa Allah kwenye kipindi cha miaka kumi na mitatu ya mwanzo ya Utume wake mjini Makkahh hadi kwenye muda wa kuhamia kwake Madinah, ni matukio yasiyo kifani kwenye historia.

Miaka kumi ya mwisho ya maisha yake mjini Madina, kuimarisha kwake juhudi za ujumbe wake kwa ajili ya uenezaji wa Uislamu, kushiriki kwake kwenye vita nyingi dhidi ya makafiri na hatimaye kutekwa kwa Makkahh bado ni matukio makuu yenye kuonekana kuwa si ya kuaminika, lakini yameandikwa kwenye historia kuwa ni mafanikio ya kimiujiza.

Mamia ya vitabu yameandika kuhusiana na maisha na ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) lakini vitabu hivi haviwezi kuchukuliwa kuwa ni wasifu kamili juu ya sifa na mafanikio yake. Hasa yale maandishi ya mustashrik yameingiliwa na chuki, makosa na tafsiri potofu.

Kitabu hiki sio tu kwamba kinatoa mambo yenye kuongoza, bali vile vile kimezitegemeza taarifa zake kwenye maandiko ya kihistoria yaliyo ukweli. Moja ya sifa zake zijidhihirishazo mno ni kwamba mwandishi amechukua hadhari kubwa katika kuyasimulia matukio ya kihistoria, na wakati huohuo amejitahidi, akiwa yu mwanachuoni mtafiti, kuyaendea matukio hayo kwa fikara zenye kuchanganua mambo pia.

Sifa nyingine, ya kitabu hiki yenye kuvutia ni kuwa kiko huru kabisa kutokana na uzushi na hadithi zilizobuniwa zilizozushwa na faida zilizofichwa. Kwa maneno mengine ni kwamba, kiko kabisa kwenye hali ya kusalia kwenye kiwango kihitajikacho cha ukweli wa kihistoria. Kwa kifupi ni kwamba, kinapelekwa kwa Waislamu kwa ujumla, bila ya upendeleo na kiburi.

Tunategemea ya kwamba kitabu hiki kitalifikia lengo lake la kukiongoza kizazi kichanga chenye shauku kuu ya kujipatia taarifa za kweli na zenye kutegemewa juu ya huyu Mtume Mkuu wa Uislamu (s.a.w.w), na tunaamini ya kwamba vijana wetu wa kiislamu watajipatia mwongozo kutokana na kitabu hiki katika kuyatengeneza maisha yao kwa mujibu wa maamrisho ya Allah pamoja na sifa tukufu za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Dhuria wake Wateule (a.s.).

Sura Ya 18: Silaha Zenye Kutu

Nguvu za kiutawala za uabudu masanamu zilikuwa kwenye hali ya ukubalikaji kila mahali kwenye Penisula ya Uarabuni. Waquraishi walikuwa wameshayatayarisha majeshi yao ili kufanya kampeni dhidi ya ibada ya Allah, Aliye Mmoja tu. Katika hatua za awali walitaka kumfanya Mtume (s.a.w.w.) aiache kazi yake kwa kumtamanisha na kumpa ahadi za utajiri na mamlaka, lakini walikabiliwa na lile jibu lake maarufu: “Naapa kwa jina la Allah! Japo muniwekee jua kwenye mkono wangu wa kulia na mwezi kwenye mkono wangu wa kushoto (yaani japo mnipe mamlaka juu ya huu ulimwengu mzima) sitaiacha

kazi hii.” Kisha wakaanza kuwahofisha, kuwatweza, na kuwatesa marafiki zake na katu hawakuchoka kuwadhuru na kuwaadhibu.

Hata hivyo, ushujaa na umadhubuti wa marafiki zake hawa waaminifu viliwafanya washinde kwenye hatari hii pia, kiasi kwamba walinunua uvumilivu wao katika njia ya Uislam kwa kuyaacha makazi yao, na kujitahidi kuieneza dini hii takatifu kwa kuhamia Ethiopia.. Hata hivyo, harakati za nguvu inayotawala ya uabudu masanamu za kuung’oa ule mche mchanga wa Uislamu zilikuwa bado hazijakoma. Badala yake, sasa walitaka kuitumia silaha iliyo kali zaidi.

Silaha hii ilikuwa ni ile ya propaganda dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa dhahiri mateso na maonevu yangaliweza kuwazuia kusilimu wale watu waliokuwa wakiishi mjini Makkah tu. Njia hii haikufaa kwa wale watu waliokuja Makkah kwa makundi kufanya Hija ya Nyumba ya Allah katika kipindi cha miezi mitakatifu. Hawa mahujaji walikutana na Mtume (s.a.w.w.) katika mazingira ya amani na utulivu, na ijapokuwa hawakuipokea dini yake, kwa uchechefu walitikisika kuhusiana na imani yao (ibada ya masanamu). Na wanapoondoka Makkahh baada ya siku chache na kurudi makwao, walilichukua jina la Mtume na Hadith ya hii dini mpya kwenye pembe zote za Bara Arabuni. Na jambo hili, lenyewe lilichukuliwa kuwa ni pigo kubwa kwa utawala wa uabudu masanamu na lilikuwa kisababisho cha ajabu kiongozacho kwenye uweneaji wa Uislamu.

Hivyo basi, wazee wa Waquraishi waliweka mpango mwingine wa uharib– ifu na kwa njia hii walitaka kuzuia ueneaji wa dini ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na hivyo kuyakata mawasiliano yake na jamii ya kiarabu.

Usingiziaji Uliokithiri

Tabia ya mwanaadamu yaweza kueleweka vizuri kwa kujiingiza kwenye matusi na masingizio ya maadui zake. Ili kuwapotosha watu daima adui hujitahidi kutoa shutuma za aina hii dhidi ya mpinzani wake ziwezazo kukubaliwa na jamii, kwa kiwango cha hata moja kwa elfu, ili kwamba, kwa huko kueneza uongo na mambo yasiyo na msingi, adui aweze kuvun– ja heshima na cheo chake kwa kadiri iwezekanavyo. Adui mwenye hekima hujitahidi kuzusha mambo dhidi ya adui yake yawezayo kusadikiwa na baadhi ya watu maalum au ambayo, kwa uchechefu yawezayo kutiliwa shaka na watu hao. Hata hivyo, hayaenezi mambo kuhusu adui yake yasiyoafikiana kabisa naye na yasiyo na mwelekeo kwenye fikira na matendo yake yafahamikayo mno, kwa sababu vinginevyo atapata matokeo yaliyo kinyume na yale ayapendayo.

Hivyo, mwanahistoria stadi anaweza kujifunza sura halisi ya upande wa pili nyuma ya uongo na masingizio, na anaweza kujifunza kuhusu mafanikio ya kijamii na kifikra hata kutoka nyuma ya mnara wa kuongozea wa adui. Huwa hivyo kwa sababu adui asiye na aibu na asiyeogopa haachi kutangaza shutuma za uongo zenye manufaa kwake na kujipatia faida kubwa kiasi iwezekanavyo kutokana na hiyo silaha kali ya propaganda kwa kadiri fikira, akili na ujuzi juu ya hali vitakavyomruhusu. Hivyo, kama hatalihusisha jambo lolote lisilo la haki kwa huyo mtu mwingine itakuwa ni kwa sababu mtu yule yu safi

kutokana na udhaifu wowote, hivyo basi jamii haitakuwa tayari kulikubali jambo lile.

Historia ya uislamu yaonyesha kwamba ingawa Waquraishi walidumisha uadui usio na kifani na chuki dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) na walikuwa na shauku ya kulivunjilia mbali jengo jipya la Uislamu kwa gharama zozote zile na kuivunjilia mbali hadhi na cheo cha mwasisi wake, lakini hawakuweza kuitumia kikamilifu silaha hii (ya masingizio). Walifikiria waseme nini wakati mali za baadhi ya watu wao wenyewe, zilikuwako nyumbani mwake Mtume (zikiwa ni amana) na umri wake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wa miaka arobaini umemthibitisha kuwa yu mtu mwaminifu.

Je, wangaliweza kumtuhumu kwa anasa? Lakini vipi wangaliweza kulileta neno hili midomoni mwao? Aliyaanza maisha yake ya utu uzima akiwa na mwanamke mtu mzima na bado angali akizipisha siku zake pamoja naye pale Waquraishi walipokutana ili kupanga propaganda zao dhidi yake! Hivyo, wakaanza kutafakari kuhusu waseme nini na hilo walisemalo liweze kurandana naye na angalau asilimia mia moja ya watu iweze kulikubali kwamba ni kweli.

Wazee wa Darun Nadwa walifadhaika kuhusu ni jinsi gani ya kuitumia silaha hii dhidi yake. Hivyo wakaamua kulifikisha jambo hili mbele ya mwenye hekima mmoja wa Kiquraishi na kuutekeleza ushauri wake. Baraza liliundwa.
Walid aliwageukia Waquraishi na kusema: “Majira ya Hajj yanakaribia, na kwenye siku hizi watu huja mjini humu kwa idadi kubwa ili kutekeleza wajibat mbalimbali na kanuni za ibada zihusianazo na Hajj. Muhammad ataitumia nafasi ipatikanayo kutokana na uhuru uliopo kwenye siku hizi na ataitangaza dini yake. Ingekuwa bora kama Waquraishi wangeelezea maamuzi yao ya mwisho juu yake na dini yake. Hivyo basi, sote tuwape Waarabu maoni ya aina moja, kwa sababu tofauti ya maoni itafanya maneno kutokuwa na athari.”

Baada ya kuyasema hayo, yule mwana hekima wa Uarabuni alilifikiria kwa makini jambo lile na akasema: “Tuseme nini” mmoja wao akashauri akisema: “Tuseme kwamba yeye yu mpiga ramli.” Walid hakulipendelea wazo hili na akasema: “Anayoyasema Muhammad sio kama ya mpigaramli.” Mwingine akasema kwamba wamwite mwendawazimu. Wazo hili nalo lilikataliwa na Walid, aliyesema: “Hakuna dalili yoyote ya uwendawazimu ionekanayo kwake.” Baada ya kulifikiria kwa kirefu waliamua hivi: “Hatuna budi kusema kwamba yu mchawi, kwa sababu jinsi yake ya kusema mambo ni ya kiuchawi na uthibitisho wa jambo hili ni kwamba, kwa kuitumia Qur’ani yake amejenga mfarakano miongoni mwa wakazi wa Makkah, ambao uhusiano wao wenye maafikiano mema ulikuwa ukitolewa mifano, na ameuvunjilia mbali umoja wao.”[1]

Wafasiri wa Qur’ani tukufu wanapoifasiri *Suratul-Muddath’thir* wametoa masimulizi mengine ya jambo hili. Wanasema: “Walid alipozisikia aya fulani fulani za *Sura al-Fussilat* kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) alibutwaa na nywele zake zikamsimama. Aliondoka na kwenda nyumbani kwake nae hakutoka tena nje. Waquraishi wakaanza kumdhihaki na kusema kwamba Walid amekuwa mfuasi wa dini ya Muhammad. Walimwendea nyumbani kwake kwa kikundi na kumuuliza juu ya ukweli wa Qur’ani ya Muhammad.

Kila mmoja wa wale waliokuwapo pale alipokuwa akitoa maoni yake juu ya maelezo tuliyoyatoa hapo juu, Walid aliyakataa. Hatimaye alitoa maoni ya kwamba, wamwite Mtume (s.a.w.w.) kuwa yu mchawi, kutokana na mfarakano aliouzusha baina yao, na waseme kwamba anayo njia ya kichawi ya kusemea mambo!

Wafasiri wa Qur'ani tukufu wanaamini ya kwamba aya ya 11–26 ya Sura al–Muddath'thir zianzazo na: "**Uniache Mimi na mwanaadamu Niliyemuumba peke yangu.**" hadi: "**Hivi karibuni Nitamwonyesha adhabu ya moto wa Jahanamu.**" Zilifunuliwa kuhusiana na Walid bin Mughayrah.2

Kushikilia Kumhusisha Na Wendawazimu

Ni ukweli wa kihistoria ukubalikao kwamba tangu mwanzoni mwa utu uzima wake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijulikana kwa unyoofu na uaminifu wake, na hata maadui zake walimwinamishia vichwa vyao bila yakupenda mbele ya sifa zake tukufu. Moja ya sifa zake zilizojitokeza mno ni ile ya kwamba watu walimwita mno 'Mkweli' na 'Mwaminifu' kiasi kwamba wenye kuabudu masanamu walikuwa na kawaida ya kuweka vitu vyao kwake hadi miaka wa kumi baada ya ubalighishaji wa jumla wa Uislamu.

Kwa vile ulinganiaji wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulichukiza mno na kutoingia akilini mwa maadui zake, juhudi zao pekee zilikuwa kwamba wawageuzie mbali watu kutoka kwake kwa kutumia maneno yenye kuzi– haribu akili zao.

Kwa kuwa walijua kwamba kuuhusisha uongo na msingizio juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakutazivutia akili za wenye kuyaabubu masanamu walio wajinga na wa daraja la kawaida, walilazimika kuukana mwito wake kwa kusema kwamba chanzo cha maoni na fikara zake kilikuwa ni wendawazimu usioendana na sifa za uchamungu na unyoofu. Walifanya mifano mingi miovu na kufanya ujanja na udanganyifu katika kuifanya propaganda hii ya kinafiki.

Kutokana na unafiki wao mkali, walijifanya kuwa waaminifu mno pale walipokuwa wakizusha hivi na wakalieleza jambo hili kwa maelezo ya kutatanisha, na wakasema:

"**Je, amezua uongo juu ya Allah au amepatwa na wazimu. . . ?**" (***Surah Saba*, 34:38**). Na hii ndio njia ya kishetani wanayotumia maadui wa ukweli pale wanapokuwa wanapowakataa watu mashuhuri na watengenezaji wa hali ya jamii. Qur'ani inasema kwamba hii njia yenye kuchukiza haikuwa ya kipekee tu kwa watu wa zama zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwani maadui wa mitume wa kabla yake nao waliitumia silaha hii ili kuwapinga. Qur'ani inasema:

{كَذَٰلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ} 52

{أَتَوَاصَوْا بِهِ ۚ بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ} 53

***"Vivyo hivyo hakuna Mtume yoyote aliyewafikia wale wa kabla yao ila walisema: "huyu ni mchawi au majinuni! Je, wameusiana jambo hili?* (*sivyo*) *bali wao wote ni watu waovu."* (*Suratudh-Dhariyat, 51:52-53*).**

Injili ya siku hizi nayo inasema kwamba Nabii Isa (a.s.) alipowashauri Wayahudi, wakasema: "Ana pepo huyu tena ana wazimu; mbona mnamsikiliza?" (**Yohana Mtakatifu**, 10:20; 7:20; 8:48).

Hakuna shaka kwamba kama Waquraishi wangalikuwa na nafasi ya kumshutumu Mtume (s.a.w.w.) kwa jambo lolote jingine wasingaliacha kufanya hivyo. Hata hivyo, maisha ya Mtume (s.a.w.w.) ya heshima ya zaidi ya miaka arobaini yaliwazuia kutamka masingizio yoyote mengine dhidi ya tabia zake ingawa walikuwa tayari kukitumia kitu japo kidogo mno dhidi yake. Kwa mfano, wakati mwingine alikuwa na kawaida ya kukaa karibu na Marwah akiwa pamoja na mtumwa wa Kikristo aliyekuwa akiitwa Jabr. Mara moja maadui zake wakachukua fursa ya kitendo chake kile na wakasema: "Muhammad anajifunza Qur'ani kutoka kwa huyu mtumwa wa Kikristo." Qur'ani tukufu inaijibu shutuma yao hii isiyo na msingi, ikisema:

{وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ ۗ لِسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَٰذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ} 103

***"Na bila shaka tunajua ya kwamba wanasema: "Hakika yuko mtu anayemfundisha." Lugha ya yule wanayemuelekea ni ya kigeni na hii ni lugha ya kiarabu fasaha na chenye bayana"* (*Surah al-Nahl, 16: 103*).** 3

Hadaa Ya Nazar Bin Haarith

Ile silaha yenye kutu ya propaganda dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) haikuthubutu kuwa ni yenye kufaa hata kidogo, kwa kuwa watu kwa heki- ma na akili zao walitambua ya kwamba Qur'ani ina mvuto wa ajabu. Pia walihisi kwamba kabla ya hapo hawajawahi kusikia maneno matamu na yenye maana nzito yenye kuuliwaza moyo mno kiasi kwamba upesi sana huzivutia fikara za mtu.

Maadui waliposhindwa kutokana na kumsingizia Mtume (s.a.w.w.) waliifikiria njia nyingine ya kitoto na wakatumaini ya kwamba kwa kuitumia njia hii wangalifaulu kumkosesha usikivu na kuamini kwa watu.

Nazar bin Haatirh aliyekuwa mmoja wa Waquraishi wenye elimu na uzoefu aliyeitumia sehemu ya maisha yake nchini Hira na Iraq alikuwa na ujuzi juu ya vyeo vya wafalme na mashujaa wa Iran kama vile Rustam na Asfand Yaar na juu ya itikadi ya Wairani kuhusu wema na uovu, aliteuliwa kufanya kampeni dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Darun Nadwah liliafiki wazo la kwamba, kwa kuutangaza ustadi wake mitaani na kwenye maeneo ya maduka na masoko na kuzisimulia hadithi za Wairani na ujasiri wa wafalme wao, Nazir ataweza kuzigeuzia mbali fikara za watu kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuzielekeza kwake.
Ili kuishusha hadhi ya Mtume (s.a.w.w.) na kuyaonyesha kwamba maneno yake na aya za Qur'ani

havina thamani alisema kwa kurudia rudia: “Enyi watu! Nini tofauti baina ya maneno yangu na yale ya Muhammad? Anakusimulieni hadithi za watu waliopatilizwa kwa ghadhabu ya Allah na adhabu kali, na anakusimulieni hadithi za wale waliobarikiwa mno na waliokuwa wakitawala usoni mwa nchi kwa miaka mingi mno.”

Njia hii ilikuwa ya kijinga mno kiasi kwamba haikudumu zaidi ya siku chache, kiasi kwamba Waquraishi wenyewe walichoshwa na maneno ya Nazar na wakamtelekeza. Zilifunuliwa aya za Qur’ani juu ya jambo hili:

{وَقَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ اكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمْلَىٰ عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا 5}

{قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا 6}

“Na wanasema: ‘Ni visa vya watu wa kale alivyoviandika, hivyo anavisomewa asubuhi na jioni’Sema: ‘Ameiteremsha Yule ajuaye siri za mbinguni na ardhini; bila shaka Yeye ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.” (***Suratul-Furqan, 25:5-6***).

Kung’ang’ania Kwa Waquraishi Kwenye Itikadi Yao

Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alitambua vizuri sana kwamba watu wengi waliifuata ibada ya masanamu kwa kuiiga itikadi ya viongozi wa kabila na itikadi hii haikushika mizizi mno nyoyoni mwao. Hivyo basi, kama ikitokea akafaulu kuwabadili viongozi hao, na akafanikiwa kumuon- goza mmoja au wawili miongoni mwao, mengi ya matatizo yangalitatuliwa.

Hivyo basi alikuwa na shauku kuu ya kumvutia Walid bin Mughayrah (ambaye baadae mwanawe Khalid alipata kuwa amirijeshi wa kiislamu na mtekaji wa nchi), kwa sababu alikuwa ndiye mzee zaidi ya wote na mtu mwenye ushawishi mkubwa zaidi miongoni mwa Quraishi na alikuwa na heshima na mwenye madaraka. Alikuwa akiitwa mwenye hekima wa Uarabuni na maoni yake yaliheshimiwa zaidi katika utatuzi wa mambo mbali mbali yaliyokuwa yakileta mizozo.

Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akizungumza naye (Walid), Ibn Ummi Maktum, kipofu huyu, alimjia Mtume (s.a.w.w.) na kumwomba amsomee aya fulani fulani za Qur’ani tukufu. Alilishikilia mno jambo hilo kiasi kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliichukia tabia ile, kwa sababu haikufahamika ni lini itapatikana nafasi tena ya kuzungumza na huyu muungwana wa Uarabuni katika hali ya amani kama ile. Hivyo basi, alimgeuzia mbali uso wake yule Ibn Ummi Maktum na akiwa na paji la uso lililokunjamana, aliachana naye.

Tukio hili likakoma. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiliwazia jambo lile wakati aya kumi na nne za mwanzoni za *Surah ‘Abasa* zilipofunuliwa:

1} عَبَسَ وَتَوَلَّىٰ{

2} أَنْ جَاءَهُ الْأَعْمَىٰ{

3} وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهُ يَزَّكَّىٰ{

4} أَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَىٰ{

5} أَمَّا مَنِ اسْتَغْنَىٰ{

6} فَأَنْتَ لَهُ تَصَدَّىٰ{

7} وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزَّكَّىٰ{

8} وَأَمَّا مَنْ جَاءَكَ يَسْعَىٰ{

9} وَهُوَ يَخْشَىٰ{

10} فَأَنْتَ عَنْهُ تَلَهَّىٰ{

11} كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ{

12} فَمَنْ شَاءَ ذَكَرَهُ{

"Alikunja uso na akageuza mgongo. Kwa sababu alimjia kipofu. Ni nini kitakujulisha huenda atajitakasa au atakumbuka na ukumbusho (wa Qur'ani) utamfaa.? Ama ajionaye hana haja, wewe ndiye unayemshughulikia. Na si juu yako kama hatajitakasa. Na ama yule anayekujia, naye yu mwenye kuogopa, wewe unampuuza. Sivyo, hakika hii (Qur'ani) ni mawaidha. Basi yule

anayependa atawaidhika." (***Surah Abasa, 80: 1-12***).

Ulama mashuhuri na wanachuoni watafiti miongoni mwa Mashi'ah[4] huichukulia sehemu hii ya Hadith kuwa si yenye msingi hata kidogo na isiyoafikiana na maadili mazuri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wanasema kwamba aya hizi zenyewe hazionyeshi ya kwamba ni yeye Mtume (s.a.w.w.) aliyekunja uso na kuugeuzia mbali uso wake kutoka kwa kipofu yule.

Imenukuliwa Hadith kutoka kwa Imam wetu wa sita, Jafar as-Sadiq (a.s.) isemayo kwamba mtu aliyedhamiriwa alikuwa ni mtu wa familia ya Umayyah. Wakati Ibn Ummi Maktum alipomjia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yule mtu alionyesha chuki juu yake na Aya hizi zilifunuliwa ili kumuonya.[5]

Wanapiga Marufuku Kuisikiliza Qur'ani Tukufu

Utawala wa waabudu masanamu wa mjini Makkah uliunda mpango mkubwa wa kuzuia ueneaji wa Uislamu. Wakaanza kuitekeleza mipango yao kivitendo, mmoja baada ya mwingine, lakini walishindwa kulifikia lengo lao.

Waliendesha propaganda kubwa zaidi dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) kila mara, lakini hawakupata mafanikio yoyote. Waliona kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa imara kwenye kazi yake na mionzi ya nuru ya Upweke wa Allah ilikuwa ikipenyeza zaidi na zaidi, siku baada ya siku.

Machifu wa Waquraishi waliamua kuwazuia watu wasiisikilize Qur'ani ili kuhakikisha kupata mafanikio katika mpango wao huo, walipeleka wapelelezi kwenye sehemu zote za mji wa Makkah ili waweze kuwazuia mahujaji na wafanya biashara waliopotembelea Makkah wasiwasiliane na Muhammad na waweze kuwazuia kwa njia yoyote ile iwezekanayo wasiisikilize Qur'ani. Mzungumzaji wa kundi hili alieneza tangazo miongoni mwa wakazi wa Makkah, ambalo Qur'ani inalizungumzia ikisema:

{وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا لِهَٰذَا الْقُرْآنِ وَالْغَوْا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَغْلِبُونَ} 26

"Wanasema wale waliokufuru: 'Msiisikilize hii Qur'ani bali ipigieni makelele pale inaposomwa, huenda mkashinda." (***Surah al-Fussilata, 41:26***).

Silaha yenye athari nzuri aliyoitumia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliyojenga hofu na woga wa ajabu nyoyoni mwa maadui ilikuwa ni hiyo Qur'ani yenyewe. Machifu wa Waquraishi waliweza kuona ya kwamba wengi wa maadui wa jadi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walikwenda kukutana nae kwa nia ya kumdhihaki au kumdhuru. Lakini mara tu walipozisikia aya chache za Kitabu hiki Kitakatifu waligeuka na kuwa wafuasi wake waaminifu. Ili kuyazuia matukio kama hayo, Waquraishi waliamua kuwazuia wa chini wao na wafuasi wao kuisikiliza Qur'ani na wakayaharamisha mazungumzo na Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Watunga Sheria Wenye Kuzivunja Sheria

Watu walewale waliozuia vikali kuisikiliza Qur'ani na kuwaadhibu wale wote waliolivunja tangazo lile, baada ya siku chache waliingia kwenye mkumbo wa wavunja sheria na kivitendo, walizivunja kwa siri sheria zile zile walizoziidhinisha wao wenyewe!

Siku moja Abu Sufyan, Abu Jahl, na Akhnas bin Shariq walitoka majumbani mwao na wakaelekea nyumbani kwa Mtume (s.a.w.w.) bila ya mmoja wao kutambua kuwa mwenzie nae anakwenda huko.

Kila mmoja wao alijificha kwenye kona, na lengo lao lilikuwa kuisikiliza Qur'ani ya Muhammad aliyokuwa akiisoma wakati wa usiku kwa sauti tamu, alipokuwa akisali. Wote walikaa pale hadi alfajiri, bila ya kutambua kule kuwapo kwa wale wenzie, na wakaisikia Qur'ani. Asubuhi ilibidi warudi majumbani mwao. Walikutana njiani na wakakemeana wenyewe kwa wanyewe wakisema kwamba kama watu wenye akili ndogo watavitambua vitendo vyao, watawafikiriaje?

Jambo hili hili lilirudiwa kwenye usiku uliofuata. Itaonekana kwamba shauku na mvuto wa ndani uliwavutia kwenda kule nyumbani kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Walipokuwa wakirejea, walikutana tena na wakakemeana tena na wakaamua kutokukirudia tena kitendo chao kile. Hata hivyo, mvuto wa Qur'ani ulikuwa mkali kiasi kwamba walikwenda tena nyumbani kwake bila ya kufahamiana na kukaa kandoni mwa nyum– ba ile na kuisikiliza Qur'ani hadi alfajiri. Walipozikiliza aya za Qur'ani, hofu yao ilizidi na kila mara, wakajiambia: "Kama hizi ahadi na vitisho vya Muhammad vikiwa sahihi, basi sisi tutakuwa tulioishi maisha ya dhambi!"

Kulipokucha waliondoka nyumbani pa Muhammad (s.a.w.w.) kwa kuchelea watu wenye akili finyu na vile vile wakakutana. Wote wakakiri kwamba hawakuweza kuvumilia mvuto wa 'mwito' na kanuni za Qur'ani. Hata hivyo, ili kuzuia tukio lolote lisilopendeza, walifunga mapatano baina yao ya kwamba hawatalirudia tendo hili tena.[6]

Kuwazuia Watu Wasisilimu

Baada ya kutekeleza ule mpango wa awali wa kuharamisha kuisikiliza Qur'ani, waliuanza ule mpango wa pili. Watu waliokuwa wakiishi kwenye sehemu za karibu na za mbali walipokuwa na mwelekeo wa kuelekea kwenye Uislamu walikuja Makkah. Wale wapelelezi walionana nao visin– gizio mbalmbalili. Hapa chini tunatoa mifano miwili ya dhahiri:

Mfano wa kwanza: Aa'asha alikuwa mmoja wa washairi wakuu wa Zama za Ujinga na mashairi yake yalikuwa yakinukuliwa kwenye mikusanyiko ya Waquraishi. Aa'asha alipata habari za maamrisho ya Allah na mafundisho mazuri ya Uislamu wakati alipokuwa yu mzee.

Aliishi kwenye sehemu iliyokuwa mbali na Makkah. 'Mwito' wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa bado haujaenea kwa ukamilifu hadi kuifikia sehemu ile, lakini hata yale machache aliyoyasikia kuhusu Uislam

kwa maelezo machache yalijenga huba kuu moyoni mwake juu ya Uislamu. Alitunga wasifu mzuri sana akimsifu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na hakuifikiria zawadi yoyote kuwa ni bora kuliko kuusoma wasifu ule mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ingawa idadi ya mistari ya wasifu huu haikuzidi ishirini na minne, mistari hii ndiyo bora zaidi iliyowahi kusomwa katika kumsifu Mtume (s.a.w.w.) katika nyakati zile.

Wasifu huu waweza kupatikana kwenye kitabu chake cha mashairi.7 Mshairi huyu anayatukuza mafundisho bora ya Mtume (s.a.w.w.) yaliyoiangaza akili yake.

Aa'asha alikuwa bado hajapata bahati ya kuja kwa Mtume (s.a.w.w.) wakati alipokutana na wale wapelelezi wa wenye kuabudu masanamu na wakazitambua hisia zake. Walijua vema kwamba Aa'asha alikuwa mtu wa anasa na mzoefu wa mvinyo. Mara moja waliitumia fursa ya ule unyonge wake na kusema: "Ewe Abu Basir! Dini ya Muhammad haiafikiani na fikara zako na hali ya utu wako." Akauliza; "Kwa nini?" wakamjibu: "Ameiharimisha zinaa." Akasema: "Sina lolote nayo, na jambo hilo halinizuii kusilimu."

Wakaendelea kusema: "Vile vile amekataza kunywa mvinyo." Aliposikia hivyo alipatwa na hali fulani ya mashaka na akasema: "Mimi bado sijakinaiwa na mvinyo. Sasa nitarudi na kunywa mvinyo hadi nishibe kwa kipindi cha mwaka mmoja na nitakuja tena mwaka ujao na kusilimu mikononi mwake!" Kisha akarudi kwake, lakini kifo hakikumruhusu kuyatekeleza yale aliyoyasema, kwa kuwa alifariki ndani ya mwaka ule ule.8

Mfano Mwingine

Tufayl bin Amr, aliyekuwa mtu mwenye hekima na mshairi mwenye sauti nzuri na aliyeheshimiwa mno na kabila lake, alikuja Makkah. Lilikuwa ni jambo lenye kuchukiza na kusumbua kwa Waquraishi kwamba Tufayl asilimu. Hivyo basi, wale machifu wa Waquraishi na wafanya kiini macho wa diplomasia walimkusanyikia na wakagumia, wakisema: "Yule mtu anayesali kandoni mwa Al-Ka'ba ameuharibu umoja wetu na kujenga mfarakano miongoni mwetu kwa masimulizi yake ya kiuchawi, nasi twachelea ya kwamba atajenga mfarakano wa aina hiyo hiyo ndani ya kabila lako pia. Hivyo basi, ingalifaa kama usingalizungumza naye kabisa."

Tufayl anasema: "Maneno yao yalinivutia mno kiasi kwamba hofu ya kwamba masimulizi ya kichawi ya Muhammad yangaliniathiri, niliamua nisizungumze naye au kusikiliza yale aliyosema. Hivyo basi, ili kujikinga na athari za uchawi wake, niliamua kutia pamba masikioni mwangu wakati nikifanya 'tawaaf,' ili sauti yake isinifikie anapoisoma Qur'ani na kusali sala zake.

Asubuhi ilipoingia niliingia msikitini baada ya kutia pamba masikioni mwangu na sikuwa na mwelekeo kabisa wa kumsikiliza hata kidogo akiongea. Hata hivyo, sijui ilitokeaje kwamba, kwa ghafla tu baadhi ya maneno yaliyo matamu mno na yenye kupendeza yalifika masikioni mwangu nami nikayafurahia mno.

Kutokana na hali hii, nilisema nafsini mwangu: “Na ulaaniwe! Wewe ni mtu wenye lugha fasaha na mwenye akili sana. Kuna madhara gani kama ukiyasikia ayasemayo mtu huyu? Kama anazungumza jambo zuri, huna budi kulikubali, la sivyo, ni sawa kama utaweza kulikataa. Hata hivyo, nilingojea ili nisiwasiliane na Mtume yule hadharani.

Mwishowe, Mtume (s.a.w.w.) alitoka kurudi nyumbani kwake na akaingia humo. Mimi nami niliomba na nikaruhusiwa kuingia nyumbani mwake. Nilimwelezea kisa kizima nikisema: “Waquraishi wanahusisha nawe vitu vingi mno, na hapo mwanzoni sikuwa na dhamira yoyote ya kuonana nawe. Hata hivyo, utamu wa Qur’ani umenivuta kwako. Sasa ninakuomba tafadhali, nieleze asili ya dini yako na unisomee sehemu ya Qur’ani. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alinifahamisha dini yake na akanisomea sehemu ya Qur’ani.”

Tufayl anaendelea kusema: “Ninaapa Wallahi! Sikupata kamwe kuyasikia masimulizi yenye kuzivutia mno na sikupata kuiona sheria iliyo ya wastani!” Kisha Tufayl akamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Mimi ni mtu mwenye uwezo na ushawishi katika kabila langu nami nitachukuwa hatua kwa ajili ya kuilingania dini yako.” Ibn Hisham anaandika ya kwamba[9] yeye (Tufayl) alikuwa pamoja na kabila lake hadi kwenye vita vya Khaybar na alibakia katika shughuli za kuubalighisha Uislamu na alijiunga na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye vita vile hasa pamoja na familia za kiislamu sabini au themanini.[10] Alisalia kuwa imara kwenye Uislamu hadi alipokufa Kishahidi mwenye vita vya Yamamah.

1. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.270.
2. Majma'ul-Bayan, Juzuu 10, uk. 387.
3. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 393.
4. Si Mashi’ah tu, hata watafiti wa kisunni akiwemo mfasiri mwanafalsafa na mchambuzi mkubwa aliye tegemeo na dira wa madhehebu ya kisunni Al- Fakhrud-Din Razi amekanusha wazo hilo. Mchambuzi huyu katoa hoja nyingi na hatimaye akasema: “Hatukubali kuwa usemi huu ulielekezwa kwa Nabii (s.a.w.).” Akajadili tena wazo hilo na kuhitimisha kwa: “Hayo hayaendani na tabia zake nzuri.” Kwa faida zaidi rejea kitabu chetu cha Kiswahili kiitwacho Uma’asumu wa Mitume, shehemu ya tatu inayohusu Uma’asumu wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) – (Mhariri).
5. Majma’ul-Bayaan, Juzuu 1, uk. 437.
6. Siirah-i Ibn Hishamu, Juzuu 1, uk. 337.
7. Diwaan-i Aa’asha, uk. 101-103.
8. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 386-388
9. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.410.
10. Dakta Haykal anasema: "Alijiunga na Mtume (s.a.w.w.) baada ya kutekwa kwa mji wa Makkahh lakini bado hatujapata ushahidi wowote wa kauli hii.

Sura Ya 19: Uzushi Wa Gharaaniq

Inawezekana kwamba baadhi ya wasomaji wetu wangalipenda kuijua asili ya ngano ya ‘Gharaaniq’ iliyonukuliwa na baadhi ya wanahistoria wa Kisunni, na hivyo wakaifahamu mikono iliyokuwa

ikijishughulisha katika kubuni na kutangaza uongo.

Wayahudi, na hasa viongozi wao wa Kidini wamekuwa, na bado wangali maadui wakuu wa Uislamu. Kikundi chao kama vile Ka'ab Ahbaar, ambacho kwa dhahiri walijifanya wamesilimu, walikuwa wakidumu katika kuuficha ukweli wa Uislamu kwa kuzusha uongo na kutangaza vitu visivyo na msingi kwa kuvihusisha na Mtume (s.a.w.w.), na badhi ya waandishi wa kiislamu, wakionyesha imani njema juu ya wanadini wenzao wote, waliukubali mwingi wa uzushi wao bila ya kuufanyia uchunguzi unaostahili na wakaukusanya ukiwa katika hali ya Ahadith na historia.

Hata hivyo, siku hizi fursa nyingi zaidi zinapatikana kwa upande wa wanachuoni kwa ajili ya kuchunguza mambo kama haya na hasa seti ya kanuni na mbinu zimetokea kwanye matumizi zikiwa ni matokeo ya juhudi za wanachuoni watafiti wa kiislamu katika kuzitofautisha kweli za kihistoria kutokana na ngano za uongo. Katika hali hii si sahihi hata kidogo kwa mwandishi, mwenye elimu kubwa katika mambo ya dini, kukubali kuwa ndio mwisho kwa kila alionalo kitabuni na kulinukuu pasi na kuthibitisha

Uzushi Wa Gharaaniq Ni Nini?

Inasemekana kwamba machifu wa Waquraishi kama vile Walid, Aas, Aswad na Umayyah walikutana na Mtume (s.a.w.w.) na wakapendekeza ya kwamba, ili kuziondoa tofauti zilizokuwapo baina yao, kila upande kati ya hizo mbili, uwatambue miungu wa ule mwingine. Wakati ule ule '*Surah al- Kafirun'* ilifunuliwa kulijibu pendekezo lao na Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa kusema hivi: **"Mimi sikiabudu kile mkiabuducho, wala ninyi hamumwabudu Yule Nimwabuduye."**

Hata hivyo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na shauku kuu ya kupatan- isha kati yake na watu nae alipenda kwamba iweze kufunuliwa amri itakayopunguza umbali baina yake na jamaa zake. Siku moja alikuwa ameketi karibu na Al-Ka'ba akiisoma *Suratun-Najm* kwa sauti ya kuvuma sana. Alipozifikia aya hizi mbili: **"Je, umeyafikiria al-Lat na al-Uzza na jingine la tatu Manat?" (Surah al-Najm, 53:19-20),** kwa ghafla shetani akafanya azitamke sentensi nyingine mbili ambazo ni: "Hawa ni Gharaaniq[1] walio na vyeo vikuu na maombezi yao yanatakabaliwa," na kisha akazisoma aya zilizosalia.

Alipoifikia ile aya ya Sajdah (aya ya mwisho ya Surah ile), yeye Mtume mwenyewe pamoja na wale wote waliokuwapo pale, ama Waislamu au waabudu masanamu, wote walisujudia masanamu ila Walid tu aliyekuwa mzee sana kiasi cha kutoweza kufanya hivyo.

Yalikuwapo makelele na furaha miongoni mwa wale waliokuwamo msikitini mle na wenye kuabudu masanamu wakisema kwamba, Muhammad amezungumza vema juu ya miungu wao. Taarifa juu ya maafikiano ya Muhammad na Waquraish zikawafikia wale waliohamia Ethiopia na matokeo yake yakawa kwamba baadhi yao walirudi kutoka maskanini mwao (Ethiopia). Hata hivyo, waliporudi waligundua ya kwamba hali imebadilika tena na malaika amemletea ufunuo Mtume na kumtaka tena awapinge wenye kuabudu masanamu na alimwambia kuwa Shetani amemfanya ayatamke maneno yale na yeye (malaika) hakuyasema katu!

Hiki ndicho kiini cha uzushi huu wa 'Gharaaniq' ambao wataalamu wa mambo ya nchi za Mashariki (Mustashriq) wanayo shauku kuu ya kuunukuu kwa majivuno mengi.2

Kuelezeka Kwa Urahisi Kwa Uzushi Huu

Unaweza kudhania kwamba Muhammad hakuwa mmoja wa wateule wa Allah, bali hekima na akili zake haviwezi kukanwa kwa vyovyote vile. Basi sasa ni vipi mtu mwenye busara akielekee kitendo kama hiki? Je, yawezekana kwamba mtu mwenye busara zake anayeona kwamba idadi ya wafuasi wake inakuwa kubwa siku hadi siku na mpasuko kwenye safu za adui unakua, katika hali hiyo, afanye jambo liwezalo kukishusha chini cheo chake mbele ya marafiki zake pamoja na maadui zake?

Je, waweza kuamini kwamba yule mtu aliyezikataa ahadi za vyeo, na uta– jiri kutoka kwa Waquraishi, kwa ajili ya dini ya Allah aanzishe tena ushirikina na ibada ya masanamu? Achilia mbali kuzungumzia juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hatuwezi kutegemea kitu cha aina hii japo kutoka kwa mwana mageuzi au mtawala wa kawaida.

Uamuzi Wa Busara Juu Ya Ngano Hii

Kwanza: Kwa mujibu wa hukmu ya busara, waalimu watakatifu daima ni wenye kinga kutokana na aina zote za makosa kutokana na nguvu ya kutokosea waliyokuwa nayo. Lakini tukikubali kwamba wao nao wana uwezekano wa kutenda makosa kwenye mambo ya kidini, ule msingi wa imani walionao watu kwenye maneno yao huvunjikia mbali.

Hivyo basi, ni muhimu kwamba hatuna budi kuyachunguza mambo ya kihistoria kwa msingi wa itikadi zetu za kiakili na tuyafumbue mafumbo haya ya historia kwa itikadi yetu iliyo madhubuti. Na haipingiki kwamba unyoofu wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) katika kuibalighisha dini ya Allah haungeruhusu kutokea kwa matukio ya aina hii.

Pili: Ngano hii imesimamia kwenye dhana ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) alichoshwa na jukumu ambalo Allah ameliweka begani mwake na alihangaishwa mno na mtengano na kitendo cha watu wake kuwa mbali nae. Hivyo basi, alikuwa na shauku ya kupata njia na jinsi ya kurekebisha hali yao. Hata hivyo, ni lazima Mitume wawe na subira mno na wavumilivu, umadhubuti wao hauna budi kuwa mfano miongoni mwa watu wote na katu wasifikirie kuiacha kazi yao.

Kama ngano hii ikiwa tukio la kweli na lililothibitishwa, litakuwa na maana ya kwamba shujaa wa masimulizi yetu kapoteza umadhubuti, na subira yake na ari yake vimeshuka na amechoka. Kwa kweli hili hali– afikiani na hukmu ya hekima na vile vile haliafikiani na maisha ya Mtume (s.a.w.w.) ya kale na yaliyofuatia, kama tuyajuavyo.

Mzushi wa Hadithi hii ameukataa ukweli uliopo kwamba, Qur'ani inaushuhudia uongo wa hadithi hii, kwa sababu Allah amembashiria ya kwamba uongo hautaingia kwenye njia Yake: ". . . . **Hiki ni Kitabu**

chenye kuheshimika. Haitakifikia batili kutoka mbele wala kutoka nyuma yake; . . . .” (***Surah al-Fussilat*, 41:41-42**).

Vile vile Allah ame- toa ahadi nzito ya kwamba ataihami Qur’ani kutokana na kila madhara kipindi chote cha historia nzima ya mwanaadamu: **“Hakika Sisi tumeit- eremsha Qur’ani na hakika Sisi ndio Wahifadhi wake.”** (***Surah Hijr;* 15:9**).

Hivyo basi, ingaliwezekana kwamba yule mlaaniwa (shetani) amshinde nguvu mteule wa Allah, achomeke uongo mwenye Qur’ani Yake na aifanye Qur’ani ambayo msingi wake hasa umesimamia kwenye kampeni dhidi ya ibada ya masanamu, kuwa mwendelezaji wa mfumo wa ibada ya ushirikina.

Inashangaza kwamba Mbunifu wa ngano hii ameimba wimbo usio na utaratibu wa sauti na ameusingizia Upweke wa Allah kwenye sehemu ile ambayo muda mfupi kabla ya hapo, Qur’ani tukufu yenyewe imepingana na masingizio haya, kwa sababu kwenye aya ya tatu, ya nne na ya tano ya Surah ile ile; Allah amesema: **“. . . .Yeye (Mtume) hasemi kwa tamaa yake. Huu ni ufunuo uliofunuliwa (kwake). Amemfundisha Yule Mwenye nguvu, Mkuu.”**(***Surah al-Najm*, 53:3-5**).
Bila ya kujali bishara hii bayana, ni vipi Yeye Allah amwache Mtume wake bila ya ulinzi wowote na aruhusu kwamba Shetani aikamate akili na fikara zake?

Tunasikitika kuijadili ngano hii kwa kirefu kuliko vile inavyostahili. Lakini ukweli ni kwamba maelezo yetu yamesimamia kwenye hoja za kiakili nayo yana faida kwa wenye kuuamini Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, hoja hizi hazitoshi kwa wale wataalamu Mustashirki, ambao bado nyoyo zao hazijaangazwa na imani juu ya Mtume (s.a.w.w.) na ambao huzinukuu na kuzieleza ngano za aina hii ili kuthibitisha ya kwamba dini hii haina matokeo mema. Hivyo basi, hatuna budi kujadiliana nao juu ya jambo hili kwa njia nyngine.

Hitilafu Ya Hadithi Hii Kwa Njia Nyingine

Historia inatuambia kwamba pale Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akiisoma Sura al-Najm, machifu wa Waquraishi ambao wengi wao walikuwa ni washairi wakuu na wasomi walikuwamo msikitini mle. Mmoja wao alikuwa ni Walid aliyekuwa mtabiri na mshairi wa Uarabuni na alikuwa maarufu kwa hekima na busara zake. Nao wote waliisikia Sura ile hadi mwishoni na wakafanya Sajdah ilipomalizikia na aya iwajibishayo Sajdah.

Hivyo basi, swali liibukalo hapa ni kwa nini watu hawa, waliokuwa washairi wakuu na wanachuoni, watosheke na sentensi mbili tu zinazowasifu miungu wao, wakati aya zinazozitangulia na zinazozifuatia hizi sentensi mbili zina maonyo na lawama kwa miungu wao?

Haifahamiki ni maoni yapi anayoyajenga huyu mzushi wa uongo huu wa dhahiri juu ya watu wale ambao lugha yao ya asili ilikuwa ni kiarabu, waliokuwa wakifikiriwa kuwa ndio washindi kwenye uwanja wa ufasaha wa lugha ndani ya jamii nzima ya kiarabu, na ambao walijua vidokezo na sitiari (achilia mbali

mambo ya dhahiri) za lugha yao, bora zaidi kuliko yeyote mwingine.

Je, ilikuwa sahihi kwao kutosheka na sentensi hizo mbili zinazoisifu miungu yao na kuzidharau sentesi zilizotangulia na zilizofuatia? Tukiachilia mbali watu wengine, haiwezekani kuwahadaa hata watu wa kawaida kwa sentensi zenye mvuto wa uzuri ziwekwazo kwenye maelezo yenye lawama kamili kwa itikadi na mwenendo wao.

Sasa tuziandike zile aya zihusikazo na tuweke madoa badala ya hizi sen- tensi mbili. Unaweza kuamua vizuri zaidi kama sentensi hizi mbili zaweza kuwekwa kwenye aya zilizofunuliwa juu ya lawama za masanamu haya: **"Je, umeyafikiria al-Lat na al-Uzza na jingine la tatu Maanaat?**[3]

Je, Yeye (Allah) awe na mabinti nanyi muwe na wana? Hakika huu ni ugawaji wa kidhalimu! Wao (masanamu) si chochote ila ni majina ambayo ninyi na baba zenu mmeyazusha. Allah hakuyapa mamlaka yoyote".

Je, mtu, hata yule wa kawaida tu, aweza kuukubali msingi wa sentensi zipinganazo kama hizo, ili kuweza kuuacha uadui wake na kuja kwenye maafikiano na mtu ambaye dini yake imejitahidi kuing'oa mizizi (ya ibada ya masanamu) kwa kipindi cha miaka kumi, na ameuhatarisha uhai wake kwa ajili ya njia ile?

Hoja Dhidi Ya Ngano Hii Kwa Mtazamo Wa Lugha

Mwanachuoni maarufu wa Kimisri, Muhammad Abduh anasema: "Katu neno *'Gharaaniq'* halikupata kutumika kwa ajili ya 'miungu' ndani ya lugha ya kiarabu na ushairi.
Maneno '*Gharnuq*' na *Gharniq*' yanapatikana kwenye kamusi nayo yana maana ya ndege maalumu wa majini au kijana wa kiume mwenye sura nzuri sana, kati ya maneno haya hakuna litoalo maana ya 'miungu.'

Ushahidi Utolewao Na Baadhi Ya Mustashirki

Sir (Bwana) William Muir ameichukulia ngano hii ya *Gharaaniq* kuwa ni ukweli wa kihistoria uliothibitika, na ushahidi alioutegemea ni huu: "Muda wa zaidi ya miezi mitatu tangu kuhama kwa Waislamu kwenda Ethiopia ulikuwa bado kupita, nao walikuwa wakiishi maisha ya amani chini ya ulinzi wa Negus. Wasingaliweza kurudi Makkah kuwaona ndugu na jamaa zao kama wasingalipata taarifa juu ya mapatano baina ya Muhammad na Waquraishi. Hivyo basi, lilikuwa ni jambo la muhimu kwamba Muhammad atoe njia ya amani na njia ile ilikuwa ni hadithi hii hasa ya '*Gharaaniq*' yenyewe"

Hata hivyo, mtu anaweza kumwuliza mtaalamu huyu maarufu wa mambo ya nchi za Mashariki. Kwanza: Kwamba ni kwa nini iwe muhimu kwamba kurejea kwa wahamiaji wale kule Makkahh kuwe ni matokeo ya taarifa zilizo sahihi? Katika maisha ya kila siku, watu wenye tamaa zao za kibinafsi hutawanya maelfu ya taarifa za uongo miongoni mwa watu kila mara. Hivyo basi, iliwezekana kabisa kwamba watu fulani

walizizusha taarifa hizo za mapatano baina ya Mtume Muhammad na Waquraishi kwa lengo la kuwafanya Waislamu warejee nchini mwao kutoka Ethiopia, na hivyo baadhi yao waliziamini taarifa zile na wakarejea, na ambapo wengine hawakudanganyika na wakaendelea kuishi huko Ehiopia.

Pili: Japo tuchukulie kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitaka kufanya amani na Waquraishi, ni kwa nini msingi wa amani ile usimamishiwe kwenye hizo sentensi mbili za uongo? Ukweli ni kwamba, ingalitosha kuzivutia nyoyo zao kwake kama angaliwapa ahidi ya kweli ya kunyamaza kabisa kuhusiana na itikadi zao.

Kwa ufupi ni kwamba, kurejea kwa wahamiaji hawa si ushahidi wa usahihi wa ngano hii, pia amani na mapatano navyo havitegemei kuzitamka sentensi hizi mbili.

1. Gharaaniq ni wingi wa neno Gharnuq au Gharaaniq kwa maana ya aina fulani ya ndege wa majini au kijana mwenye sura nzuri sana.
2. Tarikh–i Tabari, Juzuu 2, uk. 75–76.
3. Kama ukiijaza ile nafasi iliyoachwa wazi kwa kuiweka tafsiri ya zile sentensi mbili tunazozizungumzia (Hawa ni gharaaniq, walio na vyeo vikuu na maombezi yao yanatakabaliwa) bila shaka utaona kwamba zinapingana na aya zinazozitan– gulia na zinazozifuatia.

Sura Ya 20: Vikwazo Vya Kiuchumi

Njia ya rahisi na ifaayo kabisa ya kuwaangusha walio wachache kwenye jamii ni kufanya kampeni hasi, ile iliyomo kwenye msingi wa umoja na mapatano.

Kampeni chanya hulazimu vyanzo mbali mbali, kwa kuwa huwa muhimu kwamba lile kundi linalopigana linapaswa litumie silaha za kisasa na linapaswa pia lifikie lengo lake kwa kutoa mihanga ya kimwili na kiuchumi na kwa kushinda mamia ya vizuizi. Ni dhahiri kwamba aina hii ya kampeni inaandamana na maumivu na taabu nyingi. Watawala wenye hekima huitumia kampeni hii baada ya kufanya matayarisho na maandalizi ya hitajikayo na hawautumii mpango huu ila pale ikosekanapo njia nyingine na kubakiwa na njia ya vita tu.

Hata hivyo, kampeni hasi haiyahitaji yote hayo. Inakihitaji kipengele kimoja tu nacho ni umoja na mapatano ya walio wengi. Hii ina maana ya kwamba, kikundi cha watu ambao lengo lao ni kuliangusha kundi la walio wachache, huungana kwa uaminifu na kufanya mkataba na kuapa kwamba watakata uhusiano na lile kundi pinzani la wachache, wasiruhusu kufanya biashara nao, kukatisha uhusiano wa ndoa nao, hawatawaruhusu kushiriki kwenye mambo ya pamoja na hawatashirikiana nao kwenye mambo ya mtu na mtu. Katika hali hiyo, dunia pamoja na upana wake wote huu, huwa kama jela ndogo na nyembamba kwao wale wa kundi dogo, na kila wakati; shinikizo lake hulihofisha kundi hili juu ya maangamizo.

Wakati mwingine kundi hili pinzani la walio wachache kufikia hapa hujisalimisha na kutii uamuzi wa walio wengi. Hata hivyo, kundi la walio wachache la aina hiyo, halina budi kuwa la watu wale ambao upinzani wao hausukumwi na lengo la kiroho. Kwa mfano, wanaweza kuwa wamefanya kampeni ili wajipatie utajiri, vyeo muhimu na nafasi za kiserikali.
Watu kama hawa pale wanapoihisi hatari, na wakawa wanakabiliwa na matatizo ya vizuizi, wao kutokana na kutokuwa kwao na msukumo wa kiroho, na sababu zao zikawa ni za kidunia tu, hupendelea faida kuu iwezayo kupatikana kuliko zile furaha za muda mfupi na kuyakubali matakwa ya walio wengi.

Hata hivyo, wale watu ambao upinzani wao unatokana na imani hawa– hofishwi na magumu ya aina hiyo. Shinikizo la vizuizi huiimarisha imani yao na huyakubali mapigo na mashambulio ya adui kwa ngao ya subira na ustahimilivu.

Kurasa za historia ya mwanaadamu zinashuhudia ukweli uliopo ya kwam– ba kipengele chenye nguvu zaidi kwa ajili ya uthabiti na uimara wa wachache dhidi ya malengo ya walio wengi ni nguvu yao ya imani, na wakati mwingine hulitoa mhanga tone la mwisho la damu yao katika kulifikia lengo lao. Na yako mamia ya ushahidi wa kuthibitisha usahihi wa maneno haya.

Azimio La Waquraishi

Machifu wa Waquraishi walipatwa na wasiwasi mno kutokana na kukua kushangazako kwa Uislamu, nao walikuwa na shauku ya kupata njia fulani ya kujitoa kwenye hali hii. Kusilimu kwa watu wengi kama vile Bwana Hamza na mwelekeo wa wenye uoni wa dhahiri wa Quraishi kwenye Uislamu, pamoja na uhuru walioufaidi wale Waislamu walioko kule Ethiopia nako kuliongeza mashaka na mshangao wa watawala wa zama zile. Vile vile walisikitishwa mno na kushindwa kwa mipango yao, na hivyo basi wakaufikiria mpango mwingine. Walifikiria kizuizi cha uchumi juu ya Waislamu ili waweze kuzuia kupenya na kuenea kwa Uislamu, na kumzuia yule mwasisi na wafuasi wa dini ya Allah wasiyatekeleze mambo yao.

Hivyo basi, machifu wa utawala walibandika kwenye Al–Ka'ba hati ya mapatano iliyoandikwa na Mansur bin Akramah na kuidhinishwa na halmashauri kuu ya Waquraishi na wakaapa ya kwamba jamii ya Waquraishi watatekeleza hadi kifo chao mambo yafuatayo:

1. Kila aina ya biashara na kazi na wasaidizi wa Muhamad itapigwa marufuku.
2. Kushirikiana nao kwa njia yoyote ile kumepigwa marufuku kabisa.
3. Hakuna mtu yeyote aruhusiwaye kufanya mapatano ya ndoa na Waislamu.
4. Wapinzani wa Muhammad ni lazima wasaidiwe kwa hali yoyote ile.

Maandiko ya mkataba huo wenye mambo tuliyoyataja hapo juu yalitiwa saini na Waquraishi wote walio maarufu na ulitwaliwa na kuanza kutekelezwa kikamilifu dhidi yao. Bwana Abu Twalib, mfuasi mashuhuri wa Mtume (s.a.w.w.) aliwaalika ndugu zake (dhuria wa Hashim na Abdul– Muttalib) na kuwawajibisha kumsaidia Mtume (s.a.w.w.). Vile vile aliamua kwamba familia hizo zote zitoke mjini Makkah na ziende

zikaishi kwenye bonde lijulikanalo kwa jina la ‘Bonde la Abu Twalib’ lililoko baina ya milima ya Makkah, wajenge hapo nyumba ndogondogo na mahema, na wawe mbali na mazingira ya wenye kuabudu masanamu. Ili kujikinga na mashambulizi ya ghafla, yawezayo kufanywa na Waquraishi, pia alipanga kujenga minara ya doria (ziginari) hapo na kuweka doria watakaomtaarifu matukio mapya yoyote yale.[1]

Kizuizi hiki kilidumu kwa muda wa miaka mitatu na shinikizo na taabu walizozipata zilichukua ukubwa usio na kifani. Vilio vyenye kuzipasua nyoyo vya watoto wa Bani Hashim viliyafikia masikio ya watu wa Makkah wenye nyoyo za mawe, lakini havikuwa na athari zozote masikioni humo. Vijana na watu wazima walikula tende moja tu kwa kila mtu na nyakati zingine waliigawa tende nusu kwa nusu. Katika kipindi chote hiki cha miaka mitatu, watu wa ukoo wa Bani Hisham walitoka nje ya bonde lile wakati ule tu wa ile miezi mitakatifu tu (ambayo vita imeharimishwa) wakati amani ilipotawala kila mahali kwenye Penisula ya Uarabuni. Katika vipindi hivi, walinunua vitu vidogo vidogo na kisha wakarudi kule bondeni. Kiongozi wao mashuhuri, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nae aliweza kuilighania dini yake kwenye miezi hii tu. Hata hivyo, washauri na mawakala wa Waquraishi walilitekeleza lile shinikizo la kiuchumi hata kwenye miezi hii, kwa sababu, kwa kawaida wao walikuja madukani na kwenye maghala na pale Waislam walipotaka kununua kitu, wao walilipa bei kubwa kubwa kwa kitu kile na wakakin- unua wao ili kuwafanya Waislamu wasiweze kukipata. Abu Lahab alikuwa hasa ndiye mshughulikaji sana katika hili. Aliwaambia watu kwenye mitaa ya maduka kwa sauti kubwa kwamba: “Enyi watu! Pandisheni bei za vitu na muwakoseshe wafuasi wa Muhammad uwezo wao wa kununua.” Hivyo basi, ili kuhakikisha ya kwamba kunadhibitiwa bei kwenye kiwango cha juu, yeye mwenyewe alivinunua vitu kwa bei ya juu. Kwa sababu hii, kiwango cha bei kilisalia kuwa cha juu wakati mwingi.

Hali Ya Kuhuzunisha Ya Bani Hashim

Shinikizo la njaa lilikuwa limefikia hatua ambayo Sa’ad bin Waqqas anase- ma: “Usiku mmoja nilikuwa nikitoka mle bondeni katika hali ambayo kwamba nilikuwa karibuni kuzimaliza nguvu zangu zote. Mara nikaiona ngozi ya ngamia iliyokauka. Nikaiokota, nikaiosha, nikaichoma na kuifunda. Baada ya hapo niliikanda na maji na nikaitumia kwa muda wa siku tatu.”

Wapelelezi wa Waquraishi waliendelea kuzilinda njia zote ziingiazo mle bondeni ili kuhakikisha kwamba mtu yeyote asiwaletee mahitaji yoyote Bani Hashimu. Hata hivyo, ingawa walizitawala hivyo njia zile, Hakim bin Hizaam mpwawe Bibi Khadijah, Abul Aas bin Rabi,i na Hisham bin Umar, kila mara walikuwa wakiwasheheni ngamia kwa ngano na tende kwenye nyakati za usiku na kuwaleta karibu na bonde lile. Kisha walizifunga hata- mu zao shingoni mwao na kuwaachia. Wakati mwingine kuutoa msaada huu nako kuliwaletea matatizo.

Siku moja Abu Jahl aliona kwamba Hakim alikuwa amemsheheni ngamia kwa chakula na kumwongozea kwenye bonde lile. Alichukizwa mno na Hakim na akamwambia: “Nadhani nikupeleke kwa Waquraishi na kukufedhehesha.” Ugomvi wao ule uliendelea. Abul Bakhtari aliyekuwa mmoja wa maadui wa Uislam hakukikubali kitendo kile cha Abu Jahl na akasema: “Anampelekea chakula shangazi yake (Khadija).

Huna haki ya kumzuia asifanye hivyo.” Hakutosheka na sentensi hii tu, bali vile vile alimshambulia Abu Jahl.

Ukali wa kitendo cha Waquraishi katika kuyatekeleza mapatano yao haukuipunguza subira na umadhubuti wa Waislamu. Hatimaye, makelele ya vichanga na watoto yenye kuhuzunisha na hali ya kisikitisha ya Waislamu viliamsha hisia za baadhi ya watu. Walijutia mno kutia saini kwao mkataba ule na wakaanza kuzifikiria njia za kulimaliza tatizo lile.

Siku moja Hisham bin Umar alikwenda kuonana na Zuhayr bin Abi Umayyah aliyekuwa mwana wa bint yake Abdul–Muttalib na kumwambia: “Je, ni sahihi kwamba wewe uwe unakula chakula na kuvaa nguo nzuri ambapo ndugu zako wanabakia na njaa na uchi? Ninaapa kwa jina la Allah! Kama ungechukua uamuzi wa aina hiyo, juu ya nduguze Abu Jahl na ukamtaka autekeleze uamuzi huo, katu asingekubali kufanya hivyo.” Zuhayr akasema: “Mimi peke yangu siwezi kuubadili uamuzi wa Waquraishi, lakini kama mtu mwingine akiniunga mkono nitaupasua mkataba ule.” Hisham akasema: “Mimi niko pamoja nawe.” Zuhayr akasema: “Mtafute mtu wa tatu pia.” Hisham akaamka na kutoka nje kumtafuta Mut’am bin Adi.

Alikutana nae na akamwambia: “Sidhanii ya kwamba ungalipenda kwamba yale makundi mawili (yaani Bani Hashim na Bani Muttalib) ya kizazi cha Abd Munaf, familia ambayo wewe nawe unayo heshima ya kuwa ndiyo familia zako, yafe.” Akajibu akisema: “Nifanye nini? Mtu mmoja hawezi kufanya lolote kwenye jambo hili.” Hisham akajibu: “Watu wawili nao wako pamoja nawe, nao ni mimi na Zuhayr.” Mut’am akasema; “Ni muhimu kwamba watu wengine nao washirikiane nasi.”

Kisha Hisham akalieleza jambo hili kwa Abul Bakhtari, na Zam’a pia, na kuwaomba washirikiane nao. Matokeo yake ni kwamba wote walikubaliana wakutane msikitini siku iliyofuata, asubuhi na mapema.

Mkutano wa Waquraishi hawa ulifanyika na Zuhayr na wasiri wake wal– ishiriki. Zuhayr akasema: “Inafaa tu kwamba leo Waquraishi washike usukani wa kuliondoa hili doa lenye kuaibisha. Ni muhimu kwamba huu mkataba wa kikatili ni lazima upasuliwe leo hii, kwa kuwa hali yenye kuhuzunisha ya watoto wa Hashim imefanya kila mtu akose raha.”

Abu Jahl aliyaingilia mazungumzo yale na akasema: “Mpango huu hautekelezeki hata kidogo na yale mapatano ya Waquraishi ni lazima yaheshimiwe.” Kutoka ule upande wa pili, aliamka Zum’a na kumwunga mkopno Zuhayr, akasema: “Ni lazima yapasuliwe, nasi hatukuyapendelea tangu mwanzoni.” Kutoka kwenye pembe nyingine, waliokuwa na shauku ya kwamba yale mapatano yakome, waliamka na kumwunga mkono Zuhayr. Abu Jahl akatambua ya kwamba jambo lile limefika kwenye hatua iliyo ngumu na kwamba ulifanyika ushauriano wa kabla, na kwamba watu wale walikuwa tayari walishachukua maamuzi yeye(Abu Jahl) akiwa hayupo.

Hivyo hakuushikilia msimamo wake na akakaa kimya. Mut’am aliitumia fursa ile na akaenda pale ilipokuwapo ile karatasi ya mapatano ili akaipasue. Hata hivyo, aliona ya kwamba karatasi lote limeliwa na mchwa, na ni yale maneno: “Kwa jina la Allah” (ambayo kwayo wale Waquraishi waliyaanza maandiko yao) ndiyo tu yaliyobakia.[2]

Baada ya kuyaona mabadiliko yale, Bwana Abu Twalib alimsimulia mpwa wake Muhammad jambo lile na matokeo yakawa kwamba wale waliokim- bilia kwenye bonde lile wakarejea majumbani mwao.[3]

1. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 350; na Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk. 78.
2. Siirah-i Ibn Hishamu, Juzuu 1, uk. 375; na Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk. 79.
3. Kauli yenye nguvu kwetu ni kuwa ni yeye mwenyewe Mtume ndiye aliyempa Abu Talib habari za kuliwa karatasi ile, naye akaenda moja kwa moja kwa Waquraishi kuwapa habari hiyo - Mhariri.

Sura Ya 21: Bwana Abu Twalib Afariki Dunia

Kizuizi kilichowekwa na Waquraishi dhidi ya Waislamu kilimalizikia kwenye kushindwa kutokana na kuingiliwa na watu wenye nyoyo njema. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wasaidizi wake walilitoka lile "Bonde la Abu Twalib" na kurudi majumbani mwao baada ya miaka mitatu ya ukim- bizi, kuzuiliwa na shida. Kazi na biashara zao na Waislamu zikafufuliwa na iliweza kutegemewa ya kwamba hali yao ingalitengenezeka. Hata hivyo, mara kwa ghafla, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akakabiliwa na tukio liumalo mno lililoacha athari mbaya mno kwenye hamasa za Waislamu wasiokuwa na msaada wowote.

Kadiri ya athari za tukio hili kwenye hali ile mbaya haiwezi kupimwa kwa kipimo au mizani yoyote ile, kwa sababu kukua kwa wazo au fikra hutegemea visababisho viwili, navyo ni uhuru wa kuzungumza na uwezo uhitajikao kwa mtu kuweza kujitetea dhidi ya mashambulio maovu ya adui. Hivyo basi, ilitokea kwamba pale Waislamu walipojaaliwa uhuru wa itikadi, walikipoteza kile kisababisho cha pili kwa sababu yule msaidizi na mlinzi mkuu wa Uislamu alifariki dunia.

Siku ile Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpoteza msaidizi na mlinzi aliyekuwa anahusika juu ya ulinzi na usalama wake tangu pale Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa na umri wa miaka minane hadi mwishoni, alipokuwa akipita kwenye mwaka wake wa hamsini. Ni yeye aliyekuwa akimzunguka zunguka mwilini mwake kama vile afanyavyo kipepeo kandokando ya mshumaa. Ni yeye aliyempatia Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) mahitaji ya maishani mwake hadi yeye mwenyewe alipopata uwezo wa kujipatia vitu hivyo na akampendelea zaidi kuliko yeye mwenyewe pamoja na wanawe.

Mtume (s.a.w.w.) alimpoteza mtu ambaye Bwana Abdul-Muttalib (babu yake Mtume s.a.w.w) alipofariki dunia alimfanya mlezi wake kwa maneno yafuatayo:

"Ewe Abdi Munaf![1] Ninakufanya kuwa mwenye kuwajibika juu ya ulinzi wa yule anayemwabudu Mungu Mmoja tu, kama alivyokuwa baba yake." Abu Twalib akasema: "Ewe baba yangu mpenzi! Muhammad hahitaji usia wowote kwa kuwa yu mwanangu mwenyewe na vile vile yu mpwa wangu."

Mifano Ya Huba Na Huruma Za Bwana Abu Twalib

Mifano ya huba na huruma za watu mbali mbali imeandikwa kwenye kurasa za historia. Hata hivyo, kwa kawaida imesimama kwenye msingi wa fikara za kidunia na kidesturi. Nayo huzunguka kwenye mhimili wa utajiri, na uzuri na ule mwali wa huba hutosheleza nafsini mwao katika kipindi kifupi sana na kisha hufutika. Hata hivyo, hisia zilizo kwenye msingi wa uhusiano wa udugu au itikadi kwenye ubora wa kiroho wa yule apendwaye haupotei upesi mno.

Ilitokea kwamba upendo wa Bwana Abu Twalib kwa Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa kwenye msingi wa hali zote mbili, yaani alimwamini na akamkubali kuwa yu mtu mkamilifu na kigezo kisicho kifani cha utu wema, na vile vile alikuwa yu mpwa wake hasa ambaye alimpa hadhi ya ndugu na mwana moyoni mwake.

Bwana Abu Twalib aliuamini mno ukamilifu wake wa kiroho na utakatifu kiasi kwamba wakati wa ukame alikwenda naye kwenye '*musallah*' (zulia la kusalia) na kumwomba Allah kwa 'wasila' wake na akaomba mvua kwa ajili ya watu waliokumbwa na ukame ule, na dua yake ilitakabaliwa na Allah Mwenyezi. Wanahistoria wamelinukuu tukio lifuatalo:

"Wakati mmoja Waquraishi walikabiliwa na ukame mkubwa mno na ardhi na mbingu zilizuia baraka zao juu yao. Walimjia Bwana Abu Twalib huku wakitiririkwa na machozi machoni mwao na wakamwomba kwa uaminifu aende kwenye musallah na amwombe Allah kwa ajili ya mvua. Bwana Abu Twalib alimshika mkono Mtume (s.a.w.w.), ambaye wakati ule alikuwa kijana mdogo, na akaegemea ukutani mwa Al-Ka'ba na akainua kichwa chake kuelekea mbinguni na akasema: "Ee Mola! Tunyeshee mvua kwa ajili ya mtoto huyu (akimsoza kwa kidole Mtume s.a.w.w) na utubariki kwa baraka Zako zisizo na kikomo."

Wanahistoria kwa pamoja wameandika hivi: "Alimwomba Allah kwa ajili ya mvua kulipokuwa hakuna hata wingu moja mbinguni, lakini baada ya hapo lilitokea wingu upesi sana kutoka kwenye upeo wa macho. Sehemu ya wingu lile ilienea kwenye anga juu ya mji wa Makkah na viungani mwake. Ngurumo na radi vilitoa sauti kuu. Sehemu zote zikafurika maji na kila mtu akafurahi."[2]

Mabadiliko Kwenye Mpango Wa Safari

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa bado hajaufikia umri wa miaka kumi na miwili wakati Bwana Abu Twalib alipoamua kwenda Sham pamoja na msafara wa kibiashara wa Waquraishi. Wakati ngamia walipokuwa wameshasheheni na walikuwa karibuni kuanza safari, na tayari kengele ya kuondokea ishagongwa, mpwa wake Bwana Abu Twalib, kwa ghafla akaishika hatamu ya ngamia na akasema huku akitokwa na machozi machoni mwake: "Mpenzi ami yangu! Unaniacha katika dhamana ya nani? Ni lazima niende pamoja nawe."

Hapo chozi lililokuwapo jichoni mwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) lilileta mafuriko ya machozi machoni

mwa Bwana Abu Twalib.

Kwenye wakati huu mgumu, aliamua bila ya matayarisho ya kabla yake, kwenda na yule mpwa wake. Ingawa nafasi ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kwenye msafara ule haikujadiliwa, Bwana Abu Twalib aliamua kuzibeba taabu zihusikanazo na kule kufuatana naye, yeye mwenyewe. Alimpakiza kwenye ngamia wake na alichukua tahadhari iliyolazimika kwenye safari nzima kuhusiana naye. Kwenye msafara ule aliona mambo yasiyo na kifani ndani ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na akatunga beti za mashairi juu ya mambo hayo. Beti hizo zimenukuliwa mwenye vitabu vyake vya ushairi.[3]

Ulinzi Wa Itikadi Zake Takatifu

Kwa upande wa kuwa madhubuti, hakuna nguvu iliyo sawa na ile ya imani. Nguvu ya imani kwenye lengo lake mtu ndicho kipengele chenye nguvu zaidi kwa maendeleo ya mwanadamu katika daraja zote za maisha. Inamtayarisha kuuhimili usumbufu na taabu zote na kumfanya ayatoe mhanga maisha yake yenyewe kwa ajili ya kulifikia wazo lake takatifu.

Askari mwenye silaha ya nguvu ya imani yu mwenye kushinda kabisa. Anapoamini kwamba kuua au kuuwawa kwenye njia hii ni rehma, ushindi na kufaulu kwake vinathibiti. Kabla ya askari kupewa silaha za kisasa za kimaada hana budi kupata silaha ya nguvu ya imani, na ni lazima moyo wake ujazwe huba ya ukweli. Harakati zake wakati wa vita na wa amani hazinabudi kuongozwa na imani. Kwenda kwake vitani au kufanya kwake amani ni kwa ajili ya ulinzi wa itikadi yake tu.

Fikara na itikadi ni matunda ya mwelekeo na busara za mtu. Kama vile mtu awapendavyo watoto wake, vile vile anayapenda maoni yake yatokanayo na busara na moyo wake. Bali, huba yake kwa dini huwa kubwa hata kuliko ile ya wanawe. Hivyo basi, yuko tayari hata kukikumbatia kifo kwa ajili ya kuihami dini yake, lakini haendi umbali ule kuhusiana na kuwahami watoto wake.

Huba ya mwanaadamu juu ya utajiri na hadhi ina ukomo maalumu. Anaviendea vitu hivi kwa kiasi kile ambacho hahofishwi na kifo cha uhaki– ka. Hata hivyo, kuhusiana na dini yake, mtu yuko tayari kukitafuta kifo na akapendelea kifo cha heshima kuliko maisha ambayo ndani yake hataruhusiwa uhuru wa dini. Anaona kwamba maisha halisi ni yale ya ‘mujahidah’ (mwenye kujitahidi) na husema kwa kukariri: “Maisha ya kweli yanaandamana na imani na jihadi.”

Hebu yatupie jicho maisha ya Bwana Abu Twalib, muunga mkono mashuhuri na mlinzi wa Uislamu na Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Alikuwa na kichocheo gani kwenye njia hii na ni kipengele kipi kili– chomshawishi hadi kufikia kiwango cha kujihatarisha na maangamizi, kuutelekeza uhai wake, utajiri wake, cheo chake na kabila lake, na kuvitoa mhanga vitu vyote hivi kwa ajili ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.)? Ni ukweli ukubalikao kwamba hakuwa na hamasa ya kidunia na katu hakuwa na shauku ya kuipata faida yoyote ya kidunia kutoka kwa yule mpwa wake, kwa sababu kwenye siku zile, Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe hakuwa na utajiri wowote. Hakutaka kukipata cheo au nafasi yoyote ile, kwa sababu, tayari yeye alikuwa ameishika nafasi kuu zaidi kwenye jamii ya wakati ule na alikuwa ndiye

chifu wa Makkah na Batha. Na kusema kweli, angaliweza kukipoteza hata kile cheo na daraja lake kuu kutokana na kumhami Mtume (s.a.w.w.), kwa kuwa ulinzi wake ndio sababu ya machifu wa Makkah kuupinga ukoo wa Hashim na wa Abu Twalib.

Dhana Potovu

Inawezekana kwamba baadhi ya watu wenye uoni mfupi wa mambo wakadhania kwamba sababu ya kujitoa mhanga kwa Bwana Abu Twalib ni ule uhusiano wa kijamaa wa karibu zaidi uliokuwapo baina yake na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na ni kwamba ni kwa sababu hii kwamba alikuwa tayari kuyatoa mhanga maisha yake hasa kwa ajili yake. Hata hivyo, dhana hii haina msingi kiasi kwamba tafakari ndogo tu huudhihirisha upumbavu wake, kwa sababu kifungo cha udugu wa damu hakina nguvu kiasi cha mtu kuweza kuitoa nafsi yake yote kwa ajili ya mmoja wa ndugu zake na amtoe mhanga mwanawe mwenyewe (Saidina Ali a.s) kwa ajili ya mpwa wake, na kuwa tayari kumwona mmoja wao akikatwa vipande vipande kwa ajili ya mwenziwe.

Wakati mwingine hisia za kiudugu humvutia mtu kwenye kiwango cha maangamizi, lakini hakuna maana katika hisia hizi kuwa kali hivyo kwa ajili ya mtu maalum tu, ambapo Bwana Abu Twalib aliitoa mihanga yote hii kwa ajili ya mtu maalum miongoni mwa nduguze (yaani Mtume s.a.w.w) na hakufanya hivyo kuhusu dhuria wengine wa Abdul–Muttalib na Hashim.

Kichocheo Halisi Cha Bwana Abu Twalib

Kutokana na hayo tuliyoyaeleza hapo juu tunaweza kusema kwamba kichocheo halisi cha mihanga hii ya Bwana Abu Twalib kilikuwa cha kiro– ho na wala si cha kimaada, naye alikuwa tayari kulikabili shinikizo lolote lile la adui kwa ajili ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Ilikuwa hivyo kwa sababu, alimwamini kwamba yu kigezo halisi cha ubora na utu wema na ameiona dini yake kuwa ni mpango ulio bora zaidi kwa mtu kuweza kujipatia ustawi na furaha. Kwa vile alikuwa mpenzi wa ukweli, bila shaka alikuwa akiuhami ukweli.

Ukweli huu hudhihiri kutokana na beti za mashairi ya Bwana Abu Twalib, akizionesha hisia zake anasema kwamba Muhammad yu Mtume mithili ya Mitume Musa na Isa. Hii ifuatayo hapa chini ni tafsiri ya mashairi yake: “Watu mashuhuri hawana budi kutambua kwamba Muhammad yu Mtume na Kiongozi kama Mitume Isa na Musa na kila Mtume hulibeba jukumu la mwongozo wa wanadamu kwa amri ya Allah. Unaweza kuzisoma sifa zake kwenye Vitabu vya Mbinguni kwa usahihi kamili na haya ni maneno ya kweli na wala si masingizio juu ya ghaibu.”[4]

Kwenye shairi lake jingine lenye kusifia alililoliandika juu ya huyu mpwa wake, anasema hivi: “Je, hamjui ya kwamba sisi tunamwona Muhammad kama yu Mtume wa Allah kama Musa bin Imraan na tunazisoma habari zake kwenye Vitabu vilivyopita.”[5]

Beti tulizozitaja hapo juu pamoja na nyingine nyingi zinazopatikana kwenye kitabu cha ushairi cha Abu

Twalib na vile vile kwenye vitabu vya Ahadith na vya tafsiri ya Qur'ani zinadhihirisha ya kwamba kichocheo halisi cha Bwana Abu Twalib katika kumhami Mtume (s.a.w.w.) kilikuwa ni ulinzi wa dini ya kweli ya Uislamu. Hapa chini tutaitaja baadhi ya mihanga aliyoitoa, nawe unaweza kuamua vizuri, baada ya kufanya uchunguzi muhimu, kama ingaliweza kuhamasishwa na kitu chochote kile kisi– chokuwa imani ya kweli.

Mukhtasari Wa Mihanga Aliyoitoa Bwana Abu Twalib

Machifu wa Waquraishi walifanya mkutano nyumbani mwa Bwana Abu Twalib wakati Mtume (s.a.w.w.) akiwepo pia. Walizungumza wenyewe kwa wenyewe. Wale machifu waliamka kwenda zao bila ya kupata majibu ya mkutano ule, na 'Uqbah bin Abi Mu'it akaanza kusema kwa sauti kuu: "Mwacheni. Ushauri hauna faida yoyote. Ni lazima auawe; ni lazima amaliziwe mbali!"

Bwana Abu Twalib aliudhika sana alipoyasikia maneno haya lakini hakuweza kufanya lolote, kwa kuwa walikuja nyumbani kwake wakiwa ni wageni wake. Ilitokea kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitoka nje ya nyumba yake siku ile na hakurudi hadi jioni.

Ami zake walikwenda nyumbani kwake lakini hawakumkuta huko. Kwa ghafla Bwana Abu Twalib aliyakumbuka yale maneno ya 'Uqbah aliyoyatamka masaa machahce yaliyopita na akasema moyoni: "Bila shaka wameshamwua mpwana wangu na waishayamaliza maisha yake!"

Alifikiria kwamba uamuzi umekwishafanyika na kwamba ilikuwa muhimu kumhami Muhammad na kulipiza kisasi kwa wale Mafirauni wa Makkah. Aliwaita dhuria wa Hashim na Abdul–Muttalib na akatoa maelezo kwam– ba wote wafiche silaha kali ndani ya mavazi yao na wafike kwenye Masjidul Haraam kwa pamoja. Zaidi ya hapo, kwamba kila mmoja wao akae karibu na chifu mmoja wa Waquraishi na yeye Bwana Abu Twalib atakaposema kwa sauti kuu: "Enyi machifu wa Waquraishi! Ninamtaka Muhammad kutoka kwenu." Waamke mara moja na kila mmoja wao amuue yule chifu aliyekaa karibu naye, na hivyo machifu wote wawe wamekutana na hatima yao.

Bwana Abu Twalib alipokuwa karibu kuondoka, Zayd bin Harith aliingia nyumbani mle kwa ghafla na akawaona kwenye hali ya kuwa tayari tayari. Alishikwa na bumbuwazi alipoona hivyo na akasema: "Hakuna madhara yoyote yaliyompata Mtume. Yuko nyumbani kwa Mwislamu na sasa anajishughulisha na kuubalighisha Uislamu." Baada ya kuyasema hayo alitoka upesi upesi na kumwendea Mtume (s.a.w.w.) na kumwarifu ule uamuzi wa hatari aliochukua bwana Abu Twalib.

Hapo Mtume (s.a.w.w.) alikwenda nyumbani kwake. Baada ya Bwana Abu Twalib kuuona uso wa yule mpwa wake alitokwa na machozi machoni mwake na akasema: "Ewe mpwa wangu! Ulikuwa wapi? Je ulikuwa kwenye furaha huko na salama kutokana na kila dhara wakati huo?" Mtume (s.a.w.w.) alimthibitishia ami yake kwamba hakuna dhara lililojitokeza kutoka upande wowote ule.

Usiku wote ule Bwana Abu Twalib alikuwa akiwaza. Alitafakari juu ya jambo lile na akasema moyoni:

“Leo mpwa wangu hakuwa shabaha ya adui, lakini hawa Waquraishi hawatakaa kimya mpaka wamwue.” Aliona kwamba ni bora aende kule msikitini pamoja na dhuria wa Hashim na Abdul–Muttalib baada ya kuchomoza jua, wakati Waquraishi walipokuwa wamekusanyika pale, na kuwaarifu juu ya uamuzi wake ule ili kwamba, pengine huenda wakaogopa na wakaacha kupanga kumwua Muhammad. Jua lilipochomoza na muda ukafika kwa Waquraishi kutoka majumbani mwao na kwenda kujiunga na mikutano yao.

Walikuwa bado hawajaanza kuzungumza pale alipotokea Bwana Abu Twalib kwa mbali, nao wakaona ya kwamba mashujaa kadhaa wamefuatana naye. Wote wakawa makini na wakasubiri wasikie yale Bwana Abu Twalib aliyotaka kuyasema na ni kwa lengo gani kaja kule msikitini na watu wote wale.

Bwana Abu Twalib alisimama mbele ya mkutano wao na akasema: “Jana Muhammad alitoweka machoni petu kwa kitambo hivi. Nilidhani ya kwamba mmelitekeleza lile alilosema ‘Uqbah na kwamba mmemwua. Hivyo, nikaamua kuja hapa Masjidul Haraam pamoja na watu hawa. Pia niliwaagiza kwamba wawe nyuma ya kila mmoja wenu na mara tu wanisikiapo nikisema kwa sauti kuu waamke na kukushambulieni kwa silaha zao walizokuwa wakizificha. Hata hivyo, kwa bahati nimempata Muhammad akiwa hai na salama kutokana na madhara yoyote yale kutoka kwenu.” Kisha akawataka wale watu wake wazitoe silaha zao walizozi– ficha na akaiishilizia hotuba yake kwa maneno haya: “Wallahi! Kama mngalimwua, nisingalimwacha hata mmoja wenu na ningalipigana nanyi hadi mwishoni.”[6]

Kama ukitazama ndani ya wasifu wa maisha ya Bwana Abu Twalib utaona ya kwamba alimsaidia Mtume (s.a.w.w.) kwa miaka arobaini na miwili kamili na ameudhihirisha ushujaa mkubwa ajabu na kujitoa mhanga kwenye miaka kumi ya mwisho ya uhai wake iliyokuwa muhimu mno kwa sababu ya kule kuteuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume na kwa ‘mwito’ wake wakati ule. Kipengele pekee kilichomfanya aendelee kuwa madhubuti, kilikuwa ni imani yake yenye nguvu ya itikadi yake halisi na safi juu ya ile kazi takatifu ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Na kama tukiongezea ile mihanga ya mwanawe, Imam Ali (a.s.) maana ya beti za Ibn Abil Hadid, kama zilivyotafsiriwa hapa chini, hudhihirika kabisa:

“Kama Abu Twalib na mwanawe wasingalikuwako dini isingalifaulu. Alimsaidia na kumhami yeye (Mtume s.a.w.w) pale mjini Makkah, na mwanawe alipiga mbizi kwenye dimbwi la kifo mjini Yathrib kwa ajili yake.”

Wasia Wa Bwana Abu Twalib Wakati Wa Kufariki Kwake Dunia

Wakati wa kufariki kwake dunia Bwana Abu Twalib aliwaambia watoto wake: “Ninakuusieni juu ya Muhammad, kwa kuwa yu mtu mwaminifu wa Waquraishi na mtu mkweli wa Arabia na anayo maadili yote.
Ameileta dini iliyokubaliwa na nyoyo, lakini ndimi zimechagua kuikana kwa kuhofia kuchekwa na kudhihakiwa. Ninaweza kuona kwamba watu wanyonge na wasiokuwa na msaada wa Uarabuni wameamka kumsaidia Muhammad na wakamwamini, naye vile vile ameamka kuwasaidia katika

kuzivunja safu za Waquraishi. Amewafedhehesha wakuu wa Quraishi na ameyaharibu makazi yao na kuwaimarisha wasiokuwa na msaada na kuwapa hadhi." Aliyamalizia mazungumzo yake kwa maneno haya: "Enyi ndugu zangu! kuweni marafiki na wafuasi wa dini yake (Uislamu). Yeyote yule amfu- ataye atakuwa amestawi. Kama kifo kingalinipa muda zaidi, ningalizikinga hatari zote zimjiazo."7

Hatuna shaka juu ya hilo kwamba alikuwa mkweli kabisa katika kuyaelezea matakwa yake, kwa sababu huduma zake na mihanga yake, hasa kwenye kile kipindi cha miaka kumi ya mwishoni mwa uhai wake, vinaushuhudia ukweli wake. Ushahidi mwingine wa ukweli wake ni ile ahadi aliyomwahidi Muhammad mwanzoni mwa Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu yeye Mtume alipowakusanya ami na ndugu zake wote, na kuwabalighishia Uislamu, Bwana Abu Twalib alimwambia Mtume (s.a.w.w.): "Amka, ewe mpwa wangu! Wewe unacho cheo kikuu. Dini yako ndio dini tukufu zaidi miongoni mwa dini zote. Wewe u mwana wa mtu mkuu. Kama ulimi ukikudhuru, ndimi kali zaidi zitajitokeza kukuhami na panga zilizo kali zitazikata ndimi za maadui zako. Ninaapa kwa jina la Allah! Waarabu watakuwa watiifu mbele yako kama mtoto wa mnyama alivyo mbele ya mama yake."

Safari Ya Mwisho

Ingalikuwa bora kama tungaliulizia kuhusu ukweli wa itikadi ya Bwana Abu Twalib kutoka kwa akraba zake walio waaminifu, kwa kuwa mwenye nyumba ndiye mwenye kujua vizuri zaidi vilivyomo nyumbani mle.

1. Wakati Sayyidna Ali (a.s.) alipomwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu kifo cha Bwana Abu Twalib, Mtume (s.a.w.w.) alilia sana. Alimwagiza Sayyidna Ali (a.s.) atayarishe josho lake, na kisha akamwomba Allah kwa ajili ya wokovu wa roho ile iliyotoka.8

2. Alitajwa Bwana Abu Twalib mbele ya Imam wetu wa nne, Ali Zaynul Aabidin (a.s.). Yeye Imam akasema: "Nashangaa kwa nini watu wanatia shaka juu ya imani ya Abu Twalib, wakati mwanamke hawezi kuendeleza muungano wake ki-ndoa na mume asiye Mwislamu baada ya mwanamke yule kusilimu, na Fatimah binti Asad alikuwa miongoni ma wale wanawake waliosilimu kwenye siku za mwanzoni kabisa na bado akasalia kuwa mkewe Abu Twalib hadi pale alipofariki dunia

3. Imam wetu wa Tano, Muhammad Baqir (a.s.) anasema: "Imani ya Abu Twalib ilikuwa bora kuliko ile ya watu wengi, na Amir wa Waumini Ali bin Abi Twalib (a.s.) aliamrisha ya kwamba ifanyike Hajj kwa niaba yake."9

4. Imam wetu wa Sita, Jafar As-Sadiq (a.s.) amesema: "Abu Twalib alikuwa mithili ya watu wa pango. Walikuwa na imani nyoyoni mwao laki- ni wakajifanya kuwa washirikina. Kutokana na sababu hii watalipwa maradufu."10

Maoni Ya Wanachuoni Wa Kishi'ah

Wakiwafuata watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Ulamaa wa Imamiyah, kwa pamoja wanaafikiana juu ya ukweli kwamba Bwana Abu Twalib alikuwa mmoja wa Waislamu mashuhuri kabisa na alipofariki dunia alikuwa na moyo uliokuwa na imani iliyokamilika juu ya Uislamu na alikuwa mwaminifu sana kwa Waislamu. Wanachuoni hawa wameandika vitabu na makala nyingi juu ya jambo hili.

1. Wakati mwingine inasemekana kwamba jina halisi la Abu Twalib lilikuwa ni Imraan. Baadhi ya wanachuoni wanaona kwamba Abu Twalib lilikuwa ndio jina lake hasa na si "Kuniyat" (jina la ubaba) yake.
2. Siirah–i Halabi, Juzuu 1, uk. 125.
3. Diwaan–i Abu Twalib, uk. 33.
4. Majma'ul Bayaan, Juzuu 7, uk. 37; na al–Hujjah, uk. 56–57.
5. Majma'ul Bayaan, Juzuu 7, uk. 36; Ibn Hisham amenukuu beti kumi na tano za shairi hili kwenye Siirah yake, Juzu 1, uk. 352–353.
6. Taraa'if, uk. 85; na al–Hujjah, uk. 61.
7. Siirah–i Halabi, Juzuu 1, uk. 390
8. Sharh–i Nahjul Balagha, cha Abil Hadid, Juzuu 14, uk. 76.
9. Sharh–i Nahju Balagha, Juzuu 14, Uk. 68
10. Usul al–Kaafi, uk. 244.

Sura Ya 22: Mi'iraaj – Kupaa Mbinguni

Mi'iraaj Kwa Mujibu Wa Qur'anii, Hadith Na Historia

Lilikuwa tayari giza la usiku limeshaenea kwenye upeo wa macho na kimya kilishatawala juu ya uso wa maumbili. Muda ulikuwa umekwishafika wa viumbe vyenye uhai kujipumzisha na kulala ili kwamba waweze kupata nguvu kwa ajili ya amali zao siku iliyofuata.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nae hakuwa huru kutokana na kanuni hii ya maumbile (kulala) nae alitaka kujipumzisha baada ya kuzisali sala zake. Hata hivyo, mara moja aliisikia sauti. Nayo ilikuwa ni sauti ya Malaika Mkuu Jibriil (a.s.) aliyemwambia: "Usiku huu huna budi kuifanya safari isiyo kifani, nami nimeamrishwa kubakia pamoja nawe. Itakubidi kuzipitia sehemu mbalimbali za ulimwengu ukiwa umemrekebu mnyama aitwaye 'Buraaq".

Mtume (s.a.w.w.) aliianza safari yake kuu kutoka nyumbani mwa Bibi Ummi Haani (dada yake Amir wa waumini, Ali bin Abu Twalib a.s) na akiwa amemrekebu yule Buraaq, akaondoka kwenda Baytul Maqdis, uliokuwako nchini Jordan (Palestina ya siku hizi mjini Yerusalem) ambao vile vile huitwa Masjidul Aqsaa. Baada ya muda mfupi tu alishuka pale na kuzitembelea sehemu mbalimbali za msikiti ule na pia

aliutembelea mji wa Bethlehemu ulio mahali alipozaliwa Nabii Isa (a.s.) na vile vile alizizuru sehemu mbalimbali zihusikanazo na Mitume mbalimbali. Katika baadhi ya sehemu hizi vile vile alisali rakaa mbilimbili.

Baada ya hapo aliendelea na sehemu ya pili ya safari yake na kutoka pale alipaa mbinguni. Hapo sasa akaziona nyota na utaratibu wa ulimwengu na akazungumza na nafsi za Mitume waliotangulia na vile vile alizungumza na Malaika wa mbinguni. Aliviona vituo vya mibaraka na mateso (Pepo na Moto) na akayaona makazi ya watu wa Motoni na wa Peponi[1] kwa karibu zaidi, na hivyo akawa na utambuzi wa siri za maumbile, ukubwa wa ulimwengu na ishara za Allah, Mwenye nguvu zote. Kisha aliendelea na safari yake na akafika kwenye Sidratul-Muntaha[2] na kuuona ukiwa umefunikwa kabisa na uzuri, utukufu na ukuu. Hapa, safari yake ikakoma na akarejea kwa njia ileile aliyoendea. Wakati safari yake ya kurejea, vile vile alifika pale Baytul Maqdis kwanza na kisha akaja Makkah.

Akiwa njiani aliukuta msafara wa kibiashara wa Waquraish uliopoteza ngamia na uliokuwa ukimtafuta. Alikunywa maji kutoka kwenye chombo chao na akayamwaga yale yaliobakia ardhini, na kwa mujibu wa wasimulizi wengine, akaweka kizibo juu yake. Huu ulikuwa ni muda kabla ya alfajiri alipofika nyumbani kwa Ummi Haani na akashuka kutoka kwenye yule mnyama aliyempaza mbinguni. Bibi huyu alikuwa mtu wa kwanza aliyesimuliwa na Mtume (s.a.w.w.) jambo hili na vile vile siku iliy- ofuatia usiku ule alilisimulia jambo hili kwenye mkutano wa Waquraishi. Hadith ya 'kupaa' kwake na safari yake kuu, vitu vilivyosadikiwa na Waquraishi kwamba ni vitu visivyowezekana kabisa ilienea kutoka kinywa hadi kinywa kwenye vituo vyote na ikawatatanisha zaidi machifu wa Waquraish.

Kulingana na desturi zao za tangu kale, Waquraishi waliamua kumpinga na wakasema: "Hata hivi sasa wako watu humu mjini Makkah walioiona Baytul Maqdis. Kama hayo uyasemayo ni kweli basi hebu tueleze lilivyo jengo hilo." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuielezea tu jengo lile lilivyo, bali alieleza pia yaliyotokea baina ya Makkah na Baytul Maqdis na akase- ma: "Nilipokuwa njiani nilikutana na msafara wa kabila hili, uliokuwa umempoteza ngamia wao. Walikuwa na chombo kilichojazwa maji amba- cho kilikuwa sehemu ya masurufu yao. Nilikunywa maji kutoka kwenye chombo hiki na kisha nikakiziba.[3] Kwenye sehemu nyingine nilikikuta kikundi cha watu wenye ngamia aliyewakimbia na alikuwa amevunjika mguu."
Wale Waquraishi wakasema: "Hebu tuelezee juu ya ule msafara wa Waquraishi." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akawajibu akisema: "Niliwaona mahali paitwapo Tan'im (hii ni sehemu inapoanzia 'Haram' au mipaka mitakatifu ya mji wa Makkah).

Msafara wao uliongozwa na ngamia mwenye rangi ya kahawia nao walimwekea kitundu (cha kubebea watu juu ya mnyama) na hivi sasa wanaingia Makkah." Wale Waquraishi wali- sisimuliwa mno na taarifa hizi za uhakika na wakasema: "Tutautambua ukweli au uongo wako sasa hivi." Hata hivyo, haikuchukua muda mrefu kabla ya Abu Sufyani, kiongozi wa msafara ule kutokea na watu wakamweleza kwa kirefu yale aliyoyasema Mtume (s.a.w.w.). Maelezo yaliyopo hapo juu ni kiini cha yale yaliyoelezwa kwenye vitabu vya tafsiri ya Qur'anii tukufu na Hadith.[4]

Je, Mi'iraaj Ina Asili Ya Qur'anii?

Tukio la Mi'iraaj ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenda mbinguni imeta- jwa waziwazi kwenye Sura mbili za Qur'anii tukufu. Hapa chini tunatoa kwa kifupi aya zinazoitaja waziwazi Mi'iraaj.

Mwenye *Surat al-Israa* inasemwa hivi: **"Utukufu wote wamstahiki Yeye Yule aliyempeleka mja wake wakati wa usiku kutoka Masjidul-Haraam hadi Masjidul-Aqsaa ambao tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili tumwonyeshe baadhi ya Ishara Zetu; hakika Yeye (Allah) Yu Asikiaye, Aonaye." (*Surat al-Israa* 17:1).**

Kwa uwazi kabisa aya hii inayataja mambo yafuatayo:-

1. Ili kutuambia ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisafiri kuzipita dunia hizi kwenye kipindi tu, si kwa nguvu ya kibinadamu bali ni kwa kupitia nguvu ya ki-Ungu. Allah Mwenye nguvu zote anaianza kauli Yake kwa maneno: "Utukufu wote wamstahiki Yeye, yenye kuuonyesha ukweli ya kwamba Allah Yu safi kutokana na kila aina ya upungufu na mahitaji. Vile vile hakutosheka na hayo bali vile vile amejieleza kuwa Yeye ndiye chanzo cha safari ile kwa kusema: 'Asra' (Allah Amemwezesha kuifanya safari ile). Alijaalia upendeleo huu juu yake ili kwamba watu wasidhanie ya kwamba safari ile ilifanyika kwa mujibu wa kanuni za kimaumbile na kwa njia za nguvu ya kawaida, na hivyo wakaweza kuukataa uwezekano wake. Hivyo basi, imedhihirishwa ya kwamba ilifanyika kwa mapenzi ya Allah na kwa upendeleo maalumu wa Allah, Mwenyezi.

3. Safari hii ilifanyika wakati wa usiku.

4. Licha ya ukweli kwamba safari hii ilianzia nyumbani mwa Bibi Ummi Haani, binti wa Bwana Abu Twalib, Allah Mwenyezi ameitaja sehemu ya kuanzia kwa safari hii kuwa ni Masjidul-Haram, ni kwa sababu ya ukweli uliopo kwamba Waarabu wanaufikiria mji mzima kuwa ni Nyumba ya Allah, na kwa sababu hiyo, sehemu zake zote zinachukuliwa kuwa 'Masjid' na 'Haraam.'

5. Hivyo, kauli ya Allah kwamba "Alimfanya asafiri kutoka Masjidul- Haraam" ni sahihi kabisa. Hata hivyo, kufuatana na baadhi ya masimulizi, safari hii ilianzia kwenye Masjidul-Haraam yenyewe.

6. Ingawa Aya hii inaitaja sehemu ya kuanzia kwa safari hii kuwa ni

7. 'Masjidul-Haraam' na mwishilizo wake kuwa ni 'Masjidul-Aqsaa' hakuna lolote ndani yake liwezalo kutoafikiana na Mtume (s.a.w.w.) kuifanya safari nyingine ya kwenda mbinguni, kwa sababu aya hii inaitaja sehemu moja tu ya safari hii na aya za *Suratun-Najm* zinazungumzia juu ya ile sehemu nyingine ya taarifa za safari ile.

5. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliifanya safari ile kwa mwili na roho yake pamoja, na wala si kwa roho tu. Maneno 'mja wake' yanatoa ushahidi wa jambo hili, kwa sababu neno 'mja' lina maana ya 'mwili na roho'. Kama Mi'iraaj ingalifanyika kiroho tu, maneno sahihi kutumika yangalikuwa 'roho ya mja wake.'

6. Lengo la hii safari kuu lilikuwa kumfahamisha Mtume (s.a.w.w.) hali mbalimbali za kuwako kwa Ulimwengu Mkuu. Hapo baadae tutalieleza zaidi jambo hili.

Sura nyingine inayolizungumzia tukio la Mi'iraaj waziwazi ni *'Surah al- Najm'* na aya utakazozisoma hapa chini zilifunuliwa kuhusiana na jambo hili. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipowaambia Waquraishi amemwona Malaika Mkuu Jibriil akiwa kwenye umbo la kimwili, pale alipouleta ufun- uo wa kwanza, walimpinga. Kuhusu upinzani wao, Qur'anii tukufu inajibu hivi:

12} أَفَتُمَارُونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ {

13} وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ {

14} عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَىٰ {

15} عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَىٰ {

16} إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ {

17} مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ {

18} لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ {

"Je, mnabishana naye juu ya yake aliyoyaona? Na bila shaka yeye amemuona (Jibril) kwa mara nyingine (katika sura ya malaika). Penye mkunazi wa mwisho (Sidratul-Muntaha). Karibu kuna pepo, iliyo makazi ya watu wema. wakati ule Mkunazi ulipofunikwa na chenye kufunika. Macho yake hayakuhangaika wala hayakugeuka, kwa hakika aliona baadhi ya Ishara za Mola wake zilizo kuu."(Suratun-Najm, 53: 12-18).

Taarifa Juu Ya Mi'iraaj

Wafasiri wa Qur'anii tukufu na waandishi wa Hadith wamenukuu mambo mengi kuhusu Mi'iraji na aliyoyaona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), lakini taarifa zote hizo si mwishilizio na zisizokanika. Mfasiri mkuu wa Kishi'ah na stadi, Marehemu Allamah Tabrasi amezigawa taarifa hizi katika makundi manne:

1. Kundi moja la taarifa hizi ni zile zikatazo shauri na zisizopingika, kwa mfano ule ukweli wa Mi'iraaj na baadhi ya mambo yake.

2. Taarifa zilizonukuliwa kwa jinsi iliyo sahihi lakini hazikuifikia hatua ya mwishilizio, ingawa zinaafikiana na misingi na hukmu ya hekima, kwa mfano, kule kuikagua Pepo na Jahannam, safari katika anga na kule kuzungumza na roho za Mitume (a.s.).

3. Taarifa ambazo kwamba si zenye kukubalika kwa dhahiri, lakini zina uwezo wa kutafsiriwa. Kwa mfano, yale mazungumzo ya Mtume (s.a.w.w.) kwenye ule usiku wa Mi'iraaj na wale wakazi wa Peponi na Motoni ambayo yaweza kuelezwa kwa kusema kwamba aliona mizuka, maumbo na sifa zao.

4. Taarifa zilizotiwa chumvi, zilizozushwa na kuenezwa na watu waongo. Kwa mfano, wakati mwingine inasemekana kwamba kwenye usiku ule Mtume (s.a.w.w.) alikaa pamoja na Allah Mwenye nguvu zote au kwamba aliisikia sauti ya kalamu yake.[5]

Historia Ya Tukio Hili

Ingawa ilikuwa inafaa kwamba hili tukio kuu lingeandikwa katika hali zote zile, bado, kwa sababu fulani fulani, zimetokea tofauti juu yake, na moja miongoni mwa tofauti hizo ni kuhusu tarehe ya kutokea kwake. Wanahistoria wawili wa kiislamu (ibn Ishaq na Ibn Hisham) wanasema kwamba tukio hili lilitokea mwaka wa kumi wa Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mwanahistoria maarufu Bayhaqi anaamini ya kwamba lilitokea mwaka wa kumi na mbili wa Utume wake.

Baadhi ya watu wanasema kwamba lilitokea siku za awali za Utume wake, ambapo wengine wanasema kwamba muda wa kutokea kwake ulikuwa ni kipindi cha katikati cha Utume. Na wakati mwingine, ili kuziunganisha kauli hizi, imesemekana kwamba Mi'iraaj ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilitokea zaidi ya mara moja. Hata hivyo, maoni yetu ni kwamba ile Mi'iraaj ambayo sala tano za kila siku zilifaradhishwa ilitokea baada ya kifo cha Bwana Abu Twalib kilichotokea kwenye mwaka wa kumi wa Utume wa Mtume (s.a.w.w.).

Tunahitimisha hivi, kwa sababu ni moja ya mambo ya kihistoria na kiaha– dithi yaliyothubutu kwamba wakati wa usiku wa Mi'iraji Mwenyezi Mungu aliamrisha ya kwamba ni wajibu kwa wafuasi wa Mtume (s.a.w.w.) kusali sala tano kila siku na vile vile inafahamika kutokana na historia kwamba sala hazikuwajibishwa hadi alipofariki dunia Bwana Abu Twalib, kwa sababu alipokuwa kwenye kitanda cha kufia kwake, machifu wa Waquraishi walimjia ili kumaliza ugomvi baina yao na mpwa wake na kumzuia aviache vitendo vyake na kuchukua chochote kile akipendacho kiwe ni malipo yake kwa ajili ya kufanya hivyo.

Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwepo pale aliwahutubia Machifu wale akisema: "Sitaki chochote kile kutoka kwenu ila tu kwamba muthibitishe ya kwamba hakuna mungu ila Allah na kuacha kuyaabudu masanamu!"[6]

Aliyatamka maneno haya na katu hakuitaja *Salaat* (sala) au kanuni nyingine za Imani. Jambo hili lenyewe laonyesha kwamba hadi wakati ule sala ilikuwa bado haijafanywa wajibu, kwa kuwa, kama vinginevyo, kuamini tu pasi na matendo ya wajibu, kama vile sala kusingalikuwa na faida yoyote. Na ama kuhusu lile jambo la kwamba hakutaja Utume wake, ni kwa sababu kuushuhudia upweke wa Allah kuna maana ya kuuthibitisha Utume wake moja kwa moja.

Zaidi ya hayo, vile vile wanahistoria wametaja kusilimu kwa watu kama vile Tufayl bin Amr Dosi kulikotokea mapema kidogo kabla ya kuhajiri (kwenda Madina). Wakati ule pia, Mtume (s.a.w.w.) alitosheka na kuwapa maelekezo ya kukubali upweke wa Allah na Utume wake yeye lakini hakuitaja 'Sala.' Matukio kama haya yaonyesha kwamba wakati wa kutokea kwa tukio hili ambalo kwalo sala ziliwajibishwa, ulikuwa ni muda mfupi tu kabla ya Hajiri.

Wale wanaofikiri kwamba Mi'iraaj ilitokea mapema kuliko mwaka wa kumi wa Utume wa Mtume (s.a.w.w.) wanakosea kabisa, kwa sababu tangu mwaka wa nane hadi wa kumi alikuwa kazingirwa kwenye 'Bonde' na ile hali ya kusikitisha ya Waislamu haikufaa kwamba watwishwe jukumu jingine kama vile 'Swala." Na ama kuhusu miaka ya kabla ya mwaka wa nane, tukiuachilia mbali ukweli uliopo kwamba shinikizo la Waquraishi lilikuwa kali mno kwa Waislamu kiasi kwamba hawakuweza kuyahimili majukumu mengine, bado idadi yao pia ilikuwa ndogo mno!

Hivyo basi, kwa wakati kama huu ambao mwanga wa dini na kanuni zake havijaingia barabara nyoyoni mwa idadi ya watu iwezayo kutambulika, yaonekana haiyumkini kwamba jukumu lisilo la kawaida kama vile sala liwajibishwe juu yao.

Ama kuhusu kauli iliyotamkwa kwenye baadhi ya masimulizi kwamba Imam Ali, Amir wa Waumini alisali pamoja na Mtume (s.a.w.w.) kwa kipindi cha miaka mitatu kabla ya uteuzi wa Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume na akaendelea nazo baada ya hapo, inaweza kusema kwamba hii ilikuwa na maana ya sala maalumu na zisizo na ukomo na si zile Sala zenye ukomo na masharti na muda maalumu.[7] Vile vile inawezekana kwamba sala hizo zilikuwa zilizopendekezwa 'Sunnah' na zisizo za wajibu.

Je, Mi'iraji Ya Mtume Ilikuwa Ya Kimwili?

Hali ya Mi'iraj ya Mtume (s.a.w.w.) imekuwa jambo la kujadiliwa kwa kipindi kirefu na mengi yamesemwa kuhusu kuwa kwake ya kimwili au ya kiroho, ingawa Qur'anii tukufu na Ahadith vinaeleza waziwazi kwamba ilikuwa ya kimwili.[8] Hata hivyo baadhi ya dhana za kisayansi zimewazuia kikundi cha watu kuukubali ukweli huu. Hatimae wamekimbilia kwenye tafsiri zao wenyewe na kuichukulia Mi'raji ya Mtume kuwa ya kiroho hasa na wamesema kwamba ni roho yake tu ndio iliyosafiri katika dunia hizi na kasha ikarudi kwenye ule mwili wake mtukufu.

Wengine wameendelea zaidi hatua moja na kusema kwamba matukio yote haya yalikuwa ni ndoto na Mtume aliona aliona sehemu mbalimbali na kusafiri kupitia humo ndani ya ndoto.

Kauli ya kundi la mwisho iko mbali zaidi na mantiki na hali halisi kiasi kwamba haistahili kufikiriwa hata kidogo kwamba ni sehemu ya Ahadith na maoni yahusianayo na Mi'iraaj. Sababu yake ni kwamba Waquraish waliposikia kwamba Muhammad amedai kwamba amesafiri na kufika sehemu zote hizi ndani ya usiku mmoja tu, hapo walipatwa na wasiwasi mno na wakaamka kwa dhati kabisa kumwita mwongo, kiasi kwamba Miiraaj yake ikawa jambo lenye kujadiliwa kwenye mikusanyiko yote ya Waquraishi. Kama kule kusafiri kwake kwenye dunia hizi kungalikuwa kwa ndoto tu, kusingalikuwapo haja yoyote kwa upande wa Waquraishi kuamka na kumkanusha na kusababisha ghasia zote zile.

Hii ni kwa sababu, kama mtu akisema kwamba kwenye usiku mmoja, alipokuwa amelala, ameota hili na lile, haiwezi kuwa hoja ya malumbano, na ugomvi kwa kuwa ndoto ni ndoto tu na mambo mengi yasiyowezekana yaweza kuonekana kwenye ndoto. Hivyo basi, kwa sababu hii, maoni haya hayastahili kuchunguzwa zaidi. Hata hivyo, kwa bahati mbaya baadhi ya wanachuoni wa Kimisri kama vile Farid Wajdi wamelichukua wazo hili na kuliunga mkono kwa kauli zisizo na msingi. Hata hivyo, ingawa yamekuwako yote hayo, inafaa kuitupilia mbali.

Je, Ilikuwa Mi'iraaj Ya Kiroho?

Wale watu walioshindwa kutatua masuala madogo yahusianayo na Mi'iraaj ya kimwili wamelazimika kukimbilia kwenye tafsiri na wameichukulia Mi'iraj ya Mtume (s.a.w.w.) kuwa ilikuwa ni ya kiroho.

Mi'iraaj ya kiroho ina maana ya kutafakari juu ya vitu vilivyoumbwa na Allah Mwenyezi na kuuchunguza Utukufu na Uzuri wake na kuzama kwenye fikara juu Yake na kulisabihi jina lake na hatimaye ukapatikana uhuru kutokana na vipingamizi vya kimaada na faida za kidunia na kupitia kwenye kila uwezekano na kuingia kwenye hatua za ndani na zisizo za kimaada. Na baada ya kuupitia mpango wote huu, ukapatikana ukaribu zaidi na Allah, na haiwezekani kuieleza zaidi.

Kama Mi'iraaj ya kiroho ina maana ya kutafakari juu ya Utukufu wa Allah Mwenyezi, na kadiri ya maumbile, bila shaka Mi'iraaj ya aina hii si maalu– mu kwa Mtume wa uislam kwani Mitume (a.s.), na watu wengi walioangaziwa na wenye nyoyo safi nao wamekifikia cheo hiki, ambapo Qur'anii tukufu inaitaja Mi'iraaj yake kuwa ni jambo maalumu kwake na daraja la kipekee kwake.

Zaidi ya hapo, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kwenye hali tulioyoitaja hapo juu kwenye masiku mengi sana[9] ambapo Mi'iraaj imethibitika kuhusika na usiku maalumu.

Jambo lililowalazimisha watu hawa kuwa na maoni tuliyoyataja hapo juu (ya kwamba Mi'iraaj ilikuwa ya kiroho tu) ni ile dhana ya yule mnajimu maarufu wa Kigiriki aitwaye Ptolemy, dhana iliyojipatia thamani kubwa kwenye duru za wanasayansi wa nchi za Mashariki na za Magharibi kwa kipindi cha miaka elfu mbili, na mamia ya vitabu yaliandikwa juu yake, na hadi kwenye miaka ya hivi karibuni, dhana hii ilichukuliwa kuwa ni moja ya kanuni zilizothibitishwa za sayansi za kimaumbile. Inaweza kuhitimishwa kama hivi:

Hapa ulimwenguni kuna aina mbili za vitu, vitu vya kimaada na vya kimbinguni. Vitu vya kimaada vina vitu vinne maarufu (maji, ardhi, hewa na moto).

Tufe la kwanza tulionalo ni tufe la dunia ambalo ndio kitovu cha ulimwengu. Kisha huja maeneo ya maji, hewa na moto na kila moja kati yao hulizunguka jingine. Matufe hayo huishia hapo na yale maumbile ya kimbinguni huanza. Maana ya maumbile ya kimbinguni ni zile anga tisa ambazo zimeungana na kila mojawapo nyingine kama matabaka ya kitun– guu na katu havina uwezo wa kupasua na kupatanisha na kutenganisha na kuungana na hakuna kiumbe awezaye kutembea moja kwa moja kupitia vitu hivi, kwa sababu hilo litalazimisha mtengano wa sehemu za mbingu, moja kutokana na nyingine.

Mi'iraaj ya Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni ya kimwili, inalazimu kwamba apae kutoka kwenye kitovu cha ulimwengu kwa mstari ulionyooka na ayapite yale matufe manne na vile vile azipasue mbingu moja baada ya nyingine na kule kupasua na kuzipatanisha zile mbingu hakuwezekani na hakutekelezeki kulingana na elimu ya unajimu ya Kigiriki, wanafikara tuliowataja hapo juu wamelazimika kuichukulia Mi'iraaj ya Mtume (s.a.w.w.) kuwa ya Kiroho tu, kwa vile hakuwa mtu awezaye kuizuia roho kuifanya safari.

Jibu La Ukosoaji Huo Hapo Juu

Kauli hizi zilikuwa na thamani siku zile wakati elimu ya unajimu ya Ptolemy ilipokuwa bado haijapoteza thamani yake kwenye nyanja ya kisayansi na baadhi ya watu waliipenda kwa kweli na wakaielekea. Katika hali kama hii iliwezekana kwamba tungeweza kucheza na utatanishi wa Qur'anii na tungezifasiri aya za Qur'anii za waziwazi pamoja na Ahadith. Hata hivyo, dhana hizi zimezipoteza thamani zao zenye kuenea na kutokuwa kwao na msingi kumedhihirika. Ni katika baadhi ya nyakati tu kwamba unatajwa unajimu wa Ptolemy kuhusiana na historia ya sayansi.

Zaidi ya hapo, kutokana na ugunduzi wa zana mbalimbali za kinajimu na darubini zenye nguvu na kushuka kwa 'Apollo' na 'Luna' kwenye uso wa mwezi, Venus (ng'andu) na Mars na safari za wanaanga kwenye mwezi havikuacha nafasi yoyote kwa dhana hizi za kufikiria tu. Siku hizi wanasayansi huchukulia kuwako kwa zile tufe za kimaada na zile anga tisa zenye kuhusiana zenyewe kwa zenyewe kuwa ni ngano na hawajafaulu kuviona, kwa msaada wa zana za kisayansi na kinajimu na macho yaliyoandalliwa vizuri, zile dunia alizojenga Ptolemy na udhanifu wake na wanalichukulia kila wazo lililosimamia kwenye nadharia potofu za Plotemy kuwa zisizo na thamani.

Wimbo Usio Na Mahadhi

Kiongozi wa madhehebu ya Shaykhiyah (Shaykh Ahmad Ehsaai) ameim– ba wimbo mwingine kwenye jarida liitwalo '*Qatifiyah*' na amejaribu kuyatosheleza makundi yote mawili kwa namna mpya.
Yeye anasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Mi'raaj kwa njia ya barzakhi[10] (mwili wenye nguvu za ajabu). Kwa mujibu wa fikira zake mwenyewe, kwa njia hii atakuwa amewatosheleza wale waaminio Mi'iraaj ya kimwili kwa vile amekubali kwamba Mi'iraaj imefanyika pamoja na mwili na vile vile atakuwa

ameliondoa lile tatizo lihusianalo na mbingu au anga, kwa sababu, ilikuweza kupenya kwenye zile anga, si lazima kwa mwili wa 'Kibarzakhi' kuzipasua anga zile.[11]

Ingawa watu walioelimika, wenye kuutafuta ukweli na wasio na upendeleo huyachukulia maoni haya nayo kuwa si yenye thamani yoyote na yaliyo kinyume na Qur'anii tukufu na maelezo ya Ahadith yaliyodhihiri, kama vile yalivyo maoni ya awali

(yale ya kwamba Mi'iraaj ilikuwa ya Kiroho) kwa sababu, kama tulivyokwisha kusema, unapoiweka ile aya ya Qur'anii ihusianayo na Mi'iraj mbele ya mtaalamu wa lugha (ya kiarabu) atasema kwamba yule mzungumzaji ana maana ya mwili wa ulimwengu wa kimaada ambao kwamba neno 'abd' (mja) limetumika kwenye Qur'anii tukufu na wala si neno '*herculian*,' (enye nguvu za ajabu) kwa sababu jamii ya kiarabu ilikuwa haina ufahamu wa neno hili wala maneno yafananayo na neno hili, na kwenye **Surah al-Israa** ni vikundi vya kawaida na watu binafsi waliozungumzishwa.

Sasa jambo lililomfanya kujichukulia hii tafsiri ya kulazimisha ni ileile ngano ya Kigiriki juu ya mpango wa maumbile ambayo, kwa mujibu wake, ngano hii ni yenye madhubuti kama vile *'Lawh-i Mahfudh'* (ubao uliohiofadhiwa). Lakini hivi sasa kwa vile wanasayansi wote wanalikataa wazo hili haifai hata kidogo kwamba tuendelee kulifuata kama vipofu.

Kama wanachuoni wa kale wametoa kauli fulani kutokana na kuwa kwao na matarajio juu unajimu wa kizamani wanaweza kusamehewa na kwamba sio wa kulaumiwa sana, lakini si sahihi kwetu, kwenye nyakati hizi za siku hizi, kuzikataa hali halisi za Qur'anii kwa sababu ya dhana zilizokataliwa na kundi la wanasayansi.

Mi'iraaj Na Kanuni Za Kisayansi Za Kisasa

Baadhi ya wale waipendeleao sayansi ya kimaumbile wenye shauku ya kuweka chanzo asilia kwa kila tukio na kiwakilishi cha kimaada kwa kila jambo, wamechagua kuukana ule msingi wenyewe hasa wa Mi'iraaj na wanafikiria ya kwamba kanuni za kisasa za kimaumbile na za kisayansi hazithibitishi Mi'iraaj ya Mtume (s.a.w.w.). Kwa mfano, wanasema:

1. Sayansi ya kisasa inasema: 'Ili kutoka humu duniani ni lazima kuitan- gua nguvu yake ya mvutano. Kama ukiurusha mpira hewani, nguvu ya mvutano huurudisha ardhini. Kwa kadiri nguvu yoyote ile uitumiayo, nao utarudi tena ardhini. Kama ukitaka kuitangua kabisa nguvu ya mvutano, ili ule mpira uendelee kwenda na usirudi ardhini, itakulazimu kuutupa kwa kasi isiyopungua kilomita 40,000 (au maili 25,000) kwa saa.

Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) aliutoka ukanda wa nguvu ya mvutano na akakosa uzito. Lakini hapa huibuka swali la, vipi aliweza kuifanya safari ile kwa kasi hii bila ya nyenzo muhimu?

2. Hali ya hewa ambamo mtu anaweza kupumua haipatikani nje kidogo ya kilometa chache hivi kutoka ardhini. Baada ya hapo, kwa kadiri tunavyokwenda juu zaidi, hewa huwa nyepesi zaidi na kutokufaa

zaidi kwa kupumua na mara moja moja tunafika mahali pasipo na hewa kabisa.

Mtume (s.a.w.w.) aliwezaje kuwa hai bila ya hewa ya Oksijeni alipokuwa akiifanya safari yake ile kwenye kanda tulizozitaja?

3. Miyonzi yenye kuua na mawe ya mbinguni huharibu kila mwili wa kidunia uguswao na vitu hivi. Hata hivyo, vitu hivi havifiki duniani kutokana na mgongano wao na zile kanda za hewa na kwa kweli kanda hizi huwa kama deraya kwa upande wa wakazi wa duniani. Kwenye hali hii, ni kwa njia ipi Mtume (s.a.w.w.) aliweza kusalia salama kutokana na hii miyonzi iuayo?

4. Maisha ya mwanadamu huharibikiwa wakati shinikizo la hewa liongezekapo au lipunguapo na mwanaadamu anaweza tu kuishi kwenye shinikizo maalumu la hewa ambalo halipatikani kwenye kanda za juu.

5. Kasi aliyoitumia Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuifanya safari yake ni dhahiri ilikuwa kubwa kuliko kasi ya mwanga. Mwanga husafiri kwa kasi ya kilomita 300,000 kwa sekunde na sayansi ya siku hizi imethibitisha kwamba hakuna mtu awezaye kwenda kwa kasi zaidi ya ile ya mwanga. Tukiizingatia kanuni hii ya kisayansi, vipi Mtume (s.a.w.w.) aliweza kuifanya safari yake kwa kasi iliyo kubwa kuliko ile ya mwanga na kisha akarudi akiwa salama na mwenye afya njema?

Jibu La Upingamizi Huo Hapo Juu

Tunapozinyoosha kanuni za kimaumbile hadi kukifikia kiwango hiki, idadi ya matatizo huuvuka mpaka wa hayo tuliyoyataja hapo juu. Hata hivyo, tunawauliza watu hawa lengo la kuzieleza hizi kanuni za kimaumbile. Je, wana maana ya kusema kwamba kusafiri kwenye ulimwengu wa juu hakuwezekani?

Katika kulijibu swali hili hatuna budi kusema kwamba kwa bahati nzuri utafiti wa kisayansi uliofanywa na wanajimu wa nchi za Mashariki na za Magharibi umelifanya jambo hili kuwa lenye kuwezekana na la kawaida, kwa sababu, kwa kupeleka kwao setalaiti ya kwanza ya kutengenezwa mnamo mwaka 1957, iliyopewa jina la '*Sputnic*,' ilidhihirika ya kwamba ile nguvu ya mvutano inaweza kutanguka kwa kutumia roketi.

Halikadhalika, kwa kupeleka kwao vyombo vya angani vyenye kubeba wanajimu '*astronatus*' kwa kutumia roketi ilidhihirika ya kwamba lile jambo ambalo hapo awali mwanaadamu alilifikiria kuwa ni kikwazo katika kusafiri kwake kwenda kwenye anga za juu kinaweza kuponywa kwa msaada wa sayansi na teknolojia, na, kwa hizi zana za kiviwanda na kisayansi alizonazo, mwanaadamu anaweza kutatua matatizo ya miyonzi yenye kuua na lile tatizo la ukosekanaji wa hewa awezayo kuivuta mtu. Na hata hivi sasa, sayansi zihusianazo na anga zimo kwenye hali ya kupanuka na wanasayansi wana uhakika kwamba baada ya muda fulani watafaulu kuendesha maisha yao kwenye moja ya matufe ya mbinguni na watasafiri kwa urahisi kwenda mwezini na kwenye Mars.[12]
Maendeleo haya kisayansi na ufundi yanaonyesha wazi ya kwamba kiten- do kama hiki kinawezekana

kwa asilimia mia moja na si tu kilicho nje ya akili.

Inawezekana baadhi ya watu wakahoji kwamba safari ya aina hii haiwezi kufanyika bila ya vifaa vya kisayansi na kimashine, na kwa vile Mtume (s.a.w.w.) hakuwa na vifaa hivi kwenye ule usiku wa Mi'iraaj aliwezaje kusafiri kwenye malimwengu kama hayo bila ya vifaa hivi?

Jibu la kauli hii hujidhihirisha kutokana na mazungumzo tuliyoyataja hapo juu kuhusu miujiza ya Mitume (a.s.) na hasa kutokana na masimulizi marefu tuliyoyatoa hapo kabla juu ya matukio ya ule 'Mwaka wa Ndovu' na tukio la jeshi la Abrahah kuuawa kwa vikokoto vodogo, kwa kuwa ni ukweli uliothubutu kwamba vitu ambavyo watu wa kawaida huvitenda kwa zana na vifaa vya kisayansi, vinaweza kufanywa na Mitume (a.s.) kwa rehma za Allah, na bila ya njia za dhahiri na za nje.

Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alikwenda Miiraaj kwa rehma za Allah Mwenyezi, Ambaye ulimwengu wote ni wake na ambaye ndiye Muumba wa huu mfumo wa ajabu.

Yeye ndiye Aliyeipa ardhi ule mvutano na ile miali ya ulimwengu mzima kwenye jua, na ameumba matabaka tofauti tofauti kwenye angahewa. Naye Anaweza kuvirudisha Kwake vitu hivi na kuvitawala wakati wowote ule Apendapo.

Inapokuwa kwamba mpango wa hii safari ya kihistoria ya Mtume (s.a.w.w.) ulifanyika kwa amri ya Allah, kanuni zote hizi hunyenyekea kabisa kwenye Utashi Wake Allah usiokanika na ziko kwenye mikono ya nguvu Zake kwa kila wakati.

Katika hali hiyo ni ugumu gani uwezao kuwapo iwapo kama yule Mola Aliyeipa ardhi nguvu ya mvutano na ile miali ya dunia nzima kwenye maumbo ya angani anataka amtoe mja wake mteule nje ya kile kitovu cha nguvu ya mvutano kwa uwezo Wake usizo kikomo na bila ya njia yoyote ya dhahiri? Bila shaka, Allah Aliyeumba oksijeni anaweza kuiumba hewa kwa ajili ya Mtume wake mteule kwenye yale maeneo ambamo hewa haipatikani.

Ufanisi wa muujiza kimsingi ni tofauti na ule wa visababisho vya asili na nguvu ya mwanadamu. Hatupaswi kufikiria nguvu ya Allah kuwa ni yenye kikomo kama ilivyo nguvu yetu wenyewe. Kama sisi hatuwezi kuifanya kazi fulani bila ya zana tusiseme kwamba Allah mwenye nguvu zote nae vilevile hawezi kuifanya.

Tukizungumzia matatizo na utatuzi wake, kule kuwafufua wafu, kule kuibadili fimbo na kuwa chatu na kule kumweka hai Nabii Yunus (a.s.) tumboni mwa samaki kwenye kina kirefu cha bahari, ambayo ni matukio yaliyothibitishwa na Vitabu vya Mbinguni na yaliyosimuliwa kwa ajili yetu, hayako tofauti na Mi'iraaj ya Mtume wa Uislam (s.a.w.w.).

Kifupi ni kwamba, visababisho vyote vya kimaumbile na zana za nje na za dhahiri zinadhibitiwa na kushindwa na Utashi ya Allah. Mapenzi Yake hayahusiki na kile kisicho wezekana tu, bali zaidi ya hicho Yeye anaweza kukifanya chochote kile akipendacho, iwe mwanaadamu anayo nguvu ya kukifanya au la.

Bila shaka hapa tunazungumza na wale watu wamtambuao Allah kwa Sifa na tabia zisizo kifani na wale waaminio kwamba Yu Muweza wa yote na anaweza kufanya chochote kile akipendacho.

Lengo La Mi'iraaj

Mtu mmoja alimuuliza Imam wetu wa nne Ali Zaynul Abidiin (a.s.): "Je, iko sehemu maalumu kwa ajili ya Allah?" Imam (a.s.) alijibu akisema: "Hapana." Yule mtu akasema: "Basi ni kwa nini alimfanya Mtume Wake (s.a.w.w.) asafiri kuzipita mbingu?" Imam (a.s.) alimjibu akisema: "Alimpaisha ili aweze kuutambua upana wa Ulimwengu na kuviona na kuvisikia vitu vya ajabu, ambavyo mifano yao haikupata kuonekana au kusikika na masikio au macho hapo kabla yake."

Bila shaka ni muhimu kwamba huyu Mtume wa mwisho (s.a.w.w.) awe na nafasi ambayo aweza kutegemea ufahamu wake mpana zaidi na awe na uwezo wa kupeleka ujumbe kwa watu wa karne ya ishirini, ambao bado wanafikiria kusafiri kwenda mwezini na kwenye Mars, kwamba alikitenda kitendo hiki bila ya zana yoyote na kwamba Muumba wake alikuwa Yu mpole kwake na amemfanya autambue kwa ukamilifu utaratibu wa maumbile yote.

1. Majma'ul Bayaan, Surah Bani Isra'il, 17:1, Juzuu 3, uk. 395.
2. Kwa kuielewa zaidi maana ya 'Sidratul Muntaha', rejea kwenye vitabu vya Tafsiri.
3. Baadhi ya wasimuliaji wamenukuu hivi: "Nikamwaga yale yaliobakia." Yawezekana kwamba tofauti iliyopo baina ya masimulizi haya mawili yatokana na kile kitendo kurudiwa tena.
4. Kwa taarifa kamili, tunawashauri wasomaji wetu wazisome Sura zizungumzi- azo juu ya 'Mi'iraj' (kupaa) za Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 282-410 na za Tafsir-i Burhaan, Juzuu 2, uk. 390-404.
5. Majma'ul Bayaan, Juzuu3, uk. 395.
6. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 27
7. Kwa taarifa zaidi kuhusu lini Wudhu, Sala, na Adhana vilifaradhidhwa rejea 'Furu-i Kaafi' Juzuu 1, uk. 135.
8. Mwanasheria mkuu wa Kishi'ah, marehemu Tabrasi, amesema kwenye Tafsir- i Majma'ul Bayaan kwamba wanachuoni wa Kishi'ah wote wanakubaliana kwam- ba Mi'iraaj ilikuwa ya kimwili, Juzuu 3, uk. 395.
9. Wasa'il, Kitabu cha Funga (saumu), Sura ya 'Kuharimisha Funga.'
10. Mwili wa Ki-barzakhi ni kama ule mwili ambao kwawo, mwanaadamu huya- tenda matendo yote awapo mwenye ndoto.
11. Jarida liitwalo 'Qatifiyah' ni moja ya majarida yake 92 yaliyochapishwa kwa pamoja kwenye mwaka 1273 kwa jina la 'Jawaami'ul Kalim.' Maneno ya maelezo yake ni kama haya yafuatayo: "Kwenye tukio la kupaa kwa kadiri mwili upaavyo juu ndivyo unavyoviacha vile vitu vya kimaada vilivyoungana na kila moja ya yale matufe kwenye sehemu ile ile yenyewe na kusoga mbele. Kwa mfano, unaiacha ile maada ya hewa kwenye lile tufe la hewa na ile ya moto kwenye tufe la moto. Na kwenye wakati wa kurudi unajitwalia vile vyote ulivyoviacha."

Hivyo basi, kwenye ule wakati wa Mi'iraaj, Mtume (s.a.w.w.) aliiacha kila moja ya zile elementi nne za mwili wake (hapo kale elementi za msingi zilifikiriwa kuwa ni nne) kwenye yale matufe yao husika na akaenda Mi'iraaj kwa mwili usiokuwa na elementi hizi. Mwili kama huo hauwezi kuwa mwili wa kimaada na hauwezi kuwa chochote kile zaidi ya 'barzakhi' (kwa mujibu wa istilahi yake 'mwili wa her- culian' - wenye nguvu za ajabu). Kwenye kitabu kiitwacho 'Sharh-i Ziarat' uk. 28-29. Sheikh huyu anasema kwamba zile anga tisa hazina uwezo wa kupasuka wala wa kujipatanisha.

12. Baada ya miezi bandia ya kutengeneza kupelekwa angani, Mrusi mmoja mwenye umri wa miaka ishirini na saba aliyeitwa Major Gagarin kwanza aliianza safari yake ya kwenda angani mnamo siku ya Jumatano tarehe 12 April, 1961 ndani ya chombo cha anga. Yeye alikuwa mtu wa kwanza kufanya safari ya aina hii. Kile chombo chake cha anga kilipaa

kilometa 302 juu ya ardhi na akasafiri kwa kuizunguka dunia kwa muda wa saa moja na dakika thelathini. Baada ya hapo vyombo vya angani vilipelekwa angani na Wamarikani pamoja na Umoja wa nchi za Kisovieti za Urusi. Hatimaye Apolo – 12 na abiria wake wote walitua mwezini na ilikuwa ni mara ya kwanza mwanaadamu anaubandika mguu wake juu yake.

Mpango huu umekuwa ukifanyiwa majaribio mara kadhaa baada ya hapo na kwa kawaida yamekuwa yakifanikiwa. Shughuli zote hizi zinadhihirisha ya kwamba kutua kwa mwanaadamu usoni mwa matufe hayo kunawezekana. Na kitu aki–fanyacho mwanadamu kwa hizi njia za kisayansi kinafanywa na Muumba wake kwa njia ya Utashi Wake Mkuu.

Sura Ya 23: Safari Ya Kwenda Taif

Mwaka wa kumi tangu kuanza kwa Utume ukamalizika kwa matukio yake yote, mazuri na mabaya. Kwenye mwaka huu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwapoteza watetezi na wafuasi wake wakuu wawili. Kwanza kabisa yule chifu wa familia ya Abdul–Muttalib, mtetezi maarufu wa Mtume (s.a.w.w.) na mtu mashuhuri zaidi miongoni mwa Waquraishi – yaani Bwana Abu Twalib alifariki dunia. Ilikuwa bado maumivu ya msiba huu yangalimo moyoni mwa Mtume (s.a.w.w.) wakati kifo cha mpenzi mkewe Bibi Khadija[1] kiliongezea ukali wa maumivu yake. Bwana Abu Twalib alikuwa mlinzi wa uhai na heshima ya Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Khadija aliuhudumia Uislamu kwa utajiri wake mkubwa.

Tangu mwanzoni mwa mwaka wa kumi na moja wa Utume wa Mtume (s.a.w.w.), Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiutumia muda wake kwenye mazingira yaliyojaa uadui na mfundo dhidi yake. Uhai wake ulikuwa kwenye hatari endelevu na alinyimwa uwezo wote wa kuubalighisha Uislamu.

Ibn Hisham anaandika[2] kuwa siku chache tu baada ya kifo cha Bwana Abu Twalib Quraishi mmoja alimwagia vumbi Mtume (s.a.w.w.) kichwani mwake na akaingia nyumbani mwake akiwa kwenye hali ile. Macho ya mmoja wa mabinti zake yaliangukia kwenye hali ile ya kusikitisha. Binti yule[3] akilia kwa sauti kuu na huku machozi yakitiririka kutoka machoni mwake, aliamka akaleta maji na kukiosha kichwa na uso wa baba yake mpenzi. Mtume (s.a.w.w.) alimfajiri binti yake yule na akasema: “Usilie. Allah ndiye Mlinzi wa baba yako.” Kisha akasema: “Abu Twalib alipokuwa hai Waquraishi hawakufaulu kutenda kitu chochote kibaya dhidhi yangu.”

Kutokana na hali chungu ya Makkah Mtume (s.a.w.w.) aliamua kwenda kwenye mazingira mengine. Katika zama zile mji wa Taa’if ulikuwa kituo kinachosisimua na kuvutia. Hivyo, aliamua kwenda huko akiwa peke yake na kuwasiliana na machifu wa kabila la Thaqif na kuwaita kwenye Uislamu, huenda akapata kufaulu kwa kuitumia njia hii. Baada ya kufika Taa’if alikutana na machifu na wazee wa kabila lile na akawaelezea dini ya kuabudu mungu mmoja, na akaomba msaada wao. Hata hivyo, maneno yake hayakuwa na athari zozote zile kwao na wakasema:

“Kama wewe ndiy yule mteule wa Allah itakuwa ni kuyakaribisha mateso kukukataa, na kama dai lako ni la uongo, basi haistahili kuzungumza nawe.”

Mtume (s.a.w.w.) alielewa kutokana na hoja yao hii dhaifu na ya kitoto kwamba walidhamiria kujiepusha naye. Hivyo, aliamka na kuchukua ahadi kutoka kwao ya kwamba wasiwaambie watu lolote lile lihusulo jambo lile, kwa sababu ingaliwezekana kwamba jamii ya watu wa daraja la chini na duni wa kabila la Thaif wangalilifanya jambo hili kuwa ni sababu ya kumdhuru na wangaliweza kutumia fursa ya kuwa kwake peke yake na mbali kutoka mjini kwao.

Hata hivyo, wazee wa kabila lile hawakuitimiza ahadi yao na wakawachochea wahuni na wajinga dhidi yake, mara kwa ghafla Mtume (s.a.w.w.) alijikuta akizingirwa na kundi la watu waliotaka kuzitumia njia zote kumsumbua. Hakuiona njia yoyote ile nyingine ila kukimbilia kwenye bustani moja iliyokuwa mali ya watu wawili waitwao 'Atbah na Shibah'. Mtume (s.a.w.w.) aliingia bustani ile kwa taabu sana na hapo wale watu wakaacha kumfukuza. 'Atbah na Shibah walikuwa ni Waquraishi matajiri ambao pia walikuwa na bustani mjini Taif.

Mtume (s.a.w.w.) alipoingia bustani ile jasho lilikuwa likimmiminika kutoka kichwani usoni, na baadhi ya viungo vya mwili wake mtakatifu navyo vilikuwa vimejeruhiwa. Bila ya kupenda alikaa chini ya mzabibu uliopandishwa kwenye kichanja na akaomba dua ifuatayo: "Ewe Mola wangu! Ninauweka unyonge na utovu wangu wa nguvu mbele Yako. Wewe ndiye Mtunzaji Mwenye huruma. Wewe Msaidizi wa wanyonge. Unaniacha kwenye hifadhi ya nani?"

Hii na dua nyingi nyinginezo tulizozinukuu kwa ufupi, huzivutia mno nyoyo, kwa kuwa ni dua za mtu aliyeitumia miaka hamsini ya uhai wake kwa heshima kuu na utukufu akiwa chini ya ulinzi wa wafuasi waliojitolea mhanga, lakini sasa hali yake imebadilika mno kiasi kwamba imembidi kukimbilia kwenye bustani ya adui na anayasubiri majaaliwa yake huku mwili wake ukiwa umechoka na umejeruhiwa.

Wana wa Rabiyyah, ambao, ingawa walikuwa wenye kuabudu masanamu na maadui wa Uislamu walihuzunika sana walipoiona ile hali ya kusiki– tisha ya Mtume (s.a.w.w.). hivyo, wakamwamrisha mtumwa wao wa Kikristo aliyeitwa Adas, kumpelekea chombo kilichojazwa zabibu.

Adas alimpelekea Mtume (s.a.w.w.) zabibu zile na akaziweka mbele yake na akamtazama usoni mwake kwa kumkazia macho kidogo. Wakati ule lilitokea tukio lenye kuvutia. Yule mtumwa wa Kikristo aliona kwamba Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akizila zabibu zile, alianza kwa kusema: "Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Rahim." Yule mtumwa alishangaa sana kuyasikia hayo na akikivunja kimya kilichokuwapo pale akasema: "Watu wa Penisula hii (ya uarabuni) hawakuyazoea maneno haya na sikupata kumsikia mtu yeyote miongoni mwao akiyatamka. Watu wa sehemu hii huzianza kazi zao kwa majina ya 'Laat na Uzza."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuuliza kijana yule sehemu aliyozaliwa na dini yake. Yule kijana akajibu ya kwamba anatoka Naynawah na kwamba alikuwa Mkiristo. Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Unatoka mahali alipotoka yule mchamungu Yunus (Yona) mwana wa Mata (Mathew)?" Yule kijana akashangazwa zaidi kuyasikia haya na akauliza tena: "Ulimjuaje Yunus mwana wa Mata?" Mtume (s.a.w.w.) akamjibu akasema: "Ndugu yangu Yunus alikuwa yu Mtume wa Allah kama nilivyo." Maneno

ya Mtume (s.a.w.w.) yaliyozionesha dalili za ukweli yalijenga hisia za ajabu kwenye nafsi ya Adas na akavutiwa naye bila ya kupenda. Akasujudu, akaibusu mikono na miguu ya Mtume (s.a.w.w.) na akadhi-hirisha kuiamini dini yake. Baada ya hapo alimwacha na akawarudia wale wenye bustani ile.

Wale wana wa Rabiyyah walishangazwa mno kuyaona yale mapinduzi ya kiroho yaliyomtokea yule mtumwa wao wa Kikristo. Walimwuliza: "Ulizungumza nini na mgeni huyu na kwa nini ulionyesha unyenyekevu mwingi kiasi kile mbele yake?" yule mtumwa akasema: "Mtu huyu ambaye hivi sasa amekimbilia bustanini mwenu yu Sayyidi wa wanaadamu wote. Ameniambia mambo yafahamiwayo na Mitume tu, naye ndiye yule Nabii wa Ahadi hasa." Wale wana wa Rabiyyah walichukizwa mno walipoyasikia maneno ya yule mtumwa. Hata hivyo, kwa ukarimu wao wakasema waziwazi: "Na asikugeuze mtu huyu kutoka kwenye dini yako ya awali. Na dini ya 'Isa (Yesu Kristo) unayoifuata hivi sasa ni bora kuliko yake."

Mtume (S.A.W.W.) Arudi Makkah

Ukali ambao kwawo watu wa Taa'if walimwindia Mtume (s.a.w.w.) ulimalizikia kwenye ile bustani ya wana wa Rabiyyah. Hata hivyo, sasa ilimbidi kurudi Makkah, na hata huku kurejea kwake hakukuwa huru kutokana na matatizo, kwa sababu, mlinzi wake pekee alikuwa ameshafariki dunia, hivyo ulikuwapo uwezekano wa kwamba wakati wa kuwasili kule Makkah angaliweza kukamatwa na kuuawa.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliamua kubakia kidogo mahali paitwapo Nakhlah (palipo baina ya Makkah na Taif) kwa siku chache hivi. Wazo lake lilikuwa ni kumtuma mtu kutoka hapo kwenda kwa mmoja wa machifu wa Waquraishi ili ampatie ulinzi na kisha aingie mjini mle alimozaliwa akiwa chini ya ulinzi wa mtu kama yule. Hata hivyo, pale Nakhlah hakumpata mtu yeyote wa kwenda Makkahh kwa niaba yake. Baadaye aliondoka Nakhlah na kwenda kwenye mlima Hira.

Huko alikutana na mwarabu wa kabila la Khazaa'i na akamwomba aende Makkah na akazungumze na Mut'am bin Adi aliyekuwa mmoja wa watu wa Makkah walio maarufu, kuhusiana na usalama wake (yeye Mtume s.a.w.w) yule mtu alikwenda Makkah na kuufikisha ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) kwa Mut'am. Ingawa Mut'am alikuwa mwenye kuyaabudu masanamu, alikubali ombi la Mtume (s.a.w.w.) na akasema: "Na aje Muhammad moja kwa moja nyumbani kwangu. Wanangu na mimi mwenyewe tutauhami uhai wake." Mtume (s.a.w.w.) aliingia Makkah wakati wa usiku na akaenda moja kwa moja nyumbani kwa Mut'am na akalala humo usiku ule.

Asubuhi iliyofuatia Mut'am alimwambia Mtume (s.a.w.w.): "Hivyo hivi sasa uko chini ya ulinzi wangu itakuwa bora kwamba Waquraishi nao walijue jambao hili. Hivyo, kulitangaza jambo hili ni muhimu kwamba ufuatane nami hadi kwenye Masjidul-Haram." Mtume (s.a.w.w.) alilikubali wazo hili na akajitayarisha kwenda huko. Mut'am aliwaamrisha wanawe washike silaha na wamzunguke Mtume (s.a.w.w.), kisha wakaingia msikitini mle. Kuwasili kwao Masjidul-Haraam kulivutia mno. Abu Sufyani aliyekuwa akimvizia Mtume (s.a.w.w.) kwa muda mrefu alikerwa mno kuyaona mandhari haya na akaliacha lile wazo la kumnyanyasa Mtume (s.a.w.w.). Mut'am na wanawe wakakaa chini na Mtume

akaanza kufanya ibada ya ‘Tawaaf’. Baada ya kuifanya ibada hiyo aliondoka na kurudi nyumbani kwake.4

Muda mfupi baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuondoka Makkah na kwenda Madina na mwanzoni mwa mwaka wa Hijiria, Mut’am alifariki dunia mjini Makkah. Taarifa za kifo chake zikafika Madina na Mtume (s.a.w.w.) alimkumbuka kwa wema wake. Mshairi wa kiislamu, Hassan bin Thabit alisoma beti fulani fulani kwa kuikumbuka huduma yake.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimkumbuka mno Mut’am kwenye matukio mbalimbali kiasi kwamba baada ya vita vya Badr, Waquraishi walipokuwa wakirejea Makkah baada ya kupata hasara kubwa na kuiacha idadi ya watu waliotekwa na waislamu, Mtume (s.a.w.w.) alimkumbuka Mut’am na akasema: “Kama Mut’am angalikuwa hai akanitaka niwaachie mateka wote au niwatoe zawadi kumpa yeye nisingalilikataa ombi lake.”

Jambo Linalostahili Kuzingatiwa

Ile safari yenye kutaabisha ya kwenda Ta’if aliyoichukua Mtume (s.a.w.w.) inaudhihirisha umadhubuti na uvumilivu wake na ule ukweli uliopo kwamba katu hakuzisahau huduma alizozitoa Mut’am katika muda maalum, hutudhihirishia tabia zake tukufu na maadili ya hali ya juu. Hata hivyo, zaidi ya sifa hizi mbili za Mtume (s.a.w.w.) tunaweza kuona jinsi alivyokuwa na shukurani kwa huduma zenye thamani alizozipata kutoka kwa Bwana Abu Twalib. Mut’am alimsaidia Mtume (s.a.w.w.) kwa kipin- di cha masaa machache au siku chache hivi, lakini yule ami yake mtukufu alimhami kwenye kipindi chote cha uhai wake. Mut’am hakupata hata moja ya elfu ya taabu na mateso aliyoyapata Bwana Abu Twalib.
Na wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa tayari kuwaachia mateka wote wa Badri au kumpa zawadi Mut’am kwa ajili ya huduma alizozitoa, kwa masaaa machache, je Mtume (s.a.w.w.) angalifanya nini badala ya zile huduma ali- zozitoa yule kipenzi ami yake?

Ni muhimu kwamba, yule mtu aliyemsaidia Mtume (s.a.w.w.) kwa kipindi cha miaka arobaini na miwili kamili na akayahatarisha maisha yake mwenyewe kwenye kipindi cha miaka kumi ya mwisho, kwa ajili ya kumhami, bila shaka atakuwa yu mwenye kukistahili cheo kikubwa zaidi mbele ya Mtume Muhamad (s.a.w.w.) yule kiongozi wa wanaadamu. Na halafu basi, kuna tofauti ya dhahiri baina ya watu wawili hawa. Mut’am alikuwa mshirikina na mwenye kuabudu masanamu, ambapo Abu Twalib alichukuliwa kuwa mmoja wa watu mashuhuri wa ulimwengu wa kiisla- mu.

Hotuba Alizozitoa Kwenye Mitaa Maarufu Ya Biashara Ya Arabuni

Kwenye majira ya Hajj, Waarabu walikusanyika sehemu mbalimbali kama vile ‘Ukaz’, Majannah’ na ‘Dhil-Majaaz’. Washairi na wazungumzaji maarufu walikaa kwenye sehemu zilizoinuka na kuwaburudisha watu kwa beti na hotuba zao zenye kuelezea ushujaa, majisifu ya mtu na mapenzi.

Mtume (s.a.w.w.) aliitumia fursa hii kama walivyofanya Mitume wa kale. Na kutokana na kuwa salama kutokana na kero za wenye kuabudu masana- mu kufuatia kuharamishwa kwa mapigano kwenye ile miezi mitakatifu, alipanda kwenye sehemu iliyoinuka, akawageukia watu na akawahutubia akisema:

"Ushuhudieni Upweke wa Allah ili mpate kuokoka. Kwa nguvu ya imani mnaweza kuudhibiti ulimwengu mzima, mnaweza kuwafanya watu wazitii amri zenu na mnaweza kujipatia nafasi Peponi kesho Akhera."

Mualiko Kwa Viongozi Wa Makabila Wakati Wa Hajj

Wakati wa Hajj Mtume (s.a.w.w.) aliwasiliana na machifu wa Uarabuni na kuonana nao wote kwenye makazi yao husika ya muda na kuwafikishia ukweli wa dini yake. Nyakati fulani, pale Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa aki- jishughulisha na kuzungumza na machifu hawa alitokea pale Abu Lahab na akasema: "Enyi watu! Msiyaamini yale ayasemayo, kwa sababu yeye anafanya kampeni dhidi ya dini ya jadi zenu na maneno yake hayana msingi." Upinzani wa huyu ami yake Mtume (s.a.w.w.) ulizipunguza athari za hotuba zake miongoni mwa hawa viongozi wa makabila na wakaambiana: "Kama dini yake ni ya kweli na yenye faida, basi watu wa familia yake wasingalimpinga."[5]

1. Ibn Sa'ad anasema kwamba kifo cha Bibi Khadija kilitokea mwezi mmoja na siku tano baada ya kile cha Bwana Abu Twalib (Tabaqaat, Juzuu 1, uk. 106). Hata hivyo, wengine kama vile Ibn Athir, wanaamini ya kwamba alifariki kabla ya Bwana Abu Twalib (Tarikh-i Kamil, Juzuu 2, uk. 63).
2. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 25.
3. Binti huyu ni Bi Fatimah Az-Zahra ambaye alikuwa kama mama yake mpend- wa kiasi kwamba Mtume akampa jina la "Ummu Abiha" yaani Mama wa baba yake. Ukizama ndani ya kina cha bahari ya historia sahihi, basi utachota mchango wake katika Uislamu na jinsi alivyomuhami baba yake kwa mapenzi yake kwa Allah. Na hatimaye utakunywa utukufu wa hali ya juu wa binti huyu - Mhariri.
4. Tabaqaat Ibn Sa'ad , juzuu 1, uk. 210-212 na al- Bidaayah wan-Nihaayah, Juzuu 3, uk. 137.
5. Tabaqaat Ibn Sa'ad, Juzuu 1, uk. 216 na Siirah-i Ibn Hisham, Juz. 1, uk. 422-442.

Sura Ya 24: Mapatano Ya 'Aqabah

Katika nyakati zilizopita *'Waadiul Qura'* (bonde la Qura) lilikuwa ndio njia ya kibiashara itokayo Yemen kwenda Sham. Baada ya kupita pembeni mwa Makkah misafara ya kibiashara ya Yemen iliingia hili bonde refu, na pamoja nalo yalikuwapo maeneo ya kijani na yenye kupendeza, moja kati yao lilikuwa ni ule mji wa kale wa Yathrib, ambao baadae ulijulikana kwa jina la 'Madinatur Rasul' (Mji wa Rasuli). Makabila mawili maarufu yaliy- oitwa 'Aws' na Khazraji' waliokuwa Waarabu wahamiaji kutoka Yemen (Qahtaani) walifanya makazi bondeni humu kwa vile makabila maarufu ya Wayahudi (ya Bani Qarayzah, Bani Nuzayr na Bani Qaynqaa) yaliyohamia kutoka upande wa kaskazini wa Penisula ya Uarabuni yalifanya maskani yao hapo pia.

Kila mwaka kikundi cha Waarabu wa Yathrib walikwenda Makkah kufanya ibada ya Hajj, na Mtume

(s.a.w.w.) aliwasiliana nao. Mawasiliano haya yalitoa vitangulizi vya ‘kuhama’ na kuikusanyia nguvu iliyotawanyika ya Uislamu kwenye kituo hicho. Mengi ya mawasiliano haya hayakuwa yenye manufaa.

Hata hivyo, ingawa yalikuwako yote hayo, wale mahujaji watokao Yathrib, waliporudi makwao walitaja kule kutokea kwa Mtume mpya ikiwa ndio taarifa muhimu, na jambo hili liliwavutia watu wa eneo hili kwenye tukio hili kuu.

Hivyo basi, hapa chini tunataja baadhi ya mikutano hii iliyofanyika kwenye mwaka wa kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu wa Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwenye uchunguzi wa kina wa matukio haya, sababu ya kuhama kwa Mtume Kutoka Makkah kwenda Yathrib (Madina), na hatimaye kule kuikusanya nguvu ya Waislamu kwenye sehemu ile hudhihirika kabisa:

Pale wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitambua ya kwamba mtu maaru– fu kutoka miongoni mwa Waarabu amewasili mjini Makkah alikwenda kuonana naye upesi upesi na kumhubiria dini yake. Siku moja alisikia ya kwamba Sawayd bin Saamit amefika mjini Makkah. Alikutana naye upesi na akamweleza hali halisi kuhusu dini yake takatifu.

Suwayd akafikiria kwamba huenda kweli zile zilikuwa ni hekaya za Luqman ambazo yeye tayari aishakuwa nazo. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Semi za Luqman ni nzuri, lakini yale aliyonifunulia Allah ni bora na matukufu zaidi kwa sababu ni taa ya mwongozo iangazayo kila mahali.

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) alimsomea aya fulani fulani za Qur’anii na akasilimu. Kisha akarejea Madina. Suwayd aliuawa na Khazraji kabla ya vita vya Bu’aath. Alifariki dunia akiwa anazitamka ‘Shahadatain’ (yaani kule kushuhuduia ya kwamba hakuna mungu ila Allah na Muhammad yu mja na Mtume wake).[1]

Kikundi cha watu wa kabila la Bani Aamir walikutana na Mtume (s.a.w.w.) na wakasema: “Tutauamini Utume wako kwa sharti la kwamba utatufanya kuwa makhalifa wako.” Mtume (s.a.w.w.) akawaambia: “Jambo hili lamhusu Allah, nami sina mamlaka yoyote kwenye jambo hili. Hapo wakakataa kusilimu na wakarejea kwa watu wa kabila lao wakisema kwamba hiyo ilikuwa na maana ya kwamba wao wapigane kwa ajili ya jambo lile na watu wengine waifaidi matunda yake.

Walipofika makwao walilizungumzia jambo hili kwa mmoja wa wazee wa kabila lao ambaye hakuweza kwenda Hija mwaka ule kutokana na udhaifu. Mzee yule aliyeelimika aliwalaumu na akasema: “Hii ndio ile nyota iangazayo iliyochomoza kutoka kwenye upeo wa ukweli halisi.”[2]

Anas bin Raafi’i alikuja Makkah pamoja na kikundi cha watu wa kabila la Abdul Ashhal na Ayaas bin Ma’aaz alikuwa pamoja nao. Lengo lao lilikuwa kuomba msaada wa kijeshi kutoka kwa Waquraishi ili wakapigane dhidi ya kabila la Khazraji. Mtume (s.a.w.w.) alijiunga na mkutano wao na akawahubiria dini yake na vile vile akawasomea aya za Qur’anii. Ayaas, aliyekuwa mtu shupavu, alisimama akasilimu na akasema: “Dini hii ni bora kuliko ule msaada wa Waquraishi mlioujia hapa.” (Ayaas alikuwa na maana ya kwamba uislamu ni uhakika wa ustawi wa kudumu kwa sababu unaung’oa mauaji na visababisho

vyote vya uharibifu na udanganyifu).

Kusilimu kwa mtu huyu bila ya mwelekeo wa kiongozi wa kabila lile kulimkasirisha mno Anas. Ili kuizima ghadhabu yake alichota mchanga kwa mikono yake yote miwili, akaumwagia usoni mwa Ayaas, na kusema: “Nyamaza! Sisi tumekuja hapa kuomba msaada wa Waquraishi wala si Kusilimu.”

Hapo Mtume (s.a.w.w.) alisimama akaenda zake na baada ya hapo kikundi kile kilirejea Madina. Vita ya Bu’aath ilipiganwa baina ya Aws na Khazraji.

Ayaas aliyebaki imara kwenye imani yake hadi kwenye dakika ya mwisho ya uhai wake, aliauwa kwenye vita hivi.3

Vita Vya Bu’aath

Vita vya Bu’aath ni moja ya vita vya kihistoria vilivyopiganwa baina ya yale makabila mawili ya Aws na Khazraji. Bani Aws walishinda kweye vita hii na wakaichoma mitende ya maadui zao. Baada ya hapo, Abdullah bin Ubay aliyekuwa mmoja wa machifu wa Bani Khazraji hakushiriki kwenye vita hivi, na hivyo basi, makabila yote mawili yalimheshimu. Ilitokea kwamba zile pande zote mbili zilichoka kabisa na hivyo zikaelekea mno kwenye amani.

Makabila yote mawili yalishikilia kwamba Abdullah awe mtawala wao baada ya mapatano. Waliweza hata kumtayarishia taji ili aweze kulivaa kwenye wakati wa kutawaza kwake. Hata hivyo, mpango huu ulishindikana kutokana na mwelekeo wa kundi la kabila la Khazraji kwenye Uislamu. Na wakati ule Mtume (s.a.w.w.) alikutana na Wakhazraji sita mjini Makkah na wakaukubali mwito wake.

Maelezo Juu Ya Tukio Hili.

Kipindi cha Hija Mtume (s.a.w.w.) alikutana na watu sita wa kabila la Khazraji na akawauliza kama walifanya mapatano yoyote na Wayahudi. Walijibu, ndio. Hapo Mtume (s.a.w.w.) akawaambia: “Tafadhalini hebu ketini ili nikuambieni jambo fulani.” Walikaa na kuyasikiliza maneno yake.

Mtume (s.a.w.w.) aliwasomea aya za Qur’anii. Jambo hili lilikuwa na athari njema kwao nao wakasilimu palepale. Jambo lililowafanya wauele– kee Uislamu ni kwamba, walikuwa wamesikia kutoka kwa Wayahudi kwamba Nabii mwenye asili ya Uarabu, atakayeleta dini ya Upweke wa Allah na atakayeifutilia mbali ibada ya masanamu, hivi karibuni atateuliwa na Allah Mwenyezi, na hivyo, wao wakafikiria ya kwamba, kabla ya Wayahudi kuwatangulia wao katika jambo hili, wao wenyewe wamsaidie Mtume (s.a.w.w.) na kwa kufanya hivyo wawashinde maadui zao.

Kikundi hiki kilimgeukia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Mara kwa mara moto wa vita huwaka baina yetu. Tunategemea kwamba Allah Mwenyezi atauzima moto huu kwa njia ya hii dini yako tukufu. Sasa tunarejea Yathrib na tutawafikishia watu dini yako. Kama wote wakiikubali, basi hatakuwapo mtu yeyote mwingine tutakayemheshimu zaidi yako.” Watu sita hawa walifanya juhudi za kudumu kuuhubiri Uislamu

mjini Yathrib kiasi kwamba haikuwako nyumba yoyote mjini humo ambayo kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakuzungumziwa habari zake.4

Mkataba Wa Kwanza Huko ‘Aqabah

Mahubiri yaliyoendelezwa ya wale watu sita yalizaa matunda na kikundi cha wakazi wa Yathrib kilisilimu. Kwenye mwaka wa kumi na mbili wa kazi ya Utume kikundi kingine kilichokuwa na watu kumi na wawili kilikuja kutoka Yathrib na kukutana na Mtume (s.a.w.w.) mahali paitwapo

‘Aqabah na wakafanya mkataba wa kwanza wa kiislamu. Waliokuwa maarufu zaidi miongoni mwa watu hawa alikuwa ni As’ad bin Zuraarah, na ‘Ubadah bin Saamit. Maelezo ya mkataba wao na Mtume yalikuwa hivi: “Tumefunga mkataba na Mtukufu Mtume kwamba ‘Hatutamshirikisha yeyote na Allah. Hatutaiba wala kufanya zinaa. Hatutawaua watoto wetu. Hatutasingiziana na hatutaacha kutenda matendo mema.”

Mtume (s.a.w.w.) naye aliwaahidi ya kwamba kama wakiyatekeleza map– atano haya basi, nafasi yao itakuwa ni Peponi, lakini kama wakiasi, basi itakuwa ni juu yake Allah kuwasamehe au kuwaadhibu. Kwa mujibu wa istilahi za wanahistoria, *Bay’at* (kiapo cha Utii) hii inaitwa *Bay’atun Nisa’* (Bay’at ya wanawake), kwa sababu wakati wa kutekwa kwa mji wa Makkah, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifanya Bay’at ya aina hii hii na wanawake.
Watu hawa kumi na wawili walirudi Yathrib wakiwa na nyoyo zilizojaa imani na wakajishughulisha sana sana katika kuubalighisha Uislamu. Vile vile walimwandikia barua Mtume (s.a.w.w.) wakimwomba awapelekee mubalighina ili akawafundishe Qur’anii. Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka Mus’ab bin Umayr ili akawaongoze. Chini ya mwongozo wa mubalighina huyu mwenye uwezo, Waislamu wale walikuwa wakikusanyika na kumzunguka na kuzisali sala zao za jamaa wakati Mtume (s.a.w.w.) akiwa hayupo.5

Mkataba Wa Pili Wa Aqabah

Zilikuwako ghasia nyingi miongoni mwa Waislamu wa Yathrib. Walikuwa wakisubiri kwa shauku uingie wakati wa Hija ili kwamba, ukiachilia mbali kule kuzitekeleza ibada za Hija, vilevile wataweza kumwona Mtume (s.a.w.w.) kwa karibu zaidi na kuelezea kuwa kwao tayari kuitoa kila huduma kwa ajili ya Uislamu na kuukuza upeo wa mapatano kutegemeana na wingi na ubora. Msafara wa mahujaji wa Yathrib uliokuwa na zaidi ya watu mia tano ulitoka kwenda Makkah. Msafara huo ulikuwa na waislamu sabini na watatu, ambao wawili miongoni mwao walikuwa ni wanawake, na wale waliosalia walikuwa ni watu wenye mtazamo wa kadiri au wenye nusu ya mwelekeo wa kwenye Uislamu. Kikundi hiki kilikutana na Mtume (s.a.w.w.) mjini Makkah na wakaomba wawekewe muda wa kufanyia taratibu za ‘Bay’at’. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Tutakutana Mina usiku wa mwezi 13 Dhil–Hajj, watu watakapokuwa wamelala, kwenye Bonde la ‘Aqabah (Hii ni njia nyembamba ya mlimani iliyoko karibu na Mina).

Usiku wa mwezi 13 Dhil–Hj ukafika. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa wa kwanza kufika ‘Aqabah pamoja na ami yake Abbas. Sehemu ya usiku ule ilipita. Washirikina wa Uarabuni wakaenda kulala Waislamu waliamka

kutoka kwenye sehemu zao mmoja baada ya mwingine na wakaja pale ‘Aqabah kwa siri. Bwana Abbas, ami yake Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ndiye wa kwanza kuzungumza, naye alisema hivi: “Enyi Bani Khazraji! Mmeonyesha kuunga mkono kwenu dini ya Muhammad! Hamna budi kufahamu ya kwamba yeye ndiye mtu mtukufu zaidi kwenye kabila hili. Bani Hashim wote, wawe wenye kuiamini dini yake au la, wanawajibikiwa na ulinzi wake.

Hata hivyo, hivi sasa Muhammad anakuelekeeni na anapenda kuwa miongoni mwenu. Kama mnao uhakika ya kwamba mtajiambatanisha na mapatano yenu nanyi mtamhami kutokana na kila dhara litokalo kwa maadui zake, basi tuko tayari kumruhusu aende nanyi. Hata hivyo, endapo hamna uwezo wa kumhami kwenye hali ngumu, mko huru kumwacha hapa aishi miongoni mwa ndugu zake kwa utukufu mwingi na heshima.”

Wakati huu Bura’a bin Ma’rur alisimama na kusema: “Ninaapa kwa jina la Allah! Kama kungalikuwa na chochote kingine nyoyoni mwetu zaidi ya yale tuliyoyasema kwa ndimi zetu, tungalisema. Hatuna nia yoyote nyingine zaidi ya kuyatimiza mapatano haya na kujitoa mhanga katika nji ya Mtume.” Baada ya hapo wale Bani Khazraji walimwelekea Mtume (s.a.w.w.) na kumwomba azungumze lolote. Mtume (s.a.w.w.) alisoma aya za Qur’anii na kuuchochea muelekeo wao wa kuelekea kwenye Uislamu. Baada ya hapo akasema: “Ninakichukulia kiapo chenu hiki ya kwamba, mtanihami kama vile mnavyowahami wana wenu wa watu wa familia zenu.”

Alipoyasikia hayo Bura’a, alisimama tena na akasema: “Sisi tu wana wa kampeni na mapambano, nasi tumefunzwa kuwa wapiganaji mashujaa. Tumezirithi sifa hizi kutoka kwa jadi zetu.” Wakati huo huo, pale mkutano mzima ulipojawa na msisimko, sauti za Bani Khazraji zili– zokuwa dalili ya hamasa zao zisizo kifani zilipaa. Bwana Abbas, huku akiwa ameushika mkono wa Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Wamewekwa wapelelezi juu yetu na hivyo basi, ni muhimu kwamba mzungumze kwa sauti ndogo.” Hapo Bura’a bin Ma’rur, Abul Haytham bin Tayhaan na As’ad bin Zurarah waliamka kutoka kwenye sehemu zao na kuiweka mikono yao juu ya mkono wa Mtume (s.a.w.w.) kwa namna ya Bay’at.

Baada ya hapo wale wote waliokuwapo pale walifanya ‘Bay’at, mmoja baada ya mwingine. Alipokuwa akila kiapo kile, Abul Haytham alisema: “Ewe Rasuli wa Allah! Tumefanya mapatano na Wayahudi na sasa hakuna njia yoyote nyingine ila kuipuuzilia mbali. Hivyo basi, haitafaa kwamba siku moja utuache na kuwarudia watu wako.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: “ Kama mmefanya mapatano ya amani na mtu yeyote yule nin– auchukulia kuwa wa kuheshimiwa.”

Kisha akaongezea kusema: “Chagueni watu kumi na wawili miongoni mwenu kama vile Mtume Musa bin Imran alivyoteua viongozi kumi na wawili miongoni mwa Bani Isra’il, ili kwamba, kwenye hali ngumu muweze kuyategemea maoni yao.” Baada ya hapo, wawakilishi kumi na wawili wa Maansari (tisa kutoka Bani Khazraji na watatu kutoka Bani Aws) walijulishwa kwa Mtume (s.a.w.w.). Majina na taarifa zao vimeandikwa kwenye vitabu vya historia. Kule kufanyika kwa

‘Bay’at kulimalizika kwenye mkutano huu na Mtume (s.a.w.w.) aliahidi ya kwamba ataondoka Makkah

wakati ufaao na kwenda Yathrib. Baada ya hapo wale watu wakatawanyika.6

Hali Ya Waislamu Baada Ya Mkataba Wa 'Aqabah'

Sasa swali linaibuka, ni kwa nini watu wa Yathrib waliokuwa mbali kuto- ka kwenye kitovu cha wahubiri wa Uislamu waliyakubali mamlaka ya Mtume (s.a.w.w.) kwa urahisi zaidi kuliko watu wa Makkah (pamoja na kuwa kwao karibu naye) na ni kwa nini mikutano mifupi na michache baina yake na watu wa Tathrib ilikuwa na uzito mkubwa kuliko yale mahubiri ya miaka kumi na mitatu mle mjini Makkah? Tunaweza kusema kwamba mambo mawili yafuatayo ndiyo yaliyokuwa sababu ya kuendelea kwa Uislamu mjini Yathrib:

"Watu wa Yathrib walikuwa majirani wa Wayahudi tangu kale na kila mara wakitaja kwenye mikutano na mikusanyiko yao kuhusu kuteuliwa kwa Nabii wa kiarabu kwenye kazi ya Utume. Nabii huyu walimtaja mno kiasi kwamba Wayahudi walikuwa wakiwaambia wenye kuyaabudu masanamu wa mle mjini Yathrib kwamba yule Nabii wa kiarabu anayengojwa ataikuza dini ya Kiyahudi na kuiharibu ibada ya masanamu. Mazungumzo haya yalizaa utayari usio wa kifani akilini mwa watu wa Yathrib katika kuikubali dini iliyokuwa ikisubiriwa na Wayahudi, kiasi kwamba wale wakhazraji sita walipokutana na Mtume (s.a.ww.) kwa mara ya kwanza walisilimu mara moja na wakaambiana: "Huyu ndiye yule Nabii anayen- gojwa na Wayahudi na hivyo basi ni muhimu kwetu sisi kwamba tuonyeshe kumwamini kwetu kabla yao."

Hivyo basi, moja ya upinzani uliotolewa na Qur'anii Tukufu dhidi ya Wayahudi ni huu: "Mlikuwa na kawaida ya kuwaogofya wenye kuyaabudu masanamu juu ya uteuzi wa Utume kwa Nabii wa kiarabu na mkawabashiria watu ujio wake na kuzinukuu dalili zake kutoka kwenye Taurati. Basi kwa nini sasa mwazigeuzia nyuso zenu mbali naye? Inasema:

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَهُمْ وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا
كَفَرُوا بِهِ ۚ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ {89

"Na kilipowajia kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu, chenye kuthibitisha (kile) walicho nach,o, na zamani walikuwa wakiomba ushindi dhidi ya makafiri; lakini yalipowafikia yale waliyoyajua waliyakana; basi laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya makafiri."
(***Surah al-Baqarah, 2:89***).

Kipengele kingine ambacho kinaweza kuwa ndicho kilichowafanya watu wa Yathrib kusilimu ni ule uchovu wao wa kiakili na kimwili. Ule usum- bufu uliosababishwa na migogoro iliyoenea kwenye kipindi cha miaka mia moja na ishirini uliimaliza subira yao. Walikaribia kuchoshwa na maisha yao na wakaona wamefungiwa milango yote ya matumaini na wokovu wao.
Uchunguzi wa vita vya Bu'aath tu, ambavyo ni moja ya vita vilivy- opiganwa na watu wa Yathrib, kabila moja dhidi ya jingine, unatoa picha ya dhahiri ya hali yao. Kwenye vita hii, Bani Aws mwanzoni walioshindwa, walikimbilia Najd.

Wale maadui walioshinda (Bani Khazraji) waliwadhihaki. Chifu wa Bani Aws (Huzayr) alijihisi vibaya mno. Alijichoma mkuki nyongani mwake, akashuka kutoka kwenye farasi wake akawaita watu wake kwa sauti kuu akisema: “Sitaamka kutoka kwenye sehemu yangu hii hadi niuawe.”

Uthabiti wa Huzayr uliibua moyo wa heshima, ushujaa na kujihami miongoni mwa wapiganaji walioshindwa. Waliamua kurudi kwa vyovyote vile itakavyokuwa na kuyatetea maslahi yao. Wakiwa wamekata tamaa kabisa juu ya maisha yao walianza mapigano makali sana. Wakati jeshi lenye kujitoa mhanga linapopigana kwa imani thabiti daima hushinda. Hivyo wale Bani Aws walioshindwa walishinda tena. Waliwashinda Bani Khazraji na wakaichoma mitende yao.

Baada ya hapo vita na amani viliendelea kwa muda mrefu na iliwabidi kuyakabili mamia ya matukio yasiyopendeza, yenye kuhuzunisha, na yenye kuchosha. Makundi yote mawili yalihuzunishwa na hali yao na wal- itaka kupata suluhisho juu yake na walitamani kupata mwanga wa matumaini.

Ni kwa sababu hii kwamba wale Wakhazraji sita walipoyasikia maneno ya Mtume (s.a.w.w.) walijihisi kwamba wamekipata kile wali- chokipoteza na wakasema: “Pengine Allah Atatuondolea huu ugomvi kupitia kwako.”

Hizi zilikuwa baadhi ya sababu zilizowashawishi watu wa Yathrib kuupokea ule mwito wa uislamu kwa mikono miwili.

Hatua Ya Quraishi Juu Ya Mapatano Ya ‘Aqabah’

Sasa Waquraishi wakauchukua msimamo wa utepetevu, na kwa vile Uislamu ulikuwa haujapata maendeleo yawezayo kutambulika mjini Makkah, walikuwa na mawazo kwamba kuanguka kwake kumeanza na kwamba jengo lake litaporomoka punde tu. Mara kwa ghafla taarifa za mapatano ya pili ya ‘Aqabah ziliangukia miongoni mwao kama bomu. Wakuu wa uongozi wa ibada ya masanamu walifahamu kwamba kwenye giza la usiku uliopita watu sabini na watatu watokao Yathrib wamefanya mkataba na Mtume (s.a.w.w.) kwamba watamlinda kama vile wawalin- davyo watoto wao. Taarifa hizi zilileta hofu isiyo na kifani nyoyoni mwao na wakajiambia wenyewe: “Sasa Waislamu wamejipatia kituo katikati mwa Penisula ya Uarabuni na kwamba ulikuwapo uwezekano kwamba wangaliweza kuyakusanya majeshi yao yaliyotawanyika na kuanza kuibalighisha dini yao ya Upweke wa Allah, na kwa njia hii wataiogofya serikali kuu ya wenye kuabudu masanamu wa Makkah kwa vita na hatari.”

Ili kulichunguza zaidi jambo hili, machifu wa Waquraishi walionana na Wakhazraji asubuhi yake na kusema: “Tumepata taarifa ya kwamba usiku uliopita mlifanya mapatano ya ulinzi na Muhammad na mmemwahidi ya kwamba mtapigana dhidi yetu!” Hata hivyo, Wakhazraji waliapa ya kwam- ba wao hawakudhamiria kupigana vita dhidi yao.

Msafara wa mahujaji wa Yathrib ulikuwa na watu wapatao 500 hivi. Miongoni mwao ni watu sabini na watatu tu waliofanya Bay’at pale ‘Aqabah kwenye ule usiku wa manane huku wengine wakiwa wamelala

kwenye wakati ule na wakiwa hawajui lolote juu ya jambo lile. Hivyo basi, wale wasiokuwa waislamu waliapa ya kwamba hakuna lolote la aina ile lililotokea na ile hadithi nzima (ya yale mapatano) ilikuwa uzushi mtupu. Yule Khazraji Abdallah bin Ubay, ambaye matayarisho ya uchifu wake wa Yathrib nzima yalikuwa tayari yameshafanyika, alisema: “Hakuna jambo la aina hii lililofanyika, na watu wa kabila la Khazraji hawafanyi jambo lolote lile bila ya ushauri wangu.”

Kisha machifu wa Waquraishi waliamka wakaenda zao ili kwamba waweze kufanya uchunguzi zaidi juu ya jambo hili. Waislamu waliokuwapo mkutanoni pale, walitambua ya kwamba siri yao imefichuka. Hivyo basi, waliamua kuutumia ipasavyo muda uliopo na wakaambiana:
“Kabla ya kutambuliwa wale watu waliohusika na mapatano yale, ingalikuwa bora kama tungalirejea nyumbani na kutoka nje ya athari za Makkah.”

Haraka iliyoonekana katika baadhi ya watu wa Yathrib ilizidisha shaka za Waquraishi juu ya yale mapatano na wakahitimisha kwamba ile taarifa waliyoipata ilikuwa sahihi. Hivyo basi, waliwafuata wale watu wa Yathrib. Hata hivyo, kwa bahati walianzisha ufuatiliaji wao ule wakiwa tayari wameshachelewa na ule msafara wa mahujaji ulikuwa tayari uishafikia umbali usioweza kufikiwa na watu wa Makkah. Waliweza kumkamata Mwislamu mmoja tu naye ni Sa’ad bin Ubadah.

Kwa mujibu wa Ibn Hisham Waquraishi waliwakamata watu wawili miongoni mwao akiwemo Sa’ad na mwingine akiwa ni Manzar bin Umar. Yule wa pili aliwaponyoka. Hata hivyo, kuhusu Sa’ad, walizikamata nywele zake kwa ukali mwingi na wakamburuza chini, miongoni mwa Waquraishi yupo aliyechomwa mno moyoni kumwona Sa’ad akiwa kwenye hali hii ya kuhuzunisha na akamwuliza: “Je, una mapatano na mtu yeyote humu mjini Makkah?” Sa’ad akajibu:’ “Ndio, nina mapatano na Mut’am bin Adi, kwa kuwa niliihami biashara yake kutokana na wizi na nikampatia mahali pa usalama alipokuwa akivuka kupitia Yathrab.”

Yule Quraishi aliyetaka kumwokoa kutokana na mgogoro huu alimwendea Mut’am na kumwambia: “Khazraji mmoja amekamatwa naye anateswa vikali mno na Waquraishi. Sasa anataka msaada wako na anakusubiri ukamsaidie”. Mut’am alikuja mahali pale na akaona kuwa ni Sa’ad bin Ubadah, mtu yule ambaye kila mwaka kwa ulinzi wake misafara kule ilikokuwa ikienda ilikuwa ikifika kwa usalama. Alifanya Waquraishi wamwachie na kisha akampeleka Yathrib. Marafiki wa Sa’ad na Waislamu waliozipata taarifa za kukamatwa kwake waliamua kuchukua hatua ili afunguliwe. Walikuwa wakilifikiria jambo hili wakati Sa’ad alipotokea kwa ghafla kwa mbali. Baada ya kuwafikia aliwasimulia ile hadithi yenye kuogofya.[7]

Mvuto Wa Kiroho Wa Uislamu

Wataalamu wa elimu ya nchi za Mashariki wanajaribu kwa makini kunena kwa nguvu kwamba kuendelea kwa Uislamu kulifanyika kwa upanga. Kuhusiana na jambo hili husema mambo ambayo tutayajibu, moja baada ya jingine, tutakapovielezea vita vya Uislamu dhidi ya makafiri. Hata hivyo, hivi sasa tungalipenda kuzivutia fikara za wasomaji kwenye tukio lililotokea mjini Yathrib kabla ya Hijiriya.

Tukio hili lathibitisha dhahiri kwamba, hapo awali, kuenea na kuendelea kwa Uislamu kulifanyika tu kwa njia ya utamu wake na uwazi wa sheria na kanuni zake zilizopendeza nyoyo za watu. Haya yafuatayo hapa chini ndio maelezo yake:

Mus'ab bin Umayr alikuwa mubalighi na msemaji mkuu wa Uislamu aliyepelekwa Yathrib na Mtume (s.a.w.w.) kwa kuombwa na As'ad bin Zurarah. Watu wawili hawa waliamua kuwabalighishia machifu wa Yathrib kwa njia ya hoja za kimantiki. Siku moja waliingia bustani walimokuwamo baadhi ya Waislamu na Sa'ad bin Ma'aaz na Usayd bin Huzayr, waliokuwa machifu wa Bani Abdu Ashhal, walikuwapo pale nao. Sa'ad alimgeukia Usayd na kumwambia: "Ufute upanga wako na uwaendee hawa watu wawili na uwaambie waache kuibalighisha dini ya Uislamu na wasiwahadae watu wetu wajinga kwa hotuba na maelezo yao. Kwa vile As'ad bin Zurarah yu binamu yangu, (mwana wa mama mdogo/mkubwa), mimi ninaona aibu kumkabili huku nikiwa na silaha iliyofutwa." Usayd alisimama akiwakingia njia wale watu wawili kwa uso ulioghadhibika na upanga uliofutwa na akayatamka yale maneno tuliyoyataja hapo juu kwa sauti ya ukali.

Yule msemaji mkuu Mus'ab bin Umayr aliyekwisha jifunza njia ya uhubiri kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Usayd hivi: "Inawezekana kwamba uketi pamoja nasi kwa kitambo hivi ili tuweze kuzungmza. Kama yale tuyasemayo si yenye kukubalika akilini mwako, tutarudi kwa njia ile ile tuliyojia." Usayd akasema: "Umesema jambo liingialo akilini." Hivyo, akaketi kwa kitambo fulani na akauchomeka upan- ga wake alani mwake.
Mus'ab akazisoma aya chache za Qur'anii. Ukweli wenye kuangaza wa Qur'anii na mvuto na utamu wake vilivyoandamana na mantiki yenye nguvu ya Mus'ab vikamshinda nguvu. Alipoteza uwezo wake wa kujitawala na akauliza akisema: "Vipi mtu aweza kuwa Mwislamu?" Wakamjibu wakasema: "Ushuhudie Upweke wa Allah, uoshe mwili wako na nguo zako kwa maji na usali." Usayd aliyekuja kwa lengo la kuimwaga damu ya hawa watu wawili, aliushuhudia kwa moyo mkunjufu upweke wa Allah na Utume wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Alioga na akafua nguo yake na kasha akarejea kwa Sa'ad huku akizikariri 'Shahadatain' (Kuukiri Upweke wa Allah na Utume wa Muhammad). Sa'ad bin Ma'aaz alikuwa akimsubiri kwa shauku. Mara Usayd akatokea akiwa yu mwenye uso wenye furaha na tabasamu. Sa'ad bin Ma'aaz aliwageukia wale waliokuwapo pale na akasema: "Ninaapa kwa jina la Allah! Usayd ameibadilisha imani yake na hakulifikia lile lengo alililoliendea." Usayd akafika na akaielezea ile habari. Sa'ad bin Ma'aaz akaamka kwa ghadhabu kali mno ili aende akawazuie wale watu wawili wasihubiri Uislamu na kuimwaga damu yao. Hata hivyo, jambo lile lile lililotokea kwa Usayd, lil- imtokea yeye nae.

Ilimbidi yeye nae asalimu amri mbele ya hoja za kimantiki na zenye nguvu na maneno yenye kuvutia na matamu ya Mus'ab. Dalili za majuto zilijitokeza usoni mwake kwa lile alililoliamua, na sasa akatangaza kuunga kwake mkono Uislamu. Kisha alioga na akazitoharisha nguo zake. Baada ya hapo akarudi kwa watu na kuwaambia: "Nina cheo gani miongoni mwenu?" wakamjibu wakasema: "Wewe ni kiongozi na chifu wa kabila letu." Kisha akasema: "Sitazungumza na mwanaume wala mwanamke yeyote wa kabila

langu ila watakapokuwa wamesilimu.”

Haya maneno ya chifu yalipitishwa kinywa hadi kinywa kwa watu wote wa kabila lile na katika kipindi kifupi na hata kabla ya kumwona Mtume (s.a.w.w.) kabila zima la Bani Abdul Ashhal lilisilimu na likawa walinzi wa hii dini takatifu.8

Tunapata mifano mingi ya matukio ya aina hii kwenye kurasa za historia. Kwa dhahiri kabisa zinathibitisha kutokuwa na msingi kwa mazungumzo ya wataalamu wa elimu ya nchi za Mashariki juu ya sababu za kuendelea kwa Uislamu, kwa sababu kwenye matukio haya, nguvu au fedha havikutumika na wale watu waliohusika hawakumwona Mtume (s.a.w.w.), wala hawakuwa na mawasiliano naye. Hakikutumika kipengele chochote kingine kwenye matukio haya ila akili za Mwislamu msemaji zilizoleta mapinduzi ya kiroho ya ajabu kabisa kwenye kabila lile.

Waquraishi Wapatwa Na Hofu

Msaada uliotolewa na watu wa Yathrib kuwapa Waislamu uliwaamsha tena Waquraishi kutoka kwenye uzembe wao. Wakayaanzisha tena yale mateso na dhuluma zao na wakajitayarisha tena kuuzuia ushawishi na maendeleo ya Uislamu. Masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walilalamika kuhusu mateso na dhuluma walizokuwa wakitendewa na makafiri na wakaomba ruhusa ya kuhajiria kwenye sehemu nyingine. Mtume (s.a.w.w.) aliwaomba wampe muda (ili aweze kuamua la kufanya). Baada ya siku chache hivi aliwaambia: “Sehemu inayokufaeni zaidi ni Yathrib. Mnaweza kuhamia kwenye sehemu ile mmoja baada ya mwingine kwa urahisi sana.”

Baada ya Waislamu kuamrishwa kuhamia, walitoka Makkah kwa kutoa sababu moja au nyingine na wakaelekea Yathrib. Hata hivyo, kwenye hatua ya kwanza kabisa ya kuhajiri kule Waquraishi walipata kuijua siri ya safari zile. Hivyo basi, wakazuia aina zote za misafara na wakaamua kuwarudisha wale wote waliokuwamo njiani (wakielekea Yathrib). Vile vile waliamua ya kwamba iwapo mtu atakuwa akihajiri na mkewe na watoto na yule mkewe yu quraishia, wasimruhusu kuondoka na mkewe huyo. Ingawa Waquraishi walizichukua hatua zote hizi, walijizuia kumwaga damu na wakaendelea kuwaonea na kuwadhulumu Waislamu. Hata hivyo, kwa bahati matendo yao hayakuzaa matunda.9

Hata hivyo, idadi kubwa ya Waislamu iliponyoka kutoka kwenye makucha ya Waquraishi na kujiunga na watu wa Yathrib.
Wote walifanya hivyo ila Mtume (s.a.w.w.) na Sayyidna Ali (a.s.), ukiachilia mbali Waislamu waliozuiwa au waliokuwa wagonjwa, hakuna Mwislamu yeyote mwingine aliyesalia mjini Makkah. Kukusanyika kwa Waislamu mjini Yathrib kuliwatahadharisha zaidi Waquraishi. Hivyo basi, ili kuuharibu Uislamu viongozi wote wa kabila lile walikusanyika kwenye Darun-Nadwah na wakashauriana juu ya hali yao. Mapendekezo yao yote yalishindikana kutokana na sera maalum za Mtume (s.a.w.w.), hatimaye yeye naye alihajiria Yathrib kwenye mwezi wa Rabiul Awwal, katika mwaka wa kumi na nne wa uteuzi wake kwenye kazi ya Utume.

1. Seerah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 425
2. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 426.
3. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 427.
4. Tarikh–i Tabari, Juzuu 2, uk. 86.
5. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.131.
6. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.438–444; na Tabaqaat Ibn Sa'ad, Juzuu 1, uk. 221–223.
7. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.448– 450
8. A'laamul Wara', uk. 37; na Bihaarul Anwaar, Juzuu 19, uk. 10–11.
9. Tabaqat–i Ibn Sa'ad, Juzuu 7, uk. 210.

Sura Ya 25: Tukio La Kuhajiri (Kuhama)

Serikali ya watu wa Makkah ilifanana na serikali ya kikatiba. Darun–Nadwah yao ilikuwa kama baraza la ushauri ambamo viongozi wa makabila hukutana kwenye wakati wa hatari na wakabadilishana mawazo kwenye mambo magumu na kuchukua uamuzi wa pamoja.

Katika mwaka wa kumi na tatu wa utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) watu wa Makkah walikabiliwa na hatari kuu kutoka kwa Waislamu. Ilitishia uhai na uhuru wao. Kile kituo kikuu kilichoundwa na Waislamu mjini Yathrib na lile jukumu walilolibeba watu wa Yathrib kwa ulinzi wa Mtume (s.a.w.w.) vilikuwa dalili za dhahiri za tishio hili.

Katika mwezi wa Rabiul Awwal wa mwaka wa kumi na tatu wa Utume wa Mtume (s.a.w.w.), wakati kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) kulipofanyika, hakuna Mwislamu yeyote aliyesalia mjini Makkah isipokuwa Mtukufu Mtume, Ali na Abu Bakr na Waislamu wengine wachache waliokuwa wamezuiwa na Waquraishi au wale waliokuwa wazee au wagonjwa. Hata hivyo, ulikuwako uwezekano wa kila namna kwa watu hawa nao kutoka mjini Makkah na kwenda Yathrib. Wakati ule ule, kwa ghafla, Waquraishi waliuchukua uamuzi wa utata na wa hatari.

Ulifanyika mkutano wa ushauriano wa machifu kwenye Darun–Nadwah. Mtu mmoja kutoka miongoni mwao alizungumza tangu mwanzoni juu ya kukusanyika kwa majeshi ya Muhammad mjini Yathrib na yale mapatano yaliyofanywa na Bani Aws na Bani Khazraji. Baada ya hapo mtu yule aliongezea kusema: ‘Sisi watu wa Haraam, tulikuwa tukiheshimiwa na makabila yote.

Hata hivyo, Muhammad alipanda mbegu ya ugomvi na hivyo inatuletea hatari kubwa. Sasa tuishapoteza uvumilivu wetu wote. Njia pekee ya usalama wetu ni ule wa kwamba ateuliwe shujaa mmoja kutoka miongoni mwetu, na kwa siri, aumalizie mbali uhai wake. Na kama Bani Hashim wataamka kugombana nasi, tunaweza kuwalipa dia.”

Mzee mmoja asiyetambulika na aliyejitambulisha kuwa ni ‘Mnajdi’ alilikataa wazo hili na kusema: “Mpango huu hauwezi kutekelezeka hata kidogo, kwa sababu Bani Hashim hawatausaza uhai wa huyo

mwuwaji wa Muhammad na kulipa dia hakutawaridhisha. Hivyo basi, yeyote ajitoleaye kuutekeleza mpango huu hana budi kwanza aanze kujitenga na maisha yake mwenyewe, na mtu wa aina hiyo hapatikani miongoni mwenu."

Mmoja wa machifu aliyeitwa Abul Bakhtari akasema: "Jambo lililo bora ni kumfunga Muhammad na kumpa chakula na maji kwa kupitia kwenye tundu na hivyo tutaweza kuzuia kuenea kwa dini yake". Yule mzee wa Najdi akazungumza tena: "Mpango huu nao si tofauti sana na ule wa kwanza, kwa kuwa kwa tukio hilo Bani Hisham watapigana vita dhidi yenu ili kumfungulia. Na hata wao wenyewe wasifaulu kulifikia lengo hili, wataomba msaada wa makabila mengine kwenye wakati wa Hajj na watamfungulia kwa msaada wao."

Mtu wa tatu alitoa ushauri mwingine na akasema: "Ingalifaa kama tungal- imfanya Muhammad amrekebu ngamia mkaidi na kuifunga miguu yake yote miwili na kumfanya ngamia yule akimbie ili amgongegonge kwenye vilima na mawe na hivyo kuupondaponda mwli wake. Na kama kwa bahati uhai wake utabakia, na akashukia kwenye ardhi ya kabila jingine na akata- ka kuibalighisha dini yake miongoni mwao wenyewe, wale wenye kuyaabudu masanamu kwa shauku kuu, watalimaliza mbali jambo hili kuhusiana naye na watatuokoa sisi na wao wenyewe kutokana na fitna yake."

Yule mzee wa Najdi aliukataa mpango huu tena na akasema: "Mnaitambua njia ya uzungumzaji wa Muhammad. Kwa maneno yake yenye kuvutia na kushinda kwa uzuri wake. Kwa hotuba zake tamu na ufasaha wa lugha, atayafanya makabila mengine yamuunge mkono na kisha atakurukieni."

Utulivu kamili uliutawala mkutano mzima. Mara, kwa ghafla Abu Jahl, na kwa mujibu wa wasimulizi wengine, yule mzee wa Najdi mwenyewe, alilitoa wazo lake na akasema: "Njia pekee yenye kufaa na iliyo rahisi ni kwamba wateuliwe watu kutoka miongoni mwa familia zote na kwa pamo- ja waishambulie nyumba yake wakati wa usiku na kumkata vipande vipande, ili kwamba familia zote ziweze kuhusika na mauaji yake.

Ni dhahiri kwamba, katika hali hiyo, Bani Hashim hawataweza kulipiza kisasi dhidi ya familia zote." Wazo hili lilikubaliwa na watu wote kwa pamoja na wale wauaji wakachaguliwa. Hivyo ikaamuliwa kwamba utakapoingia usiku wale watu waitekeleze kazi yao hiyo.[1]

Msaada Wa Kimungu

Hawa watu wenye vichwa vilivyoshanganyikiwa walikuwa wakifikiria ya kwamba, kama yalivyo mambo mengine ya kidunia, kazi ya Utume nayo ingaliweza kuteketezwa kwa mipango kama hii. Hawakuweza kutambua ya kwamba kama walivyokuwa mitume wengine, Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alikuwa naye amejaaliwa kwa msaada wa kimungu, na ule mkono uliouhami huu mwenge uangazao kutokana na vimbunga vya ajali kwa miaka kumi na tatu, vile vile ungeweza kuvuruga mpango huu wa sasa wa maadui zake.

Kwa mujibu wa wafasiri wa Qur'anii Tukufu, Malaika Mkuu Jibrail alikuja na kumtaarifu Mtume (s.a.w.w.) juu ya ile makri ya uovu wa washirikina. Qur'anii inalizungumzia tukio hili kwa maneno haya: **"Na walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuuwe au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango."** (***Sura al-Anfal,*** **8:30**).

Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa na Allah kwenda Yathrib. Hata hivyo, haikuwa jambo rahisi kuiepuka mikono ya ukatili ya waabudu masanamu, hasa pale walipokuwa wakimpeleleza, na umbali baina ya Makka na Yathrib nao ulikuwa mrefu. Kama asingelitoka mjini Makka baada ya kupanga vizuri ingeliwezekana kwamba watu wa Makka wangelimkamata na kumtia kizuizini na kumuuwa kabla ya kuwafikia marafiki zake.

Wanahistoria na waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) wametoa maelezo tofauti tofauti juu ya kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) na tofauti zilizopo baina ya maelezo ya tukio hili hazina kifani. Mwandishi wa *Siiratul-Halabi* amefaulu kwa kiasi fulani katika kuyafanya hayo maelezo tofauti tofauti yaafikiane, lakini ameshindwa kuondoa tofauti katika baadhi ya sehemu.

Jambo lipasalo kuzingatiwa ni kwamba wengi wa wanachuoni wa hadith wa Kissuni na Kishia wamekuweka kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) katika njia ambayo mtu anaamua kwamba lilikuwa ni jaribio la kimiujiza ya kujiokoa na maadui, ambapo ukichunguza tukio hili kwa makini, itakufunukia ya kwamba kutoroka kwa Mtukufu Mtume kulikuwa ni matokeo ya uoni wa mbali wake, wa mpango wa kiuangalifu na hatua za tahadhari alizozichukua; na Allah Alipenda kumpa usalama kwa njia za kawaida na wala si kwa matendo ya kimuujiza.

Jambo lenye kutoa ushahidi juu ya maoni haya ni kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitumia sababu za kawaida na njia za kiakili (kama vile kumfanya Sayyidna Ali (a.s.) alale kitandani mwake na yeye mwenyewe kujificha pangoni n.k na hivyo akajihakikishia usalama).

Malaika Mkuu Amwarifu Mtume (S.A.W.W).

Malaika Mkuu Jibriil alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu ule mpango mwovu wa makafiri na kumtaka ahajiri. Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) alale kitandani mwake, na kupita kwenye majaribu ya hatari kwa ajili ya usalama wa Uislamu, ili kwamba makafiri wasidhanie ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) ameondoka, bali wasalie kwenye dhana ya kwamba alikuwa bado yumo mle nyumbani. Hivyo Sayyidna Ali (a.s.) alibakia mwenye kutosheka na kusalia mle nyumbani, ili kwamba yeye Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe aweze kupita kwenye mitaa ya mji wa Makka na kwenye viunga vyake kwa uhuru kabisa.

Faida iliyomo kwenye mpango huu ni kwamba maadui waliendelea kuilinda tu nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) na yeye mwenyewe kupata muda wa kufika sehemu ya usalama.

Sasa yatupasa tuone kwamba ni nani yule ajitoleaye kulala kitandani mwa Mtume (s.a.w.w.) na kuyatoa mhanga maisha yake? Bila shaka utasema: “Ni yule aliyemwamini kwanza na kumzunguka tangu siku ya kuteuliwa kwake kuishika kazi ya Utume, kama vile nondo wazungukavyo mshumaa.” Yeye ndiye apasikaye kufanya kafara kwenye njia hii na mtu yule mwenye kujitoa mhanga mwenyewe hasa ni Sayyidna Ali (a.s.). Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alimgeukia Sayyidna Ali (a.s.) na kumwambia: “Lala kitandani mwangu usiku huu na ujifunike lile shuka la kijani ninalotumia wakati wa kulala, kwa vile maadui wamefanya shauri la kuniua na hivyo basi, ni muhimu kwamba nihamieYathrib.”

Sayyidna Ali (a.s.) alilala kitandani mwa Mtume (s.a.w.w.) mapema usiku ule. Baada ya kupita robo tatu za usiku, watu arobaini waliizingira nyumba ile na kuchungulia kupitia kwenye tundu. Waliona hali ya nyumba ile kuwa ni ya kawaida na wakadhani ya kwamba yule mtu aliyelala kwenye kile chumba cha kulalia ni Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe.

Mtume (s.a.w.w.) aliamua kutoka mle nyumbani wakati maadui walipokuwa wameizingira katika pande zote, na walikuwa wakifanya mkesha kamili. Allah Mwenyezi alipenda kumwokoa yule kiongozi mkuu wa Uislamu kutoka makuchani mwa hawa watu wabaya. Mtume (s.a.w.w.) alizisoma zile aya za Surah Yasin zilizofaa katika hali yake ile katika wakati ule na baada ya kusoma hadi aya: **“. . . . . hivyo hawaoni.” (*Surah Yasin*, 36:9),** akatoka nyumbani mle upesi na kuelekea ile sehemu aliyodhamiria kwenda. Haieleweki vema jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyoweza kuyapita yale mazingira na ni kwa nini wale waliokuwa wakiizingira nyumba ile hawakuweza kumwona.

Tunajifunza kutoka kwenye Hadith iliyonukuliwa na mwanahadith maarufu wa Kishiah, marehemu Ali bin Ibrahim, alipokuwa akiifasiri aya isemayo: **“Na walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuuwe au wakutoe. Wakapamga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.” (*Sura al-Anfal*, 8:30),** kwamba, Mtume (s.a.w.w.) alipotoka nyumbani mle, wote walikuwa wamelala, walitaka kuishambulia nyumba ile alfajiri nao hawakufikiria ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliutambua mpango wao ule.

Hata hivyo, wanahistoria wengine husimulia dhahiri[2] kwamba wale maadui walibakia macho hadi ule wakati walipoishambulia nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) naye akatoka nje kimuujiza nao hawakuweza kumwona.

Hakuna shaka juu ya ukweli uliopo kwamba muujiza huo unawezekana. Lakini swali ni hili: “Je, muujiza huo ulikuwa muhimu kwenye tukio hili?” Udadisi wa hali hii ya kuhajiri unathibitisha ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliitambua makri ile ya madui kabla hawajaizunguka nyumba yake na ule mpango alioufanya ili kuweza kunusurika ulikuwa wa kawaida kabisa na haukuwa na chochote cha kimiujiza juu yake. Kwa kumfanya Sayyidna Ali (a.s.) alale kitandani mwake alitaka kujitenga na waabudu masanamu kwa njia ya kawaida na si kwa miujiza.
Hivyo, angeweza kuitoka nyumba ile kwa urahisi kabla ya kuzingirwa na hakuhitaji muujiza wowote katika lengo lile.

Hata hivyo, inawezekana kwamba Mtume (s.a.w.w.) kubakia nyumbani mle hadi ilipozingirwa ilikuwa ni kwa sababu tusizozifahamu kwa hivi sasa. Hivyo basi, mjadala juu ya jambo hili (la Mtume (s.a.w.w.) kuondoka nyumbani mle wakati wa usiku) haujafikia mwisho machoni mwa wanahistoria wote, kwa sababu, kwa mujibu wa baadhi yao, Mtume (s.a.w.w.) alitoka nyumbani mwake kabla ya kuzingirwa kwake na kabla ya kuchwa jua.3

Maadui Waishambulia Nyumba Ya Mtume (S.A.W.W.)

Askari wa ukafiri waliizingira nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) na walikuwa wakisubiri waamrishwe kuishambulia kwa ghafla na kumkata Mtume (s.a.w.w.) vipande vipande kwenye chumba chake cha kulala. Baadhi yao waling'anga'ania ya kwamba washambulie wakati wa usiku na kuutimiza mpango wao. Hata hivyo, Abu Lahab alisimama na kusema: "Wanawake na watoto wa Bani Hashim wamo nyumbani humo na hivyo, inawezekana kwamba wakadhurika wakati wa mashambulizi." Wengine wanasema kwamba sababu ya kuchelewesha kwao ni kwamba walitaka kumwua Mtume (s.a.w.w.) kwenye mwanga wa mchana kabisa mbele ya macho ya Bani Hashim, ili wao (Bani Hashim) waweze kuona kwamba mwuaji wake hakuwa mtu maalum. Hatimaye waliamua kuutimiza mpango wao wakati wa alfajiri, kutakapokuwa na mwanga.4

Sasa imeshaingia alfajiri. Ghera na shauku vilionekana miongoni mwa makafiri. Walidhania ya kwamba wangeliweza kufikia lengo lao walilolidhamiria upesi sana. Mikono yao ikiwa kwenye mipini ya panga zao, waliingia ndani ya chumba kile cha kulala Mtume (s.a.w.w.) wakipiga makelele mengi. Wakati huo huo, Sayyidna Ali (a.s.) aliamsha kichwa chake kutoka kwenye mto wake, akaitupa kando shuka ya kijani na akasema kwa upole mno: "Kuna nini?" wakamjibu: "Tunamtaka Muhammad. Yuko wapi?" Sayyidna Ali (a.s.) akawajibu akisema: "Je, kwani mlinikabidhi Muhammad ili kwamba hivi sasa niwajibike kumrudisha kwenu. Hata hivyo, hayumo nyumbani humu hivi sasa."

Nyuso za mawakala wale ziliwiva kwa hasira na makoo yao yakisongwa na jambo hili. Walijuta kwa kusubiri hadi alfajiri na wakamlaumu Abu Lahab aliyewazuia kufanya mashambulizi wakati wa usiku. Waquraishi wakazidishwa mshtuko kutokana na kuvunjika kwa mpango wao na kushindwa walikolazimika kukabiliana nako. Wakaanza kufikiria kwamba Muhammad asingeliweza kutoka nje ya mazingira ya mji wa Makka katika kipindi kifupi kiasi kile na wakaamua kwamba amejificha mahali fulani ndani ya mji wa Makka au alikuwa njiani akielekea Yathrib.
Hivyo, wakapanga wamkamate.

Mtume (S.A.W.W) Akiwa Kwenye Pango La Thaur

Ni ukweli uliothubutu kwamba aliutumia usiku wa kuhajiri pamoja na Abu Bakr (r.a) kwenye pango la Thaur, lililoko kusini mwa mji wa Makka (sehemu iliyo mkabala na mji wa Madina). Hata hivyo, haifahamiki ni vipi kufuatana huku kulifanyika na jambo hili halina maana ya dhahiri hata kidogo katika historia. Baadhi ya watu huamini ya kwamba kufuatana huku kulitokea tu kwa bahati na kwamba Mtume

(s.a.w.w.) alipomwona Bwana Abu Bakar (r.a) njiani alimchukua akaenda naye.5

Wengine wanasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikwenda nyumbani kwa Abu Bakr usiku ule na katika usiku wa manane wote wawili walitoka nyumbani mle na kwenda kwenye pango la Thaur. Kadhalika wengine wanasema kwamba Abu Bakr (r.a) alikuja kumuulizia Mtume (s.a.w.w.) na Sayyidna Ali (a.s.) alimuelekeza kwenye yale maficho yake.6

Vyovyote vile iwavyo, waandishi wa wasifa wa Mtume (s.a.w.w.) hukichukulia kitendo hiki cha kufuatana kuwa ni uthibitisho wa utukufu wa Abu Bakr (r.a) na hulinukuu tukio hili kwa umaarufu kuhusiana na ubora wake.7

Waquraishi Hawasiti Kumtafuta Mtume (S.A.W.W)

Kushindwa kulikowapata Waquraishi kuliwafanya wazibadili mbinu zao. Hivyo, wakaamua kuzifunga barabara zote, kuweka walinzi kwenye njia zote ziendazo Yathrib na pia kupata huduma za wenye uwezo wa kumtafuta mtu kwa njia ya nyayo zake, ili kwamba kwa njia hii, waweze kumpata Mtume (s.a.w.w.) kwa gharama zozote zile. Vile vile walitangaza ya kwamba yeyote yule atakayetoa taarifa sahihi kuhusu sehemu aliyojificha Muhammad atapata zawadi ya ngamia mia moja.

Waquraishi walishughulika na wakaenda upande wa kaskazini wa mji wa Makka na wakaenda barabara ielekeayo Madina, wakati ambapo Mtume (s.a.w.w.) ili kuuvuruga mpango wao, alijificha kwenye pango la Thaur. Abu Karz, mtaalamu wa kusoma tabia za watu kwa kuangalia tu, wa mjini Makka, alikuwa anazifahamu nyayo za Mtume (s.a.w.w.). Katika kumtafuta Mtume (s.a.w.w.) alifika karibu na pango lile na akasema: “Yaonekana kwamba Mtume alidhamiria kuingia kwenye sehemu hii. Inawezekana kwamba amejificha kwenye pango hili.” Hivyo, akamtuma mtu mmoja aingie pangoni mle.

Mtu yule alipolikaribia lile pango aliona utando mnene mno wa buibui umetandwa kwenye mlango wa pango lile na njiwa allikuwa ametaga mayai hapo.8 Alirudi bila ya kuingia pango lile na akasema: “Kuna utando wa buibui mlangoni mwa pango, jambo lionyeshalo kwamba hakuna mtu yeyote ndani yake.” Kazi hii iliendelea kwa muda wa siku tatu na mikesha mitatu na kisha Waquraishi wakapoteza matumaini yote na wakaacha kumtafuta.

Kujitoa Mhanga Katika Njia Ya Ukweli

Jambo muhimu zaidi kuhusiana na tukio hili ni kule kujitoa mhanga kwa Sayyidna Ali (a.s.) katika njia ya ukweli. Kujitoa mhanga kwa njia ya ukweli ni fadhila za wale waliounganishwa na jambo hili, watu wasio ujali uhai wao, mali zao na vyeo vyao, na wakatumia uwezo wao wa kiroho na kimaada kwa ajili ya kuuhuisha ukweli. Ni dhahiri kuwa watu hawa ndio wapenzi wa ukweli, na ukamilifu na matumaini wanayopata katika ufuatiliaji wake, yanawafanya wayatoe maisha yao haya yenye kupita na wayakumbatie yale yenye kudumu milele. Kulala kwa Sayyidna Ali (a.s.) kitandani kwa Mtume (s.a.w.w.) katika usiku ule wa vurugu ni mfano wa wazi mno wa huba yake juu ya ukweli. Hakikuwapo kichocheo

chochote kingine kwa tendo hili la hatari ila ni mapenzi ya kuuhuisha Uislamu, ambao ni dhamana kwa ajili ya ustawi wa jamii.

Aina hii ya kujitolea mhanga ni yenye thamani mno kiasi kwamba Allah Mwenyezi amekuita mhanga uliofanywa kwa ajili ya kuitafuta radhi ya Allah na kama ilivyonukuliwa na wengi wa wafasiri wa Qur'ani, aya ifuatayo ilifunuliwa juu ya jambo hili: **"Na miongoni mwa watu yuko ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Allah; na Allah ni Mpole kwa waja wake."** (***Sura al-Baqarah,*** **2:207**).

Ukuu na umuhimu wa kitendo hiki umewafanya watu mahodari wa Uislamu kukichukulia kitendo hiki kuwa ni moja ya fadhila kuu zaidi za Sayyidna Ali (a.s.) Amiri wa waumini, na wamemwelezea kuwa yu mtu shujaa na mwenye kujitolea mhanga. Na popote pale lilipotajwa tukio hili kwenye tafsiri ya Qur'ani na historia imekubaliwa kwamba aya tuliyoitaja hapo juu ilifunuliwa kuhusiana naye. Ukweli huu hauwezi kusahaulika. Daima sura ya ukweli inawaka kwenye boma za ndani zaidi za ushirikina na vipande vilivyotawanyika vya mawingu haviwezi kuizima nuru ya jua.

Uadui wa Mu'awiyah dhidi ya familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na hasa kwa Amiri wa waumini hauna hata haja ya kutajwa. Alipanga kuwahonga baadhi ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ili kupata uwongo uliozushwa kwa lengo la kuzitia madoa kurasa za historia ziangazazo, lakini hakufaulu.

Samrah bin Jundab aliyeishi kwenye zama za Mtume (s.a.w.w.) na baadae akajiambatanisha na baraza la Mu'awiyah alikuwa na desturi ya kubadili mambo fulani fulani na alikuwa akilipwa kwa kufanya hivyo. Siku moja alipokuwapo mbele ya Mu'awiyah, Mu'awiyah alimwomba kwa bidii sana aipande mimbari na akane ya kwamba aya tuliyoitaja hapo juu haikufunuliwa kuhusiana na Sayyidna Ali (a.s.). Vile vile alimtaka awaambie watu kwamba kwa hakika aya hii ilifunuliwa kwa ajili ya muuwaji wa Sayyidna Ali (a.s.) (yaani Abdur Rahmani bin Muljam).

Kama tuzo yake kwa kitendo hiki ambacho kingaliweza kuivunja imani ya Samrah, Muawiyah alimuahidi kumpa dirham laki moja. Samrah hakukubali. Hivyo Muawiyah akakikuza kima kile na hatimaye biashara ile ikafanyika kwa dirham laki nne. Huyu mzee mroho akaanza kuyageuza mambo ya kihistoria kuwa uwongo na kuiharibu zaidi heshima yake iliyokuwa na madoa tayari. Mbele ya mkusanyiko mmoja alisema kwamba aya tuliyoitaja hapo juu ilifunuliwa kuhusiana na Abdurahmani bin Muljam na wala si kuhusiana na Saidiana Ali (a.s.).

Watu wajinga na wenye akili potovu waliyaamini yale aliyoyasema na haikutokea kwao ya kwamba wakati wa kufunuliwa kwa aya ile Abdur Rahmani hakuwako Hijaz na pengine alikuwa bado hajazaliwa. Hata hivyo sura ya ukweli haikufichikana kwa uzushi huu. Muawiyah na familia yake wakapatwa na matatizo ya mageuzi ya nyakati. Dalili za wale waliozusha uwongo kwenye wakati ule zilifutika. Ukweli ukatawala tena. Wafasiri wakubwa na maarufu[9] wa Qur'ani Tukufu na wanahadith wa zama zote wamekubali kwamba aya isemayo: **"Na miongoni mwa watu yuko ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Allah; na Allah ni Mpole kwa waja wake."** (***Sura al-Baqarah*****, 2:207**) ilifunuliwa wakati wa 'kukesha usiku' juu ya kujitoa mhanga kwa Sayyidna Ali (a.s.).[10]

Maelezo Ya Ibn Taymiyah

Ahmad bin Abdul Halim Haraani aliyefariki kwenye jela ya Morocco katika mwaka 728 A.H. alikuwa mmoja wa wanachuoni wa Kisunni, na nyingi ya itikadi za Mawahabbi zinatokana naye. Yeye alikuwa na maoni maalum juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Sayyidna Ali Amiri wa Waumini (a.s.) na watu wengine wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) na ameziandika nyingi ya itikadi zake kwenye kitabu chake kiitwacho *'Minhaajus Sunnah'*. Kutokana na itikadi zake potovu, wengi wa maulamaa wenzake wa wakati uleule walimlaumu kwa uzushi na kuonyesha kuchukizwa kwao juu yake. Hata hivyo, mjadala juu ya mambo haya ni nje ya lengo letu.

Amesema jambo fulani juu ya sifa hii[11] ambalo linaweza kuwekwa mbele yako pamoja na masahihisho kidogo. Wakati mwingine yaonekana kwamba watu wasio na uwezo wenye elimu haba au ya kijuu juu tu wanaathiriwa na maneno yake na wanayabalighisha maoni yake miongoni mwa watu wa kawaida bila ya uchunguzi na bila ya kutaka maoni ya wale wenye elimu pana juu ya jambo hilo, na kejeli iliyopo hapa ni kwamba watu wanaweza kuwachukulia wao kama ni wanachuoni watafiti. Hata hivyo, wao wanauona dhahiri ukweli uliopo kwamba maneno haya ni ya mtu mzushi yaliyokanushwa na wanadini wenzie na alishutumiwa kwa uzushi.

Anasema: "Kule kulala kwa Ali kwenye kitanda cha Mtume (s.a.w.w.) si fadhila juu yake, kwa kuwa Ali alijua kutokana na sababu mbili kwamba hatapatwa na madhara yoyote usiku ule. Kwanza, yalikuwa ni yale maneno ya Mtume (s.a.w.w.) ambayo yalikuwa kweli kabisa, kwa sababu usiku ule alimwambia: "Lala kitandani mwangu na hutapata madhara yoyote yale." Na pili, Mtume (s.a.w.w.) alimpa vitu ambavyo watu waliviweka amana kwake, na kwa kawaida alijua ya kwamba mwakilishi wake hatauawa, kwani vinginevyo angalimpa mtu mwingine vitu hivyo. Na kutokana na mapendekezo haya, Ali yeye mwenyewe, naye alielewa kuwa hatapata dhara lolote na atafaulu kulitimiza jukumu alilopewa na Mtume (s.a.w.w.).

Majibu Kwa Tafsiri Hii Ya Uongo

Kabla ya kutoa majibu yenye maelezo marefu juu ya haya mambo mawili, tunaweza kusema kwa kifupi tu kwamba: "Kwa kuikana sifa moja Ibn Taymiyah atakuwa ameithibitisha sifa kubwa zaidi ya Sayyidna Ali (a.s.), kwa sababu itikadi yake juu ya ukweli wa Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa ni imani ya kawaida au ilikuwa ni itikadi yenye nguvu isiyo na kifani na maneno yote ya Mtume (s.a.w.w.) yalieleweka mbele yake.

Kwa mujibu wa dhana ya kwanza (yaani iwapo kama imani yake ilikuwa ya kawaida) itakuwa kwamba Sayyidna Ali (a.s.) hakuwa na ujuzi juu ya kusalimika kutokana na madhara yoyote. Hii ni kwa sababu maneno ya Mtume (s.a.w.w.) hayajengi ujuzi maalumu nyoyoni mwa watu kama hawa (na Sayyidna Ali a.s bila shaka hakuwa mmoja wao). Hata kama wakiyakubali maneno yake kuwa ni ya kweli bado husababisha uchungu mwingi nyoyoni mwao. Na kama wakilala kwenye sehemu yake wakati wa hatari

mchafuko wao wa akili huzidi zaidi na kila mara kitisho cha mauti hutokea machoni mwao. Hivyo basi, kutokana na dhana hii alilitekeleza jukumu hili kwa mwezekano wa kuuawa na wala si kwa kujua ya kwamba atasalia salama.

Kwa mujibu wa dhana ya pili, Ibn Taymiyah ameithibitisha sifa kubwa zaidi ya Sayyidna Ali (a.s.), kwa sababu kama itikadi ya mtu ni thabiti mno kiasi kwamba maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yanaeleweka wazi kabisa kwake na ubora wa itikadi kama hiyo unakipita kila kitu.

Basi matokeo ya itikadi ya aina hii ni kwamba, Mtume (s.a.w.w.) anapomwambia: "Lala kitandani mwangu hutapata madhara yoyote yale kutoka kwa maadui."
Anakwenda kwa akili iliyotulia kabisa na analala kitandani mwake na aoni woga hata kidogo moyoni mwake. Na kama maoni aliyoyatoa Ibn Taymiyah (kwamba Saidina Ali a.s aliutambua usalama wake, kwa kuwa aliambiwa na Mtume (s.a.w.w.) aliye mkweli) yanakuwa uthibitisho wa itikadi ya daraja la juu kabisa, hana budi atambue ya kwamba bila ya kujitambua ameithibitisha hii sifa kuu kabisa ya Sayyidna Ali (a.s.).

Jibu Lenye Maelezo Ya Kina

Ama kuhusu hoja ya kwanza inaweza kusemwa kwamba sentensi isemayo: "Lala kitandani mwangu na hutapata madhara yoyote yale kutoka kwa maadui," haikunakiliwa na mwanahistoria yoyote wa kutegemewa.[12]Bila shaka Ibn Athir (aliyefariki katika mwaka 630 Hijiria)[13] na Tabari (aliyefariki dunia katika mwaka 310 Hijiriya)[14] wameinukuu sentensi hii, lakini yaonekana kwamba wameipata kutoka kwenye *Siiratu–Ibn Hisham*[15] aliyelinukuu jambo hili hivi – hasa kwa sababu maelezo ya wanahistoria hawa juu ya jambo hili, ni yale yale kabisa kama ya Ibn Hisham. Zaidi ya hapo, kwa kadiri tunavyotambua sisi, jambo hili halipatikani kwenye maandishi ya wanachuoni wa Kishia.

Shaykh Muhammad bin Hassan Tusi (aliyefariki katika mwaka wa 460 Hijiriyya) amelinukuu tukio hili la kuhajiri kwenye kitabu chake cha '*Amaali*' kwa kirefu zaidi na pia ameitaja sentensi hiyo kwa mabadiliko madogo madogo. Hata hivyo, kile akizungumziacho ni tofauti na kile kilichonukuliwa kwenye maandishi ya wanachuoni wa Kisunni, kwa kuwa yeye ananakili wazi wazi kwamba ulipopita ule usiku wa kuhajiri, Sayyidna Ali (a.s.) na Hind bin Abi Hala (mwana wa Bibi Khadija na mwana wa kulea wa Mtume (s.a.w.w.) walikutana na Mtume (s.a.w.w.) katika mikesha iliyofuatia. Katika mmoja wa mikesha hiyo, Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Sayyidna Ali (a.s.): "Ewe Ali! Tangu sasa watu hawa katu hawataweza kukushinda nguvu."

Kama itakavyoonekana, hivi karibuni ni sentensi ileile iliyonukuliwa na Ibn Hisham, Tabari na Ibn Athir. Hata hivyo, kwa mujibu wa nukuu za Shaykh Tusi, Mtume (s.a.w.w.) alimpa Sayyidna Ali (a.s.) uthibitisho huu katika usiku wa pili au wa tatu wala si kwenye usiku wa kwanza. Zaidi ya yote haya ni kuwa, maneno ya Sayyidna Ali (a.s.) mwenyewe ndio ushahidi ulio bora zaidi kwenye jambo hili. Kama ionekanavyo kwenye beti (zilizotafsiriwa hapa chini) yeye mwenyewe amekichukulia kitendo hiki kuwa ni aina fulani ya kujitoa mhanga katika njia ya ukweli:

“Kwa uhai wangu nilimlinda mtu aliye bora zaidi, aliyewahi kuitandika miguu yake katika ardhi, na mtu mtukufu aliyeifanya ‘Tawaf’ ya ‘Nyumba ya Allah’ na Hajar–i Isma’il.’ Mtu yule mtukufu ni Muhammad bin Abdullah. Nami nimefanya hivi wakati makafiri walipokuwa wakipanga makri dhidi yake. Katika muda ule, Allah Mtukufu alimhami dhidi ya makri yao.

Nilisalia kitandani mwake tangu usiku hadi alfajiri na nikaenda kuwasubiri maadui, na kujitayarisha kwa ajili ya kutekwa au kuuawa.” (Suyuti ameinukuu mistari hii kutoka kwa Sayyidna Ali (a.s.) kwenye tafsiri yake ya Qur’ani tukufu itwayo ‘*Durr’ul–Manthur*’)

Mbele ya sentensi hizi zenye kujieleza na maelezo ya waziwazi hakuna haki tena ya kuyategemea maneno ya Ibn Hisham, kwa sababu ziko nafasi nyingine nyingi kwa yeye kufanya makosa. Na upo uwezekano mkubwa kwamba, kwa vile Ibn Hisham alipendelea kuyaelezea mambo kwa njia ya kuyabana, alitosheka na kuinakili sentensi yenyewe tu. Na kwa vile haikuwa na maana sana kwake, kuhusu ni lini sentensi hii ilitamkwa (ambapo kwa hakika sentensi hii ilitamkwa kwenye usiku wa pili) alidharau kuutaja ule wakati na akayaeleza mambo katika njia ionyeshayo kana kwamba matukio yote haya yalifanyika kwenye usiku uleule wa kuhajiri.
Ushahidi mwingine uthibitishao kauli hii ni ile Hadith maarufu iliyonukuliwa na wengi wa wanachuoni wa Kisunni na Kishia. Kwa mujibu wa riwaya hii, Allah aliwaambia wale Malaika Wakuu Jibriil na Mika’il kwenye usiku ule: “Kama nikiamua kumpa mmoja wenu uhai na mwingine nimpe kifo, ni nani kati yenu atakayekuwa tayari kukikubali kifo na kumwachia uhai mwenzie?” Hakuna yeyote kati yao aliyekubali mpango huu. Hapo Allah, Mwenyezi akasema: “Sasa Ali amekipendelea kifo na kautoa mhanga uhai wake kwa ajili ya Mtume.” Kisha akawaamrisha kushuka duniani na kuusimamiia usalama na ulinzi wa Ali.

Hoja nyingine aliyoitoa juu ya Sayyidna Ali kuwa alitambua hatima usalama wake ni ile amri aliyopewa na Mtume (s.a.w.w.) kuwarudisha kwa wenyewe vitu walivyoviweka amana kwake. Kufuatana na maoni yake, jambo hili laonyesha kwamba Mtume (s.a.w.w.) alijua ya kwamba Sayyidna Ali (a.s.) hatapatwa na madhara yoyote na hivyo basi, alimtaka avirudishe vitu vile. Hata hivyo, tunafikiria ya kwamba kama ukichunguza kwa makini ule mfuatano wa matukio, tatizo hili nalo laweza kutatuliwa. Na huu ufuatao hapa chini ndio ule mkondo wa matukio ya kuhajiri.

Mfuatano Wa Matukio Ya Hajira Ya Mtume (S.A.W.W)

Hatua za awali za kuponyoka kwa Mtume (s.a.w.w.) zilichukua sura ya kimatendo kwa msaada wa mipango. Mtume (s.a.w.w.) alikimbilia kwenye pango la Thaur wakati wa usiku na kuushinda mpango wa wale waliopanga makri dhidi yake. Hakuhisi mchafuko wowote wa akili, kiasi kwamba kwenye wakati mgumu alimfariji sahaba wake kwa maneno: “Usihuzunike. Allah Yu pamoja nasi.” Kwa siku tatu mchana na usiku walizifaidi baraka za Allah. Kufuatana na kauli ya Shaykh Tusi (kwenye kitabu chake ‘*Amaali*’) Sayyidna Ali (a.s.) na Hindi bin Abi Hala (mwana wa Khadija), na kwa mujibu wa wanahistoria wengi, Abdullah bin Abu Bakr na ‘Aamr bin Fuhayrah (mchungaji wa Abu Bakar) walikuwa na desturi ya

kwenda kuonana na Mtume (s.a.w.w.).

Ibn Athr anaandika hivi:[16] “Kwenye nyakati za usiku mwana wa Abu Bakar (r.a) alikuwa akimwarifu baba yake na Mtume (s.a.w.w.) juu ya uamuzi uliochukuliwa na Waquraishi, na mchungaji wake akiwapitisha mbuzi na kondoo wake karibu na pango lile walipokuwa wakienda Makka ili kwamba Mtume (s.a.w.w.) na yule sahaba wake waweze kuyatumia maziwa yao. Katika wakati wa kurejea kwake, Abdullah alikuwa akitangulia mbele ya kondoo wale ili kwamba nyayo zake ziweze kufuatwa na miguu ya wale kondoo.

Shaykh anasema katika ‘*Amaali*’: “Katika mmoja wa mikesha hiyo (baada ya usiku wa kuhajiri) wakati Sayyidna Ali na Hind walipopata heshima ya kufika mbele ya Mtukufu Mtume alimuamrisha Saidina Ali (a.s.) atayarishe ngamia wawili kwa ajili yao (yaani kwa ajili ya Mtume s.a.w.w na yule sahaba wake). Wakati uleule, Abu Bakr (a.s.) akasema: “Tayari nishatayarisha ngamia wawili kwa ajili yako na mimi mwenyewe.” Mtume (s.a.w.w.) akajibu akasema: “Niko tayari kuipokea zawadi hii kwa malipo.” Baada ya hapo alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) alipe bei ya ngamia yule.

Miongoni mwa maelekezo aliyoyatoa Mtume (s.a.w.w.) usiku ule kwenye lile pango la Thaur baadhi yake yalikuwa haya: “Katika siku ya kesho yake Sayyidna Ali (a.s.) atangaze wakati wa mchana kabisa na kwa sauti kuu kwamba kama mtu yeyote kaweka amana kitu chochote kile kwa Muhammad au kama yeye (Muhammad) alikuwa akidaiwa na mtu yeyote yule, watu hao wahusikao waje wachukue vitu vyao.”

Kisha alitoa maelekezo kuhusu kuondoka kwa ‘Fawaatim’ (neno lenye maana ya binti yake mpenzi Bibi Fatimah a.s na Fatimah binti Asad na Fatimah bint Zubayr) na akamwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) kuitayarisha safari yao pamoja na safari ya watu wengine wa ukoo wa Bani Hashim kwa kutegemea mwelekeo wao wa kuhajiri. Na kwenye tukio hili aliitamka sentensi aliyoitegemea Ibn Taymiyah kwa hoja yake ya kwanza. Alisema: “Ewe Ali! Tangu sasa watu hawa katu, hawataweza kukushinda nguvu.” Kama uwezavyo kuona, Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) kuvirudisha vitu vilivyowekwa amana kwake na watu, wakati ule ‘usiku wa mkesha’ umeishapita tayari. Amri hizi alizitoa akimpa Sayyidna Ali (a.s.) wakati yeye mwenyewe alikuwa akijitayarisha kutoka mle pangoni.

Halabi anaandika hivi: “Wakati usiku mmoja Ali alipokwenda mbele ya Mtume (s.a.w) kwenye Pango la Thaur, Mtume (s.a.w) akamwambia Ali pamoja na mambo mengine, kwamba awarudishie watu vitu walivyoviweka amana kwake (yeye Mtume s.a.w) na pia kuyalipa madeni yake.”

Kisha anayarudia yale maneno ya kwamba Ali hakukutana na Mtume (s.a.w.w.) baada ya ule usiku wa mkesha, lakini yeye mwenyewe halikubali hilo, na ananukuu kutoka kwa mwandishi wa kitabu ‘*Ad-Durr al-Manthur*’ kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alikutana tena na Mtume (s.a.w.w.) baada ya usiku wa kuhajiri.[17]

Kwa kifupi, Shaykh Tusi amewanukuu wanachuoni wategemewao wakisema kwamba amri ya kuvirudisha vitu vilivyowekwa amana kwa Mtume (s.a.w.w.) kwa wenyewe ilitolewa na yeye Mtume

(s.a.w.w.) baada ya ‘usiku wa mkesha’ hatuna haja kuyakana maelezo haya yaliyo sahihi na kujishughulisha katika kuwafurahisha watu.

Na kuhusu wale wanahistoria wa Kisunni kulinakili jambo hili katika jinsi ambayo kwa dhahiri hutoa dhana ya kwamba maelekezo yote yalitolewa na Mtume (s.a.w.w.) kwenye usiku mmoja ambao ni ule wa kuhajiri kunahitaji maelezo.

Kutoka Nje Ya Pango Lile

Kama alivyoelekeza Mtume (s.a.w.w.), Sayyidna Ali (a.s.) alipeleka ngamia watatu kule pangoni katika usiku wa nne pamoja na kiongozi wa kutumainiwa aliyeitwa ‘Urayqit’. Mtume (s.a.w.w.) aliisikia milio ya ngamia akatoka mle pangoni na yule sahaba wake. Waliwapanda wale ngamia na wakaondoka wakielekea Yathrib (Madina) kutoka upande wa chini wa mji wa Makka wakipitia njia ya pwani. Maelezo kamili ya safari hii yameandikwa kwenye vitabu vya historia.[18]

Ukurasa Wa Kwanza Wa Historia

Giza la usiku liliingia. Waquraishi waliokuwa wakizurura huko na huko mjini Makka na kwenye mazingira yake kumtafuta Mtume (s.a.w.w.), wakarudi majumbani mwao wakiwa wamechoka kabisa, na wakiwa wamepoteza matumaini yote ya kuipata ile zawadi kubwa sana (ya ngamia

100) iliyowekwa kwa ajili ya kumkamata Mtume (s.a.w.w.). Zile njia zinazoelekea Yathrib, zilizokuwa zimefungwa na wale walinzi waliowekwa na Waquraishi pia nazo zilifunguliwa[19] Katika wakati huu, sauti ya chini ya yule kiongozi aliyekuwa na ngamia watatu na chakula iliyafikia masikio ya Mtume (s.a.w.w.) na sahaba wake. Alikuwa akisema kwa sauti ya upole: “Ni muhimu kujinufaisha na giza la usiku huu na kutoka nje ya eneo liwezalo kufikiwa na watu wa Makka upesi iwezekanavyo na kuichukua njia isiyopitiwa na watu mara kwa mara.”

Historia ya zama za Uislamu huanza kwenye usiku huu hasa. Tangu hapo waliweka tarehe za matukio yote kufuatana na kalenda ya Hijiriya na kuyaandika kwenye historia kwa mujibu wa tarehe hiyo.

Kwa Nini Ule Mwaka Wa Hijra Ukawa Ndio Mwanzo Wa Historia Ya Kiislamu?

Uislamu ni dini ya kimungu iliyo kamili zaidi nayo inafuata dini ya Mtume Musa (a.s.) na Isa (a.s.) katika mfumo kamilifu zaidi unaofaa katika hali na mazingira yote. Uislamu umemletea mwanadamu neema. Ingawa Nabii Isa (a.s.) na kuzaliwa kwake ni vitu viheshimiwavyo mbele ya macho ya Waislamu, hawakuchukua kuzaliwa kwake kuwa chanzo cha zama zao, kwa kuwa wao ni taifa huru na lenye kujipambanua na isingalifaa kwamba wawafuate watu wengine katika kutwaa zama zao.

Kwa kipindi kirefu mwaka wa Ndovu (mwaka ambao Abraha alikuja Makka na jeshi la ndovu na kutaka

kuibomoa Ka'bah) ulitumiwa na Waarabu kuwa ndio chanzo cha historia, na kuzaliwa kwa Mtume (s.a.w.w.) nako kulitokea katika mwaka huo huo. Hata hivyo, Waislamu hawakuufanya mwaka ule kuwa ndio ukurasa wa kwanza wa historia ya Uislamu.

Mwaka wa Bi'that (kuteuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume) pia nao haukuchukuliwa kuwa mwanzo wa historia ya Waislamu, kwa sababu wakati ule hazikuwapo dalili za Uislamu na dini ya Kiislamu, na idadi ya Waislamu katika siku zile haikuzidi watatu. Hata hivyo, katika mwaka wa kwanza wa kuhajiri, Uislamu na Waislamu walineemeshwa kwa mafanikio makuu. Serikali huru ikapatikana mjini Madina.

Waislamu wakaondokana na kukosa maskani na kwa uhuru kabisa wakaweza kujikusanya katika sehemu muhimu. Hivyo basi, kutokana na mafanikio na ushindi huu, waliamua kuufanya mwaka ule kuwa ndio mwanzo wa historia yao.[20] Na hadi hivi sasa, wao huhesabu tarehe ya kila kitu, kilicho chema au kiovu kufuatana na mwaka huo.

Mpango Wa Safari Ya Kwenda Yathrib

Safari ambayo ilibidi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuichukua ilikuwa na umbali wa kiasi cha kilometa 400, na kuusafiri umbali huu kwenye joto kali la wakati wa kiangazi kulilazimu mpango ulio sahihi. Zaidi ya hapo, wao (yaani Mtume na masahaba zake) walikuwa pia wakiwaogopa Waarabu waliokutana nao njiani, kwani wangeliweza kuwapa Waquraishi taarifa za kule waliko, hivyo basi, walisafiri wakati wa usiku na wakapumzika wakati wa mchana.

Inaonekana kwamba mpanda ngamia mmoja baada ya kumwona Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake kwa mbali, aliwaendea Waquraishi upesi upesi na kuwaarifu juu ya njia ya safari ya Mtume (s.a.w.w.). Ili aweze kupata ile zawadi yeye peke yake, Saraqah bin Malik bin Ja'sham Madlaji aliwavunja moyo wenziwe katika kulifuatilia jambo lile na akawaambia kwamba wao (wale walioonwa na yule mpanda ngamia) walikuwa ni watu wengine. Kisha Saraqah akaja nyumbani mwake akazitwaa silaha zake, akampanda farasi mwenye mbio na upesi kwa kadiri ilivyowezekana akafika mahali alipokuwa amepumzika Mtume (s.a.w.w.) na sahaba zake.

Ibn Athir anaandika hivi:[21] "Hali hii ya mambo ilimfanya yule sahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ahuzunike mno, na ilimbidi Mtume (s.a.w.w.) amfariji tena kwa yale maneno: "Usihuzunike Allah Yu pamoja nasi." Saraqah alijivunia mno nguvu zake za kimaumbile na silaha kali na alikuwa tayari kabisa kuimwaga damu ya Mtume (s.a.w.w.) ili aipate ile zawadi kubwa sana waliyoiweka Waarabu.

Wakati huo huo Mtume (s.a.w.w.) alijiombea yeye mwenyewe na masahaba zake kwa moyo uliokuwa ukibubujika imani na matumaini na kusema: "Ee Allah! Tuokoe kutokana na uovu wa mtu huyu." Mara kwa ghafla yule farasi wa Saraqah akashtuka na kumtupa chini Saraqah kwa nguvu sana.

Saraqah alitambua ya kwamba mkono wa Allah ulikuwa ukifanya kazi na yale yaliyokuwa yakitendeka

pale yalitokana na nia mbaya aliyokuwa nayo dhidi ya Muhammad.22

Hapo akamgeukia Mtume (s.a.w.w.) katika hali ya kumsihi na akasema: “Ninakupa mtumwa wangu na ngamia wangu na niko tayari kufanya lolote lile upendalo.” Hapo Mtume (s.a.w.w.) akamjibu akasema: “Sina chochote nikitakacho kutoka kwako.”

Hata hivyo marehemu Allamah Majlis anasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: “Rudi na ukawazuie watu wengine na wasitufuate” Hivyo Saraqah alimwambia kila aliyekutana naye: “Hakuna dalili zozote za Muhammad kwenye njia hii.”23

Waandishi wa Kisunni na Kishia wameinukuu miujiza iliyotendwa na Mtume (s.a.w.w.) wakati wa safari yake ya kutoka Makka kwenda Madina. Hata hivyo, ili kupunguza maneno, tunaacha kuisimulia.

Kuwasili Kwenye Kijiji Cha Quba

Kijiji cha Quba kilikuwa kiasi cha ligi mbili (kilomita 10 hivi) kutoka Madina. Kijiji hiki kilikuwa makao makuu ya Bani ‘Amr bin Auf’. Mtume (s.a.w.w.) na masahaba wake walifika kijijini hapa siku ya Jumatatu na akafikia nyumbani kwa Kulthum Ibnul Hadim, chifu wa kabila lile. Idadi fulani ya ‘Muhajir’ (wahamaji) na ‘Ansar (wasaidizi) walikuwa wakisubiri kuwasili kwa Mtume (s.a.w.w.).

Mtume (s.a.w.w.) alikaa kijijini pale hadi mwishoni mwa juma lile na katika wakati huu aliweka jiwe la msingi la msikiti kwa ajili ya kabila la Bani Awf. Baadhi ya watu walishikilia ya kwamba aendelee na safari yake ya kwenda Madina upesi iwezekanavyo. Hata hivyo, yeye alikuwa akimsubiri binamu yake Sayyidna Ali (a.s.) afike.

Baada ya kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) Sayyidna Ali (a.s.) alisimama mahali fulani mjini Makka na akasema: “Yeyote aliyeweka amana kitu kwa Muhammad na aje akichukue kutoka kwangu.” Wale waliohusika walikuja kuchukua vitu vyao baada ya kutoa maelezo ya utambulisho wa vitu vyao. Baada ya hapo, kufuatana na maelekezo ya Mtume (s.a.w.w.), Sayyidna Ali (a.s.) aliwachukua wanawake wa Bani Hashim na kwenda nao Madina ikiwa ni pamoja na Bibi Fatimah (a.s.), binti wa Mtume (s.a.w.w.) na mama yake Bibi fatimah bint Asad, na vile vile wale Waislamu ambao hadi wakati ule, walikuwa bado hawajaweza kuhama. Sayyidna Ali (a.s.) aliifuata njia ya ‘Dhi Tuwa’ na akaelekea Madina wakati wa usiku.24

Shaykh Tusi anaandika hivi:25 “Wapelelezi wa Waquraishi walipata habari za kuhajiri kwa Sayyidna Ali (a.s.) na kikundi chake. Hivyo wakamfuata na wakakutana naye uso kwa uso kwenye eneo la ‘Zajnaan’. Walibadilishana naye maneno makali. Wakati ule vilio vya wanawake vilifika angani. Sayyidna Ali (a.s.) alitambua ya kwamba hakuwa na uchaguzi wowote mwingine ila kuihami heshima ya Uislamu na Waislamu. Hivyo basi, aliwageukia wale wapinzani wake na akasema: “Yeyote apendaye kwamba mwili wake ukatwe vipande vipande na damu yake imwagwe, basi na ajitokeze.” Dalili za ghadhabu ziliweza kuonekana usoni mwake. Wale mawakala wa Waquraishi walihisi kwamba sasa jambo lile lishakuwa

zito. Hivyo, wakachagua kufanya mapatano na wakaishika njia waliyoijia (wakarudi makwao).”

Ibn Athir anaandika hivi: “Ali alipofika Quba, miguu yake ilikuwa ikitoka damu. Mtume (s.a.w.w.) alielezwa kwamba Ali amefika, lakini hakuwa katika hali ya kuweza kufika mbele yake.

Mtume (s.a.w.w.) alikwenda upesi kule alikokuwa Ali na akamweka mapajani mwake na alipoiona hali ile ya miguu ya Ali ilivyovimba alianza kutiririkwa na machozi machoni mwake”.26 Mtume (s.a.w.w.) alifika Quba tarehe 12 Rabiul–Awwal na Sayyidna Ali (a.s.) alijiunga naye hapo katikati ya mwezi huo huo.27

Maoni haya yanaungwa mkono na Tabari kwa kusema hivi: “Ali alibakia Makka kwa muda wa siku tatu baada ya kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) na katika kipindi hiki aliwarudishia watu vitu vyao walivyoviweka amana (kwa Mtume (s.a.w.w.).28

Makelele Na Hoihoi Za Shangwe Mjini Madina

Kulikuwa na msisimko na shangwe miongoni mwa watu waliomwamini Mtume (s.a.w.w.) miaka mitatu ilioyopita na kumpelekea wawakilishi wao kila mwaka na kulitumia jina lake takatifu kila siku kwenye sala zao, pale walipopata taarifa ya kwamba kiongozi wao mkuu amefika kiasi cha mwendo wa ligi mbili tu na alitegemewa kuingia mjini mwao karibuni. Jinsi fikara na hisia zao zilivyokuwa, haziwezi kuelezwa kwa maneno.

Ansar walikuwa na kiu ya Uislamu na mpango wake mtukufu na wenye kuimarisha. Ili kuutoharisha mji wa Madina kutokana na ibada ya masanamu walikuwa wameshayachoma masanamu na kuziondoa dalili zote za ibada ya masanamu kutoka majumbani, mitaani na katika masoko ya mjini mle. Ingalifaa kama tungalinukuu hapa mfano wa moyo wa kupenda waliouonyesha Ansar katika Uislamu.

‘Amr bin Jumuh, aliyekuwa mmoja wa machifu wa kabila la Bani Salmah, alikuwa kaweka sanamu nyumbani mwake. Ili kumfanya atambue kwamba sanamu la mti ni kitu kisicho na faida yoyote, wanaume wa kabila lake walilichukua na kulitupa chini kwa kulipindua pindua juu chini; chini juu, katika shimo ambalo siku zile lilikuwa likitumika kwa kwendea chooni. Aliamka asubuhi yake na baada ya kulitafuta sana aliliona sanamu lile kwenye lile shimo. Aliliokota, akalisafisha na akalirudisha mahali pale. Mchezo huu ulirudiwa rudiwa kwa mara nyingi. Mwishowe ‘Amr aliufunga upanga shingoni mwa sanamu lile na akasema: “Kama wewe ndiwe chanzo cha nguvu yoyote ile hapa ulimwenguni, basi jihami.”

Hata hivyo, siku moja alilikuta sanamu lile kisimani likiwa limefungwa kwenye kiwiliwili cha mbwa aliyekufa, nalo halikuwa na ule upanga. Alipoyaona matukio haya, alitambua ya kwamba cheo cha mwanadamu kilikuwa kikuu zaidi kuliko kwamba yeye ainamishe kichwa chake mbele ya jiwe, mti au matope. Kisha akasoma beti fulani ambazo lengo lake ni hili: “Ninaapa kwa jina la Allah! Kama wewe ungelikuwa u mungu wa kweli, usingalilala kisimani ukiwa umefungwa kwenye mzoga wa mbwa. Sifa zote njema zamstahiki Allah Ambaye anamiliki neema zote. Yeye ndiye Mwingi wa rehema na Mwenye kustawisha na Mwenye kulipa thawabu. Yeye ndiye atupaye wokovu kabla ya kupelekwa kwetu

kaburini."[29]
Mtume (s.a.w.w.) aliendelea na akaingia Madina. Aliposhuka kutoka juu ya ngamia wake mahali paitwapo Thaniyatul Widaa' na mnyama yule akauweka mguu wake kwenye ardhi ya Yathrib, watu wakamkaribisha kwa mikono miwili na kumsalimu na wakaanza kuimba nyimbo za furaha wakisema:

"Mwezi umechomoza kutoka 'Thaniyatul Widaa'. Ni wajibu wetu kuwa wenye shukrani kwa baraka hizi hadi katika siku ambayo hakuna hata mtu mmoja usoni mwa ardhi asiyemwomba Allah na kumabudu. "Ewe uliyeletwa na Allah kwa ajili ya mwongozo wetu! Ni muhimu kwetu sisi sote kuzitii amri zako."

Kabila la Bani 'Amr bin Awf lilishikilia ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) abakie pale Quba, na wakasema: "Sisi ni watu wenye bidii nyingi, madhubuti na mashujaa." Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakulikubali hilo. Wakati watu wa makabila ya Aws na Khazraji walipotambua kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) walichukua silaha na wakaharakisha kwenda kumpokea Mtume (s.a.w.w.).

Alipokuwa akiendelea na safari yake watu walimzunguka ngamia wake na machifu wa makabila wakazishika hatamu zake.

Kila mmoja wao alishikilia kwamba Mtume (s.a.w.w.) akae kwenye eneo lake, lakini aliwajibu wote akisema: "Musimzuie huyu ngamia. Mimi nitashuka popote pale atakapopiga magoti." Yule ngamia alisimama na kukunja magoti yake kwenye uwanja mpana uliokuwa mali ya wavulana wawili yatima walioitwa Sahl na Suhayl waliokuwa wakiishi chini ya ulinzi na ulezi wa As'ad bin Zurarah[30] Uwanja huu ulikuwa ukitumika kwa kukaushia tende na kilimo, nyumba ya Abu Ayub ilikuwa karibu na uwanja huu.

Hivyo basi mama yake (Abu Ayub) akaitumia nafasi ile na akaichukua mizigo ya Mtume (s.a.w.w.) nyumbani kwake. Hivyo yakaanza mashindano na maombi ya kumchukua Mtume (s.a.w.w.), hata hivyo, yeye aliyamaliza mashindno yale na akasema: "Iko wapi mizigo yangu?" aliambiwa kuwa ilichukuliwa na mama yake Abu Ayub na kuipeleka nyumbani kwake. Hapo akasema: "Mtu na aende kule iliko mizigo yangu." Na As'ad bin Zurarah alimchukua ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) na kumpeleka nyumbani kwake.

Mbegu Ya Mfarakano

Abdullah bin Ubay anachukuliwa kuwa yu chifu wa msonge wa madaraka wa wanafiki. Kabla ya watu wa Madina kufanya mapatano na Mtume (s.a.w.w.) waliamua kumchagua Abdullah bin Ubay kuwa mtawala wao kwa wote pamoja. Hata hivyo, kutokana na kuendelea kwa uhusiano baina ya Mtume (s.a.w.w.) na Aws na Khazraji, uamuzi huu ulikoma, na tangu hapo Abdullah akawa na mfundo dhidi ya huyu kiongozi mkuu wa Uislamu naye hakumwamini hadi kwenye dakika za mwisho za uhai wake. Alipoyaona yale mapokezi aliyopewa Mtume (s.a.w.w.) na watu wa makabila ya Aws na Khazraji, alipatwa mno na wasiwasi na hakuweza kujizuia kuitamka sentensi yenye kukidhihirisha kabisa kijicho na uadui wake dhidi ya Mtume (s.a.w.w.). Aliugeuzia uso wake kwa Mtume (s.a.w.w.) na akasema: "Nenda kwa wale watu waliokupokea na usitudanganye sisi hapa."[31]

Sa'ad bin Ubadah, akichelea ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) atayachukulia maneno yake kuwa ya kweli (yaani kuyaona kuwa ndio hisia za Ansar wote) au kuyaweka moyoni, aliomba radhi kwa maneno yake yale na akamwambia Mtume (s.a.w.w.): "Ameyazungumza maneno haya kutokana na mfundo na kijicho, kwa sababu iliamuliwa ya kwamba awe mtawala pekee wa Aws na Khazraji na sasa, kutokana na kuja kwako, utawala wake umekuwa si jambo lenye kufikiriwa tena"

Kwa ujumla wanahistoria wanasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliwasili Madina mnamo siku ya Ijumaa na akaisali sala ya Ijumaa pamoja na masahaba zake mahali palipokuwa kwenye eneo la watu wa kabila la Bani Saalim.
Hapa alitoa hotuba yenye ufasaha iliyoibua hisia kali nyoyoni mwa watu ambao hawajapata kuyasikia maneno ya namna hiyo hapo kabla. Maandiko na hotuba hii yamenukuliwa na Ibn Hisham,32 Miqrizi kwenye *Amtaa'ul Asmaa'* na Allamah Majlisi.33 Hata hivyo, maneno na maelezo yaliyomo kwenye hotuba hiyo, kama yalivyonakiliwa awali ni tofauti na yale yaliyonukuliwa na Allamah Majlis.

1. Tabaqaatul Kubraa, Juzuu 1, uk. 222 –228; na Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 480 – 482
2. Tabaqaatul Kubraa, uk. 228; na Tarikhut–Tabari, Juzuu 2, uk. 100.
3. Siiratu Halabi, Juzu 2, uk. 32.
4. A'lamu wara, uk. 39; na Bihaarul An'waar, Juzuu 19, uk. 50.
5. Rai hii ndio tuichaguayo sisi, kwani ikumbukwe kuwa kuhama kwa Mtume (s.a.w.w.) kulikuwa ni siri nzito ambayo haikupasa kabisa maadui angalau kuweza kuinusa ukiachia mbali kuigundua, hivyo uzito wa siri ulipasa kuafikiana na uzito wa hatari, na kwa mantiki hiyo ilipasa siri hii aijue yule tu aliye mwaminifu kwa mujibu wa wahyi, naye si mwingine ni Ali (a.s.). Hivyo kwetu sisi rai hii ndio yenye nguvu – Mhariri.
6. Ta'rikhut–Tabari, Juzuu 2, uk. 100.
7. Lakini waweza kupima kati ya ubora huo utokanao na kitendo cha kusuhubiana na Mtume pangoni, na ule utokanao na kitendo cha kuchukua nafasi ya Mtume kitandani kwake ili adui anayekusudia kumuuwa Mtume amuuwe yeye kwa kud–hani yule aliyelala pale ndiye Mtume. Bila shaka wa pili ni bora zaidi mara dufu kuliko wa kwanza – Mhariri.
8. Tabaqaatul–Kubra, Juzuu 1, uk. 229 n.k. wengi wa waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) wameunukuu muujiza huu. Hata na yale tuliyokwisha kuyasae– ma juu ya miujiza kuhusiana na masimulizi juu ya Abraha haionekani kwamba ni jambo lenye kufaa kwamba bila ya kuwapo haja yoyote ile tuelezee au tusahihishe silsila hii ya muujiza.
9. Kwenye Sharh–i Nahjul Balagha ya Ibn Abil Hadid fadhila hii ya Sayyidna Ali (a.s.) imetajwa kwa maneno yenye kufaa (kwenye Juzuu 13, uk. 262.)
10. Samrah bin Jundab alikuwa mmoja wa watenda majinai wa zama za Bani Umayyah. Hakuyabadili mambo kwa kadiri tulivyoitaja hapo juu tu, bali kama ilivyoelezwa na Ibn Hadid aliongeza mambo fulani fulani kwenye habari hizo na akasema kwamba kile hasa kilichofunuliwa juu ya Ali kilikuwa ni aya hii ifuatayo: "Na miongoni mwa watu yuko yule ambaye kauli yake kuhusu maisha ya dunia hii inakustaajabisha, naye humshuhudilisha Allah yale yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye yu mpinzani mkubwa zaidi" (Sura al–Baqarah 2:204.)
Kwenye zama za ugavana mkuu wa wa Ziyaad bin Abih nchini Iraq, Samrah alikuwa gavana wa Basrah. Moja ya majinai ya mtu huyu ni kwamba aliua Waislamu na wachamungu wafuasi wa nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) elfu nane. Na Ziyaad alipotaka maelezo yake na alipomwuliza: "Vipi wewe ulipata moyo wa kuwauwa watu wote hawa? Je, haikupita akilini mwako ya kwamba inawezekana kwamba miongoni mwao wamo watu wasio na makosa?" Samrah alijibu akisema "Sitajali kuuwa hata zaidi yao hawa." Matendo yake yaaibishayo ni mengi mno kiasi cha kutoweza kuwekwa kwenye kurasa hizi. Mtu huyu mkai– di alikuwa ndiye yeye yule aliyeyakataa maagizo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) juu ya kuziheshimu haki za jirani, na Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: "Wewe ni mtu mwenye madhara na Uislamu hauruhusu ya kwamba mtu awatendee wenzi– we madhara au ayavumilie madhara kutoka kwao."
11. Kabla yake Jahiz aliitaja sehemu tu ya ukanusho huu kwenye kitabu chake kiitwacho 'Al–Uthmaniyah'. Tafadhali rejea juu ya jambo hili kwenye Sharhi Nahjul Balagha, cha Ibn Abil Hadid, Juzuu 13, uk. 262.

12. Kwa mfano sentensi hii haikutajwa mwenye Tabaqaatul Kubra uk. 227 – 228. Mwandishi wake alizaliwa katika mwaka 168 Hijiriya na akafariki dunia katika mwaka 238 Hijiria. Maqrizi nae hakuitaja mwenye kitabu chake. 'Al– Imta'a'.
13. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 72.
14. Tarikhut– Tabari, Juzuu 2, uk. 99.
15. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 483.
16. Tarikhul Kamil, Ibn Athir, Juzuu 2, uk. 73.
17. Siiratu Halabi, Juzuu 2, uk. 37.
18. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 491; Tarikhul Kamil, juzuu 2, uk. 75 na mwenye maelezo ya chini ya ukurasa ya Ta'rikh Ibn Athir.
19. Ta'rikhut–Tabari, Juzuu 2, uk. 104.
20. Ibn Waazih Akhbari anaandika mwenye kitabu chake cha Historia kiitwacho 'Ta'rikhu Yaqubi' kwamba kwenye mwaka wa 16 wa Hijiria khalifa wa pili alid– hamiria kuweka mwanzo wa historia ya Waislamu. Alitaka iwe ile tarehe ya kuza– liwa Mtume (s.a.w.w.) au tarehe ya kuteuliwa kwake kuishika kazi ya Utume, lakini Ali (a.s.) hakukubaliana na maoni yake na akasema kwamba kuhajiri kuwe ndio mwanzo wa historia ya Kiislamu. (Ta'rikh Yaqubi, juzuu 2, uk. 135.)
21. Ta'rikh Kamil, juzuu 2, uk. 74.
22. Wengi wa waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w) kama vile Ibn Athir (Tarikh Kamil, Juzuu 2, uk. 74) na Majlis (Bihaar Anwwar, Juzuu 9, uk. 88) wamelinuku tukio hili, kama tulivyolielekeza hapo juu, kutokana na asili yake itegemekayo. Hata hivyo, mwandishi wa 'Hayatu Muhammad' anasema: "Saraqah aliyachuku– lia matukio haya kuwa ni ndege mbaya na akafikiria ya kwamba miungu ilikuwa ikitaka kumzuia asiitende kazi ile.
23. Bihaar Anwar, Juzuu 19, uk. 75.
24. Baadhi ya wachambuzi wetu waaminifu hawakubaliani na kauli hii ya Imam Ali (a.s.) kuhama kwa msaada wa giza la usiku, na hivyo kiakili na kihistoria wanathibitisha ya kwamba alihama mchana peupe na kwa tangazo la wazi dhahiri shahiri bila kuficha kuwa yeye anahama kumfuata Mtume (s.a.w.w.), na yeyote awezaye kumzuia basi aweze kujitokeza kujaribu hilo. Ni kweli kabisa hiyo ndio hali ya kawaida ya yule simba wa Mungu asiyeshindwa, na ndio kauli yenye nguvu kwetu – Mhariri.
25. Amaali, uk. 300.
26. Tarikhul–Kamili, Juzuu 2, uk. 75.
27. Imtaa'ul Asmaa', uk. 48
28. Tarikhut–Tabari, Juzuu 1, uk. 106.
29. Usudul Ghabah, Juzuu 4, uk. 99.
30. Bihaarul Anwaar, Juzuu 19, uk. 108, lakini kwa mujibu wa baadhi ya vitabu, ikiwa ni pamoja na Tarikh–i Kamil, walikuwa chini ya ulezi wa Mu'aaz bin 'Afraa'.
31. Bihaarul Anwaar, Juzuu 19, uk. 108.
32. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 500–501.
33. Bihaarul Anwwar, Juzuu 19, uk. 126.

Sura Ya 26: Matukio Ya Mwaka Wa Kwanza Wa Hijiriya

Nyuso za Ansar zenye furaha na shauku, na makaribisho ya moyo mkunjuvu ambayo watu wa makabila ya Aws na Khazraji walikuwa wamempa Mtume (s.a.w.w.) yalimshawishi kujenga kituo cha ustawi wa jamii kwa ajili ya Waislamu kabla ya kufanya jambo lolote jingine, kituo hiki kiliitwa *'Masjid'* (Msikiti) ili

kitumike kwa kufanyia mambo ya maelekezo, maendeleo, siasa na haki.

Na kwa vile kuwaita watu kwenye ibada ya Mungu Mmoja tu na Mlezi, lilikuwa ndilo jambo la kwanza kwenye mpango huu, alifikiria kwamba lilikuwa ni jambo muhimu kwanza kabisa, kujenga maabadi ambamo Waislamu wangeliweza kujishughulisha humo katika kumdhukuru Allah na kulisabihi Jina Lake wakati wa kusali. Vile vile ilikuwa muhimu kwamba aunde kituo ambamo watu wa kawaida wa kundi la Kiislamu (kundi la Allah) waweze kukutana humo kila juma katika siku maalum iliyowekwa na kufanya mijadala na mashauriano juu ya maslahi ya Uislamu na Waislamu, na zaidi ya kukutana kila siku waweze kusali sala za Idi humo mara mbili kwa mwaka.

Msikiti haukuwa tu kituo cha ibada bali vile vile ulikuwa ndiyo sehemu ambamo kila aina ya maelekezo ya Kiislamu na amri ziliweza kutolewa, na kila aina ya elimu ya kidini na kisayansi iliweza kufundishwa, ikiwa ni pamoja na kusoma na kuandika. Hadi mwanzoni mwa karne ya nne ya Kiislamu misikiti ilitumika kama shule zilizokuwa zikifanya kazi nyakati zote, ila ile iliyotengwa kwa sala tu. Baada ya hapo taasisi za kielemu zilichukua sura maalum. Wengi wa wanachuoni wakuu walihitimu kutoka kwenye vituo vya elimu vilivyojengwa kwenye misikiti.

Kwa kipindi fulani Msikiti wa Madina ulichukua sura ya kituo cha masomo pia. Washairi wakuu wa Uarabuni ambao tungo zao zililandana na mafundisho ya maadili na kielemu ya Uislamu waliweza kuzisoma beti zao mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Ka'ab bin Zuhayr alilisoma shairi lake maarufu la kumsifu Mtume (s.a.w.w.) mbele ya Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe msikitini na akapata zawadi kubwa na joho la heshima kutoka kwake. Hassan bin Thabit, aliyeihami heshima ya Uislamu kwa njia ya beti za mashairi yake alikuwa na kawaida ya kuyasoma mashairi yake kwenye Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.).

Mikutano ya kielimu kwenye Msikiti wa Madina, katika zama za Mtume (s.a.w.w.), ilivutia mno kiasi kwamba wawakilishi wa kabila la Saqaf walivutiwa mno na mandhari ile; walishangazwa na shauku waliyokuwa nayo Waislamu katika kuitafuta elimu. Mambo ya kisheria na daawa yaliamuliwa, na humo msikitini adhabu zilitolewa kwa wale waliokosa, nao ulitumika kwa nia na makusudio maalum na baraza la kisheria ambamo malalamiko ya watu yalitatuliwa.

Zaidi ya hapo, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akitoa hotuba zenye kuamsha hisia za watu msikitini humo ili kuwafanya watu wafanye jitihada na kampeni dhidi ya ukafiri. Inawezekana kwamba moja ya siri za kuunganisha mambo ya kidini na kielimu msikitini ilikuwa kwamba yule kiongozi wa Kiislamu alitaka kuonyesha kivitendo kwamba elimu na dini, kila kimoja kinakamilisha kingine, na kama sehemu fulani ni kituo cha kidini, basi ni lazima vile vile iwe kituo cha elimu na hekima.

Na kama mambo ya kisheria na mengineyo, yakiwemo mambo yahusianayo na jihadi yaliweza kuamuliwa katika msikiti, hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya kwamba alitaka kudhihirisha ya kwamba dini yake si dini ya kiroho tu isiyokuwa na uhusiano wowote na mambo ya kidunia, bali ni dini ambayo inapowatia watu kwenye uchamungu na dini, vile vile haiyadharau mambo ya kidunia na ustawi wa jamii.

Upatanifu huu (baina ya elimu na dini) ni hamasa ya Waislamu hata katika siku zetu hizi. Wakati vituo

vya kielimu vyenye sura maalum vilipojengwa daima shule na vyuo vikuu viliasisiwa kando kandoni mwa Msikiti mkuu ili kuuthibitishia ulimwengu kwamba vitu hivyo viwili vya ustawi wa jamii havitengani.

Kisa Cha Ammaar

Pale mahali ambapo ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) alipopiga magoti palinunuliwa kwa dinari kumi kwa ajili ya ujenzi wa msikiti. Waislamu wote walishiriki katika ujenzi wa msikiti huo na katika ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi, na hata Mtume (s.a.w.w.) alikusanya mawe pamoja na masahaba wake. Usayd bin Huzayr alikwenda mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na kusema: "Ewe Mtume wa Allah! Niruhusu nilinyanyue mimi (hilo jiwe)." Mtume (s.a.w.w.) akamjibu akasema: "Nenda ukalete jingine." Kwa jinsi hii alionyesha kidokezo cha tabia yake tukufu. Alisema: "Mimi ni mtu nifanyaye mambo kwa vitendo. Mimi ni mtu wa vitendo wala si wa maneno tu." Katika tukio hilo, Muslim alisoma beti fulani za shairi zenye maana ya: "Kama tukikaa chini, na Mtume akafanya kazi, itakuwa ni chanzo cha upotofu na uovu kwa upande wetu."

Mtume (s.a.w) na Waislamu walipokuwa wakiifanya kazi hii walikuwa wakitamka maneno haya: "Maisha ya kweli ni maisha ya Akhera. Ewe Allah! Wahurumie Ansar na Muhajiriin."

Uthman bin Maz'un alikuwa mchungu sana kuhusu unadhifu wa nguo zake na alitaka kuiweka nguo yake katika hali ya usafi. Hivyo basi, yeye hakushiriki katika ujenzi wa msikiti, ili nguo yake isije ikaingia mavumbi. Sayyidna Ali (a.s.) alimlaumu kwa maneno haya: "Mtu ajengaye msikiti, akiwa amekaa au amesimama, daima yu mwenye kujitahidi kwa ajili ya maendeleo yake si kama yule ajitengaye na vumbi naye hayuko tayari kuzitia doa nguo zake katika kujenga Msikiti.[1]

'Ammar Yasir, ambaye alikuwa mtu mwenye nguvu, alikusanya mawe kwa ajili ya ujenzi wa msikiti na kuyapeleka kule ufanyikapo ujenzi. Baadhi ya watu walijinufaisha visivyostahili kutokana na upole wake na kumtwisha mawe yaliyokuwa mazito mno kwake. Alisikika akisema: "Na nyanyua jiwe moja kwa ajili yangu mwenyewe na jingine kwa ajili ya Mtume (s.a.w.w.)." Siku moja Mtume alimwona akibeba mzigo mzito, wakati alipokuwa katwishwa mawe matatu. 'Ammaar alilalamika akisema: "Masahaba zako wana nia mbaya dhidi yangu na wanataka kuniua.

Wao wenyewe wanaleta jiwe moja moja lakini mimi wananitwisha mawe matatu." Mtume (s.a.w.w.) alimshika mkono, akamfuta vumbi mgongoni mwake, na akatamka maneno haya ya kihistoria: "Wao sio wauwaji wako. Utauawa na kundi la madhalimu utakapokuwa ukiwaita kwenye haki na ukweli."[2]

Utabiri huu ni moja ya thibitisho za Utume na ukweli wa Mtume (s.a.w.w.). Hatimaye jambo hilo alilolitabiri Mtume lilitimia kweli, kwa sababu 'Ammar, aliyekuwa pamoja na Imamu Ali (a.s.) Amiri wa Waumini kwenye vita vya Siffin na wakati ule alikuwa na umri wa miaka 90 aliuawa mikononi mwa wafuasi wa Mu'awiyah. Taarifa hii ya fumbo iliendelea kuwa na athari za ajabu kwa 'Ammar katika kipindi chote cha uhai wake. Baada ya tukio hili Waislamu walimfikiria 'Ammar kuwa yu kiini cha ukweli na kila ukweli ulikuwa ukipimwa kwa uhusiano wake na 'Ammar.

Alipouawa ‘Ammar kwenye vita vile, makelele ya kushangaza yalitokea miongoni mwa watu wa Sham. Watu waliokuwa na shaka juu ya ukweli wa Sayyidna Ali (a.s.) kutokana na propaganda yenye sumu ya Mu’awiyah na Amr bin Aas, walipata mwanga. Huzaymah bin Thabit Ansar alikwenda kwenye vita vile pamoja na Imamu Ali (a.s.), lakini alichanganyikiwa kuhusu kushiriki kwake katika vita vile. Hata hivyo, aliposikia ya kwamba ‘Ammar ameuawa aliuchomoa upanga wake na kuanza kuwashambulia watu wa Shamu.

Dhul Kulaa’ Himyari akifuatana na watu ishirini elfu wa kabila lake walikuja kupigana dhidi ya Sayyidna Ali (a.s.). Mtu huyu alikuwa na msaada alioutegemea sana Mu’awiyah, naye Mu’awiyah hakuamua kupigana vita hadi alipopata uhakika wa kushirikkiana naye.
Chifu huyu aliyepotoshwa alipotambua ya kwamba ‘Ammar bin Yasir alikuwa pamoja na Sayyidna Ali (a.s.) alichanganikiwa mno. Makachero wa Mu’awiyah walijaribu kuyafanya mambo kuwa yenye kutia shaka kwa chifu huyu, na wakasema: “Hakuna suala lolote kuhusu ‘Ammar kuwapo Siffin.

Watu wa Iraq hawajali kuhusu kuzusha uwongo kama huo.” Hata hivyo Dhul Kalaa’ hakushawishika. Alimgeukia Amr Aas na kumwuliza “Je, Mtume hakusema maneno haya na haya kuhusu Ammar?” Ibn Aas akamjibu akasema: “Ndio, alisema hivyo, lakini kwa hakika ‘Amar hayuko kwenye jeshi la Ali.” Akasema: “Nitalichunguza jambo hili mimi mwenyewe.” Kisha aliwatuma watu fulani kuithibitisha hali hiyo. Mu’awiyah na ‘Amr bin Aas walitambua katika hali hii ngumu kuwa kama Dhul Kalaa atagundua kuwako kwa Ammar kwenye jeshi la Ali au juu ya kuuawa kwake kishahidi akiwa kwenye huduma ya Ali, waweza kutokea mgawanyiko kwenye jeshi la watu wa Shamu. Hivyo basi, kwa kulizuia hili, huyu chifu maarufu wa Syria aliuawa kwa njia isiyoeleweka.[3]

Hadithi hii ni maarufu mno miongoni mwa wanachuoni wa Hadithi wa kawaida na wale walio maarufu zaidi kiasi kwamba haihitaji kunukuliwa hapa taarifa yoyote ya kulithibitisha jambo hili. Ahmad bin Hanbal amenakili hivi: “Alipouawa ‘Ammar katika vita vya Siffin, Amr bin Hazm alimjia ‘Amr bin Aas na kumwambia: “Ammar ameuawa, na Mtume alisema kuhusiana naye kwamba kikundi cha madhalimu kitamwua.” Amr bin Aas alilia na akaisoma aya isemayo: **“Sisi tunatoka kwa Allah na Kwake tutarejea.” (2:156)** na akampasha Mu’awiyah taarifa hii. Mu’awiyah akasema: “Sisi si wauaji wa ‘Ammar. Yeye ameuawa na Ali na marafiki zake, waliokuja pamoja naye na wakamweka mbele ya panga zetu.”[4]

Hata hivyo, ni dhahiri kwamba tafsiri hii ya uwongo iliyotolewa na Mu’awiyah, mwana wa Abu Sufyani ili kuzipumbaza akili za askari wa Shamu haiwezi kukubalika hata kidogo katika baraza la Allah Mwenye nguvu zote, na kila mtu mwenye hekima anaweza kuelewa vizuri ya kwamba hoja yake haina msingi hata kidogo.

Yaya Mwenye Huruma Zaidi Kwa Mtoto Kuliko Mama Yake.

Hatukuweza kupata sentensi iliyo bora zaidi ya hii ili kuionyesha tabia ya mwanahistoria[5] wa karne ya nane Hijiriya aliyechagua kumuunga mkono Mu’awiyah na kuandika hivi:

“Si muhimu kwamba, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) amewataja wauaji wa ‘Ammar kuwa madhaalimu, basi wawe ni makafiri kweli, kwa sababu ingawa wameichagua njia isiyo sahihi na wakapigana dhidi ya Ali, lakini kwa vile waliichukua hatua hii kuhusiana na dini yao katika usahihi wa kitendo chao (Ijtihaad), hivyo haiwezekani kuibatilisha au kuwaita makafiri.”

Anaongezea kusema hivi: “Alichomaanisha Mtume kwa yale maneno yasemayo: “Ammaar anawaita Peponi, lakini wale wauaji wa ‘Ammar wanamwitia Motoni ni kwamba, Ammar anawaita kwenye kuushuhudia Upweke wa Allah na kuungana (na hii ndio hiyo pepo yenyewe), lakini wauaji wa ‘Ammar wanajitahidi kumpa Mu’awiyah ubora kuliko Ali, ambaye anastahili zaidi kuwa khalifa, na hivyo basi wanaunda utawala kwenye kila moja ya mikoa ya Kiislamu na matokeo yake ni kwamba unakuwapo ufa mpana mno miongoni mwa Waislamu, ingawa wao wenyewe wanaweza kuwa hawakutambua ya matokeo kama hayo (na huo ndio Moto wenyewe).”

Kwa kadiri tutakavyofikiria kuhusu ni jina gani tuipe tafsiri hii, hatuwezi kulipata jina lolote lile lifaalo ila lile la kuzibatilisha mambo. Licha ya ujuzi kiasi hiki waliokuwanao kikundi hiki cha watu wenye kuasi katika kubatilisha na kugeuza mambo na kuyafanya yawe uwongo, hawakuweza kuukana utabiri uliotabiriwa juu yao na Mtume (s.a.w.w.), na wanahistoria kama Ibn Kathir wameifanya kazi ya yaya aliye na huruma zaidi kwa mtoto kuliko mama wa mtoto yule, na wakakimbilia kwenye kuubadili ukweli ambao wao wenyewe hawakuwa wakiutambua.
Ahmad bin Hanbal anasema: “Watu wawili walimjia Mu’awiyah na kila mmoja wao alidai kwamba amemua ‘Ammar. Mwana wa Amr bin Aas (Abdullah) akasema: “Mmoja wenu ambakishe mwenziwe kwa kuwa nilimsikia Mtume akisema kwamba ‘Ammar atauawa na kikundi cha madhalimu.”

Mu’awiyah akamwambia Abdullah: “Kama sisi ni kikundi cha madhalimu, basi ni kwa nini umejiunga nasi?” Akamjibu akisema: “Siku moja baba yangu ‘Amr alilalamika dhidi yangu kwa Mtume (s.a.w.w.) na Mtume akaamrisha nimtii baba yangu. Hivyo basi, mimi niko pamoja nawe lakini sipigani.[6]

Udhuru wa Abdullah ni kama tafsiri ya Ibn Kathir asemaye kwamba Mu’awiyah alipigana vita vile kwa msingi wa ijtihad na imani, ingawa upo ukweli kwamba alikosea katika (kuifanya) ijtihad yake hii,[7] kwa sababu mtu kumtii baba yake ni muhimu pale tu inapokuwa matokeo yake sio ya kuiasi sheria ya dini. Qur’ani Tukufu inasema: “**. . .Na ikiwa watakushikilia unishirikishe Mimi na usiyokuwa na ujuzi nayo, basi usiwatii……” (*Sura al-Ankabut*, 29:8)**.

Hali kadhalika ijtihad (kutoa maoni yake mtu) ni sahihi pale tu yanapokosekana masimulizi ya dhahiri ya Mtume (s.a.w.w.), vinginevyo ijtihad ya watu kama vile Mu’awiyah na ‘Amr bin Aas, yenye kuipinga Hadith ya dhahiri ya Mtume (s.a.w.w.) si sahihi na ni batili. Na kama mlango wa ijtihad uko wazi katika hali hiyo, itakuwa muhimu kwetu kuwasamehe washirikina na wanafiki wote kwa kufanya kampeni dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) na Uislamu, na vile vile hatuna budi kusema kwamba watu kama vile Yazid na Hajjaj walikuwa na haki katika kuimwaga damu ya watu wachamungu na wasio na makosa wa taifa hili, na vile vile walikuwa na haki ya kupata malipo mazuri kwa kitendo chao hicho.Ujenzi wa msikiti ulimalizika na kila mwaka eneo lake lilipanuliwa. Vile vile palitengenezwa mahali penye mwinuko

kandoni mwa msikiti ule kwa ajili ya Muhajiriin wasio na msaada na masikini, ili kwamba waweze kuishi hapo, na Ubadah bin Saamit aliamrishwa kuwafundisha kusoma na kuandika Qur'ani.

Udugu – Dalili Kuu Kabisa Ya Imani

Kukusanyika kwa Waislamu mjini Madina kuliifungua sura mpya kwenye maisha ya Mtume (s.a.w.w.). Kabla ya kuwasili kwake pale, alikuwa akijishughulisha katika kuzivutia nyoyo na katika kuibalighisha dini yake, lakini tangu siku ile na baadae, ilikuwa muhimu kwamba auhami uhai wake pamoja na ule wa wafuasi wake kama mtawala mwenye uzoefu na asiwaruhusu maadui wa ndani na wa nje kuingia kwenye jamii ya Waislamu. Kwenye kiungo hiki, alikabiliwa na matatizo makuu matatu:

1. Hatari kutoka kwa Waquraishi na wenye kuabudu masanamu wengine wa Rasi ya Uarabuni.

2. Wayahudi wa Yathrib walioishi mjini mle na nje yake, na waliokuwa na utajiri na mali nyingi sana.

3. Tofauti zilizokuwapo baina ya wale wafuasi wake.

Kwa vile Muhajiriin na Ansar wamekulia kwenye mazingira mawili tofau- ti, ilikuwapo tofauti kubwa sana baina ya njia zao za kufikiria na utamaduni. Kisha yalikuwamo yale makundi mawili ya Ansar (yaani Bani Aws na Bani Khazraji) yaliyokuwa yakigombana kwa kipindi cha miaka mia, wakiwa maadui wakuu wao kwa wao. Kutokana na hatari na tofauti zote hizi haukuwepo uwezekano wowote ule wa kuishi maisha ya amani ya kidini na kisiasa.

Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliyashinda matatizo yote haya katika hali ya hekima kamili; kuhusu yale matatizo mawili ya kwanza alichukua hatua ambazo maelezo yake kwa kirefu tutayaeleza baadae, na kuhusu zile tofauti baina ya wafuasi wake aliziondoa kwa hekima kamili na unyofu.

Aliamrishwa na Allah kujenga udugu baina ya Muhajiriin na Ansar. Siku moja akiwa kwenye mkutano mkuu aliwageukia wafuasi wake na akasema: "Sasa hamna budi kuwa ndugu katika dini kwa jozi." Maelezo kamili juu ya watu waliokuwa ndugu wao kwa wao yameandikwa na wanahisto- ria wa Kiislamu akiwamo Ibn Hisham.[8]

Hivyo basi, kwa njia hii, Mtume (s.a.w.w.) aliweza kudumisha umoja wa Waislamu kisiasa na kiroho na umoja huu ulimwezesha kufikiria jinsi ya kuyatatua yale matatizo mawili mengine.

Tofauti Kubwa Mbili Za Sayyidna Ali (A.S.)

Wengi wa wanahistoria na wanahadithi wa Kishia na Kisunni wamezitaja sifa tofauti kuu mbili za Sayyidna Ali (a.s.) ambazo tutaziandika hapa kwa ufupi. Mtume (s.a.w.w.) alijenga udugu baina ya jozi ya wawili miongoni mwa masahaba zake mia tatu kutokana na Muhajiriin na Ansar, na kumwambia kila mmoja wao kwamba alikuwa ni ndugu wa mtu huyu. Alipomaliza kuujenga udugu ule, Sayyidna Ali (a.s.) akiwa anatokwa na machozi alimwambia Mtume (s.a.w.w.): "Umejenga udugu baina ya masa- haba

zako lakini mimi hukunifanya ndugu wa yeyote yule.” Kusikia hivyo Mtume (s.a.w.w.) alimgeukia Sayyidna Ali (a.s.) na kumwambia: “Wewe u ndugu yangu mimi, hapa duniani na kesho Akhera.”

Qanduzi amelinukuu tukio hili kwa kirefu zaidi na anasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimjibu Sayyidna Ali (a.s.) akisema: “Ninaapa kwa jina la Allah Mwenye nguvu zote (Aliyeniteuwa niwaongoze watu) nilili-ahirisha suala la udugu wako kwa sababu ya kwamba mimi nilitaka niwe ndugu yako wakati nilipokwisha kujenga udugu baina ya wale wote. Daraja lako kwangu ni kama lile la Harun na Musa, ila tu kwamba hapatakuwapo Mtume mwingine baada yangu. Wewe ni ndugu yangu na mrithi wangu.”[9]

Hata hivyo, Ibn Kathir aliutilia shaka usahihi wa tukio hili.[10] Lakini kwa vile shaka yake ni matokeo ya fikira zake maalum na si tofauti na udhuru ambao alioutoa kwa niaba ya Mu’awiyah na wasaidizi wake, tunaacha kuyanakili maelezo yake na kuyakanusha.

Sifa Nyingine Ya Saidina Al I (A.S)

Ujenzi wa msikiti ulimalizika. Zilikuwako nyumba za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na za masahaba kuuzunguka msikiti ule. Vile vile zilikuwako nyumba ambazo milango yao ilielekea msikitini, na ambazo wakazi wake waliingia msikitini kupitia milango ile. Mara kwa ghafla ilikuja amri kutoka kwa Allah kwamba milango yote inayoelekea msikitini ifungwe ila ule wa nyumba ya Sayyidna Ali (a.s.). Baadhi ya watu walikuwa wenye wasiwasi juu ya jambo hili na wakadhania ya kwamba kule kuubakisha mlango wa Sayyidna Ali (a.s.) kulifanyika kwa misingi ya hisia.

Ili kuwaelimisha watu wale juu ya jambo hili Mtume (s.a.w.w.) alitoa hotuba, pamoja na mambo mengine alisema: “Sikutoa amri ya kuifunga wala kuifungua milango kwa kupenda kwangu mwenyewe. Kwa kweli jambo hili lilikuwa ni amri itokayo kwa Allah nami sina lolote jingine ila kuitimiza amri hiyo.”

Kwa kifupi ni kwamba, kwa kuudumisha udugu wa Kiislamu, Mtume (s.a.w.w.) aliziondoa tofauti baina ya wafuasi wake zilizokuwepo kwa miaka mingi na matokeo yake ni kwamba moja ya matatizo hayo lilitatuliwa.

Tatizo la pili lilikuwa lile la Wayahudi wa Madina. Waliishi mjini na nje ya mji wa Madina nao walikuwa wameshachukua udhibiti wa uchumi na biashara za mji ule.
Mtume (s.a.w.w.) alitambua kabisa kwamba mpaka pale matatizo ya ndani yatakapotatuliwa na kuupata ushirikiano wa Wayahudi wale ndipo ataweza kujenga umoja wa kisiasa kwenye makao makuu ya serikali yake, na kama si hivyo basi mche mchanga wa Uislamu hautakuwa, naye hataweza kufikiria juu ya hatua zozote zile kuhusu wenye kuabudu masanamu wa rasi ile, hasa wale Waquraishi (yaani lile tatizo la kwanza). Vile vile alitambua kwamba ni mpaka pale tu amani na utulivu vitakapotawala ndani ya serikali, itakuwa haiwezikani kuihami serikali ile kutokana na maadui wa nje.

Katika siku za mwanzo za kuwasili kwa Mtume (s.a.w.w.) mjini Madina maelewano yalikuwapo baina ya Waislamu na Wayahudi katika hali fulani, kwa sababu jamii zote mbili zilimwabudu Allah na ziliipinga

ibada ya masanamu na Wayahudi walifikiria kwamba kama Uislamu ungalipata nguvu wao wangalikuwa salama kutokana na mashambulio ya Wakristo wa Kirumi. Zaidi ya hapo ni kuwa, uhusiano na mapatano ya tangu kale yalikuwapo baina yao kwa upande mmoja, na Bani Aus na Bami Khazraj kwa upande mwingine.

Kuhusiana na mambo haya Mtume (s.a.w.w.) aliandika mkataba kwa ajili ya kusimamisha umoja baina ya Wahajirina na Ansar, (wa kabila la Aws na Khazraji) na Wayahudi wa Madina nao pia walisaini mkataba huo na Mtume (s.a.w.w.) alikubali kuiheshimu dini yao na mali zao katika hali walizokubaliana. Waandshi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) wameandika maelezo kamili ya mkataba huo.11

Kwa vile mapatano haya ni maandiko ya kihistoria yaliyo hai na yenye kuonyesha wazi wazi jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyoiheshimu misingi ya uhuru, utaratibu na haki katika maisha, basi kwa njia ya mapatano haya akajenga umoja ulioungana dhidi ya mashambulizi ya nje, hapa chini tunayataja baadhi ya mambo yake yaliyo muhimu ikiwa ni ushahidi wa ushindi wa kisiasa katika zama zile za serikali mpya ya Uislamu.

Mkataba Mkuu Wa Kimaandishi Katika Historia

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Huu ni mkataba uliofikiwa na Muhammad, Mtume wa Allah baina ya Waislamu Waquraishi na wa Yathrib na wale watu waliowafuata na kusimama pamoja nao kwa ajili ya jihadi.

Sehemu Ya Kwanza

1. Wanaosaini mkataba huu wanaunda taifa moja. Kuhusiana na dia (malipo ya damu). Muhajiriin wa kikuraishi wanaruhusiwa kuifuata desturi yao ya tangu kale iliyokuwapo kabla ya Uislamu. Kama yeyote miongoni mwao atamuua mtu mwingine au akiwa mateka watalipa dia kwa kusaidiana na kumnunua yule mateka.

2. Bani Awf (kabila la Ansar) wanaweza pia kuzihami njia zao za maisha kama watakavyofanya Muhajirin wa kiquraishi na kwa pamoja wanaweza kulipa fidia kwa ajili ya kuachiwa kwa watu wao waliotekwa. Baada ya hapo makabila mengine ya Ansar ambayo ni Bani Sa'idah, Bani Harith, Bani Jasham, Bani Najjar, Bani 'Amr bin Awf, Bani Nabit na Bani Aws, wamekumbushwa na kuwajibishwa kwa kila mmoja wao kwamba kwa pamoja watalipa dia na kuwakomboa mateka wao kwa kuwalipa fidia.

3. Waislamu watawajibika kuwasaidia maskini na kumsaidia muumini kuhusiana na gharama kubwa awajibikazo kuzilipa katika kulipa dia au fidia ya mateka.

4. Waislamu wachamungu watapaswa kuungana dhidi ya mtu mwenye kuasi au atendaye ukatili na dhuluma, japo mkosefu huyo awe mwana wa mmoja wao.

5. Hakuna yeyote mwenye madaraka ya kufanya mapatano na mtumwa wa Kiislamu au mtoto wa

kiislamu bila ya ruhusa ya bwana wake au baba yake mtoto.

6. Muumini hatakuwa na haki ya kumuua muumini mwingine aliyemwua kafiri. Vile vile hana haki ya kumsaidia kafiri dhidi ya Mwislamu.

7. Mkataba wa Allah na ahadi yake kwa Waislamu wote ni moja. Kwa sababu hiyo, hatimaye aliye mdogo zaidi miongoni mwao anayo haki ya kulichukua jukumu kwa ajili ya mapatano na makafiri.

8. Waislamu ni marafiki na wasaidizi wa wao kwa wao.

9. Kila mmoja miongoni mwa Wayahudi wenye kutufuata sisi na akasilimu, atakuwa na haki ya kuupata msaada wetu na haitakuwapo tofauti baina yake na Waislamu wengine, na hakuna yeyote atakayekuwa na haki ya kumwonea au kumchochea yeyote mwingine kumwonea au kusaidia adui yake.

10. Waislamu hawana budi kuungana wakati wa kufanya mkataba wa amani na hakuna Mwislamu yeyote awezaye kufanya mapatano ya amani bila ya kushauriana na Mwislamu mwingine ila kwa misingi ya haki na usawa.

11. Vikundi vya Waislamu vitawajibika kwenda kupigana jihadi kwa zamu ili kwamba damu yao inayomwagika kwa ajili ya Allah igawanywe kwa usawa.

12. Waislamu wanayo dini bora zaidi na sheria madhubuti.

13. Hakuna yeyote miongoni mwa washirikina (wa Madina) aliye na haki ya kuyahami maisha na mali za washirikina wa kiquraishi au kufanya mapatano nao au kumzuia Mwislamu katika kuwazidi nguvu.

14. Kama Mwislamu akimwua Mwislamu mwingine, bila ya sababu ya haki, na kosa lake hilo likithibitika kisheria, atauawa, isipokuwa kama warithi wa yule aliyeuawa wakisamehe, na kwenye hali yoyote kati ya hizo mbili ni wajibu wa Waislamu kuungana dhidi ya muuwaji yule.

15. Yeyote yule ayatambuaye haya yaliyomo kwenye mkataba huu na akamwamini Allah na Mtume wake, hataruhusiwa kumsaidia mzushi au mkosefu au kumpa hifadhi, na mwenye kumsaidia yeye, ataipata ghadhabu ya Allah, na fidia na gharama havitakubalika kutoka kwake.

16. Mamlaka ya kumaliza tofauti zozote zile zitokeazo, daima yatakuwa na Allah na Mtume Wake Muhammad (s.a.w.w.).

Sehemu Ya Pili

17. Wakati Waislamu watakapokuwa wakipigana kwa ajili ya ulinzi wa mji wa Madina, Wayahudi watalipa fungu la gharama za vita kwa Waislamu.

18. Wayahudi wa kabila la Bani ‘Awf, (kabila moja la Ansar) ni washirika wa Waislamu, nao ni sawa na taifa moja. Waislamu na Wayahudi wako huru katika masuala ya sheria na dini zao. Watumwa wao

hawaachwi kwenye kifungu hiki, yaani wao nao wako huru katika mambo ya sheria yao, isipokuwa wale wahalifu na madhalimu ambao ambao wanajiangamiza wao wenyewe na familia zao (kwa sababu kwa kawaida watu wa familia ya dhalimu humfuata yeye). (Lengo la kutoachwa huku ni kwamba uhusiano na umoja viweze kudumu baina ya Wayahudi hao na Waislamu wasio waonevu na wadhalimu).

19. Wayahudi wa makabila ya Bani Najjar, Bani Harith, Bani Sa'adah, Bani Jasham, Bani Aws, Bani Tha'labah na Bani Shatibah ni kama Wayahudi wa kabila la Bani Awf na hakuna tofauti baina yao katika mambo ya haki na fursa. Kabila la Jafnah ni tawi la kabila la Tha'labah na taratibu zitumikazo kwa Wayahudi wa kabila la Bani Awf vile vile hutumika kwa hili tawi la Bani Shatibah.

20. Watiaji saini wa mapatano haya hawana budi kuyafanya maadili yao kushinda dhidi ya dhambi zao.

22. .Wale ambao wamefanya mapatano na kabila la Bani Tha'alabah watakuwa wako sawa nao.

23. Wale walio kwenye hali ya urafiki na Wayahudi, na wasiri wao, watabakia kuwa kwenye hali ile.

24. Hakuna mwenye haki ya kuuacha mkataba huu bila ya ruhusa ya Muhamad.

25. Kutoka miongoni mwa watu hawa damu yoyote ya mtu aliyejeruhiwa (achilia mbali yule aliyeuawa) ni yenye kuheshimika. Yeyote yule auwaye mtu atawajibika kulipa dia na hatimaye kujiangamiza mwenyewe na watu wa familia yake, isipokuwa pale tu yule muuwaji awapo ni mtu aliyeonewa.

26. Gharama za vita zitakazopiganwa na Wayahudi na Waislamu kwa pamoja ni wajibu wa kila mmoja wao, na wakati mtu yeyote mwingine apiganapo dhidi ya kundi lililo kwenye mkataba huu ni jukumu lao kupigana naye kwa pamoja.

27. Uhusiano wa pande zihusikazo na mapatano haya unategemeana na wema na ni muhimu kwamba wajiepushe na maovu.

28. Hakuna mtu atakayemuonea mwenziwe aliyefanya mapatano naye, vinginevyo, yule aliyeonewa italazimu kusaidiwa.

29. Sehemu ya ndani ya mji wa Madina panatangazwa kuwa 'Haram' kwa wale waliousaini mkataba huu.

30. Uhai wa majirani na wa wale waliopewa kimbilio ni kama uhai wetu wenyewe, na wasinyanyaswe.

31. Hakuna mwanamke atakayepewa kimbilio bila ya idhini ya watu wake.

32. Muhammad ndiye msuluhishi wa kuamua tofauti zitakazotokea baina ya watiaji saini wa mapatano haya wawe ni Waislamu au wasio Waislamu. Allah Yu pamoja naye yule ayaheshimuye zaidi mapatano haya.

33. Waquraishi na wale wafanyao mapatano nao hawatapewa kimbilio (hifadhi).

Sehemu Ya Tatu

34. Watiaji saini wa mapatano haya watabeba jukumu la pamoja kwa ajili ya ulinzi wa Yathrib.

35. Pale Waislamu wanapowaomba Wayahudi kufanya amani na adui; hawana budi kuukubali mpango huo, na Waislamu nao hawana budi kuukubali mpango wa aina hiyo ufanywao na Wayahudi, ila tu pale uwapo ukweli wa kwamba adui yule anaipinga dini ya Uislamu na uhubiri wake.

36. Wayahudi wa kabila la Aws, wawe ni watumwa au mabwana, wao nao wamo kwenye mapatano haya.

Sehemu Ya Nne

37. Mapatano haya hayamwungi mkono mwonevu au mtenda majinai.

38. Yeyote yule asaliaye mjini Madina atahifadhiwa humo, na yeyote atakayeondoka humo anahifadhiwa ili mradi tu si mwonevu na mtenda majinai.

Mkataba huu ulihitimishwa kwa sentensi ifuatayo: "Allah ndiye Mlinzi wa walio wema na wachamungu na Muhammad ni Mtume wa Allah."[12]
Mapatano haya ya kisiasa na Sheria ya msingi ya Uislamu ya wakati ule, vilivyoelezwa kwa kifupi hapo juu, ni mfano halisi wa mtazamo wa uhuru wa imani, ustawi wa jamii na umuhimu wa ushirikiano katika mambo ya pamoja katika Uislamu, na zaidi ya yote umeifafanua mipaka na mamlaka ya kiongozi na wajibu wa watia saini wote.

Wayahudi wa kabila la Bani Quraydha, Bani Nuzayr na Bani Qaynqaa hawakushiriki kwenye maamuzi ya mkataba huu, na ni Wayahudi wa mak– abila ya Aws na Khazraji tu waliokuwa washirika wa mapatano haya. Hata hivyo, baadae watu hawa walifikia mapatano na Mtume (s.a.w.w.) na sentensi zifuatazo zimechukuliwa kutoka kwenye yaliyomo ndani ya map– atano hayo:

"Mtume (s.a.w.w.) anayafanya mapatano haya na makundi matatu kwa matokeo kwamba hawatamdhuru yeye na marafiki zake kwa ndimi na kwa mikono yao, na kwamba hawatatoa silaha na wanyama wa kupanda kwa maadui wake. Iwapo watakwenda kinyume na yaliyomo katika mkataba huu, basi Mtume (s.a.w.w.) atakuwa na haki ya kumwaga damu yao, kuzichukua mali zao na kuwateka wanawake na watoto wao". Kisha Hay bin Akhtab alisaini kwa niaba ya Bani Nuzayr, Ka'ab bin Asad kwa niaba ya Bani Quraydha na Mukhayriq kwa niaba ya Qaynaqaa.[13]

Kwa njia hii Yathrib na maeneo tegemezi yaliyokuwa karibu ya mji ule yalitangazwa kuwa eneo la amani na usalama na 'Haram.' Sasa ulikuwa umefika muda ambapo kwamba Mtume (s.a.w.w.) afikirie njia na jinsi ya kulitatua lile tatizo la kwanza, yaani lile la Waquraishi, kwa sababu kwa kadiri adui huyu asimamavyo kwenye njia yake, basi Mtume (s.a.w.w.) hataweza kufaulu katika kuubalighisha Uislamu na kuzisimamia sheria zake.

Vizuizi Vya Wayahudi

Mafundisho matukufu ya Uislamu na maadili mema na tabia za Mtume (s.a.w.w.) vikawa sababu vya kuongezeka kila siku kwa idadi ya Waislamu. Hali yao ya kijeshi, kiuchumi na kisiasa pia viliongezeka kwa kiasi fulani. Haya maendeleo ya mfululizo ya Uislamu, yalizua fadhaa ya ajabu na kutokutulia katika duru za kidini za Wayahudi, kwa sababu walifikiria kwamba kwa nguvu zao wangaliweza kumvutia kwao Mtume (s.a.w.w.) na katu hawakudhania ya kwamba siku moja, nguvu zake mwenyewe zitazipita hata zile za Wayahudi na za Wakristo.

Kwenye hali ile walianza kujitia kwenye matendo yanayofarakisha watu. Kwa kuuliza maswali ya kidini yaliyo magumu walijitahidi kuitikisa itikadi ya Waislamu juu ya Mtume (s.a.w.w.), lakini silaha hizi zilizo butu hazikuwa na athari yoyote juu ya safu madhubuti za Waislamu. Sehemu kubwa ya midahalo hii imesimuliwa kwenye Qur'ani Tukufu kwenye *Sura Al–Baqarah* na *Suratun– Nisa*.

Kwa kuzichunguza hizi Sura mbili zilizotajwa, wasomaji wapenzi wanaweza kuuelewa vizuri uadui na ukaidi wa Wayahudi.

Walipewa jibu la waziwazi kwa kila swali waliloliuliza lakini ili kuepuka kuubeba mzigo wa Uislamu, waliujibu kwa ukaidi ule mwito wa Mtume (s.a.w.w.) wa kuwaita kwenye Uislamu: "Nyoyo zetu zimezibwa wala hatuyafikirii yale uyasemayo kuwa ni sahihi."

Abdullah Bin Salaam Asilimu

Midahalo hii ilizidisha uadui na mfundo wa Wayahudi, lakini katika muda fulani midahalo hii ikawa chanzo cha kusilimu kwa baadhi ya watu. Abdullah bin Salaam alikuwa mmoja wa makasisi na wanachuoni wa Wayahudi. Alisilimu baada ya kufanya majadiliano marefu na Mtume (s.a.w.w.).[14] Mara baada ya hapo mwanachuoni wao mwingine aliyeitwa Makhyriq naye alijiunga naye.

Abdullah alifikiria ya kwamba kama jamaa zake wakifahamu kusilimu kwake, watamtusi na kumkashifu. Hivyo basi, alimwomba Mtume (s.a.w.w.) kwamba asitangaze kusilimu kwake mpaka watu wa kabila lake waithibitishe elimu na uchamungu wake. Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) aliwauliza Wayahudi: "Nini maoni yenu juu ya Abdullah?" Wote wakajibu wakasema: "Yeye yu kiongozi wetu wa dini na mwana wa kiongozi wetu wa dini na mwanachuoni mkuu." Kisha Abdullah akaenda kwenye eneo lake na kuwaarifu watu wa kabila lake kuhusu kusilimu kwake. Mara tu baada ya taarifa za kusilimu kwake kuenea miongoni mwa Wayahudi, walisisimka kwa hasira. Ingawa kwa pamoja waliithibitisha elimu na uchamungu wake masaa machache tu yaliyopita, vivyo, sasa wote wakaanza kumwita mtu asiye na tabia njema na mjinga.[15]

Mpango Mwingine Wa Kuipindua Serikali Ya Kiislamu

Mdahalo na maswali magumu ya Wayahudi hayakuiimarisha tu itikadi ya Waislamu juu ya Mtume (s.a.w.w.), lakini vile vile yalikuwa sababu ya sifa zake tukufu na elimu ya dini kueleweka kwa kila mtu. Matokeo ya mijadala hii ni kwamba makundi mbalimbali ya wenye kuabudu masanamu na Wayahudi walimwelekea Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, ili kulifikia lengo lao, Wayahudi waliunda mpango mwingine na wakarejea kwenye mpango wao wa “wagawe ili uwatawale”.

Walifikiria kuuhuisha ule uadui wa kale wa miaka 120 wa Bani Aws na Bani Khazraji uliotoweka chini ya msaada wa imani, Uislamu, udugu na usawa. Walitaka kwamba mapigano na kumwaga damu vianze miongoni mwa safu za Waislamu nao. Kwa njia hii wangaliweza kuliwa na miali ya migongano ya ndani.

Siku moja baadhi ya watu wa kabila la Bani Aws na Bani Khazraji walikuwa wamekaa pamoja. Umoja na udugu wa watu wa kundi hili, ambao hadi siku chache zilizopita walikuwa maadui wenye kiu ya damu dhidi ya wao kwa wao, ulichukiwa mno na Myahudi mfitini ambaye alijiunga nao kwa nia ya kuanza hila ya uovu ya kujenga mfarakano na ugomvi miongoni mwa Waislamu. Aliwakumbusha watu wa makabila ya Bani Aws na Bani Khazraji zile kumbukumbu chungu za vita za zamani baina ya hayo makabila mawili na akasimulia kwa kirefu matukio ya vita ya Bua’ath, ambavyo hatimaye Bani Aws waliibuka kuwa washindi. Aliyatanua mno haya matukio ya tangu kale na yaliyosahaulika kiasi kwamba ugomvi na majisifu yakaanza baina ya yale makundi mawili ya Waislamu (Aws na Khazraji).

Kulikuwa na uwezekano kabisa kwamba vita vya mara kwa mara vingeweza kuanza, lakini wakati ule taarifa zilimfikia Mtume (s.a.w.w.) naye akautambua ule mpango mwovu wa Wayahudi. Hivyo akafika mahali pale akiwa pamoja na baadhi ya masahaba wake na akayakumbusha yale makundi mawili kuhusu lengo la Uislamu na ule mpango wake mtukufu, alisema: “Uislamu umekufanyeni ndugu wa kila mmoja wenu na umeufanya uadui wote na mifundo kuwa vitu vya kale vilivyosahauliwa.” Aliwashauri kwa muda fulani hivi na akawakumbusha matokeo ya ugomvi wao. Mara wote wakaanza kulia na kutokwa na machozi na wakakumbatiana ili kuuimarisha tena udugu wao na wakamwomba Allah awaghufirie.

Hila za Wayahudi hazikuishia hapo, bali walikikuza kiwango cha makri, majinai na kuvunja ahadi, na wakadumisha mawasiliano maalum na makafiri wa makabila ya Bani Aws na Bani Khazraji, na pia wakawasiliana na wale watu wenye akili ya kigeugeu kwenye mambo ya Uislamu na dini yao. Kwa dhahiri wakaingilia kwenye vita walizopigana Waislamu dhidi ya Waquraishi, na walijishughulisha mno katika kuyakuza maslahi ya waabudu masanamu.

Kushirikiana kwa dhahiri na kwa siri kwa Wayahudi na washirikina wa Kiquraishi, kulizaa vita vya kumwaga damu baina ya Waislamu na Wayahudi ambavyo hatimaye viliishia kwa kuwang’oa Wayahudi kutoka Madina. Maelezo kwa urefu ya matukio haya yatatolewa baadae pamoja na matukio ya mwaka wa tatu na wa nne wa Hijiriya, na itadhihirika jinsi gani Wayahudi walivyomlipa Mtume (s.a.w.w.) kwa matendo yake mema yaonekanayo dhahiri kwenye ile mikataba miwili aliyofanya nao, kwa wao kuvunja

ahadi, matendo yao ya dhahiri dhidi ya Uislamu na Waislamu wenyewe, makri zao dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) na kuwapa msaada maadui zake, na hivyo wakamlazimisha Mtume (s.a.w.w.) kwa matendo yao, kuipuuza ile mikataba tuliyoitaja hapo juu.

1. Siiratu Halabi, Juzuu 2, uk. 76–77.
2. Siiratu Halabi, Juzuu 2, uk. 76–77
3. Mustadrakul Haakim, Juzu 3, uk. 385.
4. Musnad Ibn Hanbal, Juzu 2, uk. 199.
5. Al–Badaayah wan Nihaayah, Juzuu 3, uk. 218.
6. Musnad Ibn Hanbal, Juzuu 2, uk. 162.
7. Hapa hakuna suala la kupatia au kukosea (katika muktadha wa ijtihad) kwa sababu hii ni ijithad ya makosa kuanzia mwanzo, tena kwa makusudi – Mhariri.
8. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk.25– 126.
9. Yanabi'ul Mawaddah, Juzuu 1, uk. 55.
10. Al–Bidayah wan–Nih?yah, Juzuu 2, uk. 226.
11. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 501.
12. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu1, uk. 503 –504; na Al–Ammaal, uk. 125 na 202.
13. Bihaarul–Anwaar, Juzuu 19, uk. 110–111.
14. Maelezo juu ya majadiliano haya na Mtume (s.a.w) tazama Biharul Anwwar, Juzuu 19, uk. 131.
15. Siirah–i Ibn Hisham, Juzuu1, uk 516.

Sura Ya 27: Baadhi Ya Matukio Ya Mwaka Wa Kwanza Na Wa Pili Hijiriya

Hapa tunakusudia kuzieleza siri za nyororo ya kudhihiri kwa hali ya kivita kulikoendelea tangu kwenye mwezi wa nane wa mwaka wa kwanza wa Hijiriya hadi kwenye mwezi wa Ramadhani wa mwaka wa pili, na kwa hakika zilikuwa harakati na mbinu za kijeshi za kwanza za Waislamu.

Tafsiri sahihi na maelezo ya siri za matukio haya tutaweza kuyapata pale tu tutakapoweza kupata maelezo ya matukio haya kutoka kwenye vitabu vya historia[1] bila ya kuongeza au kutoa chochote kile, na kuyaweka maoni ya kiuamuzi ya wanachuoni watafiti wa historia mbele ya msomaji. Haya yafuatayo hapa chini ndio kiini cha matukio haya:

1. Si zaidi ya miezi nane kupita tangu Mtume (s.a.w.w.) kuwasili Madina, ilipombidi kuitoa bendera ya kwanza kwa amir jeshi wake shujaa aliyeitwa Hamza bin Abdul Muttalib na akawapeleka, chini ya uamiri jeshi wake askari thelathini wapandao wanyama kutoka miongni mwa Muhajirina hadi kwenye pwani ya Bahari ya Sham, iliyokuwa njia iliyotumiwa na misafara ya Waquraishi. Mahali paitwapo 'Ais' alikutana na msafara wa Waquraishi uliokuwa na watu mia tatu, ukiongozwa na Abu Jahl. Hata hivyo, kutokana na upatanishi wa Majdi bin Amr, aliyekuwa na uhusiano mwema na pande zote mbili, waliachana na hatimaye wale askari wa Kiislamu wakarudi Madina.

2. Sambamba na kupelekwa kwa kikosi hiki cha watu, Ubaydah bin Harith bin Abdul Muttalib alipelekwa kwenye msafara wa Waquraishi pamoja na askari sitini au themanini wapandao wanyama kutoka miongoni mwa Muhajiriin. Alikwenda hadi kwenye bahari iliyoko chini ya Thaniyatul Murrah na akakutana na ule msafara wa Waquraishi wenye watu mia mbili ukiongozwa na Abu Sufyani. Hata hivyo, makundi mawili haya yaliachana bila ya kundi moja kulipiga jingine. Ni Sa'ad bin Abi Waqas pekee aliyetupa mshale. Zaidi ya hapo Waislamu wawili waliokuwamo kwenye msafara wa Abu Sufyani walijiunga na kile kikosi kilichotumwa na Mtume (s.a.w.w.).

3. Mara nyingine tena Sa'ad bin Abi Waqas alitumwa kwenda Hijaz na watu wengine nane. Vile vile alirudi bila ya kukabiliana na mtu yeyote. Katika istilahi za wanahistoria, vita ambavyo Mtume (s.a.w.w.) hakushiriki zinaitwa *"sariyyah'* na zile alizoshiriki zinaitwa *"Ghaz'wah."*

4. Kwenye mwezi wa kumi wa 'kuhajiri', Mtume (s.a.w.w.) alimkabidhi Sa'ad bin Ma'az mambo ya kidini ya mji wa Madina na yeye mwenyewe akaenda hadi akafika Abwa' akifuatana na kundi la Muhajiriin na Ansar kuufuatia msafara wa Waquraishi na pia kufanya mapatano na kabila la Bani Hamza. Hakukutana na ule msafara wa Waquraishi lakini aliyafanya yale mapatano na lile kabila.

5. Kwenye mwezi wa kwanza wa mwaka wa pili alimteua Saa'ib bin Uthman au Sa'ad bin Ma'aaz kuwa mwakilishi wake mjini Madina na yeye mwenyewe akaenda hadi akafika Bawaat akifuatana na watu mia mbili kuufuata msafara wa Waquraishi. Hata hivyo hakuona msafara ule uliokuwa na watu mia moja, na uliokuwa ukiongozwa na Umayyah bin Khalaf, na akarudi Madina.

6. Katikati ya mwezi wa Jamadiul Awwal ilifika taarifa ya kwamba msa– fara wa Waquraishi ulikuwa ukitoka Makka kwenda Shamu ukiwa chini ya uongozi wa Abu Sufyani. Mtume (s.a.w.w.) alimteua Aba Salmah kuwa mwakilishi wake mjini Madina, yeye mwenyewe akaenda hadi akafika 'Dh?tul Ashirah' akifuatana na kikundi cha watu. Aliusubiri ule msafara pale hadi mwanzoni mwa Jamadiul Aakhir lakini hakuweza kuukamata. Wakati wa kukaa kwake pale alifanya mapatano na watu wa kabila la Bani Madlaj. Maelezo ya mapatano haya yameandikwa kwenye vitabu vya historia.
Ibn Athir anasema: "Kwenye sehemu hii, ambayo Mtume (s.a.w.w.) na masahaba wake walikuwa wakisubiri, siku moja Mtume (s.a.w.w.) alikuja kitandani pa Ali na Ammar na akawakuta wakiwa wamelala. Mtume (s.a.w.w.) aliwaamsha wote wawili. Wakati ule aliona ya kwamba chembe chembe ndogo za vumbi zilikuwamo kichwani na usoni mwa Sayyidna Ali (a.s.). Alimgeukia Sayyidna Ali (a.s.) na kumwambia: "Ewe Abu Turaab! Una nini?"

Tangu pale Sayyidna Ali (a.s.) alifahamika miongoni mwa Waislamu kwa jina la 'Abu Turaab' (baba wa vumbi), kisha akawageukia wote wawili na akawaambia: "Je, mnapenda nikuambieni ni nani walio waovu zaidi hapa duniani?" wakajibu wakisema: "Ndio, ewe Mjumbe wa Allah." Akasema: "Watu waovu zaidi katika uso wa ardhi ni wawili. Wa kwanza alikuwa yule aliyekata miguu ya yule ngamia–jike wa (Mtume) Salehe. Na mwingine ni yeye yule atakayepiga dharuba ya upanga kwenye fuvu la kichwa chako (akamsoza Sayyidna Ali a.s kwa kidole) na kuzipaka rangi ndefu zako kwa damu ya kichwa chako."[2]

7. Baada ya kupoteza matumaini ya kuupata msafara ule, Mtume (s.a.w.w.) alirejea Madina. Hata hivyo, ilikuwa bado hazijapita siku kumi tangu awasili mjini mle, zilipofika taarifa ya kwamba Karz bin Jaabir amewateka na kuwachukua ngamia na kondoo wa Madina. Ili kumfuatia mteka nyara huyu, Mtume (s.a.w.w.) akifuatana na kikundi cha watu, alikwenda hadi wakafika kwenye eneo la 'Badr' lakini ilimbidi kurudi bila ya kupata ushindi wowote. Baada ya hapo alikaa mjini Madina hadi mwishoni mwa Sha'aban.

8. Kwenye mwezi wa Rajab wa mwaka wa pili wa Hijiriya Mtume (s.a.w.w.) alipeleka watu themanini kutoka miongoni mwa Muhajiriin chini ya uamiri jeshi wa Abdallah bin Jahash. Wakati wa kuondoka kwao alimpa barua yule amiri jeshi na kusema: "Ifungue barua hii baada ya kusafiri kwa siku mbili na kisha utende kufuatana na hayo uliyoagizwa kwenye barua hii,[3] na usimlazimishe mtu yeyote katika wafuasi wako kuifanya kazi fulani." Baada ya kusafiri kwa muda wa siku mbili aliifungua ile barua na akaona ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimpa amri zifuatazo: "Utakapoitazama barua yangu endelea na safari yako na ukapige kambi kwenye nchi ya 'Nakhlah' iliyoko baina ya Makka na Taa'if na wasubiri hapo Waquraishi na uniarifu kuhusu vitendo vyao."

Abdullah alitenda kama alivyoagizwa kwenye barua ile na wafuasi wake wote walimfuata na wakatua kwenye sehemu ile. Wakati ule ule, kwa ghafla ulitokea msafara wa Waquraishi uliokuwa ukitoka Taa'if kwenda Makka chini ya uongozi wa 'Amr Khazrami. Vile vile Waislamu walikuwa wamepiga kambi karibu nao. Ili kuhakikisha ya kwamba adui haitambui siri yao walinyoa nywele za vichwa vyao, ili kutoa picha ya kwamba walikuwa wakienda Makka kufanya Hija ya Nyumba ya Allah. Sura zao ziliwaridhisha Waquraishi na wakaambiana: "Waislamu hawa wanakwenda kufanya 'Umra' na hawana lolote lile lihusianalo nasi."

Wakati huu Waislamu walikusanyika kwa ajili ya kushauriana juu ya vita na wakaanza kubadilishana maoni. Hatimaye walitambua ya kwamba iwapo wangesubiri siku ile, ambayo ilikuwa siku ya mwisho ya Rajab, bila shaka ule mwezi mtakatifu utamalizika na kama wakati huo huo Waquraishi wataondoka pale, wataingia kwenye eneo la 'haram', na kupigana kwenye eneo lile pia kulikuwa kumeharimishwa. Hivyo basi, wakaamua ya kwamba ni bora wapigane kwenye ule mwezi mtakatifu kuliko kupigana mwenye eneo la 'Haram'. Hivyo kwa kuwashitukiza maadui walimwua 'Amr Khazrami[4] yule kiongozi wa msafara ule, kwa mshale. Kuhusu wafuasi wake, wote walikimbia ila Uthman bin Abdullah na Hakam bin Kaysaan ambao walitekwa na Waislamu. Abdullah bin Jahash akazileta bidhaa za Waquraishi na wale mateka wawili mjini Madina.

Mtume (s.a.w.w.) aliudhika alipogundua ya kwamba yule amiri jeshi wa kikundi kile alizihalifu amri zake na amepigana kwenye mwezi mtakatifu badala ya kutekeleza wajibu wake. Alisema: "Mimi sikukuamrisha hata kidogo kupigana katika mwezi mtakatifu."

Waquraish walilitumia tukio hili kuwa ni silaha ya propaganda na wakazieneza habari kwamba Muhammad amekiuka heshima ya mwezi mtakatifu. Wayahudi walilichukulia tukio hili kuwa ni ndege mbaya na wakataka kuleta matata. Waislamu walimkemea Abdullah na wafuasi wake. Mtume (s.a.w.w.) hakuzitwaa zile ngawira za vita naye alikuwa akisubiri ufunuo wa Allah. Mara kwa ghafla Malaika Mkuu

Jibriil kaileta aya ifuatayo:

“Wanakuuliza kuhusu kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasende katika njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye, na kuzuilia watu wasende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuwa……” (*Surat al-Baqarah*, 2: 217)

Kwa aya hii Waquraishi wameambiwa ya kwamba kama Waislamu wamepigana vita kwenye mwezi mtakatifu na hivyo wakafanya jambo lisilo halali, lakini wao (Waquraishi) wametenda jinai kubwa ziadi kwa kuwa wamewatoa wakazi wa Masjidul Haraam (Waislamu) kutoka maskanini mwao na wakaunda uovu kwa kuwaonea na kuwatesa. Kutokana na majinai yao haya yaliyo makuu, hawana haki ya kuikana hatua waliyoichukua Waislamu.

Kufunuliwa kwa aya hii kulitia uhai mpya kwenye kundi la Waislamu. Mtume (s.a.w.w.) akazigawa zile ngawira. Waquraishi walipendelea kuwanunua wale watu wawili waliotekwa na Waislamu. Akilijibu ombi lao, Mtume (s.a.w.w.) aliwajibu akisema: “Hamna budi kuwarudisha askari wawili wa Kiislamu mliowateka kutokana na kuwa mbali kutoka kwa wenzao ili mimi nami niwaachie mateka wenu. Na kama mkiwaua, sisi nasi tutawaua watu wenu.” Waquraishi walilazimika kuwarudisha wale mateka wa Kiislamu na kutokana na kurudi kwao vile vile zilitolewa amri za kurudishwa kwa wale mateka wa Kiquraishi. Hata hivyo, mmoja wao alisilimu na yule mwingine akarudi Makka.

Nini Lengo La Hizi Harakati Za Kijeshi?

Lengo hasa la kuvipeleka hivi vikundi na kufanya mapatano ya kijeshi na makabila yalioishi karibu na ile njia ya kibiashara ya watu wa Makka lilikuwa ni kuwajulisha Waquraishi juu ya nguvu ya kijeshi na uwezo wa Waislamu, hasa pale Mtume (s.a.w.w.) binafsi aliposhiriki kwenye harakati hizi na kukaa kwenye njia ile ya kibiashara ya Waquraishi akifuatana na kundi kubwa la watu. Huyu kiongozi maarufu wa Uislamu alitaka kuifanya serikali ya Makka itambue kwamba njia zao za kibiashara, zote zimekuwa chini ya utawala wa waislamu na wangaliweza kuisimamisha biashara yao wakati wowote watakapopenda.

Biashara ilikuwa kitu kilicho muhimu sana kwa maisha ya watu wa Makka, na zile bidhaa zilizokuwa zikisafirishwa kutoka pake kwenda Taa’if na Sham, zilijenga ule msingi wenyewe hasa wa uhai wa uchumi wao. Na kama njia hizi zikitishiwa na majeshi ya adui hodari na washirika wake kama vile Bani Zumrah na Bani Madlaj, msingi wa maisha yao ungalianguka.

Lengo la kuupeleka huu ujumbe wa kijeshi na vikundi kwenye njia za maadui lilikuwa kwamba, Waquraishi waweze kujua ya kwamba njia zao za kibiashara zimeangukia mikononi mwa Waislamu na kama waking’ang’ania kwenye ukaidi wao na wakazuia mahubiri ya Uislamu na wakawatesa Waislamu waishio mjini Makka, basi mishipa yao ya uhai itakatwa kwa nguvu ya Uislamu.

Kifupi lengo lilikuwa kwamba Waquraishi wapaswe kulitafakari jambo hili na kwa kuyatilia maanani mambo yote haya, watawaruhusu Waislamu kuuhubiri Uislamu kwa uhuru kabisa na watawafungulia njia ili wakafanye Hija ya Nyumba ya Allah na kuihubiri dini ya Allah, ili Uislamu uweze kuzivutia nyoyo kwa njia ya mafundisho yake ya kiakili na matukufu, na nuru ya dini hii iweze kuenea kila mahali katika Rasi yote ya Uarabuni chini ya himaya ya uhuru.
Mhadhiri anaweza kuwa fasaha na mwenye kuvutia sana, na mkufunzi anaweza kuwa mwaminifu na mwenye uthabiti, na isipokuwa pale wapatapo mazingira huru na hadi pale misingi ya uhuru na demokrasia itakapodumishwa, kabla ya hapo hawataweza kupata ushindi halisi katika kuwaongoza wenzao na kuyahubiri maoni yao.

Zana kuu zaidi iliyokingama kwenye njia ya maendeleo ya Uislamu ni kukosekana kwa uhuru kamili na ile hali ya mazingira ya kuhuzunisha iliyosababishwa na Waquraishi. Hivyo basi, njia pekee ya kukiondolea mbali hiki kizuizi ilikuwa kuzitishia zile njia za uchumi wao zilizokuwa mishipa ya uhai wao, na mpango huu ulipewa sura ya kivitendo kwa njia ya harakati za kivita na mikataba ya kijeshi.

Mtazamo Wa Mustashirik Kuhusu Matukio Haya

Mustashirik walikuwa wamekosea vibaya kabisa katika kuyachanganua matukio haya na wamesema mambo yaliyo kinyume na misingi ya Uislamu na malengo na shabaha za dini hii tukufu. Wanasema kwamba lengo la Mtume (s.a.w.w.) lilikuwa kuziongeza nguvu zake kwa njia ya kuteka nyara na kunyang'anya mali za Waquraishi.

Hata hivyo, maoni haya hayapatani na moyo wa hali halisi ya watu wa Yathrib, kwa sababu kuteka nyara na unyang'anyi ni matendo ya makabila ya mabedui yanayoishi majangwani, mbali kabisa na sehemu zilizostaarabika, na Waislamu wa Yathrib walikuwa na desturi ya kilimo na ambao katu hawakuwahi kushambulia msafara wowote katika maisha yao yote na hawakuwahi kuteka nyara mali za makabila yaliyokuwa yakiishi nje ya mazingira yao.

Mapigano baina ya Aws na Khazraji yalikuwa mambo ya ndani na moto wake ulikuwa unawashwa na Wayahudi ili kuyakuza maslahi yao na kuidhoofisha nguvu ya Waarabu. Sasa kuhusu Waislamu wa kundi la Muhajiriin waliohusiana na Mtume (s.a.w.w.) ingawa mali zao zimenyang'anywa na watu wa Makka, hawakuwa na mpango wa kuzifidia hasara zao. Jambo hili lathibitishwa na ukweli uliopo kwamba hawakuushambulia msafara wowote wa Waquraishi baada ya vita vya Badr. Zaidi ya hapo vingi katika vikundi hivi vilipelekwa kukusanya habari na kutoa taarifa muhimu. Vikundi vya watu thelathini au sitini na nane kwa kweli havikuwa na nguvu kiasi cha kuweza kunyang'anya, wakati idadi ya wale waliokuwa wakilinda msafara ilikuwa kubwa zaidi kuliko hii.

Wakati mwingine wanasema: "Lengo lilikuwa kulipiza kisasi kwa Waquraishi, kwa sababu Mtume na sahaba zake walipokuwa wakiyafikiria yale maonevu na mateso ambayo walikuwa wamepatishwa, hisia zao za kulipiza kisasi na heshima ya kikabila zilichochewa, nao wakadhamiria kuzichomoa panga zao ili kulipiza kisasi na kumwaga damu."

Mtazamo huu vile vile ni dhaifu na usio na msingi kama ule wa kwanza, kwa kuwa ushahidi mwingi wa kutosha unapatikana kwenye maandishi ya historia ambayo hupinga mtazamo huu na huonyesha kwamba lengo hasa la kuvipeleka vikundi hivi halikuwa kujiingiza katika mapambano ya vita au kumwaga damu au kulipiza kisasi. Yafuatayo hapa chini ni nukta ambazo hukanusha mtazamo huu wa mustashirik:

1. Kama lengo la Mtume (s.a.w.w.) katika kuvipeleka vikundi hivi ingalikuwa ni vita na kujipatia ngawira basi ingalikuwa muhimu kwamba angaliongeza idadi yao, na kupeleka jeshi lenye silaha za kutosha kule kwenye eneo la pwani. Hata hivyo, ukweli uliopo ni kwamba alipeleka watu thelathini tu pamoja na Bwana Hamza bin Abdul Muttalib, watu sitini na Ubaydah bin Harith na idadi isiyoweza kuthaminiwa iliyokwenda pamoja na Sa'ad bin Abi Waqqas. Idadi ya waquraishi walioteuliwa kulinda msafara ule ilikuwa kubwa maradufu kuliko watu hawa.

Hamza alikabiliwa na Waquraishi mia tatu na Ubaydah alikabiliwa na Waquraishi mia mbili. Na hasa pale Waquraishi walipotambua ya kwamba Waislamu wamefanya mapatano na makabila mbalimbali waliongeza idadi ya walinzi wa misafara yao. Hivyo basi, kama wale maamiri jeshi wa Kiislamu walipelekwa kupigana, kwa nini ilitokea kwamba hakuna hata tone moja la damu lililomwagwa na katika safari moja pande zote mbili hazikutaka kupambana kutokana na kuingiliwa na Majdi bin 'Amr?
2. Ile barua ambayo Mtume (s.a.w.w.) alimpa Abdullah bin Jahash yaonyesha dhahiri kwamba kupigana hakukuwa lengo hata kidogo, kwa sababu ndani ya barua ile alimpa maelekezo yafuatayo: "Piga kambi kwenye nchi ya Nakhlah iliyoko baina ya Makka na Taa'if na uwasubiri waquraishi hapo na uniarifu lengo lao."

Barua hii yaonyesha dhahiri kwamba Abdullah hakupelekwa kule kupigana, kwa kuwa kazi pekee aliyopewa ilikuwa kukusanya taarifa na yale mapigano pale Nakhlah, ambayo matokeo yake ni kuuawa kwa 'Amr bin Khazrami, yalikuwa ni matokeo ya kushauriana kwake na wafuasi wake juu ya vita. Hivyo Mtume (s.a.w.w.) alipotambua kule kumwagika kwa damu, kulikotokea, alimkaripia na kumkemea vikali Abdullah na wafuasi wake na akasema: "Sikukuamrisha hata kidogo kupigana vita."

Ni dhahiri kwamba lengo la misafara yote hii au mingi kati yao lilikuwa ni kutafuta taarifa tu, na hata kidogo hatuwezi kusema kwamba Hamza bin Abdul Muttalib alipelekwa pamoja na watu thelathini kwenda kupigana vita. Ama kuhusu Abdullah bin Jahash alipelekwa na watu thelathini kukusanya taarifa, na hali ni kwamba kile kikundi kilichopelekwa kukusanya taarifa kilikuwa ni kikubwa mara tatu zaidi kuliko kile ambacho, kwa mujibu wa kauli za mustashirik kilipelekwa kupigana vita.

Na sababu ya kila mara kuwachagua Muhajirin katika kuunda vikundi hivi ilikuwa kwamba pale Aqabah, Ansar walifanya mapatano ya ulinzi na Mtume (s.a.w.w.) nao waliahidi kuulinda uhai wake litokeapo shambulio la adui. Hivyo basi, yeye hakutaka kuwatwika jukumu la safari zile mwanzoni kabisa, na yeye mwenyewe akabakia mjini Madina. Hata hivyo, baadae, wakati yeye mwenyewe alipotoka mjini mle Madina, vile vile aliwachukua baadhi ya Ansar pamoja naye ili kuimarisha uhusiano baina yao na Muhajirina. Ni kwa sababu hii kwamba Muhajiriin na Ansar waliipata heshima ya kufuatana naye kwa

pamoja wakati wa safari zake kwenda Bawaat na Dhaatul Ashirah.

Kutokana na hoja ya mustashirik juu ya kupelekwa kwa vikundi hivi, na kwa kuchunguza yale yaliyosemwa hapo juu kwa uaminifu, mtazamo wao juu ya misafara hii aliyoshiriki Mtume (s.a.w.w.) vile vile hubatilika, kwa sababu wale waliofuatana naye kwenda Bawaat na Dhaatul Ashirah hawakuwa Muhajiriin tu lakini vile vile kikundi cha Ansar kilikwenda naye. Na pale ambapo Ansar walikuwa hawajafanya mapatano ya kijeshi naye, vipi angeliweza kuwaita kwenye vita na umwagaji wa damu?

Vita ya Badr, ambavyo maelezo yake yatatolewa baadaye vinashuhudilia kauli yetu. Mtume (s.a.w) hakuamua kupigana vita hivi mpaka Ansar waliporidhia kushiriki kwenye vita vile. Na sababu ya 'kwa nini' wanahistoria wa Kiislamu waliipa misafara hii jina la Ghaz'wa' ni kwamba walitaka wakusanye matukio yote haya chini ya kichwa cha habari kimoja na si vinginevyo, basi lengo hasa la harakati hizi halikuwa utekaji nyara wala ngawira za kivita.

1. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 222. na kuendelea; Biharul Anwar, Juzuu 19, uk.186– 190; Imtaa'ul Asmaa', uk. 51; Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 77–78; na Maghaazil– Waqidi, Juzuu 1, uk. 9–19.
2. Tarikhul Kamil, Juzuu 3, uk. 78.
3. Inasemekana kwamba hadi kwenye vita vya pili vya Dunia wanajeshi waliomaliza mafunzo yao ya kijeshi walipewa, pamoja na cheti, barua iliyofung– wa ikiwa ni amana ya kijeshi, na walielekezwa kuifungua barua ile pale tu wawapo kwenye mkusanyiko mkuu wakiwa tayari kwenda vitani na kutenda lile waliloambiwa kwenye barua ile.
4. Baadhi ya wanahistoria wamelitaja jina lake kuwa ni Waaqid bin Abdullah na wengine wakasema kwamba ni 'Amr bin Abdullah.

Sura Ya 28: Matukio Ya Mwaka Wa Pili Hijiriya

NDOA: Mwelekeo wa tamaa za kujinsia hujitokeza mwilini mwa kila mtu katika hatua maalum ya maisha na wakati mwingine inatokea kwamba kutokana na kukosa mafunzo yastahiliyo, na kwa sababu ya upatikanaji wa njia za kuitoshelezea hamu ya kingono, kijana hujikuta akiwa ukingoni mwa genge. Katika hatua hii, hutokea mambo yasiyostahili kutokea.

Ndoa ndio njia bora zaidi ya kuulinda utakatifu wetu, kulingana na utaratibu wa kimaumbile Uislamu nao umemfanya mwanaume na mwanamke kuwa na wajibu wa kuoana katika hali zilizoainishwa, na umetoa maelekezo mbalimbali kuhusiana na jambo hili. Qur'ani Tukufu inasema:
"Na waozeni wajane miongoni mwenu na wema katika watumwa wenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu atawatajirisha kwa fadhila Yake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa Mwenye kujua." (*Suratun–Nur*, 24:32).

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: "Yeyote yule apendaye kutokea mbele ya Allah akiwa na nafsi safi basi naaoe." 1
Vile vile amesema: "Katika Siku ya Hukumu nitajifaharisha juu ya nyumati nyinginezo kutokana na idadi

ya wafuasi wangu.”

Matatizo Ya Ndoa Katika Zama Hizi

Matatizo ya ndoa katika zama hizi si kidogo. Wanaume na wanawake wa siku hizi hawako tayari kuwa na ndoa kutokana na hali zisizofaa na mbaya. Vyombo vya habari vya kitaifa vinaonesha idadi ya matatizo katika mtandao wa familia, lakini matatizo mengi huzungukia zungukia katika nukta hii, nayo ni kwamba wanaume na wanawake wa jamii yetu hawalengi katika kuunda familia ambayo itahakikisha ustawi wao halisi.

Baadhi ya watu wanataka kuzishika nafasi kubwa katika jamii na utajiri kwa njia ya ndoa. Jambo ambalo watu hulipa mazingatio madogo mno siku hizi ni usafi (wa matendo) na adabu, na ingawa katika baadhi ya nyakati linaweza likafikiriwa, kwa kawaida huwa halipewi umuhimu. Uthibitisho wa jambo hili ni kwamba wanaume wanawapenda mno wasichana wa familia kubwa ingawa katika mtazamo wa kimaadili hawafai hata kidogo, na wengi wa wasichana wema na wachamungu wanaishi kwenye umaskini mkubwa sana katika baadhi ya sehemu za jamii na hakuna yeyote anayewajali.

Zaidi ya yote hayo, ziko zile sherehe za harusi ambazo ni chanzo kikuu cha usumbufu kwa upande wa bwana harusi na vilevile kwa upande wa wazazi wa bibi harusi. Tatizo kuu jingine ni suala la mahari. Kutokana na matatizo haya, wako watu wengi wasiopenda ndoa na huzimalizia tamaa zao za kingono kwa njia zisizo halali.

Mtume (S.A.W.W) Alifanya Kampeni Dhidi Ya Matatizo Haya

Haya ni baadhi ya matatizo ya kijamii ambayo yako kwa kiasi kikubwa katika kila jamii na hata zama za uhai wa Mtume (s.a.w.w.) nazo hazikuwa huru kutokana nayo. Watu watukufu wa Uarabuni waliwaoza mabinti zao kwa wale watu walio sawa nao katika nasaba, nguvu na utajiri, na waliwakataa wachumba wengine.

Kwa sababu ya desturi hii ya tangu kale watu wa familia tukufu, walitamani kumwoa Bibi Fatimah (a.s.) binti mpenzi wa Mtume (s.a.w.w.), wao walikuwa wakidhania kwamba Mtume (s.a.w.w.) hatakuwa mkali katika mambo ya ndoa ya binti yake, kwa sababu, kutegemeana na fikra zao walikuwa na kila kitu kiwezacho kumvutia bibi harusi na baba yake, na hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakuwa mkali kuhusiana na ndoa za mabinti zake wengine (Ruqayyah, Zainab, n.k).

Hata hivyo, wao walikuwa hawauelewi ukweli kwamba binti huyu wa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa tofauti na wale wengine. Alikuwa ni binti aliyekuwa na cheo kikubwa mno kwa mujibu ya aya (ya *Surah Aali Imran*, 3:61) ihusianayo na ‘Mubahilah’ (kuapizana na Wakristo).

Wale waposaji walikosea katika fikara zao, kwa sababu hawakuelewa ya kwamba ni yule mtu aliyekuwa kama yeye katika mambo ya uchamungu na imani ndiye tu angaliweza kuwa sawa na mwenzi kwa ajili

yake. Kufuatana na aya ya ‘Tatw’hir’ (Utakaso – *Surah al Ahzaab 33:33*).

Bibi fatimah (a.s.) ametangazwa kuwa yu safi kabisa kutokana na dhambi zote, hivyo, na mumewe naye vilevile ni lazima awe ‘Ma’asum’ (Asiye na dhambi). Kuonyesha utajiri na wa vitu vya kidunia sio kipimo cha usawa. Ingawa Uislamu unapendekeza kwamba mabinti waozwe kwa wanaume walio sawa nao, lakini vile vile imeelezwa ya kwamba huo usawa wao uwe ni katika mambo ya imani na Uislamu.

Mtume (s.a.w.w.) ameelekezwa na Allah kuwaambia hao wachumba kwamba ndoa ya Fatimah itafanyika kwa mujibu wa amri ya Allah na katika kuutoa udhuru huu, kwa kiasi fulani aliweza kuondoa kutoelewa kwao. Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) walitambua ya kwamba ndoa ya Bibi Fatimah (a.s.) halikuwa jambo rahisi na hakuna awezaye kumuoa kwa utajiri wake.
Vile vile walielewa kwamba mume wake anaweza tu kuwa yule mtu aliye wa pili kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) katika ukweli, imani, ubora wa kiroho na ubora wa tabia, na mtu wa aina hiyo hawezi kuwa yeyote mwingine ila Sayyidna Ali (a.s.). Ili kulijaribu jambo hili, walimshawishi Sayyidna Ali (a.s.) kumchumbia binti wa Mtume (s.a.w.w.). Sayyidna Ali (a.s.) naye alipenda kufanya hivyo na alikuwa akisubiri tu kuyatimiza yale masharti muhimu kabla ya kwenda kuchumbia.

Amiri wa Waumini alikwenda mbele ya Mtume (s.a.w.w.) binafsi. Utulivu na haya vilikuwa vimemzidi nguvu. Aliinamisha kichwa chake na ilielekea kwamba alitaka kusema jambo fulani lakini akiona aibu. Mtume (s.a.w.w.) alimpa moyo wa kusema na akalidhihirisha lengo lake kwa sentensi chache tu. Aina hii ya uchumba ni dalili ya uaminifu. Hata hivyo, taasisi zetu za mafunzo bado hazijafaulu kuwafunza wachumba watarajiwa uhuru huu ulioandamana na uchamungu, imani na uaminifu.

Mtume (s.a.w.w.) alikubali kulitimiza ombi la Sayyidna Ali (a.s.) na akasema: “Subiri kidogo ili nimweleze binti yangu jambo hili.” Alipomweleza Fatimah (a.s.) jambo hili (yeye Fatimah a.s) alinyamaza kimya kabisa. Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: Allah Yu Mkubwa! Kimya chake kinamaana ya kukubali.” Hata hivyo, katika siku zile Sayyidna Ali (a.s.) hakuwa na chochote ila upanga na deraya.

Alishauriwa na Mtume (s.a.w.w.) kuiuza ile deraya ili aweze kuzilipa gharama za doa ile. Kwa moyo mmoja akaiuza ile deraya na akamletea Mtume (s.a.w.w.) fedha alizopata kutokana na mauzo yale. Mtume (s.a.w.w.) alimpa Bilal gao (ukofi) mmoja la pesa zile bila ya kuzihesabu aende akamnunulie bibi Zahraa (Fatimah a.s) manukato. Zile zilizosalia alizikabidhi kwa Abu Bakr (r.a) na Ammar ili waende kwenye mitaa ya maduka ya Madina wakanunue vifaa vya muhimi kwa maisha ya wanandoa wale. Mambwana hawa wawili waliamka na kama walivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) wakaenda wakanunua vitu vifuatavyo (ambavyo kwa hakika ndivyo vilivyokuwa mahari ya bibi Fatimah Zahraa (a.s.) na kuvileta kwa Mtume (s.a.w.w.).

Mahari Ya Binti Wa Mtume (S.A.W.W)

Gauni lililonunuliwa kwa dirham saba, mtandio ulionunuliwa kwa dirhamu moja; joho jeusi la kuogea, ambalo halikutosha kuufunika mwili mzima; kitanda kilichotengenezwa kwa mbao na nyuzi za mtende;

magodoro mawili ya katani ya Misri, ambayo moja kati yao lilikuwa la sufi na jingine lilitengenezwa kwa nyuzi za mtende; mito minne ambayo miwili kati ya hiyo ilitengenezwa kwa sufi na ile mingine miwili ilitengenezwa kwa nyuzi za mtende; pazia, mkeka wa hajr; mawe mawili ya kusagia; kiriba kimoja cha kubebea maji; bakuli la mti la kutilia maziwa; mtungi, vibia, vyungu; bangili mbili za fedha na chombo kimoja cha shaba.

Mtume (s.a.w.w.) alipoviona vitu hivi alisema: "Ee Mola wangu! Yabariki maisha ya wale ambao vyombo vyao vingi ni vya udongo."2

Mahari ya binti yake Mtume (s.a.w.w.) yastahili kufikiriwa. Mahari yake haikuzidi *'Mahrus sunnah'* ambayo ni Dirham mia tano3.

Kwa kweli huu ulikuwa ni mfano kwa wengine yaani kwa wasichana na wavulana ambao wanalia kutokana na mzigo mzito wa mahari na wakati mwingine wakayaachilia mbali majukumu ya ndoa kwa sababu hiyo.

Kimsingi maisha ya ndoa hayana budi kuwa yenye kufaa na matamu kwa njia ya uaminifu na huba, kwani vinginevyo, mahari kubwa haileti nuru yoyote ile kwenye maisha.

Siku hizi walezi wa bibi harusi humtwisha mkwe wao mzigo mzito wa mahari ili kuimarisha hali ya msichana ili kwamba, yule mume siku moja asije akakimbilia kwenye talaka kutokakana na choyo chake. Hata hivyo, kitendo hiki hakitupatii uhakika kamili wa kulifikia lengo tulilolitaja, na tiba ifaayo na ya kweli ya maradhi haya ni kuyatengeneza maadili ya mwanadamu. Mazingira yetu ya kitamaduni na kijamii hayana budi kuwa katika hali ya kwamba fikara za aina hii hazitii mizizi akilini mwa wanaume. Vinginevyo, wakati mwingine hutokea kwamba msichana hukubali kuiachilia mahari yake ili kuweza kuachana na mumewe.

Sherehe Za Ndoa

Baadhi ya watu walialikwa kutoka upande wa bibi harusi na bwana harusi, na Sayyidna Ali (a.s.) alitayarisha karamu (*walimah*) kwa heshima ya mwenzi wake mpenzi. Baada ya karamu kwisha, Mtume (s.a.w.w.) alimwita Bibi Fatimah (a.s.). Alikuja mbele ya Mtume (s.a.w.w.) akiwa ni mwenye kuona haya mno. Alipomtazama tu, mguu wake uliteleza na karibuni aanguke. Mtume (s.a.w.w.) akamshika mkono binti yake mpenzi na akamwombea dua akisema: "Allah na Akuhifadhi kutokana na mitelezo yote."

Usiku ule Mtume (s.a.w.w.) alidhihirisha mno upendo na uaminifu, kiasi kisichoweza kuonyeshwa katika jamii za siku hizi ingawa zina maendeleo na mabadiliko. Mtume (s.a.w.w.) aliushika mkono wa binti yake na akauweka mkononi mwa Sayyidna Ali (a.s.) na akamwelezea kuhusu wema wa mumewe. Vile vile alizitaja sifa tukufu za binti yake na akasema kwamba: "Kama Ali asingalizaliwa, asingalikuwapo mtu yeyote wa kuwa sawa na yeye (Fatimah a.s). Kisha akawagawiya kazi ya nyumbani na majukumu ya maisha. Alimpa Bibi Fatimah (a.s.) mambo ya nyumbani na akamfanya Sayyidna Ali (a.s.) kuwa

mwenye madaraka ya kazi za nje ya nyumba yao. Ndoa hii ilifanyika baada ya Vita vya Badr.[4]

Kufuatana na baadhi ya taarifa, kisha Mtume (s.a.w.w.) aliwaomba wanawake wa Muhajirin na Ansar kumzunguka yule ngamia jike wa binti yake na kumpeleka kwa mumewe na kwa hilo sherehe za ndoa ya huyu mwanamke mashuhuri zaidi hapa duniani zilifikia mwisho.

Hapa chini tunainukuu Hadih inayotoa dokezo la daraja kuu alilokuwa nalo huyu binti wa Mtume (s.a.w):

“Kwa kipindi cha miezi sita Mtume alikuwa akitoka nyumbani mwake wakati wa sala ya Alfajiri na kwenda msikitini na wakati huo akisimama mara kwa mara mbele ya nyumba ya Fatimah na kusema: “Enyi watu wa nyumba yangu! Hudhurieni kwenye sala. Allah Anataka kukuondoleeni kila aina ya uchafu, ninyi Ahlul Beit (watu wa nyumba).[5]

1. Man la Yahdhurul Faqih, uk. 410.
2. .Biharul-Anwaar, Juzuu 43, uk. 94; na Kashful Ghumah, Juzu 1, uk. 359.
3. Wasa'ilush-Shi'ah, Juzuu 15, uk. 8.
4. Biharul Anwar, Juzuu 48, uk. 79 na 111.
5. Musnad Ahmad Ibn Hanbal, Juzuu 2, uk. 259.

Sura Ya 29: Mabadiliko La Qiblah

Ilikuwa bado haijapita miezi michache hivi tangu Mtume (s.a.w.w.) kuhajiria Madina wakati Wayahudi walipoamka kumpinga. Katika mwezi wa kumi na saba hasa tangu kuhajiri iliteremshwa amri ya Allah kwamba tangu pale na kuendelea, Qiblah cha Waislamu kiwe ni ile Ka’abah na watakaposali wazielekeze nyuso zao kwenye Masjidul Haram.

Maelezo Kamili Ya Tukio Hilo Hapo Juu:

Katika miaka kumi na tatu ya Utume wake, Mtume (s.a.w) akiwa mjini Makka, alikuwa akisali na kuuelekeza uso wake Baytul-Maqdis (Yerusalemu) na hata baada ya kuhajiri kwake kwenda Madina amri ya Allah ilikuwa ile ya kwamba Baytul-Maqdis iendelee kuwa Qiblah na Waislamu wanaposali wazielekeze nyuso zao kwenye Qiblah hicho hicho wanachozielekeza nyuso zao Wayahudi. Jambo hili, lenyewe lilikuwa aina fulani ya ushirikiano na njia ya kuzileta karibu hizi dini mbili – moja ikiwa ni ya kale na nyingine ikiwa ni mpya.
Lakini Wayahudi wakapatwa na woga kutokana na maendeleo ya Waislamu, kwa sababu ushindi wao uliokuwa ukiongezeka daima ulionyesha ya kwamba karibuni tu, dini ya Kiislamu itaenea katika Rasi zima na nguvu na ushawishi wa Wayahudi utakoma. Hivyo wakaanza kujitumbukiza katika matendo ya kuzuia ueneaji wa Uislamu na kuwadhuru Waislamu na yule kiongozi wao mtukufu kwa njia nyingi. Miongoni mwa vitu vingine waliuliza swali kuhusu kusali kwa kuelekea ‘Baytul-Maqdis’ na wakasema:

“Muhammad anadai ya kwamba dini yake ni dini yenye kujitegemea na sheria yake inazipita sheria zote, lakini vivyo hana Qiblah chenye kujitegemea na anasali kwa kukielekea Qiblah cha Wayahudi.”

Habari hizi zilimuumiza Mtume (s.a.w.w.). Alitoka nyumbani mwake usiku wa manane na akatazama angani. Alikuwa akisubiri ufunuo. Wakati ule ule alifunuliwa amri kama ilivyo katika aya ifuatayo: **“Kwa yakini tukiona unavyogeuza uso wako mbinguni. Basi tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho…” (*Surat al-Baqarah*, 2:144).**

Kutokana na aya hii ya Qur’ani inaonekana kwamba kubadilika kwa Qiblah hakukufanyika tu kwa sababu za upinzani wa Mayahudi, bali kuna sababu nyingine za mabadiliko haya. Ilikuwa kwamba jambo hili lilikuwa na hali ya mtihani. Lengo lilikuwa kwamba waumini wa kweli na wale wasiokuwa waaminifu katika imani zao waweze kutambulika, na Mtume (s.a.w.w.) aweze kuwatambua vizuri watu hao, kwa sababu amri ya pili ambayo katika kuitii kwake mtu atageuza uso wake kwenye Masjidul Haraam wakati anaposali, ilikuwa ni ishara ya imani katika dini mpya, na kuiasi na kuichelewesha ni ishara ya ukigeugeu na unafiki. Qur’ani yenyewe inataja ukweli huu waziwazi kwenye aya ifuatayo: “. . . **Na hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho ila tupate kumjua yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale aliowaongoa Mwenyezi Mungu…” (*Surat al-Baqarah*, 2:143.**

Hapana shaka, ziko sababu nyinginezo katika badiliko hili tunazozipata kwenye historia ya Uislamu na kutokana na kuzichunguza hali zilizokuwapo wakati ule kwenye Rasi ile, kwa mfano:

1. Ka’bah iliyokuwa imejengwa na Nabii Ibrahim (a.s.) ilikuwa ikiheshimiwa na jamii yote ya Waarabu. Kuifanya sehemu hiyo kuwa Qiblah kutazaa kuridhia kwa Waarabu kwa ujumla na kuwavutia kwenye Uislamu. Na isingelikuwako shabaha tukufu zaidi ya kwamba, washirikina wakaidi waliokuwa nyuma mno kwenye msafara wa ustaarabu, waweze kuipokea ile dini ya kweli, na Uislamu uweze kuenea kwenye sehemu zote za ulimwengu kupitia kwao.

2. Halikuwapo tegemeo kwamba Wayahudi wa siku zile wangalisilimu na hivyo basi ilionekana kwamba Waislamu wakae mbali nao kwa sababu wao walijiingiza kwenye vitendo vya kuizuia dini na waliupoteza muda wa Mtume (s.a.w.w.) kwa kuuliza maswali magumu, ambayo kwayo, kwa mujibu wa fikira zao walidhihirisha elimu na hekima zao. Badiliko la Qiblah lilikuwa moja ya midhihiriko ya kutafuta umbali na Wayahudi kama vile kufunga kulivyopigwa marufuku katika siku ya Ashurah (mwezi 10 Muharram) kwa lengo hilo. Kabla ya kuanza kwa Uislamu Wayahudi walikuwa na desturi ya kufunga kwenye siku ya Ashurah na Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu nao waliamrishwa kufunga katika siku ile. Hata hivyo, hapo baadae amri inayohusu kufunga kwenye siku ya Ashurah iliondolewa na badala yake funga katika mwezi wa Ramadhani ikawajibishwa.

Hata hivyo, Uislamu ulio dini bora kuliko dini zote kwenye mambo yake yote, haunabudi kujidhihirisha katika njia ambayo, mambo ya ukamilifu na ubora wake viwe wazi kabisa. Kutokana na sababu hizi Malaika Mkuu Jibriil alikuja wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa tayari kaishazisali rakaa mbili za sala ya

Adhuhuri na akambalighishia amri ya Allah kwamba tangu pale na kuendelea aelekee kwenye Masjidul-Haraam.

Katika baadhi ya masimulizi imesemwa kwamba, yule Malaika Mkuu aliushika mkono wa Mtume (s.a.w.w.) na akamgeuzia kwenye Masjidul Haraam. Wanaume na wanawake waliokuwamo mle msikitini walimfuata na tangu siku ile na kuendelea Ka'abah ikawa Qiblah cha kudumu cha Waislamu.

Elimu Ya Kimuujiza Ya Mtume (S.A.W.W)

Kufuatana na mahesabu ya wanajimu wa zamani, Madina iko kwenye nyuzi 25 za latitudo na nyuzi 75 za longitudo na nukta 20. Kwa mujibu wa mahesabu haya, mwelekeo wa Qiblah kama ulivyowekwa pale Madina usingalipatana na 'Mihraab' (mahali pa kusalia mbele ya msikiti; Kibla) ya Mtume (s.a.w.w.) ambayo bado iko kwenye sehemu yake ya awali. Tofauti hii ilikuwa yenye kushangaza kwa baadhi ya wataalamu na wakati mwingine walitoa maelezo ili kuondoa zile tofauti.

Hata hivyo, hivi karibuni Sardaar Kabuli, mwanasayansi maarufu alithibitisha, kufuatana na ukadiriaji wa siku hizi kwamba; Madina iko kwenye nyuzi 24 za latitudo na nukta 75 na nyuzi 39 za longitudo na nukta 59.[1]

Matokeo ya mahesabu haya hugeuka na kuwa hivi: Qiblah cha Madina huelekea nyuzi 45 kutoka ncha ya kusini na upatikanaji huu unalingana kabisa na mwelekeo wa Mihrab ya Mtume (s.a.w.w.). Jambo hili lenyewe ni muujiza wa kisayansi. Kwa sababu kwenye zama hizo, hazikuwapo zana za kisayansi na hakukuwapo kitu kama vile mahesabu ya kukokotoa.

Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akisali aligeuka kutoka Baytul-Maqdis na kuielekea Ka'abah katika njia ambayo haukuwapo ukoseaji japo ulio mdogo kutoka kwenye mwelekeo wa Ka'abah[2] na kama tulivyoeleza hapo juu, Malaika Mkuu Jibriil alimshika mkono na kumgeuzia Ka'abah.[3]

1. Tuhfatul Ajillah, fi Ma'rifatil Qiblah, uk. 71.
2. Man la Yahzarul Faqih, Juzuu 1, uk. 88.
3. Tukio la Mtume (s.a.w.w.) kugeuka kutoka Baytul Maqdis kuelekea kwenye Kaabah alipokuwa akisali, limenukuliwa na Hur Aamili katika Wasaa'il (Surah za Qiblah, Juzu 3, uk. 218).

Sura Ya 30: Vita Vya Badr

Vita vya Badr ni mojawapo ya vita vya Kiislamu vilivyo vikubwa na maarufu, na wale walioshiriki kwenye vita hivi wana heshima maalumu miongoni mwa Waislamu. Kila mara Mujahidiin wa Badr, mmoja au zaidi, aliposhiriki au alipotoa ushahidi juu ya jambo lolote lile watu walikuwa wakisema: "Ahhil Badr (watu wa Badr) kadhaa wanakubaliana nasi" neno '*Ahlul Badr*' linatumiwa kwenye maandiko juu ya maisha ya

masahaba zake Mtume (s.a.w.w.) kwa wale watu walioshiriki kwenye vita ya Badr, na sababu ya umuhimu wao utatambulika kutokana na maelezo marefu juu ya tukio hili.

Tayari tumeshaeleza kwamba katikati ya mwezi wa Jamadul Awwal mwaka wa pili wa Hijiria ilifika taarifa mjini Madina kwamba msafara mmoja ulikuwa ukisafiri kutoka Makka kwenda Sham ukiwa chini ya uongozi wa Abu Sufyan, na Mtume (s.a.w.w.) alikwenda hadi Dhaatul Ashirah kuufuatilia msafara huu na akakaa hapo akiusubiri hadi mwanzoni mwa mwezi uliofuatia, lakini hakuweza kuukamata. Wakati wa kurejea kwa msafara ule ulikuwa ukitambulika, kwa sababu mapema kwenye wakati wa kipupwe (*autumn*), misafara ya Waquraishi ilikuwa ikirejea kutoka Sham kuja Makka.

Kwenye kampeni zote, kupata taarifa ndio hatua ya kwanza ya kuelekea kwenye ushindi. Ni mpaka tu hapo amiri wa jeshi lolote lile awezapo kuitambua nguvu ya maadui, mahali walipojikusanyia na moyo wa kupigana wa wanajeshi wao ndipo anapoweza kushinda, la sivyo anaweza akashindwa kwenye mapigano ya awali kabisa.

Moja ya sera zipasikazo kusifiwa alizozitumia Mtume (s.a.w.w.) kwenye vita zote (ambazo maelezo yake yataelezwa baadae) ilikuwa ile ya kwamba alikuwa akikusanya taarifa juu ya nguvu ya adui na mahali alipo. Hadi hivi leo, suala la kukusanya taarifa lina muhimu sana kwenye vita za ulimwengu mzima pamoja na zile za ndani ya nchi moja. Kufuatana na kauli ya Allamah Majlisi[1] Mtume (s.a.w.w.) alimtuma Adi (na kwa mujibu wa mwandishi wa '*Hayaatu Muhammad*' kama alivyonakili kutoka kwenye vitabu vya historia, alimpeleka Talhah bin Ubaydullah na Sa'id bin Zayd) kukusanya taarifa juu ya njia na utaratibu wa msafara ule, idadi ya walinzi wake, na hali ya bidhaa zao.
Taarifa iliyopokelewa ilikuwa hivi:Ni msafara mkubwa na watu wote wa Makka walikuwa na mafungu kwenye bidhaa zake.Kiongozi wa msafara ule alikuwa ni Abu Sufyani na walikuwako watu wapatao arobaini wanaoulinda. Bidhaa hizo zilipakiwa kwenye ngamia elfu moja na thamani yake ni kama dinari elfu hamsini.

Kwa vile Waquraishi walikuwa wametaifisha mali za Waislamu Muhajiriin waliokiishi mjini Makka, ilikuwa inafaa tu kwamba Waislamu nao wazinyakue bidhaa zao, na kama wakishikilia kuzizuia mali za Waislamu Muhajiriin kutokana na uadui na ukaidi wao, basi Waislamu nao kwa kulipiza kisasi, wazigawe bidhaa zao miongoni mwao zikiwa ni kama ngawira za Vita.

Hivyo Mtume (s.a.w.w.) aliwageukia masahaba zake na kusema: "Enyi watu! Huo ni msafara wa Waquraishi. Mnaweza kwenda nje ya mji wa Madina kuzikamata mali za Waquraishi, inawezekana kwamba hali zenu zikabadilika zikawa bora kuliko hivi sasa."[2]

Kwenye hali hii, Mtume (s.a.w.w.) alitoka mjini Madina akifuatana na watu 313, kwenye mwezi wa Ramadhani wa mwaka wa pili Hijiria ili kwenda kutaifisha mali za Waquraishi na waliokuwa wamepiga kambi kandoni mwa kisima cha Badr.

Abu Sufyani alipokuwa akienda Sham alitambua ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiufuatilia msafara wake. Hivyo basi, alikuwa akitahadhari wakati wa kurejea kwake na alikuwa akiulizia misafara

mingine kama Muhammad amezikalia njia za biashara. Aliarifiwa ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) kaishaondoka Madina pamoja na masahaba zake hivyo inawezekana kwamba anaufuatilia ule msafara wa Waquraishi.

Abu Sufyan akajizuia kuendelea zaidi na safari. Hakuona njia nyingine ya kufanya ila kuwaarifu Waquraishi juu ya hatari iliyokuwa ikiusubiri msafara ule. Kwa hiyo yeye alimkodi mpanda ngamia mwenye mbio sana aliyeitwa Zamzam bin Amr Ghafari na akampa maelekezo yafuatayo: "Nenda Makka na uwaarifu watu mashujaa wa Waquraishi na wamiliki wa bidhaa hizi watoke Makka waje waulinde msafara huu dhidi ya mashambulio ya Waislamu."

Zamzam aliharakisha kwenda Makka. Kama alivyoamrishwa na Abu Sufyan, aliyakata masikio ya ngamia wake, akamtoboa pua na akayapindua matakia yake juu chini, chini juu, na akalipasua shati lake kwa upande wa mbele na wa nyuma. Kisha alisimama juu ya ngamia wake na akapiga ukelele akisema: "Enyi watu! Ngamia waliochukua miski wako hatarini. Muhammad na marafiki zake wanadhamiria kuzinyakua bidhaa zile. Nina shaka kwamba hazitaweza kuifikia mikono yenu, saidieni saidieni![3]

Hali ya kusikitisha ya yule ngamia ambaye damu ilikuwa ikimchuruzika kutoka masikioni na puani na hisia aliyoijenga Zamzam kwa maombolezo yake yaliyokuwa yakiendelea na kuomba msaada, na wale mashujaa wakawa tayari kwenda, ila Abu Lahab, ambaye hakushiriki kwenye vita ile na akamkodi Aas bin Hisham kwa dirhamu elfu nne ili aende akapigane kwa niaba yake.

Umayyah bin Khalaf, aliyekuwa mmoja wa machifu wa Waquraishi haku- penda kushiriki kwenye vita ile kwa sababu fulani fulani na aliambiwa ya kwamba Muhammad amesema: "Umayyah atauawa mikononi mwa Waislamu." Viongozi wa jamii ile walihisi ya kwamba kutokuwapo kwa mtu yule aliye muhimu kiasi kile bila shaka kutaleta madhara katika lengo lao.

Umayyah alipokuwa ameketi ndani ya Masjidul-Haraam pamoja na watu wengine, watu wawili waliojitolea kupigana dhidi ya Muhammad walikuja na kumwekea sinia na kisanduku cha wanja mbele yake na wakasema: "Ewe Umayyah! Hivyo umejitoa katika kuihami nchi yako, utajiri wako na biashara yako na umechagua kuishi maisha ya kutawishwa kama mwanamke badala ya kupigana kwenye mstari wa mbele wa vita, inafaa kwamba uyapake wanja macho yako kama mwanamke na jina lako lifutiliwe mbali kutoka kwenye orodha ya watu mashujaa."

Masuto haya yalikuwa na athari kubwa kwa Umayyah, kiasi kwamba upesi upesi alikusanya masurufu ya safari yake na akaenda pamoja na Waquraishi kwenda kuulinda ule msafara.[4]

Tatizo Lililowakabili Waquraishi

Muda wa kuondoka ulitangazwa kwa njia fulani maalumu. Hata hivyo machifu wa Waquraishi walikumbushwa ukweli uliopo kwamba vilevile walikuwa na adui mwingine aliye mbaya kama vile kabila la Bani Bakr, na ingaliwezakana kuwashambulia kwa nyuma. Uadui wa Bani Bakr na Waquraishi

ulitokana na umwagaji wa damu, ambao maelezo yake kwa kirefu yametolewa na Ibn Hishamu.[5] Wakati uleule Suraqah bin Malik aliyekuwa mmoja wa wazee wa Bani Kananah (sehemu ya Bani Bakr) aliwahakikishia Waquraishi ya kwamba hakuna lolote la aina ile (ya kushambuliwa na Bani Bakr kwa nyuma) liwezalo kutokea na kwamba wangali– weza kutoka Makka bila ya wasiwasi japo ulio mdogo mno.

Majeshi Ya Haki Na Ya Batili Yakabiliana

Majeshi ya haki na yale ya batili yalikabiliana kwa mara ya kwanza kwenye Bonde la Badr. Idadi ya jeshi la ukweli haikuzidi 313 ambapo jeshi la upotovu lilikuwa kubwa mara tatu ya lile la haki. Waislamu hawakuwa na silaha za kutosha, usafiri wao ulikuwa na kiasi cha ngamia sabini na kiasi cha farasi wachache, ambapo yule adui alikuja na nguvu kamili ili kuupiga Uislamu. Hata hivyo, ingawa mambo yalikuwa hivyo, uhaki ilishinda na adui akarudi Makka baada ya kupata hasara kubwa.

Mtume (s.a.w.w.) alipiga kambi kwenye njia ya kaskazini ya Badr chini ya mlima uitwao *'Al–Udwatud Dunya'* na alikuwa akiusubiri ule msafara upite ndipo alipopata taarifa mpya. Taarifa hii iliyabadilisha mawazo ya maamiri jeshi wa jeshi la Waislamu na ikaifungua sura mpya kwenye maisha yao. Mtume (s.a.w.w.) aliarifiwa ya kwamba wale watu wa Makka waliotoka kuja kuuhami msafara ule, walikuwa wamejikusanya kwenye eneo lilelile na makabila mbali mbali yameshiriki katika kuliunda jeshi hilo.

Yule kiongozi mkuu wa Waislamu alijikuta njia panda. Yeye na masahaba zake wametoka Madina kuja kuziteka bidhaa nao hawakuwa katika hali ya kuweza kukabiliana na jeshi kubwa la watu wa Makka kiasi kile, kutokana na idadi na zana zao za kijeshi, na sasa kama wakirejea kule walikotoka, watakuwa wameupoteza utukufu walioupata kwa njia ya mikakati na utendaji wa kivita.

Kwa vile kulikuwa na uwezekano kabisa kwamba adui angeweza kuendelea mbele na kuanza kuyashambulia makao makuu ya Uislamu (Madina), Mtume (s.a.w.w.) alifikiria kwamba ni bora wasirudi nyuma bali wapigane mapigano ya makubwa kwa kuitumia nguvu iliyopo hadi dakika ya mwisho.

Jambo lipasalo kuzingatiwa hapa lilikuwa kwamba, wengi wa askari walikuwa ni Ansar na walikuwepo Muhajiriin sabini na nne tu miongoni mwao, na katika yale mapatano waliyoyafanya Ansar na Mtume (s.a.w.w.) pale 'Aqabah' yalikuwa ni mapatano ya ulinzi na wala hayakuwa mapatano ya vita. Kwa maneno mengine ni kwamba, Ansar walikubali kumhami Mtume (s.a.w.w.) yeye binafsi mle mjini Madina kama watakavyowalinda ndugu zao, lakini hawakujiwajibisha na kwenda naye nje ya mji wa Madina kwenda kupigana vita dhidi ya adui. Sasa swali lililoibuka pale lilikuwa yule amiri jeshi wa jesli zima angefanya nini? Hapo Mtume (s.a.w.w.) hakuliona lolote jingine la kufanya bali kushauriana na masahaba zake juu ya kupigana vita na kulitatua tatizo lile kwa njia ya mtazamo wao.

Mashauriano Ya Kijeshi

Mtume (s.a.w.w.) alisimama na akasema: “Mna maoni gani juu ya jambo hili?” Abu Bakr (r.a) alikuwa wa kwanza kusimama, naye akasema: “Machifu na wapenda vita wa Waquraishi wamejiunga na jeshi hili. Katu Waquraishi hawajaonyesha imani juu ya dini na hawajaanguka kutoka kwenye kilele cha utukufu na kuangukia kwenye shimo la fedheha. Zaidi ya hapo, hatukutoka Madina tukiwa tumejitayarisha vya kutosha.”6 (Alikuwa na maana ya kusema kwamba isingalifaa kupigana nao, hivyo warudi Madina).

Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Kaa chini” Kisha Umar akasimama na akayarudia yale aliyoyasema Abu Bakr, Mtume (s.a.w.w.) alimwomba yeye naye akae.

Baada ya hapo Miqdad (Ansar) alisimama na akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Nyoyo zetu ziko pamoja nawe, hivyo basi, huna budi kulitekeleza lile uamrishwalo na Allah. Ninaapa kwa jina la Allah! sisi hatutakuambia kama vile Bani Isra’il walivyomwambia Musa alipowaamrisha kwenda kupigana jihadi, wao wakasema: ‘Ewe Musa! Wewe na Mola wako nendeni mkapigane jihadi, nasi tutakaa hapa.’ Kwa vyovyote vile, sisi tunakuambia kinyume kabisa na hayo, na tunakwambia: ‘Pigana jihadi chini ya msaada wa baraka za Allah na sisi nasi tuko pamoja nawe na tutapigana.”
Mtume (s.a.w) alifurahishwa mno kuyasikia maneno ya Miqdad na akamwombea du’a.

Kuuficha Ukweli

Ingawa upendeleo, kuficha ukweli wa mambo na ushupavu wa kidini (ushabiki), ni mambo yasiyo sahihi kwa mwandishi yeyote, bali ni zaidi kwamba hayafai kabisa kwa mwanahistotia. Historia ni kioo ambacho nyuso za watu zaweza kuonekana waziwazi. Hivyo basi, kwa faida ya vizazi vijavyo, mwanahistoria hana budi kuuondoa ushupavu (ushabiki) wote wa kidini.7

Ibn Hisham,8 Miqrizi9 na Tabari10 wameyataja haya mashauriano ya kivita ya Mtume (s.a.w.w.) na vile vile wameyanukuu yale maneno ya majibu ya Sa’ad bin Ma’aaz na Miqdadi kwenye vitabu vyao vya historia, lakini wameepuka kuyanukuu kikamilifu majibu ya mabwana Abu Bakr na Umar.

Wamesema kwa kifupi tu kwamba hawa watu wawili walisimama na wakatoa maoni yao wakasema mambo mazuri. Sasa mtu anaweza kuwauliza hawa mashujaa wa historia kwamba: “Kama maoni yaliyotolewa na hawa ‘*Shaykhayn*’ (Mashekhe wawili – Abu Bakr na Umar) yalikuwa mazuri, kwa nini waliepuka kuyanukuu maneno yao?”

Hata hivyo, majibu yao yalikuwa ni kama tulivyoyanukuu hapo juu, na kama wanahistoria hao tuliowataja wameuficha ukweli, lakini wengine wameyanukuu maneno yao.11 Na kama uwezavyo kuona vema kabisa, hawakusema maneno mazuri. Maneno yao yanaonyesha kwamba walipatwa na hofu na waliwachukulia Waquraishi kuwa ni watukufu zaidi na wenye nguvu kiasi kwamba wao (Abu Bakr na Umar) hawakuweza japo kufikiria ya kwamba wao (Waquraishi) wangaliweza kushindwa.

Athari mbaya za maneno yao katika fikara za Mtume (s.aw.w) zinaweza kutambulika vizuri sana kutoka kwenye vipande vya historia alivyovinukuu Tabari kwenye ukurasa uleule, kwa sababu kama uonavyo, hawa *Shaykhayn* walikuwa watu wa kwanza kuifungua midomo na Miqdaad na Sa'ad bin Ma'aaz waliyatoa mawazo yao baadae.

Tabari anamnukuu Abdullah bin Mas'ud kwamba alisema: "Katika siku ya Badr nilitamani kwamba ningalikuwa kwenye nafasi ya Miqdaad, kwa sababu alianza kuongea na akasema: 'Katu sisi sio kama Bani Isra'il (wana wa Isra'il) ili kwamba tukwambie kuwa wewe na Mungu Wako nendeni na kapiganeni nasi tutakaa hapa . . . . .'

Kwa muda fulani wakati uso wa Mtume (s.a.w.w.) ulipokuwa umejawa na hasira, akayasema maneno haya (na akaileta njia ya raha na furaha kwa Mtume (s.a.w.w.), na nilipenda ya kwamba ningalilipata mimi nafasi ile."

Sasa je, hasira ya Mtume (s.a.w.w.) ilisababishwa na kitu chochote kingine badala ya maneno ya kukatisha tamaa waliyoyatamka Abu Bakr na Umar na kushikilia kwao kurejea Madina?12

Bila shaka huu ulikuwa ni mkutano wa ushauriano na kila mmoja alikuwa na haki ya kutoa maoni yake mbele ya amiri jeshi mkuu. Hata hivyo, ilithibitishwa kwamba maoni aliyoyatoa Miqdaad yalikuwa karibu zaidi na ukweli kuliko yale yaliyotolewa na wale '*Shaykhayn*' (masheikh wawili).

Maoni yaliyotolewa yalikuwa na mwelekeo wa kibinafsi. Hata hivyo, lengo kuu la kuitisha mkutano wa ushauriano lilikuwa ni kuyapata maoni ya Ansar. Ni pale tu watakaposhiriki, ndipo itakapowezekana kutoa uamuzi wa mwisho. Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliyakariri maneno yake ili kupata maoni ya Ansar na akasema: "Nifahamisheni mawazo yenu."

Sa'ad bin Ma'az Ansar alisimama na akasema: "Je, una maana ya sisi (Ansar)?" Mtume (s.a.w.w.) akajibu akasema: "Ndio." Baada ya hapo Sa'ad akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Sisi tumekuamini na tumeshuhudia ya kwamba dini yako ni dini ya kweli, nasi tumekuahidi na kukubali ya kwamba tutakutii na kuyafuata maamuzi yako.

Tunaapa kwa jina la Allah Mwenye nguvu zote, Aliyekuteuwa kuishika kazi ya Utume kwamba kama ukienda baharini (yaani Bahari ya Sham) sisi tutakufuata na hakuna yeyote miongoni mwetu atakayebakia nyuma katika kukufuata. Katu sisi hatuogopi kumkabili adui. Inawezekana kwamba tutaweza kutoa huduma zetu na kutoa mihanga katika jambo hili liwezalo kuyaangaza macho yako. Katika kuitii amri ya Allah unaweza kutupeleka mahali popote uonapo kuwa panafaa."

Maneno ya Saad yalimfanya Mtume kuwa na furaha mno na kile kivuli cha kisirani cha kukata tamaa kilipotea usoni mwake na ikadhihiri nuru ya matumaini, umadhubuti, subira na uvumilivu katika njia iendayo kwenye lengo.

Maneno ya Saad yalikuwa yenye kuvutia mno kiasi kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitoa amri ya haraka ya

kwenda mbele na akasema: “Songeni mbele nami ninakubashirieni kwamba mtakutana na msafara ule na kuzinyakua zile bidhaa au mtapigana dhidi ya majeshi yaliyokuja kuusaidia ule msafara. Hivi sasa hapa ninaweza kukuona kushindwa kwa Waquraishi na kuona kwamba wamepata hasara kubwa.”

Jeshi la Waislamu liliendelea likiwa chini ya uamiri jeshi wa Mtume (s.a.w.w.) na kupiga kambi karibu na visima vya Badr.[13]

Kupata Taarifa Juu Ya Adui

Kanuni za kijeshi za kisasa na mbinu za kivita zimekuwa na mabadiliko makubwa mno zinapolinganishwa na hapo kale. Muhimu wa kupata taarifa juu ya hali ya adui na ujuzi wa siri zake za kivita, na mikakati ya vita na jeshi analolileta kwenye uwanja wa vita bado upo. Hata katika siku zetu hizi, jambo hili lina mchango mkubwa kuhusiana na kushinda au kushindwa katika vita. Hakuna shaka yoyote kwamba siku hizi jambo hili limeitwaa sura ya kielimu, na madarasa na shule vimejengwa kwa ajili ya kufundisha kanuni za upelelezi.
Wakuu wa ushirika wa nchi za Masharika na za Magharibi hufikiria ya kwamba sehemu kubwa ya ushindi wao inatokana na upanuaji wa mipango yao ya upelelezi ili kwamba waweze kuzitambua mbinu za kivita za adui kabla ya kuanza kwa uadui na waweze kuwachanganya mawazo.

Majeshi ya Uislamu yalichukua nafasi yao kwenye sehemu ambayo iliafikiana na kanuni za majificho (*camouflage*), na kila harakati kama hiyo ambayo ingeweza kusababisha kufunuka kwa siri zao ilizuiwa. Vikundi mbalimbali vikaanza kukusanya taarifa juu ya Waquraishi na vilevile kuhusu ule msafara wao. Taarifa hizi zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali katika njia zifuatazo:

1. Kwanza kabisa yeye Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alitoka akifuatana na askari mmoja shujaa na wakakutana na kiongozi wa kabila moja na akamwuliza, akisema: “Je, una taarifa gani kumhusu Muhammad na marafiki zake?” “Nimearifiwa ya kwamba Muhammad na masahaba zake waliondoka Madina kwenye siku kadhaa. Kama mtu huyu aliyenipa taarifa hizi yu mkweli, basi yeye (Mtume s.a.w.w na masahaba zake) watakuwa wako sehemu fulani na sehemu fulani, hivi sasa.

2. Kikundi cha doria walimokuwamo Zubayr, ‘Awaam, na Sa’ad Abi Waqqas walikwenda kwenye kisima cha Badr wakiwa chini ya Sayyidna Ali (a.s.) ili wakatafute taarifa nyingine. Hapa palikuwa ni mahali pa kukutanikia ambapo watu walipashana habari. Karibu na hicho kisima kikundi kile kiliwakuta watumwa wawili wa Waquraishi wakiwa na ngamia aliyechukua maji. Waliwakamata wote wawili na wakawaleta mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Baada ya kuwahoji ilifahamika ya kwamba mmoja wa watumwa wale alikuwa ni wa Banil Hajjaj na mwingine alikuwa wa Banil Aas nao walitumwa kuja kuwachotea maji Waquraishi. Mtume (s.a.w) aliwauliza: “Wako wapi Waquraishi?”

Wakamjibu kwamba walikuwa upande wa pili wa mlima uliokuwako jangwani. Kisha aliwauliza kuhusu idadi yao, wakajibu ya kwamba hawakuwa na uhakika nayo. Akawauliza: “Kila siku wanachinja ngamia wangapi?” wakamjibu ya kwamba wanachinja ngamia kumi siku moja na siku nyingine wanachinja

ngamia tisa. Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema kwamba idadi yao ilikuwa ni baina ya mia tisa na elfu moja. Baada ya hapo aliwauliza kuhusu machifu wa Waquraishi. Walijibu ya kwamba 'Utbah bin Rabiyyah, Shaybah bin Rabiyyah, Abul Bakhtari bin Hisham, Abu Jahal bin Hisham, Hakim bin Hizaam, Umayyah bin Khalaf n.k. walikuwa miongoni mwao. Mtume (s.a.w.w.) aliwageukia masahaba zake na akasema:

"Mji wa Makka umevitoa vipande vya moyo wake (yaani wanawe walio wapenzi zaidi, kwa mji huo).[14] Baada ya hapo aliamrisha kwamba wale watu wawili wazuiwe wakiwa ni mateka ili uchunguzi uendelee.

3. Watu wawili walitumwa kwenda kwenye kijiji cha Badr kwenda kukusanya taarifa juu ya ule msafara. Walishuka upande wa kilima kilichokuwa karibu na kile kisima na wakajifanya kwamba walikuwa na kiu hivyo wamekuja kunywa maji. Kwa bahati wakawaona wanawake wawili kandoni mwa kisima kile waliokuwa wakizungumza. Mmoja wao alimwambia mwenzie: "Kwa nini hunilipi deni langu? Je, hufahamu kwamba mimi nami ni mhitaji?" Yule mwenziwe alimjibu akisema: "Msafara utafika kesho au keshokutwa. Nitautumikia msafara huo na kisha nitakulipa deni lako." Majdi bin Amr aliyepata kuwapo pale aliyathibitisha yale aliyoyasema yule mdaiwa na kisha akawaamua.

Wale wapanda ngamia wawili walifurahi sana kuzisikia habari hizi. Wakizizingatia kanuni za kujificha walifika mbele ya yule Amiri–jeshi Mkuu wa majeshi ya Waislamu na wakamwarifu yale waliyoyasikia.

Sasa kwa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kaishapata taarifa kamili kuhusu kuwasili kwa ule msafara na mahali walipo Waquraishi, sasa ikawa muhimu kwake kurejea kwenye matayarisho ya kazi yake.

Msafara Wa Abu Sufyani Wakimbia

Abu Sufyani kiongozi wa msafara ule aliyeshambuliwa na kikundi cha waislamu wakati wa kwenda Shamu, alijua vyema kwamba wakati wa kurejea kwake bila shaka watamshambulia tena. Hivyo, alipofika kwenye eneo lenye athari za Uislamu aliusimamisha ule msafara wake mahali fulani na akaenda kwenye kijiji cha Badr kwenda kupata taarifa. Hapo alikutana na Majdi bin 'Amr na akamuuliza kama amewahi kumwona mtu yeyote kwenye eneo lile ambaye angaliweza kumhisi. Majdi alimjibu akisema: "Sikuona kitu chochote ambacho kingeliweza kuziamsha hisia zangu.

Niliwaona wapanda ngamia wawili tu. Waliweka ngamia wao kwenye kilima kile, wakashuka chini hapa, wakanywa maji na kisha wakaenda zao." Abu Sufyani akakipanda kile kilima, akavunja kipande cha mavi ya ngamia wale, na alipoona kokwa za tende ndani yake, alitambua fika wale walikuwa ni watu wa Madina. Hivyo basi, aliibadili njia ya msafara ule, na kwa kwenda hatua mbili za msafara kwa wakati mmoja, aliweza kuutoa nje ya eneo la athari za Uislamu.

Vilevile alimteua mtu mmoja kwenda na kuwaarifu Waquraishi kwamba msafara wao uko salama kutokana na mashambulizi ya Waislamu, na hivyo basi, warudi Makka na wawaachie Waarabu kulimaliza jambo lile na Muhammad.

Waislamu Watambua Kutoroka Kwa Msafara

Taarifa za kutoroka kwa ule msafara zilienea miongoni mwa Waislamu. Wale waliokuwa wakizitupia jicho la ulafi bidhaa za msafara ule waliudhishwa mno na matokeo haya. Allah akazifunua Aya zifuatazo ili kuzitia nguvu nyoyo zao:

"Na Allah Alipokuahidini moja kati ya mataifa mawili ya kwamba ni lenu, nanyi mkapenda mpate lile lisilo na nguvu liwe lenu, na Allah anapenda kuitimiza haki kwa maneno Yake, na aikate mizizi ya makafiri. Ili kuthibitisha haki na kuondoa batili hata kama wakichukia wabaya" (***Surah al-Anfal, 8:7-8***).

Tofauti Za Maoni Miongoni Mwa Waquraishi

Abu Sufyan alipofaulu kuusalimisha msafara wake kwa kuifuata njia nyingine badala ya ile ya Badr, upesi sana aliwapelekea ujumbe wale watu waliokuja kuuokoa ule msafara akiwaarifu kuhusu usalama wa msafara na kuwaomba warejee kwa njia waliyokuja nayo, kwa kuwa lengo hasa la kukusanya jeshi lile lilikuwa ni kuuhami ule msafara na lengo hilo limeshafikiwa. Yule mjumbe wa Abu Sufyan alipoufikisha ujumbe wake kwa machifu wa Waquraishi, ulitokea mfarakano wa ajabu miongoni mwao.

Watu wa kabila la Bani Zuhrah na Akhnas Shariq na washirika wao walirejea kwa ile njia waliyokuja nayo. Wao walisema: "Lengo letu lilikuwa kuzihami bidhaa nyingi za Bani Zuhrah na lengo hilo limeshafikiwa." Twalib bin Abu Twalib aliyelazimishwa na Waquraishi kutoka mjini Makka na kwenda kuuhami ule msafara naye alirudi baada ya ugomvi wa maneno ambao ndani yake aliambiwa: "Nyoyo zenu ninyi Bani Hashim anazo Muhammad."

Kinyume na ushauri wa Abu Sufyani, Abu Jahl alishikilia kwamba waende kwenye ukanda wa Badr, wakakae hapo kwa muda wa siku tatu, wachinje ngamia, wanywe mvinyo, na wasikilize wasichana malenga wakiimba ili kwamba ushujaa wao ufike masikioni mwa Waarabu na wapate kuheshimiwa mno daima.

Maneno ya kupumbaza ya Abu Jahl yaliwafanya Waquraishi wasubiri katika sehemu ile, walikwenda na wakatua kwenye sehemu ya mwinuko ya jangwani, nyuma ya kilima.
Mvua kubwa iliufanya mwendo kwenye sehemu ile kuwa mgumu kwao na ikawazuia wasiendelee mbele. Hata hivyo, mvua haikuleta athari mbaya kwenye mteremko wa jangwa (*al- Udwatud Dunya*) ambako Mtume (s.a.w.w.) alipiga kambi. Hivyo basi, Waislamu waliweza kutembea kama walivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) wakaichukua nafasi kandoni mwa visima vya Badr.

Badr ni ukanda mpana. Upande wake wa kusini umeinuka (*al-Udwatul- Qaswa*) na eneo lake la kaskazini ni bonde lenye mteremko (*al-Udwatul- Dunya*). Maji yalipatikana kwa wingi kwenye jangwa hili kutoka kwenye visima vilivyochimbwa na wakati wote sehemu hii ilikuwa sehemu ya kupumzikia kwa misafara.

Hubaab bin Manzar, aliyekuwa mmoja wa askari wazoefu alimuuliza Mtume (s.a.w.w.): "Je umetua hapa kwa mujibu wa amri ya Allah, au umeifikiria sehemu hii kuwa ni yenye kufaa kwa kupigana vita?" Mtume (s.a.w.w.) akamjibu: "Hakuna amri maalum iliyofunuliwa kuhusiana na jambo hili na kama unafikiria sehemu ifaayo zaidi, unaweza kuitaja ili nibadili sehemu, kama masharti ya vita yanawajibisha kufanya hivyo." Hubaab akasema: "Ni bora kwamba tukae sehemu iliyoko kandoni mwa maji ambayo iko karibu zaidi na adui. Tujenge tangi hapo, ili kwamba paweze kuwa na maji wakati wote kwa ajili ya watu na wanyama: "Mtume (s.a.w.w.) alilipendelea wazo la Hubaab na akaliamrisha jeshi kwenda mbele. Tukio hili ladhihirisha ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliona umuhimu mno kufanya ushirikiano na aliyaheshimu maoni ya watu katika masuala ya kijamii.[15]

Mnara Wa Kuamrishia

Sa'ad bin Ma'aaz akamwambia Mtume (s.a.w.w.): "Tunakusudia kukujengea kibanda juu ya kilele cha kilima ambacho kutokea hapo uwanja mzima wa mapambano utaonekana. Kilima hicho kitalindwa na walinzi, na amri za Amir jeshi Mkuu zitatolewa kutoka hapo kwenda kwa wale maamiri jeshi wadogo. Zaidi ya mambo yote hayo, kama jeshi la Waislamu likishinda katika vita hii, itakuwa vizuri na vizuri zaidi, na kama watu wako wakishindwa na wakauawa, wewe utaweza kufika Madina kwa kumpanda ngamia mwenye mbio zaidi ukifuatana na wale walinzi wa ule Mnara wa kuamrishia baada ya kutumia mbinu za ucheleweshaji, zitakazomzuia adui kukukamata.

Wako Waislamu wengi huko ambao bado hawajaitambua hali yetu ya sasa, na kama wakijua hali hii, watakupa msaaada kamili na watafanya mambo hadi dakika ya mwisho ya uhai wao kwa mujibu wa mapatano waliyoyafanya na wewe." Mtume (s.a.w) alimwombea du'a Sa'ad bin Ma'aaz na akaamrisha ujenzi wa kile kibanda juu ya kilima, kitakachouangalia uwanja wa vita na kituo kikuu cha kuamrishia kihamishiwe kibandani hapo.

Kulichunguza Suala La Ujenzi Wa Kibanda Cha Kivuli

Ujenzi wa kivuli kwa ajili ya Mtume (s.a.w.w.) na ulinzi wake uliofanywa na Sa'ad bin Ma'aaz na kikundi cha Ansar ni tukio lililonukuliwa na Tabari kutoka kwa Ibn Is'haaq na wengineo wamemfuata.[16] Hata hivyo, kwa sababu fulani fulani hadithi hii ni yenye kutia shaka. Kwanza, kitendo cha aina hii kina athari mbaya katika nyoyo za askari. Amiri jeshi anayefanya mipango kwa ajili ya usalama wake, naye hana shauku juu ya usalama wa askari wake hawezi kuziamrisha na kuzitawala akili zao.

Pili, kitu cha aina hii hakilandani na bishara aliyoibashiri Mtume (s.a.w.w.) kwa masahaba zake, kwa msingi wa Ufunuo wa Allah. Kabla ya kukabiliana uso kwa uso na Waquraishi, aliwaambia Waislamu maneno haya: **"Na Allah Alipokuahidini moja kati ya mataifa mawili (ule msafara na wale waliokuja kuulinda) ya kwamba ni lenu, nanyi mkapenda lile lisilo na nguvu liwe lenu, na Allah anapenda kuitimiza haki kwa maneno Yake, na aikate mizizi ya makafiri. Ili kuthibitisha haki na kuondoa batili hata kama wakichukia wabaya" (*Surah al- Anfal*, 8:7-8).**

Kwa mujibu wa Tabari, wakati kile kibanda kilipokuwa kinajengwa kwa ajili ya Mtume (s.a.w), ule msafara ulikuwa umeshatoroka na walibakia tu wale watu waliokuja kutoka Makka kuuhami. Na kwa mujibu wa ahadi tuliyoitaja hapo juu, wao (Waislamu) walikuwa na uhakika kwamba ushindi ni wao. Katika hali hiyo mazungumzo yoyote yale juu ya kushindwa kwa Waislamu na ujenzi wa kibanda kwa ajili ya Mtume (s.a.w.w.) na kumweka ngamia mwenye mbio karibu na kile kibanda vingalikuwa sio mahali pake kabisa.

Ibn Sa'ad ananakili hivi, kutoka kwa Umar bin Khattab.[17] "Ilipofunuliwa aya isemayo: **'Hivi karibuni majeshi yao yatashindwa na watakimbia' (*Surah al-Qamar*, 54:45)**, Mimi nilisema moyoni: 'Ni jeshi lipi ambalo kushindwa kwake kumetabiriwa katika aya hii?' Kisha niliona katika siku ya Badr kwamba Mtume (s.a.w.w.) amevaa deraya na alikuwa akiisoma aya hii kwa nguvu. Wakati ule nilielewa kwamba jeshi hili litashindwa na kuangamizwa.'" Kwa kuuzingatia ukweli huu, hivi inaweza kudhaniwa ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake watafikiria kushindwa na kukimbia kwao?"

Tatu, tabia ya Mtume (s.a.w.w.), ambaye mkao wake katika uwanja wa vita ulielezwa na Sayyidna Ali, Amiri wa Waumini (a.s.) haziafikiani hata kidogo na mbinu hii. Kumhusu Mtume (s.a.w.w.) anasema: Kila wakati mapigano yalipokuwa makali tulitafuta mahali pa kukimbilia. Hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa karibu zaidi na adui kuliko yeye."[18]

Je, inaweza kudhaniwa kwamba mtu ambaye mwanafunzi wake wa kwanza anamwelezea kwa namna hii, kwamba ajitwalie njia ya usalama wake mwenyewe na kukimbia kwenye vita ya awali kabisa waliyopigana Waislamu? Tunafikiria kwamba ujenzi wa kibanda ulikuwa ni kwa ajili ya kumpatia Mtume (s.a.w.w.) mahali palipo juu kuliko ule uwanja wa vita ili aweze kuviona vizuri vita vile, na kutoka hapo aweze kutoa maelezo sahihi kwenye jeshi lake.

Kusonga Kwa Waquraishi

Katika mwezi 17 Ramadhani ya mwaka wa pili wa Hijiriya Waquraishi walishuka alfajiri na mapema kutoka nyuma ya kilima chenye mchanga na kuja kwenye jangwa la Badr. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipowaona aliuinua uso wake mbinguni na kuomba akisema: "Ee Allah! Waquraishi wamefika kwa kiburi na majivuno ili wapigane dhidi Yako na kumkana Mtume Wako! Basi Tuletee ule msaada uliotuahidi na uwaangamize leo (hii)!"

Kushauriana Kwa Waquraishi

Majeshi ya Waquraishi yalikusanyika mahali fulani pale Badr, lakini hawakuitambua nguvu ya Waislamu. Walimtuma Umayr bin Wahab, aliyekuwa mtu shujaa na mtaalamu wa kutathmini nguvu za majeshi, kwenda kupata idadi ya masahaba wa Muhammad. Akimpanda farasi wake aliizunguka kambi ya jeshi la Waislamu na kutoa taarifa pale aliporejea kwamba walikuwa kiasi cha mia tatu hivi. Hata hivyo, alisema kwamba atazunguuka tena ili aone kama walikuwako wengine waliojificha ili kuvizia na vilevile kama kuna majeshi ya msaada au la.

Alizunguuka huko na huko jangwani pande zote na kisha akaleta taarifa zenye kuhadharisha. Alisema: “Waislamu hawana wavamiaji wala hifadhi. Hata hivyo, nimewaona ngamia wanaokuleteeni taarifa za kifo kutoka Madina.” Kisha akaongeza kusema: “Nimekiona kikundi cha watu wasiokuwa na kimbilio lolote jingine zaidi ya panga zao.”[19] Waqidi na Allamah Majlisi wameinukuu sentensi nyingineyo pia –yaani

“Je, hamwoni kwamba wako kimya na wala hawasemi japo neno moja na nyuso zao zaonyesha zile nia zao zilivyo, na wanazisogeza ndimi zao vinywani mwao kama nyoka wenye sumu kali mno?”[20]

Tofauti Za Maoni Miongoni Mwa Waquraishi

Maneno ya yule askari shujaa yaliibua makelele miongoni mwa Waquraishi. Jeshi zima la adui likapatwa na hofu kuu. Hakim bin Huzaam alimwendea ‘Utbah na kumwambia: “Ewe Utbah! Wewe ni chifu wa Waquraishi. Waquraishi wametokea Makka kuja kuzilinda bidhaa zao; lengo hili limeshatimia na hakuna jambo lolote lililobakia ila dia ya Hazrami na fidia ya mali iliyonyang’anywa na Waislamu hapo nyuma. Hamna budi kumlipa dia yake ninyi wenyewe na mjiepushe na kupigana na Muhammad.” Maneno ya Hakim yalikuwa na athari zenye nguvu kwa Utbah.

Aliamka na kutoa hotuba yenye kuvutia sana mbele ya watu na akasema: “Enyi watu! Waachieni Waarabu walimalize jambo hili na Muhammad. Kama Waarabu wakifaulu kuipindua dini yake na kubomoa msingi wa nguvu zake sisi nasi tutakuwa na furaha kwa jambo lile. Na kama Muhammad akishinda hatutapatwa na dhara lolote kutoka kwake kwa sababu tutakuwa tumeepuka kupigana naye ingawa sisi tuko kwenye kilele cha nguvu zetu. Hivyo basi, itakuwa bora kama tukirejea makwetu.”

Hakim alimweleza Abu Jahl maoni ya ‘Utbah na akona kwamba alikuwa akijishughulisha kuvaa deraya yake. Abu Jahl aliudhishwa mno kusikia habari za hotuba ya ‘Utbah na akamtuma mtu kwenda kwa Abu ‘Aamir Hazrami, nduguye ‘Amr Hazrami, na ujumbe huu: “Mshirika wako (yaani Utbah) anawazuia watu kuipata dia ya ndugu yako. Unaweza kuiona damu ya nduguyo kwa macho yako mwenyewe. Amka na uwakumbushe Waquraishi yale mapatano waliyoyafanya na ndugu yako na uimbe beti za huzuni kwa ajili yake”.

Abu Aamir aliamka, akaondoa kilemba chake na akasema kwa kulalamika: “Ole wako! Ewe Amr!” Vilio na maombolezo ya Abu Aamir viliibua hisia za heshima ya Waquraishi na kuwafanya waamue kupigana. Hivyo wakayatupilia mbali maoni ya Utbah yahusuyo kutoka pale Badr. Hata hivyo, Utbah huyo huyo aliyependekeza kuondoka Badr, alishawishiwa na hisia za kidunia za wafuasi wake. Aliamka mara moja, akaivaa sare yake ya kijeshi na akawa tayari kwa ajili ya vita.

Wakati mwingine mwanadamu anaipoteza hekima yake kutokana na ushawishi wa hisia na hasira zisizo na msingi, na akashindwa kuyaangaza maisha yake. Yule mtu aliyekuwa na msimamo wa amani na akawaita wenzie kwenye maisha na kuwaacha wengine nao waishi, akawa katika hisia kali mno kiasi kwamba alikuwa wa kwanza kujitolea ili apigane.

Sababu Zilizoifanya Vita Vya Badr Kutoepukika

Aswad Makhzumi alikuwa mtu mwenye ghadhabu. Alipoliona lile tangi lililojengwa na Waislamu aliapa ya kwamba atafanya moja ya mambo matatu: Atakunywa maji kutoka kwenye tangi hili, au atalibomoa, au atauawa.

Alitoka kwenye safu za makafiri na akakutana na kamanda shujaa wa Uislamu Hamza karibu na tangi lile. Mapigano yalianza baina yao. Hamza alimpiga dhoruba mguuni mwake na kuukata. Hivyo basi, alianguka chini kandoni mwa lile tangi, huku mguu wake ukiwa unatoa damu. Ili kukitimiza kiapo chake, aliufikia ukingo wa tangi lile ili anywe maji, Hamza akampiga dhoruba jingine na akauawa.

Tukio hili lilifanya vita hiVi kuwa jambo lisiloepukika, kwa sababu hakuna jambo lenye kuibua mno hisia za kundi la watu kuliko umwagaji damu. Baadhi ya watu ambao nyoyo zao zilikuwa zikiungua kwa mfundo na chuki walikuwa makini kupata sababu ya kupigana na sasa tukio hili lilikuwa sababu iliyo bora zaidi kwao. Wakajifikiria kuwa ni wenye wajibu wa kupigana.

Mapambano Ya Mtu Na Mt

Ilikuwa ni desturi ya Waarabu ya tangu kale kwamba mwanzoni mwa vita mapigano ya watu wawili wawili huanza, na baada ya hapo ndipo ipiganwe vita ya watu wote.

Baada ya kuuawa kwa Aswad Makhazumi mashujaa watatu maarufu wa Waquraishi walitoka kutoka kwenye safu zao na wakasai (wakaalika wapinzani kutoka ili wapigane). Watu hawa walikuwa ni ndugu wawili – ‘Utbah na Shaybah, wana wa Rabiyyah, na Walid bin Utbah na wote walikuwa na silaha kikamilifu. Wakaunguruma na kuwakimbizia farasi wao kwenye uwanja wa vita na wakasai. Mashujaa watatu kutoka miongoni mwa Ansar, ambao ni Awf, Ma’uz na Abdullah bin Rawaahah walitoka kwenye safu za Waislamu. Hata hivyo, Utbah alitambua kwamba walikuwa ni watu wa Madina, akawaambia: “Hatuna la kufanya nanyi.” Kisha mtu mmoja (kutoka miongoni mwa Waquraishi) alipiga ukelele akasema: “Ewe Muhammad! Tuletee watu walio sawa yetu wapigane nasi.” Mtume (s.a.w.w.) aliugeuzia uso wake kwa Ubaydah, Hamza na Sayyidna Ali (a.s.) na akawaambia: “Simameni.” Hawa mashujaa watatu wakavifunika vichwa vyao na nyuso zao na wakatoka wakaenda kwenye uwanja wa vita. Wote watatu wakajitambulisha.

Utbah akawakubali wote kwamba wafanye nao yale mapambano ya wawili wawili, na akasema: “Ndio, ninyi ni sawa Baadhi ya watu wanasema kwamba katika mapambano haya, kila shujaa alipigana na mpinzani wake wa hirimu lake. Sayyidna Ali (a.s.) aliyekuwa kijana zaidi miongoni mwao alipambana na Walid (mjomba wake Muawiyah), na aliyekuwa na umri wa katikati miongoni mwa Waislamu (Hamzah) alimkabili Utbah (babu mzaa mama wa Mu’awiyah) na Ubaydah, aliyekuwa na umri mkubwa zaidi miongoni mwa hawa wapi– ganaji wa Kiislamu alipigana na Shaybah, aliyekuwa mtu mzima zaidi kutoka ule upande wa pili. Hata hivyo, Ibn Hisham anasema kwamba mpinzani wa Hamzah alikuwa ni Shaybah, na wa Ubaydah alikuwa ni Utbah. Sasa hebu na tutazame ni lipi kati ya haya maoni mawili lililo sahi– hi.

Kwani kwa kuyachunguza maoni haya, hali halisi hudhihirika.

1. Wanahistoria wanasema kwamba Saidiana Ali (a.s.) na Hamza waliwaua wapinzani wao mwanzoni kabisa mwa mashambulio yale na kisha wakaharakisha kwenda kumsaidia Ubaydah na wakamwua yule mpinzani wake nae.21

2. Katika barua aliyoandika Sayyidna Ali (a.s.) Amiri wa Waumini, akimwandikia Mu'awiyah, anamkumbusha kwa maneno haya: "Ule upan– ga ambao kwawo niliwamaliza mababu zako walomzaa mama yako ('Utbah, baba wa mamie Muawiyah–Hindi) na mjomba wako (Walid bin Utbah) na kaka yako (Hanzala) bado u pamoja nami (yaani bado ninazo nguvu zile zile)"22 Barua hii yaonyesha dhahiri kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa na mkono katika kuuwawa kwa babu mzaa mama wa Mua'wiyah, na kisha vile vile tunajua ya kwamba Hamza na Sayyidna Ali (a.s.) waliwaua wapinzani wao pale pale.

Kama mpinzani wa Hamza angalikuwa ni 'Utbah (babu mzaa mamaie Muawiyah), Sayyidna Ali (a.s.) asingaliweza kusema: "Ewe Muawiyah! Babu yako ('Utbah) aliyapoteza maisha yake kutokana na dharuba ya upanga wangu." Hivyo, isingaliwezekana kusema kwamba mpinzani wa Hamza alikuwa ni Shaybah na yule wa Ubaydah alikuwa ni 'Utbah na baada ya kuwaua wapinzani wao Hamza na Sayyidna Ali (a.s.) walimwelekea 'Utbah na wakamwua kwa dharuba za panga zao.

Mapambano Ya Wote Jumla Yaanza

Matokeo ya kuuawa kwa wale mashujaa watatu wa Waquraishi ni kuanza kwa mapambano ya watu wote. Na Waquraishi wakaanza kushambulia kwa vikundi. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba Waislamu waepuke kushambulia bali wazuie maendeleo ya uadui kwa njia ya kupigana mishale.

Kisha akashuka kutoka kwenye ule mnara wa kuamrishia na akazipanga safu za askari wake kwa fimbo. Katika wakati ule Sawaad bin Ghazbah alikuwa kasimama mbele kidogo akilinganishwa na ule mstari. Mtume (s.a.w.w.) alimpiga kwa ile fimbo tumboni mwake na akamwambia: "Usiende mbele ya hawa askari wengine,"23 Hapo Sawaad akasema: "Pigo hili nililopigwa halikuwa la haki, nami ninataka kulipiza kisasi." Mtume (s.a.w.w.) akalivua shati lake mara moja na akasema: "Lipiza kisasi chako kwangu." Kisha askari wote waliona ya kwamba Sawaad alikibusu kifua cha Mtume (s.a.w.w.) na akaiweka mikono yake shingoni mwake na akasema: "Nilitaka kukibusu kifua chako kwenye muda wa mwisho wa uhai wangu."

Kisha Mtume (s.a.w.w.) alirejea pale kwenye mnara wa kuamrishia na huku moyo wake ukiwa umejawa na imani, aliugeuzia uso wake kwa Allah Mwenye nguvu zote na akaomba, akasema: "Ee Mola wangu! Kama kundi hili litaangamia hivi leo, hakuna yeyote mwingine atakayekuabudu kwenye huu uso wa ardhi.24

Maelezo kamili ya haya mashambulizi ya watu wote yamenukuliwa kwa kiasi fulani kwenye historia ya Uislamu. Hivyo ni kweli kwamba wakati Mtume (s.a.w.w.) aliposhuka pale kwenye kituo cha kuamrishia

aliwahimiza Waislamu wapigane katika njia ya Allah na kumshambulia adui. Akaja tena kwa ghafla na akawaambia Waislamu kwa sauti kuu: “Ninaapa kwa jina la Allah Anayeitawala roho ya Muhammad kwamba, leo mwenye kupigana kwa umadhubuti na kupigana kwake kukawa kwa ajili ya Allah na akauawa, Allah Atamwingiza Peponi.”

Maneno ya yule Amir jeshi Mkuu yalikuwa na athari kubwa mno kiasi kwamba Waislamu walizivua deraya zao kutoka miilini mwao na wakaan– za kupigana ili kwamba waweze kupata kifo cha kishahidi mapema iwezekanavyo. Umayr Hamaam alimwuliza Mtume (s.a.w.w.): “Kuna umbali gani baina yangu na Pepo?” Mtume akamjibu hivi: “Kupigana na machifu wa kufuru.” Alizitupa tende chache alizokuwa akizishika mkononi na akaanza kupigana.

Kisha Mtume (s.a.w.w.) alichota mchanga na akautupia upande wa Waquraishi na akasema: “Nyuso zenu na ziumbuke!”25 Baada ya hapo alitoa amri ya mapigano ya watu wote. Dalili za ushindi wa Waislamu zilianza kujitokeza upesi upesi. Maadui walipigwa na hofu na wakaanza kukimbia. Waislamu, waliokuwa wakipigana kwa msaada wa imani yao, na wakajua ya kwamba vyote viwili kuua na kuuawa vilikuwa baraka za Allah, hawakuwa na shaka hata kidogo na hakuna kilichozuia kusonga mbele kwao.

Kuchunga Haki

Kuchunga haki za makundi mawili ya watu kulikuwa ni muhimu sana. Katika upande wa jeshi la watu wa Makka yalikuwamo makundi mawili: Wale waliowatendea Waislamu mambo mema kule Makaka na kuwasaidia, kwa mfano Abil Bakhtari, aliyetoa huduma kuu kwa Waislamu kwa kuviishilizia vizuizi vya kiuchumi. Wengine ni wale waliotoka Makka kuja kuuhami ule msafara kwa kulazimishwa na kwa hakika wao walikuwa wapenzi wa Uislamu na Mtume (s.a.w.w.) kwa mfano, wengi wa Bani Hashimu, kama vile Abbas, baba mkubwa wa Mtume (s.aw.w) n.k. Hivyo kuzijali haki za makundi haya mawili kulikuwa muhimu, na kwa kuwa Mtume wa Uislamu alikuwa ni Mtume wa rehma na amani, alitoa amri kali kwamba damu ya makundi haya mawili isimwagwe.

Umayyah Bin Khalaf Auwawa

Umayyah bin Khalaf na mwanawe walikamatwa kupitia kwa Abdur Rahmani bin Awf. Kwa vile ulikuwako urafiki baina ya Umayyah na Abdur Rahman, Abdur Rahman alitaka kumtoa yeye na mwanae mle kwenye uwanja wa vita wakiwa hai ili kwamba waweze kuchukuliwa mateka.
Bilal, Mhabeshi wa Ethiopia, alikuwa mtumwa wa Umayyah hapo kale. Kwa vile Bilal alisilimu akiwa yu mtumwa, Umayyah alikua akimtesa vikali mno. Ili kumfanya autoke Uislamu alikuwa akimlaza kwenye mchanga ulio moto sana kwenye majira ya kiangazi na kumbandika jiwe kubwa kifuani mwake. Hata hivyo alipokuwa kwenye hali ile Bilal alikuwa akisema: *“Ahad! Ahad!”* (Allah Yu Mmoja tu! Allah Yu Mmoja tu!).

Huyu Mtumwa wa Ethiopia alipata taabu sana mpaka Mwislamu mmoja alipomnunua kumpa uungwana, (na inasemekana kwamba aliyemnunua na kumwacha huru alikuwa ni Abu Bakr).

Kwenye vita ya Badr macho ya Bilal yalimwangukia Umayyah na akatambua kwamba Abdur Rahman alitaka kumpendelea. Hivyo alipiga ukelele akisema: “Enyi Kundi la Allah! Umayyah yu mmoja wa machifu wa makafiri, asiruhusiwe kubakia hai.” Waislamu wakamzunguka Umayyah pande zote na wakamwua yeye na mwanawe. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ameamrisha ya kwamba Abul Bakhtari, aliye-wasaidia Bani Hashim katika siku za vizuizi vya kiuchumi, asiuawe.26

Ilitokea kwamba mtu mmoja aliyeitwa ‘Majzar alimkamata na alikuwa akijaribu kumleta mbele ya Mtume (s.a.w.w.) akiwa hai, lakini yeye naye aliuawa.

Idadi Ya Waliouawa Na Hasara

Kwenye vita hivi watu kumi na wanne kutoka miongoni mwa Waislamu waliuawa. Ama kuhusu Waquraishi, watu sabini kutoka miongoni mwao waliuawa na wengine sabini walitekwa. Wale waliotekwa ni pamoja na machifu wao waitwao Nazar Haarith, ‘Uqbah bin Mu’it, Abu Ghurrah, Suhayl Amr, Abbas na Abu Aas.27

Mashahidi wa Badr walizikwa kwenye pembe ya ule uwanja wa vita. Makaburi yao bado yapo pale na Waislamu wachamungu huyakimbilia kwenda kuyazuru na kutoa heshima zao.

Baadae Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba maiti za Waquraishi zikusanywe na kutumbukizwa kisimani. Maiti ya ‘Utbah ilipokuwa ikiletwa kisimani pale, macho ya mwanawe Abu Huzayfah yalipoiangukia, naye akapauka. Mtume (s.a.w.w.) aliliona hilo akamwuliza, akisema: “Je, kuna shaka yoyote ile imekupitia akilini mwako?” Abu Huzayfah akajibu akisema: “Hapana, bali nilidhania ya kwamba baba yangu alikuwa mtu mwenye hekima, elimu na subira, nami nilidhani ya kwamba sifa hizi zingalimwongoza kwenye Uislamu. Hata hivyo, sasa nimetambua ya kwamba yale yote niliyokuwa nikiyafikiria hayakuwa sahihi.”

Kisha Mtume (s.a.w.w.) alikwenda akasimama kandoni mwa kile kisima. Alilitaja jina la kila mmoja wa machifu wa makafiri, na akasema: “Ewe Utbah, Ewe Shayb! Ewe Umayyah! Ewe Abu Jahl! Je, mmekwishakuyaona yale ambayo mungu wenu alikuahidini kuwa ni sahihi? Mimi nimeyaona yale ambayo Allah wangu Aliniahidi kuwa ni sahihi na madhubuti.”

Wale masahaba zake Mtume (s.a.w.w.) wakauliza wakisema: “Je, unazungumza na maiti?” Mtume (s.a.w.w.) akajibu, akasema: “Wanayasikia maneno yangu lakini hawana uwezo wa kujibu.”28

Baada Ya Vita Vya Badr

Wengi wa wanahistoria wa Kiislamu wanaamini kwamba kwenye Vita vya Badr, mapambano ya mtu na mtu na mapambano ya watu wote yaliendelea hadi adhuhuri na vita ilimalizika baada ya adhuhuri pale Waquraishi walipokimbia na baadhi yao kutekwa. Baada ya kuwazika mashahidi, Mtume (s.a.w.w.) alisali sala ya Alasiri kwenye sehemu ile na akalitoka jangwa la Badr kabla ya kuchwa jua.

Sasa Mtume (s.a.w.w.) kwa mara ya kwanza alikabiliwa na tofauti baina ya masahaba zake kuhusu ugawaji wa ngawira, na kila kikundi kilidai kwamba kilikua bora zaidi ya vile vingine. Wale walioulinda mnara wa kuamrishia wa Amiri jeshi mkuu walidai kwamba wao wameuhami uhai wa Mtume (s.a.w.w.) na hakuna liwezalo kuwa muhimu zaidi ya hili. Wale waliokusanya ngawira walidai ubora juu ya wengine. Na wale waliomfuatia adui hadi dakika ya mwisho kuuwezesha ukusanyaji wa ngawira walijifikiria kuwa wenye kustahili zaidi kuliko wengine.

Hakuna jambo lenye madhara zaidi kwa jeshi kuliko kuibuka tofauti miongoni mwa mtu mmoja mmoja. Ili kuzizuia tamaa za kidunia na kukomesha makelele, Mtume (s.a.w.w.) aliziweka ngawira zote chini ya Abdullah bin Kaad na akawateuwa watu fulani kumsaidia kuzisafirisha na kuzihifadhi kwa usalama hadi litakapopatikana suluhisho la tatizo lile.

Kanuni ya usawa wa haki ilihitajia kwamba jeshi zima liwe limegawana ile ngawira zile, kwa sababu wote walikuwa wamefanya kazi na kubeba majukumu na hakuna hata mtu mmoja pekee ambaye angaliweza kupata lolote lile mpaka pale wale wenzie nao walipofanya kazi pia. Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa njiani, alizigawa zile ngawira sawa kwa sawa. Ama kuhusu Waislamu waliouawa kishahidi aliyatenga mafungu yao na kuwapa warithi wao.

Kile kitendo cha Mtume (s.a.w.w.) cha kuzigawa zile ngawira sawa kwa sawa kilikuwa kimemuudhi Sa'ad bin Waqqas aliyemwambia Mtume (s.a.w.w.): "Je, unanifikiria mimi niliye mmoja wa watu watukufu wa Bani Zuhrah, kuwa sawa na hawa wapagazi wa maji na wakulima wa Yathrib?" Mtume (s.a.w.w.) alihuzunishwa mno kuyasikia maneno haya na akasema: "Lengo langu kwenye vita hivi lilikuwa ni kuwasaidia wanyonge dhidi ya wenye nguvu nami nimeteuliwa kuishika kazi ya Utume ili kuung'oa ubaguzi na ubora wa kidhana, na kuweka usawa katika haki za wanadamu badala ya hayo."

Kama ilivyoelezwa kwenye Aya ya Qur'ani ihusuyo Khumsi: "..... **Moja ya tano ya ngawira za vita ni kwa ajili ya Allah, rasuli wake, jamaa wa karibu, yatima, masikini na msafari." (*Surah al-Anfal*, 8:41).** Hata hivyo kwenye tukio hili Mtume aliigawa khumsi pia miongoni mwa wanajeshi. Inawezekana kwamba aya ihusianayo na khumsi ilikuwa bado haijafunuliwa; au Mtume (s.a.w.w.) aliyatumia mamlaka aliyopewa, akaacha kuichukua Khums ili kuyazidisha mafungu ya Mujahidiin.

Mateka Wawili Waliuwawa Njiani

Kwenye kimoja cha vituo vya mapumziko wale mateka waliletwa mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Miongoni mwao Nazar bin Haarith, aliyekuwa mmoja wa maadui wakuu wa Waislamu alinyongwa kwenye njia nyembamba ya 'Safraa' na Uqbah bin Abi Mu'it aliuawa kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) mahali paitwapo Irquz Zabiyyah. 29

Sasa swali linaibuka hapa kuhusu ni kwa nini, ingawa ulikuwako ukweli kwamba maamrisho ya Uislamu juu ya wafungwa wa vita ni yale yasemayo kwamba wao ni watumwa wa Waislamu na Mujahidiin, nao wanaweza kuuzwa kwenye soko kwa bei nafuu, Mtume (s.a.w) alikubali kunyongwa kwa watu hawa

wawili, na vipi aliweza kuuchukua uamuzi huu wakati alikuwa tayari kaishawaambia Waislamu kuhusiana na mateka wa Badr: “Muwe wema kwa mateka.”[30]

Abu Aziz, mshika bendera wa Waquraishi kwenye vita vya Badr, anasema: “Tangu siku ambayo Mtume (s.a.w.w.) alitoa mapendekezo yake juu yetu, tulikuwa waheshimiwa mno mbele ya Waislamu kiasi kwamba hawakukigusa chakula mpaka tulipolishwa kwanza.”

Katika mazingira haya, kunyongwa kwa hawa mateka wawili kuliamrishwa kwa ajili ya ustawi wa Waislamu wote na wala hakikuwa kitendo cha kulipiza kisasi, kwa sababu hawa watu wawili walikuwa machifu wa makafiri nao walikuwa wapangaji wa makri dhidi ya Uislamu na wachocheaji wa makabila. Inawezekana kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na uhakika kwamba kama wakiachiwa watajitumbukiza tena katika vitendo hivyo vya hatari.

Watu Walitumwa Na Mtume (S.A.W.W) Kwenda Madina

Abdullah bin Ramahah na Zayd Harithah walitumwa na Mtume (s.a.w.w.) waende Madina na wafike huko upesi iwezekanavyo na kuwapasha habari njema Waislamu kwamba Uislamu umeshinda na viongozi wa makafiri kama vile ‘Utbah, Shaybah, Abu Jahl, Zam’ah, Abul Bakhtari, Umayyah, Nabiyyah, Manbah n.k wameuawa. Walifika wakati Waislamu walipokuwa wakirejea kutoka kwenye mazishi ya binti wa Mtume (bibi Ruqaiyah), aliyekuwa mkewe Bwana Uthman, na hivyo furaha ya ushindi katika vita hivi ilichanganyika na huzuni juu ya kifo hicho.

Wakati huo huo, washirikina na Wayahudi walishtuka mno na kufadhaika, kwa sababu katu hawakutegemea kwamba, Waislamu watabarikiwa kwa ushindi wa aina ile. Hivyo basi, walijitahidi kuwafanya watu waamini kwamba taarifa zile zilikuwa za uwongo. Hata hivyo, ukweli ulithibitika kabisa kwa kuwasili kwa lile jeshi la Uislamu pamoja na wale mateka wa Kiquraishi.

Watu Wa Makka Waja Kutambua Kuuawa Kwa Machifu Wao

Haysam?n Khaz?’i alikuwa mtu wa kwanza kuwasili Makka na kuwaarifu watu kuhusu lile tukio la kumwaga damu kule Badr, pamoja na kuuawa kwa machifu wao kwenye vita ile. Abu Raafi aliyekuwa mtumwa wa Abbas siku zile na baadaye akawa sahaba wa Mtume na wa Amiri wa Waumini (a.s.) anasema: “Katika siku hizo, Uislamu uliiangaza nyumba ya Abbas.

Yeye, mkewe Ummul Fadhl na mimi mwenyewe tulisilimu, lakini tuliificha itikadi yetu kwa kuwachelea watu. Taarifa za kuuawa kwa maadui wa Uislamu kule Badr zilipoenea tulifurahi mno. Hata hivyo, Waquraishi na wasaidizi wao walihuzunika na kushituka mno.

Abu Lahab ambaye hakushiriki kwenye vita hivi na badala yake alimpeleka mtu mwingine, alikuwa ameketi karibu na kisima cha Zamzam. Mara kwa ghafla watu wakaleta taarifa ya kwamba Abu Sufyan ibn Harb amefika. Abu Lahab akasema: “Mwambie aonane nami upesi iwezekanavyo.”

Abu Sufyani alikuja, akakaa karibu na Abu Lahab na akampa tarifa kamili ya matukio ya Badr. Abu Lahab akakumbwa na fadhaa na woga moyoni mwake kama aliyepigwa na radi. Baada ya kuunguzwa na homa kali kwa muda wa siku saba alikufa kwa maradhi yasiyoeleweka.

Hadith ya kushiriki kwenye vita vya Badr kwa baba mkubwa wa Mtume (s.a.w.w.) (aliyekuwa mmoja wa watu waliotekwa na Waislamu) ni moja ya matatizo ya historia. Yawezekanaje kwamba Abbas aliwasisitiza watu wa Madina wakati wa mapatano ya 'Aqabah' kumsaidia Mtume (s.a.w.w.) na kisha aambiwe kwamba alishiriki katika vita hii?

Utatuzi wa tatizo hili umo katika yale maneno aliyoyasema yule mtumwa wake Raafi. Anasema kwamba alikuwa mmoja wa watu ambao, kama alivyokuwa kaka yake Abu Twalib, aliuamini Upweke wa Allah na Utume wa mwana wa nduguye, lakini aliificha itikadi yake, akiyazingatia mahitaji ya wakati ule, ili aweze kumsaidia mwana wa nduguye na kumtaarifu juu ya mipango miovu ya Waquraishi, kama alivyofanya wakati wa Vita vya Uhud.

Kuenea kwa taarifa za kuuwawa kwa watu sabini kutoka miongoni mwa wapenzi wa Waquraishi zilizababisha wasiwasi kwenye familia nyingi na kuzifanya kuwa na huzuni na majonzi.[31]

Mayowe Na Maombolezo Yapigwa Marufuku

Ili kuwaweka Waquraishi katika hali ya ghadhabu na uchungu na kuhakikisha kwamba daima watu watakuwa tayari kulipiza kisasi cha damu ya mashujaa wao, Abu Sufyan ibn Harb alitoa amri ya kwamba hakuna yeyote atakayekuwa na haki ya kulia au kuomboleza wala mshairi yeyote yule asisome beti za maombolezo kwa kuwa vitu hivi hupunguza hisia za kulipiza kisasi na matwezo ya mara kwa mara ya maadui. Ili kushawishi chuki miongoni mwa watu, vile vile alitangaza ya kwamba hatalala na mwanamke yeyote mpaka atakapolipiza kisasi juu ya waislamu kwa ajili ya damu ya wale waliouawa kule Badr.

Aswad bin Muttalib alipatwa na uchungu mwingi kutokana na kuwapoteza wanawe watatu. Mara, ghafla akasikia mayowe ya kilio cha mwanamke mmoja. Alifurahi na akadhania ya kwamba kule kuwalilia wale waliouawa Badr kumeruhusiwa. Alituma mtu kwenda kuithibitisha dhana yake. Hata hivyo, matokeo ya uchunguzi huu hayakuwa sawa na alivyotaka, kwa sababu yule mwanamke alikuwa akimlilia ngamia wake aliyepotea, na kumlilia ngamia aliyepotea hakukupigwa marufuku kufuatana na ile amri ya Abu Sufyan. Aswad alilihisi mno jambo hili na akatunga beti za shairi. Hapa chini tunatoa tafsiri ya beti mbili miongoni mwazo:

"Je, anamlilia ngamia wake aliyepotea, na je anakesha katika nyakati za usiku kwa kule kumpoteza kwake? Hapana. Haistahili wakati huu kwamba amlilie ngamia wake. Bali ni muhimu kwamba alie kwa ajili ya wale waliouawa na ambao kwa kifo chao furaha, heshima na utukufu navyo vimepotea."[32]

Uamuzi Wa Mwisho Juu Ya Mateka

Kwa mujibu wa sheria za Kiislamu wafungwa wa kivita huwa watumwa wa Waislamu na kila mmoja wao anahitajika kufanya kazi kwa nguvu zake zote. Watu walioelimika hutumikishwa katika kuwaelimisha wenzao na wataalamu wa viwanda hutoa elimu kwenye nyanja ya viwanda. Watumwa hawa hawawezi kuwa huru mpaka wanunuliwe kwanza na mtu fulani, hii imekuwa ni kawaida aliyokuwa akiitumia Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu kwenye vita vilivyopiganwa na utekaji wa nchi walioufanya.

Hivyo, kuhusiana na vita hivi (vya Badr), iliamuliwa ya kwamba watu wenye elimu wangeliweza kuwa huru kama wangeliwafundisha wavulana kumi kusoma na kuandika. Wengine wangeliweza kununua uungwana wao kwa kulipa fidia ya kiasi cha kuanzia dirhamu elfu moja hadi elfu nne. Na kuhusu watu walio maskini, waliweza kuachiliwa bila ya kutozwa fidia yoyote.

Taarifa hizi zilipofika Makka zilileta furaha kuu miongoni mwa ndugu wa wale mateka na wakapeleka pesa za kulipia fidia mjini Madina ili waweze kuachiliwa. Suhayl bin Amr alipoachiliwa kwa kulipa fidia, Sahaba mmoja wa Mtume (s.a.w.w.) aliomba ruhusa kumng'oa Suhayl meno yake ya mbele ili baada ya hapo asije akausema tena Uislamu kwa ubaya. Mtume (s.a.w.w.) hakutoa ruhusa ya kufanya hivyo na akasema kwamba hiyo ilikuwa sawa na kumtia mtu kilema, jambo lisiloruhusiwa kwenye Uislamu.

Abil Aas, mkwewe Mtume (s.a.w.w.) na mume wa binti yake[33] Zaynab, alikuwa mfanya biashara mwenye kuheshimika wa mjini Makka. Alimwoa Zaynab kwenye zama za Ujinga[34] naye hakusilimu baada kuanza kwa kazi ya Utume. Vilevile alishiriki kwenye vita ya Badr na alitekwa wakati mkewe Zaynab alikuwa mjini Makka. Ili kumkomboa mumewe alipeleka Madina kidani alichopewa na mama yake, Bibi Khadija wakati wa ndoa yake.
Mtume (s.a.w.w.) aliwahi kukiona kile kidani alichokileta binti yake. Alilia na akaikumbuka mihanga mikubwa mikubwa aliyoitoa Bibi Khadija kwa ajili ya Uislamu na utajiri mwingi alioutumia kwa ajili ya maendeleo ya dini ya Allah. Ili kuithibitisha heshima kwa mali ya umma aliwageukia wafuasi wake na kuwaambia: "Kidani hiki ni mali yenu nanyi munayo haki kamili juu yake. Kama mtakubali kinaweza kurudishwa na Abil Aas anaweza kuachiliwa bila ya kumtoza fidia yoyote ile." Masahaba zake walikubali maoni yake.

Kauli Ya Ibn Abil Hadid

Anasema: "Nililitaja tukio la kidani cha Zaynab mbele ya mwalimu wangu Ja'afar Basri Alawi na akaithibitisha, lakini akaongezea kusema: "Je, haikufaa kwamba makhalifa wangalimfariji Fatimah kwa kumrudishia Fadak japo idhaniwe kwamba ilikuwa ni mali ya Waislamu?" Nikasema: "Kwa mujibu wa Hadith moja, Mitume hawaachi urithi wowote na kwa sababu hiyo, Fadak ni mali ya Waislamu. Katika hali hii, vipi mali ya Waislamu apewe binti wa Mtume?" Yule mwalimu akasema: "Je, kile kidani alichokipeleka Zaynab kwa ajili ya kuachiliwa kwa Abil Aas, hakikuwa mali ya Waislamu?'

Abil Hadid anasema: "Nikasema kwamba Mtume alikuwa ndiye mtoa sheria naye alikuwa na mamlaka

kwenye mambo yote, ambapo wale makhalifa hawakuwa na madaraka ya aina hiyo.35 Mwalimu akasema: Sisemi kwamba wale makhalifa waichukue Fadak kwa nguvu kutoka kwa Waislamu na kumpa Fatimah. Ninalosema mimi ni kwamba mtawala wa wakati ule hakuwataka ushauri Waislamu kuhusu kurudisha Fadak. Kwa nini hakusimama kama alivyofanya Mtume na kusema: “Enyi watu! Fatimah yu binti wa Mtume wenu. Anataka kwamba bustani ya Fadak iwe chini ya mamlaka yake kama ilivyokuwa kwenye zama za uhai wa Mtume. Je, mnakubali kwamba Fadak irudishwe kwake?”

Ibn Abil Hadid anaandika mwishoni hivi: “Sikuweza kusema lolote katika kuyajibu maelezo ya kiufasaha ya yule mwalimu na nilisema haya tu katika kuyaunga mkono: ‘Abul Hassan Abdul Jabbar naye amewalaumu makhalifa kuhusiana na jambo hili na anasema kwamba ingawa matendo yao yaliafikiana na sheria,36 hawakujali heshima na cheo alichostahiki Zahra.37

1. Biharul Anwaar, Juzuu 19, uk. 217.
2. Maghaazil-Waaqid, Juzuu 1, uk. 20.
3. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 81.
4. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 138, na Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 82.
5. Siiratu Ibn Hishamu, Juzuu 2, uk. 248-249.
6. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 48.
7. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 82.
8. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu1, uk. 615.
9. Al-Imtaa'ul Asmaa' uk. 74.
10. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 140.
11. Maghaazil-Waaqidi, Juzu 1, uk. 248; SiiratuI Halabi, Juzuu 2, uk. 160; na Bihaarul Anwaar, Juzuu 19, uk. 217.
12. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 140.
13. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, Uk. 48; Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 615.
14. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 617.
15. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 620; na Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 144.
16. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 145. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 620;
17. Tabaqaat, Juzuu 2, uk. 25.
18. Nahjul Balaghah, Kalimaatu Qasaar, uk. 214.
19. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 622.
20. Maghaazi, Juzuu 1, uk. 62; na Bihaarul Anwaar, Juzuu 2, uk. 234.
21. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 148; na Siiratu Ibn Hisham, Juzuuu 1, uk. 625.
22. Nahjul Balaghah, Barua 28 na 46.
23. Tarikhu Ibn Hisham, Juzuu I, uk. 626.
24. Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 149.
25. Siiratu Ibn Hisham, Juzuuu 1, uk. 628.
26. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juzuu 2, uk. 23.
27. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 206-207; Maghaazi, Juzuu 1, Uk. 137-138.
28. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 117.
29. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 645.
30. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 645..
31. Fahristun-Najaashi, uk. 5.
32. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 648.
33. Binti wake wa kulea.
34. Maelezo haya ni hoja yenye nguvu mno kuthibitisha kuwa mabinti hawa watatu, Zainab, Ruqayya na Ummu Kulthum

hawakuwa mabinti wa kuzaa wa Mtume, kwani ni dhahiri isingelifikirika kwa mtu kama Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa na shakhsia ya tawhidi kabla ya kukabidhiwa utume, kuwaoza mabinti zake kwa mtu aliyekuwa na kila dalili ya miale ya moto wa shirk – Mhariri

35. Sasa twaweza kumuuliza Abil Hadid ikiwa hivyo ndivyo, ni mantiki gani imewasukuma kuuridhia uharamisho wa Umar juu ya ndoa ya muda? Na kwa nini mwawahimiza wafuasi wenu kuiendea sala ya tarawehe iliyoasisiwa na Umar? – Mhariri.

36. Kwa mtazamo wake yameafikiana na sheria, na kama hadithi za kuzushiwa Mtume ndio sheria anayoifikiria yeye, basi ajue ipo Siku ya malipo. Lakini kama Qur'ani ndio sheria, basi hamna shaka kuwa kwa mujibu wa Qur'anii kitendo hicho ni unyang'anyi na dhulma dhidi ya mali na milki ya Fatimah Zahra (a.s.) –Mhariri.

37. Sharhun– Nahjul Balaghah cha Ibn Abil Hadid, Juzuu 14, uk. 191.

Sura Ya 31: Mipango Ya Hatari Ya Wayahudi

Vita vya Badr vilikuwa dhoruba ya kuogofya iliyovuma katikati ya Rasi ya Uarabuni. Hii ni dhoruba iliyong'oa mizizi mingi ya kale ya ushirikina na ibada za masanamu. Baadhi ya mashujaa na watetezi wa Waquraishi waliuwawa au kutekwa na wengine walikimbia katika hali ya kufedhehesha mno. Taarifa za kutimuliwa kwa Waquraishi zilienea kila mahali Uarabuni. Hata hivyo, baada ya dhoruba hii, ilikuwapo aina fulani ya utulivu kwa kitambo hivi ulioandamana na hofu na mshtuko wa fikara, utulivu huu wa kitambo fulani ulipitwa mara kwa mara na taswira ya hali ya ujumla ya siku zijazo ya Rasi ile.

Makabila yaliyokuwa yakiabudu masanamu, Wayahudi matajiri wa Madina na Wayahudi wa Khaybar na Wadiul Quraa walikuwa wakiyaogopa sana maendeleo endelevu ya ile serikali mpya, na waliyaona maisha yao kuwa yako kwenye hatari kwa sababu hawakuamini ya kwamba Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) atakuwa na nguvu kiasi kwamba atawaangamiza Waquraishi waliokuwa na nguvu zenye umri wa karne nzima.
Wayahudi wa kabila la Bani Qaynaq? waliokuwa wakiishi mjini Madina nao waliutawala uchumi wa mji ule, waliogopa zaidi kuliko wengine, kwa sababu maisha yao yalichanganyika kabisa na yale ya Waislamu na ilikuwako tofauti baina yao na wale Wayahudi wa Khaybar na Wadiul Quraa walioishi nje ya mji wa Madina na mbali kutoka kwenye ukanda ulio chini ya mamlaka ya Waislamu. Hivyo basi, kwa sababu hii, kabila la Qaynaq? likajishughulisha zaidi kuliko wale wengine na wakaanzisha vita baridi vya propaganda kwa kueneza maneno yenye kuchochea na mashairi ya uchochezi. Hivyo, kivitendo wakayakataa yale mapatano yaliyofanywa katika mwaka wa kwanza wa Hijiriya.

Hata hivyo, vita hivi baridi havikuhalalisha kwamba majeshi ya Uislamu yajibu kwa silaha kali, kwa sababu, kama fundo laweza kufunduliwa kwa vidole, basi si lazima kulifundua kwa meno. Zaidi ya hapo Mtume (s.a.w.w.) aliweka mbele umuhimu wa kudumisha umoja wa kisiasa na sheria na kanuni njema.

Akitoa onyo lake la mwisho kwa Wayahudi, Mtume (s.a.w.w.) alitoa hotuba kali kwenye soko la Bani Qaynaq?'. Katika hotuba hii aliwaeleza Wayahudi mambo mengi likiwamo hili: "Majaaliwa ya Waquraishi

yamewatendea haki. Ni fundisho kwenu ninyi vile vile. Ninachelea ya kwamba msiba huu huu unaweza kukukamateni. Wako wasomi na wanachuoni wa kidini miongoni mwenu. Hamna budi kuthibitisha kutoka kwao ili kwamba waweze kukuelezeni wazi wazi kwamba mimi ni Rasuli wa Allah na kwamba ukweli huu umeandikwa kwenye kitabu chenu (Taurati).”

Wayahudi hao wakaidi na wenye kiburi, sio tu kwamba hawakunyamaza baada ya kuyasikia maneno ya Mtume (s.a.w.w.), bali walimjibu kwa kauli yenye kukasirisha, wakasema: “Je, unafikifi sisi ni wanyonge na tusiozijua mbinu za kivita kama Waquraishi? Mlilikabili kundi lisilokuwa na ujuzi wa kanuni na mbinu za mapigano. basi nguvu ya wana wa Qaynaq? itakudhihirikieni mtakapokutana nao kwenye uwanja wa vita.”1

Maneno machungu na ya dharau ya Bani Qaynaq?’ na kule kuimba yale maneno ya uchochezi wa vita na tenzi za watetezi wao havikuwa hata na athari zozote mbaya katika tabia za Waislamu. Hata hivyo, walipewa onyo la mwisho kwa mujibu wa kanuni ya siasa za Kiislamu na ilidhihirika ya kwamba wakati ule, lile fundo lilibidi kufunguliwa kwa njia nyingine au sivyo ujasiri, uasi, na udhalimu vitaongezeka siku hadi siku. Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) alisubiri apate fursa ya kuwapa Wayahudi wale adhabu kali.

Cheche Yawasha Moto Wa Vita

Wakati mwingine inatokea kwamba jambo dogo hupelekea kwenye mapinduzi makubwa na mabadiliko ya kijamii, yaani tukio dogo hupelekea kwenye tukio kuu na makundi husika huchukua njia ya kumaliza matukio mengi mengineyo pia (ukiachilia mbali tukio lile).

Sababu ya kuanza kwa vita vya kwanza vya dunia, ambavyo ni moja ya tukio kuu la historia ya mwanadamu, ilikuwa ni tukio dogo tu, lililotoa sababu kwa mataifa makuu kujitumbukiza kwenye vita. Tukio lililokuwa sababu ya kuanza kwa vita hivyo lilikuwa ni kuuawa kwa mwana wa Mfalme Fransis Ferdinand aliyetegemewa kuwa mrithi wa kiti cha enzi cha Austria. Tukio hili lilitokea mnamo tarehe 28 Juni 1914 na baada ya mwezi mmoja na siku chache, Vita vya kwanza vya Dunia vilianza kwa Ujerumani kuishambulia Ubelgiji. Matokeo ya vita hivi ni kwamba watu milioni kumi waliuawa na wengine milioni ishirini walijeruhiwa.

Waislamu waliudhishwa mno na ukaidi na kiburi cha Wayahudi na walikuwa wakisubiri watende tukio baya ili Waislamu waamke dhidi yao. Siku moja ilitokea kwamba mwanamke mmoja wa kiarabu alikwenda kwenye mtaa wa masoko wa Bani Qaynaq? kuuza kitu fulani karibu na duka la sonara wa kiyahudi. Yule mwanamke alijihadhari kwamba mtu yeyote asiuone uso wake (yaani alivaa Hijab). Hata hivyo, Wayahudi wa Bani Qaynaq? walishikilia ya kwamba afunuliwe uso wake. Kwa kuwa alikataa kufanya vile, yule mwuza duka alitoka dukani mwake na kuushona ukaya wa vazi lake mgongoni mwake.
Matokeo yake ni kwamba yule mwanamke alipoamka baada ya kitambo kidogo, sehemu ya mwili wake ikawa wazi. Baada ya hapo wale wanaume (wa Bani Qaynaq?) wakamdhihaki.

Suala la sifa na heshima, jambo lililo muhimu kwenye kila jamii, lilipewa muhimu sana miongoni mwa Waarabu, na hasa miongoni mwa makabila ya kibedui ambao walikimbilia umwagaji damu kutokana na shutuma ndogo mno juu ya heshima yao. Hivyo basi, hali ya kusikitisha ya yule mwanamke mgeni, iliibua hisia za Mwislamu, naye akamuua yule sonara.

Kwa kawaida kitendo hiki kilichotendwa kwenye eneo la Wayahudi wenyewe kisingeliweza kuachwa bila ya kuchukuliwa hatua kutoka upande wao. Hivyo, wakamshambulia yule mwislamu kwa pamoja na wakamwua.

Hatuhusiki juu ya ukweli ya kwamba mauji ya yule Myahudi yaliyotokana na kumtusi yule mwanamke yaliafikiana na kanuni na sababu za kiakili au la. Hivyo, Mwislamu mmoja tu kushambuliwa na mamia ya Wayahudi kwa pamoja, kulikuwa jambo la kuudhi mno.

Hivyo, taarifa za mauaji ya kimsiba na kusikitisha ya yule mwislamu zilizikoroga hisia za kiutu za Waislamu waliodhamiria kuliweka sawa jambo lile na kukiharibu kabisa kituo cha ufisadi.

Wasomaji wa tenzi wa Bani Qaynaq? walitambua kwamba jambo lile limekuwa gumu nalo halikuwezekana tena kwao kushauriana na kuendelea na biashara zao kwenye masoko na mitaa ya Madina. Hivyo, upesi sana wakakimbilia kwenye nyumba zao zilizo kwenye ngome ndefu na madhubuti na kuingia humo ingawa walikuwa wakizisoma zile tenzi zao kwa ushujaa mkuu.

Pia walifanya kosa kwa kupanga kufanya hivi. Kama wangalijuta kwa yale waliyoyatenda na wakaomba msamaha bila shaka wangaliweza kusuluhisha mambo na Waislamu kutokana na tabia ya msamaha ya Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, kule kujifungia kwenye ngome zao kulikuwa ni dalili ya upinzani na uadui unaoendelea. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ile ngome ya adui izingirwe.

Majeshi ya Waislamu yaliizunguka ngome yote tangu kwenye mwishilizio mmoja hadi ule mwingine. Kuzingirwa huku kulidumu kwa siku kumi na tano na kuingia kwa mahitaji ya maisha kwenye ngome hiyo kulizuiwa. Mawasiliano yoyote na watu hawa yalipigwa marufuku pia.

Wayahudi walipiga magoti ikiwa ni matokeo ya vizuizi vya kiuchumi. Walilifungua lango la ngome ile, baada ya kutoa ishara za masharti yaliyotakiwa wakajisalimisha kwa Waislamu. Vile vile waliamua ya kwamba uamuzi wa Mtume (s.a.w.w.) vyovyote vile iwavyo, wataufuata.

Mtume (s.a.w.w) alidhamiria kutoa adhabu kali kwa wakaidi na wapinzani wa umoja wa kisiasa mjini mle Madina.

Hata hivyo, aliepuka kuchukua hatua kutokana na msisitizo wa Abdullah bin Ubay aliyekuwa mmoja wa wanafiki wa Madina na akasilimu kwa dhahiri. Hivyo basi, iliamuliwa kwamba Wayahudi wasalimishe silaha na utajiri wao na wautoke mji wa Madina upesi iwezekanavyo na jukumu hili litimizwe chini ya ukaguzi wa afisa mmoja aliyeitwa Ubadah bin Saamit.

Wayahudi hawakupata njia yoyote nyingine ila kuutoka mji wa Madina na wakaenda Wadiul Qara na

baada ya hapo kwenda Azra'aat kwenye ukanda wa Shamu.

Umoja wa kisiasa wa Madina ulirudi tena kwa kutolewa kwa Wayahudi wa Qaynaq?'. Wakati huu umoja wa kisiasa uliungwa na umoja wa kidini pia, kwa sababu tukiwaachilia mbali Waislamu, hakukuwepo watu wengine walio wengi mjini Madina, na idadi ya Waarabu wenye kuabudu masanamu na wanafiki ilikuwa ndogo mno ikilinganishwa na ile ya waumini.[2]

Taarifa Mpya Zafika Madina

Katika maeneo madogo, kwa kawaida tarifa huenea upesi kama radi, kutoka mtu hadi mtu. Kwa sababu hii, taarifa zenye kuhusu njama za kufanya mabaya na mikutano dhidi ya Waislamu kwenye kila mkoa zilifika makao makuu ya Uislamu upesi sana kupitia kwa wasafiri waadilifu na marafiki walio macho. Zaidi ya hapo Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe binafsi alikuwa mfahamivu mno na alizikomesha njama za kufanya ubaya tangu mwanzoni kabisa. Mara tu baada ya taarifa kupokewa kwamba kabila fulani lilikuwa likipanga kukusanya silaha na watu, upesi sana alipeleka kikosi kulizuia lile lengo la yule adui, au yeye mwenyewe alikwenda upesi sana akifuatana na jeshi litoshelezalo, na kulizingira lile eneo la adui na kuushinda mpango wake. Zifuatazo hapa chini ni mukhtasari wa baadhi ya Ghazwaah (vita ambazo Mtume s.aw.w alishiriki) zilizopiganwa katika mwaka wa pili wa Hijiriya.

Ghazwatul Kadar

Jimbo la ukanda wa kati wa kabila la Bani Salim uliitwa Kadar. Ilipokewa taarifa mjini Madina kwamba watu wa kabila lile walikuwa wakipanga kukusanya silaha na kuja kuyashambulia makao makuu ya Uislamu. Mtume (s.a.w.w.) alipotoka mji wa Madina alimteuwa mtu mwingine kuwa mwakilishi wake na kuyaweka mambo ya serikali mikononi kwake.

Safari hii alimteuwa Ibn Ummi Makhtum kuwa naibu wake mjini Madina, na yeye akatoka pamoja na kikosi kwenda kwenye mkoa wa katikati wa Kadar.

Hata hivyo, wale maadui walikuwa wametawanyika kabla ya kuwasili kwa Waislamu. Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alirejea Madina bila ya mapigano yoyote yale, lakini kwa kujiridhisha kwake alipeleka tena jeshi mahali pale pale chini ya uongozi wa afisa mmoja aliyeitwa Ghalib Abdullah. Jeshi hili lilirudi na ushindi baada ya mapigano madogo ambayo ndani yake watu wao watatu waliuawa.[3]

Ghazwatus-Sawiiq

Waarabu wa zama za ujahilia walikuwa wakifanya viapo vya ajabu. Kwa mfano, baada ya vita vya Badr Abu Sufyan aliapa kwamba hatamkaribia mkewe mpaka alipize kisasi juu ya Waislamu kwa kuuawa kwa Waquraishi. Ili kukitimiza kiapo chake hiki alilazimika kuendesha mashambulizi. Alisafiri na watu mia mbili na kwa msisitizo wa Salam bin Mushkam, chifu wa kabila la Kiyahudi la Bani al-Nuzayr, waliokiishi nje ya Madina, Abu Sufyan alimuuwa mwislamu mmoja na akachoma bustani ya mitende kwenye jimbo

la Arz. Upesi sana mtu mmoja akatoa taarifa ya tukio lile mjini Madina. Mtume (s.a.w.w.) alitoka mjini Madina na kumfuatilia yule adui kiasi cha umbali fulani. Hata hivyo, Abu Sufyan na wapiganaji wake walikuwa wameshakimbia. Yule adui akiwa njiani aliacha mifuko ya 'Sawiiq' (chakula kilichotayarishwa kwa unga na tende). Waislamu waliichukua mifuko ile na wakavipa vita hivi jina la '*Ghazwatus Sawiiq*.'[4]

Ghazwah Zil Amr

Taarifa zilifika mjini Madina kwamba watu wa kabila lililokuwa likiitwa 'Ghatfan' wamekusanyika pamoja na walidhamiria kuuteka mji wa Madina. Mtume (s.a.w.w.) alitoka na watu mia nne na hamsini kwenda kuwakabili maadui hawa. Maadui wakawa na woga na wakakimbilia kwenye milima. Wakati ule ule ilinyesha mvua kubwa na nguo za Mtume (s.a.w.w.) zililowa. Hivyo, alikwenda umbali fulani kutoka pale lilipokuwa jeshi lake. Hapo akazivua nguo zake akakaa chini ya kivuli. Wale maadui walikuwa wakimwona Mtume (s.a.w.w.) pale.
Shujaa mmoja kutoka miongoni mwao akajinufaisha na hali ile. Alishuka kutoka kule mlimani akiwa kashika upanga uliofutwa na akiwa amesimama karibu na Mtume (s.a.w.w.) alisema kwa sauti ya ukali: "Ni nani awezaye kukuokoa wewe leo hii kutokana na upanga wangu mkali?"

Mtume (s.a.w.w.) akamjibu kwa sauti kuu: "Allah." Neno hili lilikuwa na athari kubwa mno juu ya mtu huyu kiasi kwamba alianza kutetemeka kwa woga, na ule upanga ukamponyoka ukaanguka. Mtume (s.a.w.w.) akasimama upesi, akauokota, akaanza kumkabili na kumwambia: "Ni nani sasa awezaye kukuokoa kutokana nami?" Kwa kuwa yule mtu alikuwa muabudu masanamu na alijua ya kwamba miungu wake wa miti hawakuwa na uwezo wa kumhami kwenye ule wakati mgumu, alijibu akisema: "Hakuna."

Wanahistoria wanasema kwamba yule mtu alisilimu pale pale lakini kitendo hiki hakikutokana na woga kwa sababu alibakia kuwa madhubuti kwenye imani yake. Sababu ya kusilimu kwake ni mwamko wa tabia yake, kwa sababu kushindwa kwake asikotegemea na kwa kimiujiza kulizigeuzia fikara zake kwenye ulimwengu mwingine na akatambua kwamba Mtume (s.a.w.w.) anao uhusiano na ulimwengu ule. Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka kwenye ulimwengu wake (uhusianao na kusilimu kwake) na akamrudishia upanga wake. Baada ya mtu yule kwenda mbele kidogo akampa Mtume (s.a.w.w.) ule upanga wake, na akasema: "Kwa vile wewe u kiongozi wa hili jeshi la kuongoza watu waliopotea, unayo haki zaidi ya kuimiliki silaha hii."[5]

Waquraishi Wabadili Njia Yao Ya Msafara Wa Kibiashara

Pwani ya Bahari ya Shamu imekuwa na hatari kwa Waquraishi kutokana na jeshi la Kiislamu na watu waliofanya mapatano na Waislamu. Hivyo basi, walifanya mkutano wa ushauriano na kuisoma ile hali. Wakaambiana: "Kama biashara yetu ikiahirishwa, pole pole tutaipoteza mitaji yetu na matokeo yake yatakuwa ni kusalimu amri kwa Waislamu. Na kama tukiendelea na biashara, hatuna tegemeo la kufaulu, kwa sababu kwa kawaida Waislamu huzinyakua bidhaa zetu tunapokuwa njiani."

Mmoja wao alishauri kwamba waende Shamu kupitia Iraq na ushauri huu ulikubaliwa na watu wengi kwa pamoja. Hivyo matayarisho yakafanywa kupeleka msafara pamoja na bidhaa. Abu Sufyan na Safwaan bin Umayyah binafsi walisimamia msafara ule na mtu mmoja aliyeitwa Furaat Hayyaan, wa kabila la Bani Bakr, alikuwa mwongozaji wao.

Maqrizi anaandika hivi: "Mtu mmoja wa Madina aliangalia mwenendo wa msafara ule. Aliporejea Madina alilieleza jambo lile kwa rafiki yake. Mtume (s.a.w.w.) alilitambua upesi sana na akapeleka jeshi kuelekea kwenye njia ya msafara ule chini ya uongozi wa afisa mmoja aliyeitwa Zayd bin Haarith. Kwa kuwakamata watu wawili na kuzikamata bidhaa zao waliwazuiya maadui kuendelea na safari yao." 6

1. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 176.
2. Maghaazil-Waaaqidi, Juzuu 1, uk. 177-179; na Tabaqaatul-Kubra, Juzuu 2, uk. 27-38.
3. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 182; na Tabaqaatul Kubra; Juzuu 2, uk.30.
4. Maghaazil-Waqidi, Juzuu 1, uk. 181.
5. Manaqib, Juzuu 1, uk. 164; na Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 194-196.
6. Al-Imtaa', uk. 112.

Sura Ya 32: Matukio Ya Mwaka Wa Tatu Hijiriya

Mwaka wa tatu wa hijiriyya ulianza na mapambano madogo madogo na vita vilivyotawanyika, zenye sura ya kujihami na zilizopiganwa kwa lengo la kukomesha njama za makabila ya wenye kuyaabudu masanamu katika hatua ya mwanzo kabisa. Hata hivyo, vita vya Uhud vyastahili kuzingatiwa mno miongoni mwa matukio ya mwaka wa tatu. Vita hivi ni mfano ung'arao wa kuihami dini takatifu ya Uislamu, itikadi ya upweke wa Allah na uhuru wa kuabudu.

Haitafaa hata kidogo kuipa jina la 'Vita' au 'Ghazwah' ile mihanga waliyoitoa Waislamu, kwa sababu hawakupanga wao kupigana vita bali walilazimika kuzishika silaha kwa ajili ya kuuhami Uislamu tu na kuhakikisha ya kwamba unapatikana uhuru wa kuabudu.

Waliwarudisha nyuma baada ya kuwatia hasara kubwa, wale watu waliokuja kutoka Makka na sehemu za jirani yake kuja kuushambulia mji wa Madina ili kuwaangamiza wenye kumwabudu Allah na watafutaji wa uhuru, na Waislamu hawakuwa na lolote jingine la kufanya isipokuwa kuwajibu wadhalimu katili na watesaji kwa jeshi na silaha kali.

Sababu Za Vita Ya Uhud

Mashambulizi ya pamoja yaliyofanywa na wenye kuabudu masanamu yalikuwa ni matokeo ya nyororo ya visababisho vya ndani na vya nje vilivyolileta jeshi kubwa mjini Madina ili kulipiza kisasi.

Mtu mmoja hatari sana aliyekuwa akiitwa Ka'ab bin Ashraf ndiye aliuwasha moto huu. Alikuwa Myahudi

kwa mama yake, lakini yeye mwenyewe alikuwa muabudu masanamu. Alikuwa akiufaidi ulinzi wa Dola ya Kiislamu na hakupatwa na dhara lolote kwenye Vita vya Badr, lakini kutokana na uadui aliokuwa nao dhidi ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alikwenda Makka na akamiminikwa na machozi ya mamba kwenye mikutano ya Waquraishi na kuwakumbusha jinsi machifu wao walivyouawa na kutekwa. Aliudhihirisha ubingwa kwenye kazi hii kiasi kwamba wazee na vijana wa Waquraishi wakawa tayari kwenda kupigana na Mtume (s.a.w.w.) na kuiangusha serikali ya Kiislamu.

Ili kuziibua hasira za watu wa Makka, Ka'ab aliusifu uzuri wa wanawake wa Kiislamu kwa jinsi ambavyo watu wa Makka wote waliidhihirisha nia yao ya kwenda kupigana dhidi ya Waislamu ili waweze kuwashinda na kuwateka wanawake wao na kuzitosheleza tamaa zao mbaya. Vile vile aliziimba beti fulani fulani za tenzi zihusianazo na jambo hili na ndani ya beti hizo aliweka bila ya aibu yoyote yale majina na maelezo ya wanawake fulani na kuwaeleza kwa maelezo yasiyo ya adabu njema juu yao. Baada ya kutekeleza mpango wake alirejea Madina na kukimbilia kwenye ngome yake.

Nini jukumu la Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu kuhusiana na mtu huyu aliyeibua hasira za watu? Aliuwasha moto ambao miali yake iliwachoma hadi kuwa majivu askari mashujaa wa Uislamu sabini akiwamo Hamza, na ukasababisha kutiririka kwa damu ya wacha Mungu katika ardhi ya Uhud.

Watu wa kabila la Aws waliamua kuwaondolea Waislamu ufisadi wa Ka'ab. Watu wawili waitwao Muhammad bin Maslamah na Abu Naa'ilah waliwasili kwenye ngome yake kwa kujifanya marafiki na wakamlaumu Mtume (s.a.w.w.) na dini yake.

Waliongezea kusema kwamba tangu kufika kwa Mtume mjini Yathrib watu wote wamekuwa wakizungukwa na misiba na watu wao na mali zao vimeangamizwa. Wakaikuza mno maudhui hii kiasi kwamba Ka'ab akafikiria kwamba maoni yao juu ya maudhui ile yalikuwa sawa na yake. Kisha wakasema: "Sasa tumekuja kununua nafaka kutoka kwako na tunalazimika kuweka rehani kitu fulani, kwa sababu hivi sasa hatuna pesa."

Ka'ab alikubali kuwauzia nafaka, lakini kuhusu kile kitu cha kuweka rehani, alitamka maneno yaliyodhihirisha tabia zake mbaya na chafu, kwa kuwa alitamka tena bila ya aibu, hivi: "Ni lazima wanawake na watoto wenu wabakie kwenye mamlaka yangu kwa njia ya rehani." Maelezo yake yaliwashitua mno hawa watu wawili kiasi kwamba walimjibu wakisema: "Je, yawezekana?"

Kusema kweli watu hawa wawili hawakutaka kununua nafaka. Walirudi na kuunda makri ya kumwua. Hivyo basi, mara moja waliomba waziache silaha zao kwake ili ziwe kama dhamana. Lengo lao la kuomba hivyo lilikuwa kwamba, watu hawa wawili wenye silaha watakapoiendea ile ngome yake atadhania ya kwamba wamekuja kuziacha silaha zao kwake ili ziwe rehani na wala sio kwamba walikuwa wamepanga mpango mwovu dhidi yake.

Wakati wa usiku kikundi cha watu wa Aws wenye silaha walijikusanya kuizunguka ngome yake, wakijifanya kwamba wamekuja kununua nafaka. Muhammad bin Maslamah, aliyekuwa ndugu wa kambo wa Ka'ab alimwita Ka'ab, lakini mkewe alikataa mumewe asitoke nje kwenye giza la usiku, lakini

kutokana na yale mazungumzo ambayo Ka'ab alikuwa tayari kaishayafanya nao, alitoka nje ya ile ngome kwa matumaini kamili wala hakuwa na shaka yoyote kutokana na kuwa kwao na silaha. Baada ya kumzunguka, walielekea kwenye bonde, kana kwamba walikuwa wakienda kuonyesha bidhaa au kwenda kuichukua.

Walikuwa bado hawajakwenda mbali zaidi kutoka kwenye ile ngome wakati wale watu wa Aws ghafla walipomvamia na kumkata vipande vipande. Kwa njia hii adui hatari, mpelelezi fisadi na mtu mwovu, ambaye tamaa yake kuu daima imekuwa ni kuwapiga pigo Waislamu, aliondolewa kutoka kwenye njia yao.

Mara baada ya kuuwawa kwa Ka'ab Myahudi mmoja aitwaye Abu Raafi, aliyezifuata nyayo za Ka'ab na wakati mmoja alikuwa pamoja naye kwenye jambo la upepelezi na uchochezi, naye aliuawa. Ibn Athir ameliandika tukio hili kwa kirefu kwenye historia yake.[1]

Waquraishi Waamua Kuzikabili Gharama Za Vita

Mbegu ya maangamizi na ghasia ilikuwa tayari imeshapandwa mjini Makka kwa kipindi kirefu hivi. Kule kupigwa marufuku kuwaomboleza waliouawa Badr kuliimarisha hisia ya kulipiza kisasi. Kufungwa kwa ile njia ya kibiashara ya watu wa Makka kupitia Madina na Iraq kumewafanya wakose raha kabisa. Ka'ab bin Ashraf aliongeza mafuta kwenye moto huu na kuuwasha.

Kwa sababu hii, Safwaan bin Umayyah na 'Ikrimah bin Abu Jahl walimshauri Abu Sufyan kwamba, kwa vile machifu na askari wa Waquraishi wameuwawa kwa ajili ya kuhami msafara wa biashara wa Makka, ingalifaa kwamba kila mmoja wa wale waliokuwa na mafungu ya bidhaa zilizokamatwa katika msafara wao ule atoe fungu kwa ajili ya kuzikabili gharama za vita. Mpango huu ulipata idhini ya Abu Sufyan na ukatekelezwa upesi sana.

Machifu wa Waquraishi waliokuwa wakiitambua nguvu ya Waisilamu na kwa karibu zaidi wameuona ushujaa wao na kujitolea mhanga kwao kwenye Vita vya Badr, waliona kwamba ingalifaa kumkabili Muhammad kwa jeshi lililotayarishwa vizuri lenye watu wa makabila mbalimbali walio mashujaa na wenye uzoefu.

Amr bin Aas na mwengineo walitumwa kwenda kuonana na watu wa makabila ya Kinanah na Saqif na kuomba msaada wao. Walishauriwa waende wakawaalike mashujaa wao kupigana na Muhammad wakiwa wanazo silaha za kutosha kabisa, na kuwaahidi kwamba gharama za vita na mahitaji yoyote ya safari ile zitalipwa na Waquraishi.

Baada ya kufanya kazi vizuri walifaulu kuipata huduma ya baadhi ya watu mashujaa wa makabila ya Kinanah na Tahaamah na katika kutayarisha jeshi lenye watu elfu tatu hadi nne kushiriki kwenye vita vile.[2]

Tuliyoitaja hapo juu ni idadi ya wanaume tu walioshiriki kwenye vita vile, na kama idadi ya wanawake

waliokuwapo pale inajumlishwa, basi idadi itaongezeka. Haikuwa desturi miongoni mwa Waarabu kuwachukua wanawake na kwenda nao kwenye uwanja wa vita lakini safari hii wanawake nao walishiriki kwenye vita hivi pamoja na wanaume. Mpango wao ulikuwa kwamba wanawake hawa wapite katikati ya safu za vikosi, wakipiga dufu, kuwahamasisha kulipiza kisasi, kusoma beti za tenzi na kutoa hotuba za kuhamasisha.

Wamewaleta wanawake pamoja nao ili kwamba njia za askari wanaokimbia kwenye uwanja wa vita ziweze kufungwa, kwa sababu kukimbia kutakuwa na maana ya kuwaacha wasichana na wanawake watekwe na maadui, na hisia za ushujaa za Waarabu zisingaliweza kuvumilia kulitenda jambo hili la fedheha.
Idadi kubwa ya watumwa walijiunga na jeshi hili la Waquraishi kutokana na ahadi za kutamanisha walizopewa. Wahshi bin Harb alikuwa mtumwa Mwethiopia wa Mut'am. Alikuwa na ustadi mkubwa wa matumizi ya mkuki naye alikuwa kaahidiwa kupewa uungwana kama akimwua yeyote kati ya watu wakuu watatu wa Uislamu (ambao ni Muhammad, Ali au Hamza). Kwa kifupi, baada ya kufanya kazi kwa juhudi mno, walitayarisha jeshi lililokuwa na watu mia saba waliovaa deraya, elfu tatu wapanda ngamia, askari wapanda farasi mia mbili, na kundi la askari waendao kwa miguu.

Taasisi Ya Upelelezi Ya Mtume (S.A.W.W) Yatoa Taarifa

Abbas, baba yake mkubwa wa Mtume (s.a.w.w.) ambaye kusema kweli alikuwa Mwislamu lakini alikuwa bado hajaitangaza waziwazi imani yake, alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) ile mipango ya Waquraishi. Aliandika barua aliyoitia saini yake na akaifunga, kisha akampa mjumbe wa kabila la Bani

Ghifaar na kuichukua ahadi yake kwamba ataifikisha kwa Mtume (s.a.w.w.) ndani ya muda wa siku tatu. Yule mjumbe aliileta ile barua iliyofungwa kwa Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa kwenye bustani moja nje ya mji wa Madina na akampa barua ile baada ya kutoa heshima yake kwa Mtume (s.a.w.w.). Mtume (s.a.w.w.) aliisoma barua ile lakini hakuyataja yale yaliyomo kwenye barua ile kwa masahaba zake.[3] Allamah Majlis ananukuu kutoka kwa Imamu Sadiq (a.s.)[4] kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kuandika lakini aliweza kusoma barua. Hatimaye ilikuwa muhimu kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwaarifu masahaba zake juu ya mpango wa adui upesi upesi iwezekanavyo. Hivyo, aliporejea mjini, ile barua ilisomwa ili kuwapasha habari.

Jeshi La Waquraishi Laanza Safari

Jeshi la Waquraishi liliamua kuanza safari, na baada ya kwenda masafa fulani walifika Ab'wa alipozikwa mama yake Mtume (s.a.w.w.). Baadhi ya watu wapuuzi miongoni mwa Waquraishi walisisitiza kwamba mwili wake uchimbuliwe. Hata hivyo, waliokuwa wakiona mbali miongoni mwao walililaumu vikali wazo hili na wakaongeza kusema: "Inawezekana kwamba kitendo hiki kikawa ni desturi hapo baadae, na maadui zetu wa kabila la Bani Bakr na Bani Khuzaa'ah wanaweza kuyachimbua makaburi ya maiti wetu."

Mtume (s.a.w.w.) aliwatuma Anas na Munis bin Fazalah kwenda kuleta taarifa juu ya Waquraishi. Watu hawa wawili walileta taarifa ya kwamba jeshi la Waquraishi limeshafika karibu na Madina nao wamewaachilia wanyama wao wa kupanda kulisha kwenye mashamba ya Madina. Habib bin Munzir alileta taarifa ya kwamba viongozi watanguliao wa jeshi lWaquraishi wameshafika karibu na Madina. Wakati wa alasiri wa siku ya Alhamisi ilithibitishwa kwamba sehemu kubwa ya jeshi la Waquraishi ilikuwa imeukaribia mji wa Madina. Waislamu waliogopa maadui wasije wakamdhuru Mtume (s.a.w.w.) kwa kufanya mashambulizi ya usiku. Hivyo basi, machifu wa Aws na Khazraji waliamua kuchukua silaha na kukesha usiku ule msikitini ili kuilinda nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) na malango ya mji ule hadi walipopewa kazi nyinginezo kwa mujibu wa mipango ya kivita baada ya kuchomoza jua.

Ukanda Wa Uhud

Bonde kubwa na refu lililoungana na ile njia ya biashara iendayo Shamu na Yaman linaitwa Wadiul Qura. Makabila mbalimbali ya Waarabu na Wayahudi walifanya maskani yao kwenye sehemu yalimopatikana mahitaji ya maisha. Kwa hiyo, idadi ya vijiji ilikuwepo na pembezoni mwake vilizungushiwa uzio wa mawe. Yathrib (ambao baadae uliitwa Madinatul Rasuli – yaani Mji wa Rasuli) ulichukuliwa kuwa ndio mji mkuu wa vijiji hivi.
Yeyote yule aliyekuja Madina kutoka Makka alilazimika kuingia mjini mle kupitia upande wa kusini. Hata hivyo, kwa vile ukanda huu ulikuwa na mawe mengi, na ilikuwa vigumu kwa jeshi kuingia humo, jeshi la Waquraishi liliipinda njia yake na kwenda kutua kwenye sehemu ya kaskazini ya Madina kwenye bonde liitwalo 'Aqiq' lililoko chini ya mlima Uhud. Sehemu hii ilifaa kwa aina zote za harakati za kijeshi kwa kuwa haikuwako mitende kwenye sehemu hii na vile vile ardhi ilikuwa tambarare. Madina iliweza kushambuliwa vizuri zaidi kutoka upande huu kwa sababu vilikuwako vizuizi vya kimaumbile vichache mno kwenye upande huu.

Majeshi ya Waquraishi yalipiga kambi chini ya Mlima Uhud katika siku ya Alhamisi mwezi 5 Shawwal, mwaka wa 3 Hijiriya. Mtume (s.a.w.w.) alibakia mjini Madina siku ile na vile vile usiku wa kuchea Ijumaa. Aliunda halmashauri ya kijeshi siku ya Ijumaa na akawaomba maafisa na watu wengine walio na uzoefu kutoa maoni yao kuhusiana na ulinzi wa mji.

Kushauriana Kuhusu Ulinzi

Allah, Mwenye nguvu zote Alimwamrisha Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kuomba ushauri wa masahaba zake katika mambo yaliyo muhimu na kuufikiria ushauri wao anapofanya uamuzi, na kwa kufanya hivyo alitoa mfano bora zaidi kwa wafuasi wake na kujenga moyo wa demokrasia, ukweli na uhakika miongoni mwao. Je, alifaidika kutokana na maoni yao au la? Ulamaa na wanachuoni wa theolojia wamelijibu swali hili. Hata hivyo, ni ukweli ukubalikao kwamba, mashauriano haya ni mifano iliyo hai ya kanuni za kikatiba zilizotufikia kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.). Njia yake hii ilikuwa yenye mafunzo na ya kuvutia mno kiasi kwamba makhalifa wa Uislamu nao waliifuata baada ya kufariki dunia kwake na kuyakubali kabisa maoni bora zaidi ya Imamu Ali, Amiri wa Waumini (a.s.) kuhusiana na mambo ya kijeshi na matatizo ya

kijamii.

Kwenye mkutano mkubwa uliohudhuriwa na maafisa na askari mashujaa wa jeshi la Waislamu, Mtume (s.a.w) alisema: “Hebu nipeni maoni yenu” – Yaani aliwaomba wale maafisa na askari kutoa maoni yao kuhusiana na ulinzi wa Uislamu uliokuwa ukitishiwa na Waquraishi.

Abdullah bin Ubay aliyekuwa mmoja wa wanafiki wa mjini Madina, alishauri utumike ulinzi wa kwenye ngome. Ina maana ya kwamba Waislamu wasitoke mle Madina bali waitumie minara na majengo. Wanawake wampige mawe adui kutoka kwenye mapaa ya nyumba na minara na wanaume wapigane bega kwa bega kwenye mitaa ya mji. Alisema: “Zamani tulikuwa tukiitumia njia ya ulinzi wa ngome na wanawake walitusaidia kutoka kwenye mapaa ya nyumba na ni kwa sababu hii kwamba mji wa Yathrib umebakia katika hali ya kutoguswa.

Adui hakufaulu kuitumia njia hii. Kila tulipojihami kwa njia hii, tulishinda na kila tulipotoka nje ya mji, tulipata madhara.”

Wazee wazoefu kutoka miongoni mwa Muhajirin na Ansar waliliunga mkono wazo hili. Hata hivyo, vijana na hasa wale ambao hawakushiriki kwenye vita vya Badr nao walikuwa na shauku ya kupigana, walilipinga vikali wazo na wakasema:

“Njia hii ya ulinzi itamshawishi adui, nasi tutapoteza heshima tuliyoipata kwenye Vita vya Badr. Si aibu kwamba wenye kumwabudu Allah walio mashujaa na wenye kujitolea mhanga wajifiche majumbani mwao na kumruhusu adui afike pale? wakati wa Vita vya Badr nguvu yetu ilikuwa ndogo mno ikilinganishwa na hii ya hivi sasa, na ukiachilia mbali hayo, tulishinda. Tumekuwa tukisubiri kwa muda mrefu ili tupate nafasi na sasa tumeipata.”

Hamza, alisema: “Ninaapa kwa jina la Allah, Aliyeifunua Qur’ani, leo sitakula chakula changu mpaka nimepigana na adui nje ya mji.” Kundi hili lilishikilia kwamba jeshi la Waislamu litoke nje ya mji na kumpa kipigo yule adui.[5]

Kupiga Kura Ya Kuuwawa

Mzee mmoja mchamungu aliyeitwa Khaysamah alisimama na kusema: “Ewe Rasuli wa Allah! Waquraishi wamekuwa wakijishughulisha kwa mwaka mzima nao wamefaulu kuyaweka sawa pamoja nao makabila ya Waarabu. Kama hatutatoka hivi sasa kuihami sehemu hii, basi upo uwezekano wakauzingira mji wa Madina. Pia inawezekana kwamba wanaweza wakayaondoa kuzingira huko na kurudi Makka.

Hata hivyo, jambo hili litawatia moyo, nasi katika siku zijazo hatutakuwa na usalama kutokana na mashambulio yao. Nasikitika kwamba sikuweza kushiriki katika Vita vya Badr wakati mimi na mwanangu tulipenda sana kushiriki kwenye vita vile na kila mmoja wetu alitaka kumtangulia mwenziwe.

Wakati wa Vita vya Badr nilimwambia mwanangu: Wewe bado ni kijana na unayo tamaa ya kufanya mambo mengi na unaweza kuitumia nguvu ya ujana wako katika njia ambayo unaweza kuipata radhi ya Allah. Kwa kadiri mimi nihusikavyo, umri wangu hivi sasa karibuni ushakwisha na maisha yangu ya siku zijazo si yenye furaha. Hivyo basi, ni muhimu kwamba nishiriki kwenye jihadi hii takatifu (Vita vya Badr), nawe utapaswa kuyabeba majukumu yahusuyo wote wanaonitegemea.

Hata hivyo, mwanangu alipenda sana kushiriki kwenye vita ile kiasi kwamba tuliamua kupiga kura. Kura ilimwangukia yeye, na akafa kishahidi kwenye Vita vya Badr. Usiku wa jana kila mtu alikuwa akizungumzia juu ya kule kuzingirwa na Waquraishi, nami nikaenda kulala na fikira hizi akilini mwangu. Nilimwota mwanangu. Alikuwa akitembea kwenye bustani za peponi na alikuwa akiyafaidi matunda yake. Alizungumza nami kwa huba na akasema: "Baba yangu mpenzi! Ninakusuburi." Ewe Mjumbe wa Allah! Ndevu zangu zimekuwa na mvi na mifupa yangu imepoteza nyama zake. Ninakuomba uniombee kufa kishahidi katika njia ya haki."[6]

Utawaona watu wengi walio mashujaa na wenye kujitolea mhanga kama mtu huyu kwenye kurasa za historia ya Uislamu. Shule za mafunzo zisizoasisiwa juu ya itikadi na imani juu ya Mungu Muweza na Siku ya Hukumu, haziwezi kuwafunza askari wanaojitolea mhanga kama Khaysamah. Moyo huu wa kujitolea mhanga umfanyao askari kukitafuta kifo chake katika njia ya unyoofu huku machozi yakimdondoka machoni mwake, ni ari ambayo haiwezi kufundishwa kwenye shule yoyote ile isipokuwa kwenye shule ya uchamungu.

Katika nchi za viwanda za ulimwenguni huu, siku hizi umuhimu zaidi umewekwa kwenye hali za maisha ya maafisa na wakuu wengine wa majeshi. Hata hivyo, kwa vile lengo la vita za siku hizi ni kupata maisha bora na matengenezo yake, malengo yao makuu ni kuyaokoa maisha yao. Hata hivyo, kwenye shule ya wachamungu, lengo la kupigana ni kuitafuta radhi ya Allah, na kwa lengo hili laweza kufikiwa kwa kuuawa. Askari wa Allah huzikabili taabu zote kwa uimara bila kuyumba.

Matokeo Ya Ushauriano

Mtume (s.a.w.w.) aliyachukulia maoni ya walio wengi kuwa ndio yenye kukata shauri na akatayarisha kwenda nje ya mji badala ya kuitumia ile njia ya ulinzi wa ngomeni na mapigano ya bega kwa bega. Haikufaa hata kidogo kwamba baada ya msisitizo wote wa maafisa kama vile Hamza na Sa'ad bin Ubaadah awe anaupendelea ushauri wa Abdullah Ubay, aliyekuwa mmoja wa wanafiki wa Madina.

Ingawa kwa mtazamo wa ulinzi na kanuni za vita, ushauri wake (Abdullah Ubay) ulithibitisha ushindi, au kwa uchache ulithibitisha ya kwamba Waislamu wasishindwe, lakini ulikuwa ni makosa kabisa kisaikolojia kwa sababu zifuatazo:

1. Mapigano yasiyo na utaratibu mwema ya bega kwa bega kwenye mitaa myembamba ya Madina na kuwaruhusu wanawake washiriki kwenye haya mapigano ya kiulinzi na kusalia kwenye maficho majumbani mwao na kuiacha njia ikiwa wazi kwa adui, ingalikuwa dalili ya unyonge na ujinga wa

Waislamu na isingeliafikiana na ile nguvu waliyoionyesha kwenye Vita vya Badr.

2. Madina itakapozingirwa na maadui na barabara zake kumilikiwa na maadui na kikathibiti kimya cha askari wa Kiislamu mbele ya yote haya, kungeliuuwa kabisa moyo wa kupigana katika nafsi zao.

3. Je, isingeliwezekana kwamba Abdullah bin Ubayy aliyekuwa na mfundo dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) alitaka kumpiga pigo kali kwa njia hii?

Mtume (S.A.W.W.) Achukua Uamuzi

Baada ya kuliandaa jeshi la ulinzi, Mtume (s.a.w.w.) aliingia nyumbani mwake. Alivaa deraya, akavaa upanga kiunoni, akaweka ngao mgongoni mwake, akaning'iniza upinde begani mwake, akaushika mkuki mkononi mwake, na baada ya kujiandaa kwa silaha kiasi hicho, alijitokeza mbele ya watu. Mandhari hii iliwapa Waislamu mshituko mkubwa.

Baadhi yao walifikiria kwamba kule kushikilia kwao kutoka nje ya mji hakukuafikiana na kanuni za Uislamu na walimshauri Mtume (s.a.w.w.) jambo lisilo la lazima kutoka nje kwenda kupigana. Hivyo basi, ili kusahihisha kosa hilo, walisema kwamba walikuwa tayari kufuata maoni yake na watakubaliana na uamuzi wowote ule atakaoutoa, yaani kama haifai kutoka nje basi wako tayari kubakia mle mjini. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alijibu akisema: 'Mtume anapovaa deraya haimfalii kuivua mpaka apigane dhidi ya adui."[7]

Mtume (S.A.W.W.) Aenda Nje Ya Mji Wa Madina

Mtume (s.a.w.w.) alisali sala ya Ijumaa na kisha akatoka mjini Madina na kwenda Uhud akifuatana na jeshi lenye watu elfu moja. Hakwenda na watu kama vile Usama bin Zayd bin Haarith na Abdullah bin Umar kutokana na udogo wa umri wao, lakini vijana wawili ambao ni Samurah na Raafi, ambao umri wao haukuzidi miaka kumi na mitano, walishiriki kwenye vita hii kwa sababu, ingawa walikuwa bado wangali watoto, walikuwa wapiga mishale wazuri.

Walipokuwa njiani, baadhi ya Wayahudi waliokuwa washirika wa Abdullah bin Ubay walionyesha kupendelea kwao kushiriki katika ulinzi wa mji, lakini Mtume (s.a.w.w.) kutokana na sababu fulani fulani hakuona kuwa inafaa kuwaruhusu kufanya hivyo. Wakati huo huo Abdallah bin Ubay naye alikataa kushiriki mwenye jihadi kwa sababu ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) ameukubali ushauri wa vijana na kuuacha wake. Hivyo basi, yeye alirudi baada ya kufika katikati ya safari ile pamoja na watu mia tatu wa kabila la Aws waliokuwa ndugu zake.

Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake walipendelea kuipitia njia iliyofupi zaidi ili waweze kufika kwenye sehemu ya kupigia kambi zao upesi. Kwa lengo hili walilazimika kupitia kwenye bustani ya mnafiki mmoja aliyeitwa Jumuh. Mtu huyu alionyesha kuudhika sana kwa ukaidi kwa sababu ya jeshi la Kiislamu kuingia kwenye konde yake na akamvunjia heshima Mtume (s.a.w.w.). Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.)

walitaka kumwua lakini Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Mwacheni mtu huyu aliyepotoshwa na mkaidi.”8

Askari Wawili Waliojitolea Mhanga

Walipofika mahali fulani Mtume (s.a.w.w.) aliwakagua askari wake. Moyo wao wa kujitolea mhanga na nyuso angavu zilikuwa ziking’aa kupitia mwanga wa panga zao. Jeshi alilolileta Mtume (s.a.w.w.) chini ya Mlima Uhud lilikuwa na watu ambao umri wao ulitofautiana mno. Wengi wao walikuwa wazee wenye vichwa na nyuso nyeupe, lakini vile vile waliweza kuonekana vijana mashujaa, ambao umri wao haukuzidi miaka kumi na mitano.

Jambo lililowahimiza watu hawa kushiriki kwenye vita hivi halikuwa lolote jingine ila huba ya ukamilifu ambao unaweza kupatikana tu chini ya msaada wa ulinzi wa Uislamu. Katika kuiunga mkono kauli hii tunasimulia hapa chini hadithi za watu wawili yaani mzee mmoja na kijana mmoja aliyekuwa ameoa usiku mmoja tu kabla ya hapo:

1. Amr bin Jumuh: Alikuwa ni mzee aliyekuwa na mgongo uliopinda, ambaye nguvu zake za mwili zilikuwa zimekwisha, na alikuwa mtu ambaye mmoja wa miguu yake ulijeruhiwa katika ajali. Alikuwa na wana wanne mashujaa aliowapeleka kwenye uwanja wa vita na alikuwa na furaha kwamba walikuwa wakipigana kwa ajili ya haki na ukweli.

Hata hivyo, alifikiria nafsini mwake kwamba haikuwa sahihi kukaa mbali kutoka kwenye vita vile na hivyo kuweza kupoteza rehema (za jihadi). Ndugu zake walikataa vikali kushiriki kwake kwenye vita vile na wakasema kwamba sheria ya Uislamu imemsamehe majukumu yote ya aina hii. Hata hivyo, maneno yao hayakumtosheleza hivyo yeye mwenyewe akamwendea Mtume (s.a.w.w.) na akasema: “Ndugu zangu wananizuia kushiriki kwenye jihadi. Nini maoni yako juu ya jambo hili?”

Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: “Allah Anakufikiria kuwa umesamehewa na hakuna jukumu lililo juu yako.” Hata hivyo, alimsisitiza na kumsihi alikubali ombi lake. Wakati ndugu zake wakiwa wamemzunguka, Mtume (s.a.w.w.) aliwageukia na kusema: “Msimzuie kufa kifo cha kishahidi katika njia ya Uislamu.” Alipotoka nje ya nyumba yake alisema: “Ee Allah! Nifanye mshindi katika kuuweka uhai wangu katika njia Yako na usinifanye nirudi nyumbani mwangu.”

Mtu aendaye kukutana na kifo kwa mikono miwili yu mwenye uhakika wa kuufikia mwishilizo wake. Mashambulizi ya kilema huyu yalikuwa yenye kushitusha. Alimshambulia adui vikali mno ingawa alikuwa na mguu uliolemaa, na akasema: “Mimi ninaitamani Pepo.” Mmoja wa wanawe naye alikuwa akisonga mbele pamoja naye. Matokeo yake ni kwamba wote wawili walipigana hadi wakaipata heshima ya kufa kishahidi.9

2. Hanzalah: Alikuwa yu kijana ambaye bado hajautimiza umri wa miaka ishirini na minne. Imesemekana hivi: ‘Anawatoa wana safi kutokana na wazazi wasio safi. Hanzalah alikuwa mwana wa Abu ‘Amr, adui wa Mtume (s.a.w.w.). Baba yake alishiriki kwenye vita vya Uhud katika upande wa Waquraishi naye

alikuwa mmoja wa watu mafasiki waliowachochea Waquraishi kupigana vita dhidi ya Mtume (s.a.w.w.). Alijishughulisha na matendo yaliyo dhidi ya Uislamu hadi kwenye kifo chake na alikuwa mmoja wa waasisi wa Masjidi Dhiraar. Maelezo marefu juu ya msikiti yatatolewa kuhusiana na matukio ya mwaka wa tisa wa Hijiriya.

Hisia za utoto hazikumfanya Hanzalah akengeuke kutoka kwenye njia iliyonyooka. Usiku wa kuchea siku ya Vita vya Uhud ulikuwa usiku wa harusi yake. Alimwoa binti wa Abdullah bin Ubay mtu mashuhuri wa kabila la Bani Aws na alilazimika kuzifanya sherehe za ndoa usiku ule ule. Alipousikia mwito wa jihadi alitatanika. Hakuipata njia yoyote nyingine ila kuomba ruhusa kuto kwa yule Amir–jeshi Mkuu kuutumia usiku ule mjini Madina na kwenda kwenye uwanja wa vita siku iliyofuatia. Kama ilivyonukuliwa na Allamah Majlis,[10] aya ifuatayo ilifunuliwa juu yake:

"Hakika wenye kuamini ni wale wamwaminio Allah na Mtume Wake, na wanapokuwa pamoja naye kwenye jambo linalohusiana na wote, hawaondoki mpaka wamwombe ruhusa, kwa hakika wale wakuombao ruhusa hao ndio wamwaminio Allah na Mtume Wake. Hivyo watakapokuomba ruhusa kwa ajili ya mambo yao, basi mruhusu umpendaye miongoni mwao na uwaombee msamaha kwa Allah, hakika Allah ni Mwingi wa kusamehe Mwenye kurehemu." (***Surah an–Nur* 24:62**).

Mtume (s.a.w.w.) alimpa ruhusa ya usiku mmoja kusherehekea ndoa yake. Asubuhi yake aliwasili kwenye uwanja wa vita hata kabla ya kuoga janaba. Alipotaka kutoka nyumbani mwake, machozi yalimchuruzika yule bibi harusi ambaye ndoa yake ilifanyika usiku mmoja tu kabla ya pale. Aliiweka mikono yake shingoni mwa mumewe kumwomba asubiri kidogo. Kisha akawaita watu wanne waliosalia mjini mle Madina kutokana na sababu fulani fulani, ili washuhudie ya kwamba ndoa ilifanyika baina yao usiku uliopita.

Hanzallah alipotoka, yule bibi harusi aliwageukia wale watu wanne waliotajwa hapo juu akawaambia: "Usiku uliopita niliota kwamba mbingu ilipasuka vipande viwili na mume wangu akaingia na baada ya hapo vile vipande viwili vya mbingu vikaungana tena. Kutokana na ndoto hii, ninaona kwamba mume wangu na roho yake watapaa kwenda Peponi."

Hanzalah alijiunga na jeshi lile. Macho yake yakamwangalia Abu Sufyan aliyekuwa akitembea baina ya majeshi mawili. Alimshambulia shambulio la kishujaa dhidi yake kwa upanga wake lakini uliupiga mgongo wa farasi wa Abu Sifyan na yeye mwenyewe akaanguka chini.

Vilio vya Abu Sufyan viliibua mazingatio ya askari wa Waquraishi.Shaddad Dulaythi akamshambulia Hanzalah, na matokeo yake ni kwamba Abu Sufyan akatoroka. Askari wa mkuki kutoka miongoni mwa askari wa Waquraishi alimshambulia Hanzalah na kumchoma mkuki mwilini mwake. Ingawa alikuwa na jeraha kubwa, Hanzalah alimfuatia mtu yule na kumpiga dharuba ya upanga. Yeye naye akaanguka chini na akakata roho kutokana na lile jeraha alilotiwa na askari yule.

Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Nimewaona malaika wakimwosha Hanzalah." Hii ndio sababu iliyomfanya

aitwe ‘Ghasilul Malaa’ikah’ (yaani yule aliyeoshwa na malaika). Watu wa kabila la Aws walipokuwa wakizihesabu sababu za utukufu na heshima yao walikuwa wakisema: “Mmoja wetu alikuwa ni Hanzalah aliyeoshwa na malaika.”

Abu Sufyan alikuwa akisema: “Kama wamemwua mwanangu Hanzalah kwenye Vita vya Badr, mimi nami nimemwua Hanzalah wa Waislamu kwenye Vita vya Uhud.”

Hapana shaka kwamba fikara, uaminifu na imani ya wanyumba hawa vinashangaza, kwa sababu baba zao walikuwa maadui wakuu wa Uislamu. Baba wa bibi harusi alikuwa ni Abdallah bin Ubay bin Salul aliyekuwa chifu wa wanafiki wa Madina, na Hanzalah alikuwa mwana wa Abu Amr, aliyekuwa Mtawa katika zama za ujinga na baada ya kuingia kwa Uislamu alijiunga na wenye kuabudu masanamu wa Makka. Yeye ndiye aliyemkaribisha Hercules (mfalme wa Warumi wa Kigiriki) kuishambulia na kuiharibu Dola mpya ya Kiislamu.[11]

Safu Za Yale Majeshi Mawili

Asubuhi ya mwezi 7 Shawwal, mwaka 3 Hijiriya, jeshi la Kiislamu lilijipanga mkabala na jeshi la Waquraishi linaloshambulia na kuhujumu. Jeshi la Waislamu lilichagua sehemu ya kupigia kambi yao katika sehemu iliyokuwa na kizuizi na hifadhi ya kimaumbile nyuma yake ambayo ni Mlima Uhud. Hata hivyo, ilikuwako nafasi maalumu katikati ya mlima ule na ulikuwapo uwezekano kwamba majesahi ya adui yangaliweza kugeuka nyuma ya mlima ule na kutokea nyuma ya jeshi la Waislamu kwa kupitia kwenye nafasi ile na kuweza kuwashambulia kwa nyuma.
Ili kuiondoa hatari hii, Mtume (s.a.w.w.) aliweka makundi mawili ya askari wa mishale kwenye kilima kidogo na kumwambia kamanda wao Abdallah bin Jaabir hivi: “Muwafukuze maadui kwa kupiga mishale. Msiwaruhusu kuingia kwenye uwanja wa vita kwa kupitia nyuma na kutushambulia kwa kutushitukiza. Iwe tumeshinda au tumeshindwa, musiiitoke sehemu hii.”

Matukio ya Vita ya Uhud yanadhihirisha kwamba nafasi hii ilikuwa nyeti mno na kushindwa kwa Waislamu baada ya kupata ushindi kunatokana na ukweli kwamba, wale askari wa pinde walionyesha utovu wa nidhamu na wakaitoka hii sehemu iliyo muhimu mno na yule adui aliyekuwa kishashindwa na alikuwa kakimbia alishambulia shambulio la ghafla kupitia kwenye sehemu hii.

Ile amri kali aliyoitoa Mtume (s.a.w.w.) kuwapa askari wa pinde, ya kutoitoka sehemu ile ilikuwa ni ushuhuda wa ujuzi wake uliokamilika juu ya kanuni za vita. Hata hivyo, ujuzi wa kamanda wa kanuni za vita hauhakikishi kupata ushindi kama askari wataonyesha utovu wa nidhamu.

Kuimarisha Hamasa Za Askari

Mtume (s.a.w.w.) hakuacha kuimarisha hamasa za askari kwenye vita. Katika wakati huu, vile vile askari mia saba walipojifunga dhidi ya watu elfu tatu, aliziimarisha nyoyo zao kwa hotuba. Mwanahistoria mkuu wa Uislamu, Waaqidi, amesema: “Mtume (s.a.w.w.) aliweka askari wa kupiga mishale hamsini kwenye

shingo ya mlima iitwayo Ainayn na kuuweka Mlima Uhud nyuma na mji wa Madina mbele ya majeshi ya Waislamu. Alipokuwa akitembea kwa miguu alivipanga vikosi na kuweka nafasi ya kila afisa. Alikiweka kikundi kimoja mbele na kingine nyuma. Alizipanga safu kwa uangalifu kiasi kwamba kama bega la askari yeyote yule lilikuwa mbele ya wenziwe, mara moja alimtaka askari yule kurudi nyuma.

Baada ya kuzipanga safu, Mtume (s.a.w.w.) aliwahutubia Waislamu kwa maneno haya: "Ninakushaurini kuyafuata yale mliyoamrishwa na Allah Mwenye nguvu zote kwenye Kitabu chake. Ninakukumbusheni kuzitii amri za Allah na jiepusheni na kumwasi." Kisha aliongeza kusema hivi: "Ni jukumu gumu na zito kupigana na adui, na kuna watu wachache mno wawezao kubakia madhubuti mbele yao ila wale walioongozwa na kusaidiwa na Allah, kwa kuwa Allah Yu pamoja na wale wamtiio na shetani yu pamoja na wale wamwasio Allah. Juu ya kitu chochote kile lazima mbakie imara katika jihadi na kwa njia hii mtapata baraka aliyokuahidini Allah. Mjumbe, Malaika Mkuu Jibriil ameniambia kwamba hakuna yeyote afaye kwenye ulimwengu huu mpaka ameila ile chembe ndogo ya riziki yake ya kila siku aliyowekewa na Mola wake... Na mtu asianze kupigana mpaka pale itakapotolewa amri ya kupigana."[12]

Adui Azipanga Safu Zake

Abu Sufyan aliligawa jeshi lake katika makundi matatu. Aliwaweka wale askari wa miguu wenye deraya katikati, kundi jingine lililokuwa chini ya uongozi wa Khalid bin Walid upande wa kulia, na kundi jingine chini ya uongozi wa Ikrimah upande wa kushoto. Vile vile aliweka kikosi maalum mbele ya jeshi kwa namna ya watangulizi, na vile vile kwenye kundi hili walikuwemo wale washika bendera, wote wakitokana na kabila la Abdud Daar. Kisha akawahutubia akasema: "Ushindi wa jeshi lolote lile hutegemeana na umadhubuti na uvumilivu wa washika bendera. Katika siku ya Badr tulishindwa kwenye uwanja huu. Kama kabila la Abdud Daar halionyeshi ustadi katika kuihami bendera, inawezekana kwamba heshima ya kuishika bendera inaweza kuhamishiwa kwenye kabila jingine." Talhah bin Abi Talhah aliyekuwa mtu shujaa na mshika bendera wa kwanza kabisa, aliyahisi maneno haya. Alipiga hatua moja mbele upesi sana akasai akamwita mpinzani aje kupigana.

Vichocheo Vya Kisaikolojia

Kabla ya kuanza kwa vita Mtume (s.a.w.w.) alishika upanga mkononi mwake, na ili kuichemsha damu ya askari mashujaa, aliwageuzia uso wake na kusema: "Ni nani mtu yule atakayeushika upanga huu mkononi mwake na kuupa haki yake?" Baadhi ya watu walisimama lakini Mtume (s.a.w.w.) hakuwapa upanga ule. Kisha Abu Dujaanah, aliyekuwa askari shujaa alisimama na akauliza akisema: "Ni ipi haki ya upanga huu na ni vipi tunaweza kuitoa?" Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Unapaswa kupigana sana ukiwa nao kiasi kwamba mpaka upate kupinda." Abu Dujanah akasema: "Mimi niko tayari kuulipa haki yake." Kisha akajifunga leso nyekundu kichwani mwake aliyoiita leso ya kifo" na akauchukua ule upanga kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.). Hivyo, kwa kukifunga kile kitambaa kichwani mwake alikuwa na maana ya kwamba atapigana hadi pumzi zake za mwisho. Alitembea kama chui mwenye kujiona na alikuwa na furaha mno kuipata ile heshima aliyoipata, na ile leso nyekundu iliiongeza heshima yake.[13]

Hakuna shaka kwamba mikogo hii ni kichocheo bora zaidi cha kulishawishi jeshi linalopigana kwa ajili ya kuuhami ukweli na mambo ya kiroho na lisilokuwa na nia yoyote nyingine ila kuueneza uhuru wa kuabudu, na halina madhumuni mengine ila huba ya ustawi. Labda kitendo hiki cha Mtume (s.a.w.w.) hakikuwa tu kwa ajili ya kuichochea nafsi ya Abu Dujaanah, kwa kuwa, kwa njia hii vile vile aliwashawishi wale wengine na kuwahamasisha kwamba ushujaa wao na nia zao nazo ni lazima ziwe kwenye kipimo kama hiki kiasi kwamba wastahiki kuzipata medali za kijeshi.

Zubayr bin Awaam, ambaye yeye mwenyewe alikuwa ni askari shujaa, alijikuta akiwa si mwenye raha, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) hakumpa ule upanga. Hivyo, alijisemea mwenyewe: Nitamfuatilia Abu Dujanah ili nikione kiwango cha ushujaa wake." Anasema: "Nilimfuatilia mle kwenye uwanja wa vita. Alimkatilia mbali kila shujaa aliyemkabili.." Kisha akasema: 'Alikuwako shujaa mmoja miongoni mwa Waquraishi, ambaye upesi upesi alivikata vichwa vya Waislamu waliojeruhiwa. Nami nilishitushwa mno kutokana na hiki kitendo chake kisicho cha kawaida. Kwa bahati njema shujaa yule alikuja uso kwa uso na Abu Dujaanah. Walibadilishana mapigo machache na hatimaye yule shujaa wa Waquraishi aliuawa mikononi mwa Abu Dujaanah."

Abu Dujaanah alisema: "Nilimwona mtu mmoja akiwashawishi Waquraishi kupigana. Nilimwendea na alipouona upanga ukining'inia kichwani mwake alianza kuomboleza na kulia. Mara kwa ghafla nilitambua ya kwamba alikuwa ni mwanamke (Hind mkewe Abu Sufyan) na nikauchukulia upanga wa Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni safi mno kiasi cha kutostahili kupigwa kichwani mwa mwanamke (kama Hind)."[14]

Vita Vyaanza

Ibn Hisham anaandika hivi:[15] "Vita vilianza kupitia kwa Abu 'Amr aliyekuwa mmoja wa wale waliokimbia kutoka Madina. Yeye alitokana na kabila la Bani Aws, lakini kutokana na uadui wake dhidi ya Uislamu, alikimbilia Makka na watu kumi na watano wa Bani Aws walikuwa pamoja naye. Alikuwa akifikiria ya kwamba kama watu wa kabila la Bani Aws wakimwona watamtoka Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, alijitokeza mbele ili kulifikia lengo hili. Hata hivyo alipowakabili Waislamu ilimbidi kuzikabili dhihaka na matusi yao.[16] Hivyo basi, baada ya mapigano mafupi alitoka kwenye mstari wa mbele.
Kujitolea mhanga kwa baadhi ya mashujaa kwenye Vita vya Uhud kunatambulika vyema miongoni mwa wanahistoria, na kujitolea mhanga kulikofanywa na Sayyidna Ali (a.s.) kunafaa kutajwa. Ibn Abbas anasema: "Kwenye vita vyote Ali alikuwa mshika bendera na daima mshika bendera alikuwa akiteuliwa kutoka miongoni mwa watu wenye uzoefu na uthabiti, na kwenye Vita vya Uhud bendera ya Muhajiriin ilikuwa mikononi mwa Ali." Kufuatana na kauli ya wengi wa wanahistoria, baada ya Mus'ab bin Umayr, mshika bendera wa Waislamu kuuliwa kishahidi, Mtume (s.a.w.w.) alimpa Sayyidna Ali (a.s.) bendera ile, na sababu iliyomfanya Mus'ab aishike bendera ile pale mwanzoni labda ni kwa sababu alikuwa anatokana na familia ya Abdud Daar na mshika bendera wa Waquraishi naye alitokana na familia hii hii." (maoni haya yamechukuliwa kutoka Balazari).

Talhah Abi Talhah, aliyekuwa akiitwa Kabshul Katibah (mtu aliyesawa na kikosi kizima cha mbele cha

jeshi) akaingia katika uwanja wa vita huku akipiga makelele, akisema: “Enyi masahaba wa Muhammad! Mnaamini ya kwamba watu wetu wanaouawa, wanakwenda Motoni ambapo wenu wanakwenda Peponi. Katika hali hiyo, je, yuko yeyote miongoni mwenu ambaye ninaweza nikampeleka huko Peponi au anipeleke Motoni?” Sauti yake ilikuwa ikivuma katika ule uwanja wa vita. Sayyidna Ali (a.s.) alijitokeza mbele na baada ya kubadilishana mapigo kadhaa hivi, Talhah alianguka chini.

Baada ya Talhah kuuawa, ndugu zake wawili wakawa washika bendera, mmoja baada ya mwingine. Hata hivyo, wote wawili waliuawa kwa mishale iliyopigwa na Aasim bin Thaabit.

Tunajifunza kutokana na hotuba aliyoitoa Sayyidna Ali (a.s.) mbele ya kamati ya ushauri iliyoundwa ili kumteua Khalifa baada ya kifo cha Khalifa wa pili kwamba, jeshi la Waquraishi liliwaweka akiba watu tisa kwenye nafasi ya mshika bendera na iliamuliwa ya kwamba waishike bendera ile kwa zamu, mtu kwanza akiuawa wa pili aishike ile bendera na kuendelea hadi waishe wote. Washika bendera wote hawa watokanao na kabila la Bani Abdud Daar waliuawa mikononi mwa Sayyidna Ali (a.s.). Baadda yao, mtumwa Mwethiopia, aliyeitwa Sawaab, aliyekuwa na umbo la kuogofya na sura ya kutisha aliiokota ile bendera na akasai. Yeye naye alianguka kutokana na dharuba ya Sayyidna Ali (a.s.).

Kwenye mkutano mkuu, ambao masahaba zake Mtume (s.a.w.w.) walihudhuria, Sayyidna Ali (a.s.) alisema: “Je, mnakumbuka kwamba nilikuondoleeni ufisadi wa watu tisa wa kabila la Bani Abdud Daar, ambapo kila mmoja wao aliishika ile bendera kwa zamu na akasai?” Wale wote waliokuwapo pale waliyathibitisha maneno ya Sayyidna Ali, Amiri wa Waumini (a.s.).[17]

Aliongeza kusema: “Je, mnakumbuka kwamba baada ya wale watu tisa, yule mtumwa Mwethiopia, Sawaab aliingia katika uwanja wa vita na hakuwa na lengo lolote ila kumwua Mtume wa Allah! Alikuwa mwenye ghadhabu kali mno kiasi kwamba alitokwa na povu kinywani na macho yake yalikuwa mekundu. Mlipomwona shujaa yule nyote mlishikwa na bumbuwazi na mkarudi nyuma, ambapo mimi nilikwenda mbele na baada ya kumpiga dharuba mgongoni mwake, nikamwangusha chini?” Wale waliokuwapo pale waliyathibitisha maneno haya pia.[18]

Nani Waliokuwa Wakipigana Kwa Ajili Ya Tamaa?

Tunajifunza kutokana na beti za mashairi alizokuwa akizisoma Hindi na wanawake wengine huku wakipiga dufu ili kuwahamasisha mashujaa wa Kiquraishi na kuwachochea katika umwagaji wa damu na kulipiza kisasi kwamba, watu hawa hawakuwa wakipigana kwa ajili ya mambo ya kiroho, usafi, uhuru na tabia njema. Kinyume na hayo, wao walikuwa wakisukumwa na mambo ya ngono na dunia. Ule wimbo waliouimba wale wanawake kwa dufu na sauti maalum katikati ya safu za jeshi ulikuwa: “Sisi ni mabinti wa Taariq. Tunatembea kwenye mazulia ghali. Kama mkimkabili adui, tutalala pamoja nanyi, lakini kama mkimwonyesha adui migongo yenu na kukimbia, tutajitenga nanyi.”

Ni ukweli ukubalikao kwamba kuna kutoafikiana kwa dhahiri kabisa na tofauti kubwa baina ya watu, ambao mambo yao ya kivita yanasukumwa na tamaa za kingono na wasio na lengo lolote jingine ila

kujitosheleza katika faida za kiulimwengu na anasa za kimwili na wale watu wapiganao kwa lengo takatifu la kiroho kama vile kudumisha uhuru, kuinua kiwango cha fikara na kumwondolea mwanadamu ibada ya mti na jiwe. Kutokana na hivyo vichocheo viwili tofauti viliyomo akilini mwa makundi mawili haya, haikuchukua muda mrefu kabla ya kutoa matokeo ya kujitolea mhanga kwa maafisa wa Uislamu kama vile Sayyidna Ali (a.s.), Hamza, Abu Dujaanah, Zubayr na wengineo. Jeshi la Waquraishi lilizitupa chini silaha na vyakula vyao na wakakimbia kwa fedheha kutoka kwenye uwanja wa vita. Utukufu mwingine ulifikiwa kwa namna hiyo na wale mashujaa wa Uislamu.[19]

Kushindwa Baada Ya Ushindi

Tunaweza kutaja hapa kwa nini mashujaa wa Uislamu walishinda. Ilitokana na ukweli kwamba hadi katika dakika ya mwisho ya ushindi wao hawakuwa na lengo jingine lile ila jihadi katika njia ya Allah, kuitafuta radhi Yake, kuubalighisha ujumbe wa Allah na kuondoa kila kizuizi njiani mwake.

Basi vipi walishindwa baada ya hapo? Ilikuwa ni kwa sababu baada ya kuupata ushindi, nia na lengo la wengi wa Waislamu lilipatwa na mabadiliko. Mwelekeo wa nyoyo zao kwenye ngawira zilizotupwa na jeshi la Waquraishi kwenye uwanja wa vita na wao wenyewe kukimbia, ziliathiri uaminifu wa kundi kubwa na wakaiasi amri waliyopewa na Mtume (s.a.w.w.).

Haya yafuatayo ni maelezo ya tukio hili kwa kirefu: “Tulipokuwa tukiielezea hali ya kijiografia ya Uhud tulieleza ya kwamba kilikuwapo kipenyo maalum katikati ya Mlima Uhud, na Mtume (s.a.w.w.) aliwapa wapiga mishale hamsini chini ya uongozi wa Abdullah Taabar jukumu la kulilinda bonde lililokuwapo nyuma ya mstari wa mbele wa uwanja wa vita, na alimpa kamanda wa kikundi hiki amri hii: “Mzuieni adui asipitie kwenye kipenyo hiki cha mlima kwa kumpiga mishale na msiitoke sehemu hii kwa vyovyote vile itakavyokuwa, tuwe tumeshindwa au tumeshinda.” Moto wa vita uliwaka katika pande zote mbili.

Kila wakati maadui walipotaka kupitia kwenye bonde hili walirudishwa nyuma na wale wapiga mishale. Jeshi la Waquraishi lilipozitupa chini silaha zao na kukiacha kila kitu ili kuokoa uhai wao, maofisa mashujaa wachache wa Uislamu ambao viapo vyao vya utii vilikuwa vyenye uaminifu kamili waliwafuata wale maadui nje ya ule uwanja wa vita. Lakini wengi waliacha kule kuwafuatilia wale maadui na wakaziweka chini silaha zao na kuanza kukusanya ngawira na wakadhania kwamba vita imemalizika.

Wale watu wanaolilinda lile bonde lililokuwako nyuma ya mstari wa mbele wa vita nao waliamua kuitumia fursa ile na wakaambiana: “Hakuna faida yoyote kwetu kubakia hapa na ni jambo lenye faida kwamba sisi nasi tukusanye ngawira.” Hata hivyo, kamanda wao aliwakumbusha kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba jeshi la Waislamu lipate ushindi au kushindwa wasitoke kwenye sehemu yao ile. Wengi wa askari wa mishale waliokuwa wakikilinda kipenyo kile, walimpinga kamanda wao na kusema: “Kukaa kwetu hapa hakuna faida na Mtume alikuwa na maana tu ya kwamba tukilinde kipenyo hiki vita ilipokuwa ikiendelea lakini hivi sasa mapigano yamekwisha.”

Kwa msingi wa dhana hii potovu, watu arobaini walishuka kutoka kwenye ile sehemu ya doria na watu

kumi tu ndio waliobakia pale. Khalid bin Walid, aliyekuwa shujaa na mzoefu na alijua tangu mwanzoni kwamba kinywa cha kipenyo kile kilikuwa ufunguo wa ushindi, na kwa mara nyingi sana alijaribu kufika katika ule mstari wa mbele wa vita kupitia kwenye kipenyo hiki, lakini alikabiliwa vikali na wale wapiga mishale. Wakati huu alijinufaisha kutokana na ile idadi ndogo ya walinzi.

Aliwaongoza askari wake kuelekea ule upande wa nyuma wa jeshi la Waislamu na kufanya mashambulizi ya kushtusha na hatimaye alifika kwenye kundi la Waislamu. Mara baada ya hapo wale Waislamu wasio na silaha na wazembe walishambuliwa vikali mno kwa nyuma.
Baada ya kuikamata ile sehemu nyeti Khalid aliomba ushirikiano wa lile jeshi la Waquraish lililoshindwa lililokuwa kwenye hali ya kukimbia, na wakauimarisha moyo wa upinzani na uvumilivu wa Waquraishi, kwa makelele na vilio vya kurudia rudia. Kutokana na mfarakano na rabsha zilizokuwako kwenye safu za Waislamu, mara moja jeshi la Waquraish likawazunguka mashujaa wa Kiislamu na mapigano yakaanza tena baina yao.

Kushindwa huku kulitokana na kutojali kwa wale watu waliokitoka kile kipenyo kwa ajili ya faida zao za kidunia na bila ya kudhamiria wakawafungulia njia maadui kwa jinsi ambayo askari wapanda wanyama waliokuwa chini ya uongozi wa Khalid bin Walid waliingia katika uwanja wa vita kutokea nyuma ya Waislamu.

Mashambulizi ya Khalid yalisaidiwa na mashambulizi ya Ikrimah bin Abi Jahl na mvurugiko wa utaratibu usio na kifani na wa kushtusha ulitokea kwenye safu za Waislamu. Waislamu hawakuwa na lolote jingine ila kujihami katika hali ya vikundi vilivyotawanyika. Hata hivyo, kwa vile mawasiliano na kamanda nayo yamekatwa hawakufaulu katika kujihami na walipatwa na msiba mkubwa mno kiasi kwamba baadhi ya askari wa Kiislamu waliuawa na Waislamu wenzao kwa uzembe.

Mashambulizi ya Khalid na Ikrimah yaliuimarisha moyo wa jeshi la Waquraishi. Wale askari waliokuwa wakirudi nyuma na kukimbia waliingia tena kwenye uwanja wa vita na kuwapa msaada. Waliwazingira Waislamu pande zote na kuua idadi fulani miongoni mwao.

Tetesi Juu Ya Kuuwawa Kwa Mtume (S.A.W.W) Zaenea

Shujaa mmoja wa Waquraishi aitwaye Layth alimshambulia Mas'ab bin Umayr, yule mshika bendera jasiri wa Uislamu, na baada ya kubadilishana idadi fulani ya dharuba yule mshika bendera wa Uislamu aliuawa. Kwa kuwa wale mashujaa wa Kiislamu walikuwa wamezificha nyuso zao, Layth alifikiri kwamba yule mtu aliyeuawa alikuwa ni Mtume wa Uislam (s.a.w.w.).

Hivyo alipiga ukelele na kuwajulisha wale machifu wa jeshi kwamba Muhammad ameuawa. Tetesi hii ilienea toka kwa mtu hadi kwa mtu mwingine kwenye jeshi la Waquraish. Machifu wao walifurahi mno kiasi kwamba sauti zao zilivuma mle kwenye uwanja wakisema: "Enyi watu! Muhammad ameuawa! Enyi watu! Muhammad ameuawa!"

Kuenea kwa taarifa za uwongo kulimhamasisha adui na jeshi la Waquraishi likaja kuendelea na vita. Kila mmoja wao alipendelea kushiriki katika kukata viungo vya Muhammad ili kwamba aweze kukipata cheo kikubwa kwenye ule ulimwengu wa washirikina.

Taarifa hizi zilizidhoofisha nyoyo za mashujaa wa Kiislamu zaidi ya vile zilivyozipa nguvu nyoyo za jeshi la maadui. Kwa kiasi kwamba idadi fulani miongini mwa Waislamu waliacha kupigana na wakakimbilia mlimani na hakuna yeyote aliyebakia kwenye uwanja wa vita ila wachache tu ambao waliweza kuhesabiwa katika vidole vya mikono.

Je, Yawezekana Kukana Kule Kukimbia Kwa Baadhi Ya Watu?

Haiwezekani kukana kwamba baadhi ya masahaba walikimbia kutoka kwenye uwanja wa vita, na hivyo ukweli wa kwamba walikuwa ni masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) au kwamba baadae walijipatia vyeo na heshima miongoni mwa Waislamu usituzuie kuukubali ukweli huu ulio mchungu.

Ibn Hisham, mwanahistoria maarufu, anaandika hivi: "Anas bin Nazr, ami yake Anas bin Malik anasema: "Jeshi la Waislamu lilipoelemewa, na taarifa za kuuwawa kwa Mtume zilipoenea, wengi wa Waislamu waliufikiria uhai wao wenyewe na kila mtu alikimbilia kwenye pembe moja au nyingine." Anaongeza kusema: "Nililiona kundi la Muhajiriin na Ansar wakiwamo Umar bin Khattab na Talhah bin Ubaydullah Taymi, waliokuwa wamekaa kwenye pembe na walikuwa na hofu ya hatari juu yao wenyewe. Niliwauliza kwa sauti ya kutopendelea: "Kwa nini mnakaa hapa?" Walijibu: "Mtume ameuwawa na hivyo basi, hakuna faida yoyote ya kupigana." Niliwaambia: "Kama Mtume ameuwawa, basi hakuna faida ya kuishi. Simameni na mkutane na kufa kishahidi kwenye njia ile ile aliyofia."[20]

Kwa mujibu wa kauli ya wanahistoria wengi, Anas alisema: "Kama Muhammad ameuwawa Mola wake yupo hai." Na kisha akaongeza kusema: "Niliona kwamba maneno yangu hayakuwa na athari yoyote kwao. Nilikiweka kiganja changu kwenye silaha yangu na nikaanza kupigana kwa ushupavu." Ibn Hishamu anasema kwamba, Anas alipata majeraha makubwa kwenye vita hivi na hakuna aliyeweza kuitambua maiti yake ila dada yake tu.[21]

Kikundi fulani cha Waislamu walikuwa wamedhoofishwa mno kiasi kwamba ili kuhakikisha usalama wao, walipanga kumwendea Abdullah bin Ubay ili aweze kuwapatia usalama kutoka kwa Abu Sufyan.[22]

Qur'ani Tukufu Yafichua Baadhi Ya Mambo

Aya za Qur'ani Tukufu zinalipasua pazia la ushabiki wa kidini na ujinga na zinadhihirisha vya kutosha kwamba baadhi ya masahaba walifikiria kwamba, ahadi aliyoiahidi Mtume (s.a.w.w.) juu ya ushindi na kufuzu haikuwa na msingi, na Allah Mwenye nguvu zote anasema hivi kuhusiana na kundi hili: **"..... Na kundi jingine limeshughulishwa na nafsi zao, wakimdhania Mwenyezi Mungu lisilokuwa haki, dhana ya kikafiri. Husema: Tuna kitu katika jambo hili? ... . ." (*Surah Aali Imran* 3:154).**

Unaweza kuzitambua habari zilizojificha juu ya vita hivi kwa kuzisoma aya za Sura Aali Imran. Aya hizi zinaunga mkono kikamilifu mambo wanayoyaamini Mashi'a. Wao wanaamini kuwa sio kweli kwamba masahaba wote walikuwa wenye kujitolea mhanga au wapenzi wa Uislamu.

Baadhi ya watu miongoni mwao walikuwa wanafiki. Na wakati ule ule miongoni mwa masahaba lilikuwemo kundi kubwa la waumini wa kweli na wachamungu na watu waaminifu. Siku hizi kikundi cha waandishi wa Kisunni wanajaribu kulitanda pazia juu ya mengi ya matendo yasiyo na thamani ya masahaba (mifano yao umeiona kwenye maelezo yanayohusu vita hivi). Wamevihami vyeo vyao wote kwa kutoa maelezo ya kweli yaonyeshayo ushupavu wao wa kidini tu, lakini nayo hayawezi kuzificha habari halisi za historia.

Ni nani awezaye kukikana kiini cha aya hii ambayo wazi wazi inasema hivi: **"Kumbukeni mlipokuwa mkikimbia mbio wala hamkumtazama yeyote na hali Mtume akiwaiteni kwa nyuma yenu….."** (***Surah Aali Imran*, 3:153**).

Aya hii inazungumzia juu ya watu wale wale aliowaona Anas bin Nazr kwa macho yake walipokuwa wameketi kwenye pembe, nao walikuwa wakiyahofia maisha yao ya baadaye. Aya ifuatayo inaelezea zaidi kuliko ile tuliyoimukuu hapo juu:

إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ إِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا ۖ وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ {155}

"Hakika wale waliokimbia miongoni mwenu siku* (*ya Uhud*) *yalipokutana majeshi mawili, hakika ni shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya waliyoyachuma.
Na Allah Amekwisha wasamehe, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mvumilivu."
(***Surah Aali Imran, 3:155*).**

Katika Aya ifuatayo Allah anawakaripia wale watu waliozifanya taarifa za kuuawa kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni udhuru wa kuacha kupigana, nao walikuwa wakifikiria kumwendea Abu Sufyan kupitia kwa Abdullah bin Ubayy ili awathibitishiye usalama wao:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۚ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ۚ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ {144}

"Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume aliyepitiwa na Mitume kabla yake. Basi je, akifa au akiuliwa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu? Na atakayerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaoshukuru."
(***Surah Aali Imran, 3:144*).**

Uzoefu Mchungu

Tunapochunguza matukio ya Uhud ukweli fulani wenye uchungu na mtamu hupatikana; nguvu ya uthabiti na uvumilivu wa kundi moja na utovu wa uthabiti wa kundi jingine unaweza kuonekana waziwazi. Wanahistoria, wachanganuzi wa mambo na wengineo ambao huandika habari za matukio, unaposoma taarifa zao, inakuwa dhahiri kabisa kwamba masahaba wote hawawezi kuchukuliwa kuwa ni wachamungu kabisa na waadilifu, eti kwa sababu tu kwamba wao walikuwa ni masahaba, hivyo miongoni mwa wale watu waliokitoka kile kilima cha wapiga mishale, na wale walioupanda ule mlima katika wakati ule nyeti na kuuacha mwito wa Mtume (s.a.w.w.) walikuwamo masahaba walewale wanaoheshimiwa.

Mwanahistoria mashuhuri wa Uislamu, Waaqid anasema: "Katika siku ya Uhud watu wanane walikula kiapo cha utii kwa Mtume (s.a.w.w.) wakimthibitishia kuyatoa maisha yao kwa ajili yake. Miongoni mwao watatu walikuwa Muhajiriin (Ali, Talhah na Zubayr) na wale watano waliosalia walikwua Ansar na ukiwachilia mbali hawa watu wanane, watu wote walikimbia katika wakati ule nyeti."

Ibn Abil Hadid anaandika hivi:23 "Katika mwaka wa 608 Hijiriya nili– hudhuria kwenye mkutano mmoja mjini Baghdad ambao watu fulani walikuwa wakikisoma kitabu cha Maghaazil–Waaqidi mbele ya mwanachuoni mkuu Muhammad bin Ma'ad Alawi. Walipoifikia hatua ambayo Muhammad bin Maslamah anasimulia waziwazi kuwa: "Katika siku ya Uhud niliona kwa macho yangu kwamba Waislamu walikuwa wak– iupanda mlima na Mtume alikuwa akiwaita kwa majina yao maalum na alikuwa akisema: "Ewe fulani! Ewe fulani!" Lakini hakuna hata mmoja wao aliyeitika mwito ule wa Mtume." Mwalimu aliniambia: "Maneno 'fulani na fulani' yalikuwa na maana ya walewale watu waliojipatia vyeo na nafasi baada ya Mtume. Huyu msimuliaji hakuyataja majina halisi kutokana na hofu, na kwa sababu ya heshima ambayo alitegemea kuwapa."

Katika tafsiri yake vilevile amesimulia kwamba wengi wa wasimuliaji wanapatana juu yake kwamba Khalifa wa tatu alikuwa mmoja wa watu wale ambao hawakuwa imara na thabiti kwenye uwanja wa vita katika wakati ule nyeti.

Baadae utaisoma sentensi ya Mtume (s.a.w.w.) juu ya mwanamke wa Uislamu aliyejitolea mhanga aliyeitwa Nasibah aliyemhami Mtume (s.a.w.w.) kwenye uwanja wa vita wa Uhud. Kwenye sentensi ile, vilevile kuna dokezo la kushuka daraja na sifa za wale waliokimbia. Hatuna haja ya kutoa taarifa za yeyote miongini mwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.). Lengo letu ni kuleta hali halisi kwenye mwanga na kuelezea ukweli. Tunakulaumu kukimbia kwao sawa kabisa na vile tunavyosifu uthabiti na uvumilivu wa lile kundi jingine na kuichukulia tabia yao kuwa ni nzuri sana.

Watu Watano Wapanga Kumuua Mtume (S.A.W.W)

Wakati ule ambao jeshi la waislamu lilikabiliwa na mvurugiko wa utaratibu na ghasia, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akishambuliwa kutoka pande zote. Watu watano wabaya kutoka miongoni mwa Waquraishi

walidhamiria kuyamalizia mbali maisha ya Mtume (s.a.w.w.) kwa vyovyote vile iwavyo. Watu hawa walikuwa ni:

1. Abdullah bin Shanaab aliyelijeruhi paji la uso la Mtume (s.a.w.w.).

2. ‘Utbah bin Abi Waraqa, ambaye kwa kumtupia mawe manne alimvunja meno yake ya upande wa kulia.24

3. Ibn Qumi’ah Laythi aliyemjeruhi Mtume (s.a.w.w.) usoni. Jeraha hili lilikuwa kali sana kiasi kwamba pete za kofia yake ya chuma zilimchoma kwenye mashavu yake! Pete hizi zilichomolewa na Abu Ubaydah Jarraah kwa meno yake naye alipoteza meno yake manne katika kufanya hivyo.

4. Abdullah bin Hamid, aliyeuawa mikononi mwa shujaa wa Uislamu Abu Duj?nah wakati wa kushambulia.

3. Abi Khalf. Alikuwa mmoja wa watu wale waliokufa mikononi mwa Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Alimkabili Mtume (s.aw.w) wakati yeye (Mtume s.a.w.w) alipofaulu kulifikia lile bonde huku baadhi ya masahaba wakiwa wamemkusanyikia baada ya kumtambua. Abu Khalf alimsogelea Mtume (s.a.w.w.) ndipo Mtume (s.a.w) akauchukua mkuki kutoka kwa Hasis bin Simmah na kuuchoma shingoni mwa Abi Khalf na matokeo yake ni kwamba Abi Khalf alianguka chini kutoka kwenye farasi wake.

Ingawa lile jeraha alilotiwa Abi Khalf lilikuwa dogo tu, alipatwa na hofu mno kiasi kwamba marafiki zake walipomfariji hakuweza kutulia akasema: “Nilimwambia Muhammad kule Makka kwamba nitamwua naye alinijibu akisema kwamba ataniua, naye katu hasemi uongo.”

Yote yalimalizika kwake kutokana na lile jeraha na woga, na baada ya muda fulani alikufa alipokuwa njiani akienda Makka.25

Hakuna shaka yoyote kwamba tukio hili laonyesha udhaifu wa mbali kabisa wa washirikina. Ingawa upo ukweli kwamba walikubali kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mkweli na katu hakusema uwongo, lakini walitaka kuimwaga damu yake.

Mtume (s.a.w.w.) hakusonga kutoka mahali alipokuwa. Alisalia kuwa thabiti kama mwamba na akaendelea kujihami yeye mwenyewe na Uislamu. Ingawa ulikuwepo ukweli kwamba umbali baina ya maisha yake na kifo umekuwa mfupi sana na aliweza kuona vizuri kwamba jeshi la adui lilikuwa likimgeukia kama wimbi, lakini hakusogea kutoka pale alipokuwa, wala hakutamka neno lolote lile ambalo lingaliweza kuisaliti hofu yoyote ile au maumivu kwa upande wake.

Na pale alipokuwa akiipangusa damu kutoka kwenye paji la uso wake alisema: “Vipi watu wataweza kuupata wokovu kama wanaupaka uso wa Mtume wao damu anapowaita kwenye ibada ya Allah?” Na hii yaonyesha upole mwingi na huruma hata kwa maadui zake.

Sayyidna Ali, Amiri wa Waumini (a.s.) anasema: “Mtume alikuwa karibu sana na adui kwenye uwanja

wa vita na akatupatia kimbilio wakati mambo yalipokuwa magumu.” Hivyo, moja ya sababu zilizomwezesha Mtume (s.a.w.w.) kubakia salama ni kule kujihami kwake yeye mwenyewe na Uislamu, lakini vilevile ilikuwako sababu yingine iliyomthibitishia uhai wake, nayo ni kujitolea mhanga kwa marafiki zake wachache walio waaminifu na wakweli na masahaba walioyanunua maisha yake kwa gharama ya maisha yao wenyewe, na kuubakisha salama mshumaa uwakao kutokana na kuzimishwa. Mtume (s.a.w.w.) alipigana pigano kali mno katika siku ile ya Uhud na alitupa mishale yote iliyokuwamo kwenye podo lake, kiasi kwamba upinde wake ulivunjika na kamba yake nayo ikakatika.26

Idadi ya wale waliomhami Mtume (s.a.w.w.) haikuzidi ile ya watu wachache.27 Hata hivyo, umadhubuti wao wote haukaniki, lakini ni dhahiri kutokana na historia isemavyo, la uhakika na lenye kukata maneno miongoni mwa wanahistoria ni ule uthabiti wa kundi dogo mno. Taarifa za ulinzi walioufanya zinatolewa hapa.

Ulinzi Ulioandamana Na Kufuzu Na Kushinda Upya.

Haitakuwa vibaya kama hii sehemu ya historia ya Uislamu tukiipa jina la “ushindi uliopatikana upya.’ Maana ya ushindi huu ni kwamba, kinyume na mategemeo ya maadui, waislamu walifaulu kumwokoa Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kifo. Huu ndio ule ushindi uliopatikana tena ulio- liangukia kura ya jeshi la Waislamu.

Kama tukiushirikisha ushindi huu na lile jeshi zima la Waislamu tutakuwa tunafanya hivyo ikiwa ni dalili ya heshima kwa wale mashujaa wa Uislamu. Hata hivyo, kwa kweli ule mzigo mzito wa ushindi huu umean- gukia mabegani mwa watu wachache walioweza kuhesabiwa katika vidole vya mkono. Hawa walikuwa wale watu waliomhami Mtume (s.a.w.w.) kwa kuyahatarisha maisha yao wenyewe, na hakika ilikuwa ni kutokana na kujitolea mhanga kwa hili kundi la watu wachache kwamba Dola ya Kislamu ilibakia kuwa na ujuzi wa utendaji wa mambo katika wakati wa shida, na hivyo ule mshumaa uangazao ukaendelea kuwaka badala za kuzimika.

Yafuatayo hapa chini ni maelezo ya matendo ya ujasiri ya hawa watu waliojitolea mhanga:

1. Sayyidna Ali bin Abi Twalib (a.s.): Mtu wa kwanza mwaminifu na madhubuti alikuwa ni afisa shujaa, ambaye wakati ule alikuwa kaumaliza mwaka wa ishirini na sita tu wa maisha yake, na aliyekuwa akimhudumia Mtume (s.a.w.w.) tangu utotoni mwake hadi katika wakati wa kifo cha Mtume (s.a.w.w.), naye hakuacha kujitolea mhanga na kumsaidia japo kwa muda mfupi tu. Afisa huyu mkuu na mchamungu halisi alikuwa ni Imamu Ali, Sayyidi wa wachamungu na Amiri wa Waumini, ambaye huduma na kujitolea kwake katika njia ya Uislamu vimeandikwa kweye historia.

Kimsingi huu ushindi uliopatikana tena ulifikia kama ule ushindi wa kwanza kwa njia ya ushujaa na kujitolea mhanga kwa yule mtu mwaminifu, kwa sababu ni dhahiri kwamba sababu ya kukimbia kwa Waquraishi kwenye ile hatua ya awali kabisa ya vita vile ni kwamba washika bendera wao wali- uwawa, mmoja baada ya mwingine, na wote waliuwawa mikononi mwa Sayyidna Ali (a.s.), na matokeo yake ni

kwamba jeshi la Waquraishi lili– tishwa mno kiasi kwamba waliipoteza nguvu yao ya kubakia pale uwanjani na kuzuia mashambulizi ya Waislamu. Waandishi wa Kimisri wa zama zetu hizi walioliachanganua tukio hili, hawakumtendea haki Sayyidna (a.s.) kulingana na kile cheo chake au habari halisi zilizoandikwa kwenye historia na wamezichukulia huduma za Amiri wa Waumini (a.s.) kuwa sawa na zile za wale wengine. Hivyo basi, tunaona kuwa ni muhimu kutoa hapa taarifa fupi za kujitolea kwake na mihanga aliyoitoa.

Ibn Athir anasema:28 "Mtume akawa shabaha ya mashambulizi ya kila kisehemu cha jeshi la Waquraishi kutoka pande zote. Ali alishambulia kufuatana na maamrisho ya Mtume kila kisehemu cha jeshi lile kili– chomshambulia (Mtume), na akawatawanya au akawaua baadhi yao, na jambo hili lilitokea kwa mara kadhaa pale Uhud. Wakati huo huo, Malaika mkuu Jibriil alikuja na akakusifu kujitolea kwa Ali mbele ya Mtume na akasema: "Haki ni kilele cha kujitolea mhanga ambacho afisa huyu anakionyesha." Mtume akayathibitisha yale maelezo ya Jibriil na akasema: "Mimi ninatokana na Ali na Ali anatokana na mimi." Kisha ilisikika sauti mle kwenye uwanja wa vita ikisema: *"La Saifa ila Dhulfiqar, La Fataa illa Ali*" Yaani "Hakuna upanga utoao huduma ila Dhulfiqar iliyokuwamo mkononi mwa Ali na hakuna mtu aliye shujaa ila Ali."

Ibn Abil Hadid ametoa maelezo marefu zaidi ya tukio hili na anasema: "Kila kimoja cha vile visehemu vya jeshi vilivyokuwa vikijaribu kumwua Mtume kilikuwa na watu hamsini, na ingawa alikuwa hana mnyama wa kupanda lakini alivitawanyisha vyote."

Kisha akatoa maelezo ya kuja kwa Jibril na akasema: "Ukiuachilia mbali ukweli uliopo kwamba tukio hili ni jambo likubaliwalo kwa maoni ya his– toria, nimesoma taarifa za kuja kwa Jibriil kwenye kitabu cha Muhammad Bin Is'haq kiitwacho '*Kitaabul Ghazwaat*' na siku moja nikabahatika kuulizia kuhusu usahihi wake kutoka kwa mwalimu wangu Abdul Wahhaab Sakinah. Alisema: 'Ni sahihi'. Kisha nikauliza: 'Kwa nini Hadith hii haikuandikwa na wakusanyaji wa Sihah?'29Akajibu akisema: "Tunayo idadi ya Hadith Sahihi ambazo wakusanyaji wa Sihah wameziacha kuziweka kwenye vitabu vyao."30

Katika hotuba ndefu aliyoitoa Sayyidna Ali (a.s.) kwa ajili ya 'Raas al– Yahud' mbele ya kikundi cha wafuasi wake, anarejelea kwenye kujitolea kwake mhanga kwa maneno haya: "... Jeshi la Maquraishi lilitushambulia kama jeshi moja tu, Ansar na Muhajiriin walikimbilia majumbani mwao nami nilipata majeraha makubwa nikimhami Mtume."

Kisha yeye (Ali) akalivutia kando vazi lake na akazionyesha zile sehemu ambazo alama za majeraha (kovu) zilikuwa bado zinaonekana.31 Zaidi ya hapo, kama ilivyoandikwa mwenye '*Ilalusha Sharaa'i*'32 Ali (a.s.) alipokuwa akimhami Mtume (s.a.w.w.), alionyesha ushujaa mwingi na kujitolea mhanga kiasi kwamba upanga wake ulikatika vipande viwili. Hapo Mtume (s.a.w.w.) alimpa upanga wake uitwao '*Dhulfiqaar*' na kwa upanga huu aliendeleza jihadi katika njia ya Allah.

Kwenye kitabu33 chake chenye thamani, Ibn Hishamu ameitaja idadi ya wale waliouawa kutoka miongoni mwa wenye kuabudu masanamu kuwa ni ishirini na wawili na vilevile imeyataja majina na sifa

zao na akitoa pia jina la kabila n.k. Miongoni mwa hawa watu ishirini na wawili, kumi na wawili waliuawa na Sayyidna Ali (a.s.) na wale kumi waliobakia waliuawa na Waislamu wengine. Waandishi wa wasifu wa maisha ya Mtume (s.a.w) tuliowataja, wameyataja waziwazi majina na sifa za wale waliouawa.

Tunakubali kwamba haikuwezekana kwetu sisi kutoa kwenye kurasa hizo, sura halisi ya huduma alizozitoa Sayyidna Ali (a.s.) kama ilivyoelezwa kwenye vitabu vya madhehebu zote mbili, hasa kwenye kitabu kiitwacho *Bihaarul Anwaar*.34

Inatambulika kutokana na kuchunguza maelezo na Hadith mbalimbali kwamba, pale Uhud hakuna aliyekuwa kama vile alivyokuwa Sayyidna Ali (a.s.) na hata Abu Dujaanah aliyekuwa afisa wa Uislamu hodari na shujaa hakuweza kuwa sawa naye katika suala la ulinzi.

2. Abu Dujaanah: Baada ya Amiri wa Waumini, Abu Dujaanah alikuwa afisa wa pili aliyeihami nafsi ya Mtume (s.a.w.w.) katika hali ambayo ali– jifanya kuwa kofia ya chuma kwa ajili yake. Mishale ilikuwa ikimkaa mgongoni na kwa njia hiyo alikuwa akimhami Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kuwa shabaha yao.

Marehemu Sipahr, ameandika sentensi moja juu ya Abu Dujaanah kwenye kitabu chake kiitwacho '*Nasikhut Tawaarikh*,35 hatukuweza kuipata asili yake. Anaandika hivi: "Mtume na Ali walipozungukwa na wenye kuyaabudu masanamu macho ya Mtume yalimwangukia Abu Dujaanah na akamwambia: "Ewe Abu Dujaanah! Ninakutoa kwenye kiapo chako. Hata hivyo Ali yu wangu na mimi ni wake." Abu Dujaanah alilia sana na akasema: "Mimi niende wapi? Je, niende kwa mke wangu ambaye hana budi kufa? Je niende kwenye nyumba yangu itakayobomoka? Je, niuendee utajiri wangu na mali zangu zitakazoharibiwa? Je, nikimbilie kifo ambacho ni lazima kije?"

Mtume alipoyaona machozi machoni mwa Abu Dujaanah alimruhusu kupigana, na wote wawili, yeye na Ali walimhami Mtume (s.a.w.w.) kutokana na mashambulizi makali ya Waquraishi.

Kwenye vitabu vya Historia tunaona majina ya watu wengine kama vile Aasim bin Thaabit, Sahl Hunayf Talhah bin Ubaydullah n.k. katika nyadhifa za wa wale waliobakia kuwa madhubuti, na baadhi ya wanahistoria wameitaja idadi ya watu hao kuwa ni karibuni thelathini na sita. hata hivyo, kile kilicho dhahiri kutokana na historia ni kule kutobadilika kwa Sayyidna Ali (a.s.), Abu Dujaanah, Hamza, na Bibi aitwaye Ummi Amir. Ama uimara wa watu wengine wenyewe ni wenye kutuhumiwa, ila kwa hawa wanne na katika hali nyingine ni wenye kutiliwa mashaka.

3. Hamza bin Abdul Muttalib: Yeye ni mfano wa kujitolea mhanga kwa afisa shujaa. Kumekuwako idadi fulani ya maofisa shujaa na wenye kujitolea mhanga na mashujaa wenye nguvu na uwezo kwenye jeshi la Uislamu lakini ushujaa wa Hamza bin Abdul Muttalib umeandikwa kwenye kurasa za historia, na kwa hakika unatoa majani ya dhahabu ya historia ya vita vya Uislamu.

Hamza ami yake Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alikuwa mmoja wa watu waliokuwa mashujaa zadi barani Arabu na afisa maarufu wa Uislamu. Ni yeye aliyeshikilia kwa uaminifu kwamba jeshi la Uislamu liende nje ya Madina na kupigana dhidi ya Waquraishi. Ni yeye Hamza aliyemhami Mtume (s.a.w.w.)

mjini Makka kwenye ule wakati nyeti kwa nguvu zake zote na ili kulipiza kisasi cha matusi na madhara aliyofanyiwa Mtume (s.a.w.w.) na Abu Jahl, alikivunja kichwa cha Abu Jahl kwenye mkutano mkuu wa Waquraishi na hakuna yeyote aliyethubutu kumpinga. Alikuwa afisa mkuu na shujaa aliyemwua yule mtetezi shujaa wa Waquraishi aliyeitwa Shaybah na wengineo. Vile vile akakijeruhi kikundi cha maadui kwenye Vita vya Badr. Hakuwa na lengo lolote akilini mwake ila kuuhami ukweli na maadili na kudumisha uhuru katika maisha ya wanadamu.

Hind, mkewe Abu Sufyan alikuwa bint yake Utbah. Mwanamke huyu alikuwa na mfundo dhidi ya Hamza na alikusudia kumlipizia kisasi baba yake katika upande wa Waislamu kwa gharama yoyote ile. Wahshi, shujaa wa Kiethiopia alikuwa mtumwa wa Jaabir bin Mut'am na ami yake Jaabir naye aliuawa kwenye Vita vya Badr. Yeye (Wahshi) aliteuliwa na Hind kumsaidia katika kulifikia lengo lake kwa vyovyote vile. Alimwomba auwe miongoni mwa watu watatu (ambao ni Mtume s.a.w, Ali au Hamza) ili kwamba aweze kulipiza kisasi cha kifo cha baba yake. Yule shujaa wa Kiethiopia akamjibu akisema: "Siwezi kabisa kumkabili Muhammad, kwa sababu masahaba zake wako karibu zaidi naye kuliko yeyote mwingine.

Ali naye yu mwangalifu mno awapo kwenye uwanja wa vita. hata hivyo, Hamza yu mwenye ghadhabu mno kiasi kwamba anapopigana haangalii upande wowote mwingine, na inawezekana kwamba nikiweza kumwan– gusha kwa njia fulani au kwa kumshtukizia."

Hind alitosheka na maneno haya na akamwahidi kwamba kama akifaulu kuifanya kazi ile atampa uungwana. Baadhi ya watu wanaamini kwamba Jaabir ndiye aliyeitoa ahadi hii kwa huyu mtumwa wake (Wahshi) kwa kuwa ami yake (Jaabir) aliuawa kwenye vita vya Badr.

Wahshi, yule mtumwa anasema: "Katika siku ya Uhud nilikuwa nikimfuatia Hamza. Alikuwa kama simba aliyeghadhibika. Alimwua kila mmoja aliyeweza kumfikia. Nilijificha kiasi kwamba hakuweza kuniona. Alikuwa akijishughulisha mno na mapigano.
Nilitoka kutoka kwenye yale maficho. Nilikuwa ni Mwethiopia, nilikuwa na desturi ya kuitupa silaha yangu kama wao (yaani kama Waethiopia) na mara chache sana niliikosa shabaha niliyo kusudia. Hivyo, nilimtupia mkuki wangu kutoka kwenye umbali maalumu baada ya kuutayarisha mtupio kwa jinsi maalumu. Silaha ile ilimchoma ubavuni na ikatokea baina ya miguu yake miwili. Alitaka kunishambulia lakini maumivu makali yalimzuia kufanya hivyo. Alibakia kwenye hali hiyo hadi roho yake ilipotoka mwili wake. Kisha nilimwendea kwa uangalifu na baada ya kuichomoa silaha yangu kutoka mwilini mwake, nilirejea kwenye jeshi la Waquraishi na kuusubiri ungwana wangu.

Baada ya vita ya Uhud niliendelea kuishi mjini Makka kwa muda mrefu sana hadi Waislamu walipouteka mji wa Makka. Kisha nilikimbilia Taa'if, lakini upesi sana Uislamu ulifika sehemu ile pia. Nilisikia ya kwamba vyovyote vile ubaya wa jinai la mtu uwezavyo kuwa, Mtume alimsamehe mtu huyo. Hivyo nilimwendea Mtume na 'Shahaadatayn' midomoni mwangu (yaani nilishuhudia kwamba hakuna mungu ila Allah na vile vile nikashuhudia ya kwamba Muhammad yu Mtume).

Mtume aliniona na akasema: "Wewe ndiwe Wahshi Mwethiopia?" Nikajibu: "Ndio." Baaada ya hapo

akasema: “Ulimwuaje Hamza?” Nilitoa maelezo ya tukio lile. Mtume (s.a.w.w.) alihuzunika sana na akasema: “Nisione uso wako kwa kadiri uwavyo hai, kwa sababu msiba wenye kuupasua moyo ulimwan- gukia ami yangu mikononi mwako.”

Ni moyo mkuu uleule wa Mtume wa Uislamu uliomfanya amwachie huru mtu huyu ingawa angeweza kumnyonga kutokana na makosa mengi. Wahshi anasema: “Kwa kadri Mtume alivyokuwa hai nilijificha kutoka machoni pake. Baada ya kifo chake ilitokea Vita dhidi ya Musaylimah Kazzaab. Nilijiunga na jeshi la Waislamu na nikaitumia silaha ileile dhidi ya Masaylimah na nikafaulu kumwua kwa msaada wa mmoja wa Ansar. Kama nilimwua mtu aliyekuwa bora zadi miongoni mwa watu, (yaani Hamzah) kwa silaha hii, mtu mwovu naye hakuweza kukiepuka kitisho chake kikuu.”

Kushiriki kwa Wahshi kwenye vita dhidi ya Musaylimah ni jambo analol- idai yeye mwenyewe, lakini Ibn Hisham anasema: “Kwenye siku za mwis- honi mwa uhai wake Wahshi alikuwa kama kunguru mweusi aliyekuwa daima akichukiwa na Waislamu kutokana na ulevi wake na aliadhibiwa mara mbili kutokana na kunywa mvinyo. Kutokana na tendo hili baya, jina lake lilifutwa kwenye kumbukumbu za kijeshi na Umar bin Khattab alikuwa akisema: Mwuwaji wa Hamza hastahili kusamehewa huko kwenye ulimwengu wa Akhera.”[36]

4. Nasibah bint Kaab: Mwanamke mwenye kujitolea mhanga. Hakuna apingaye kwamba jihadi ni haramu kwa wanawake katika dini ya Uislamu. Kuhusiana na jambo hili tunaweza kusema hapa kwamba mwak- ilishi wa wanawake wa Madina aliyepata heshima ya kufika mbele ya

Mtume (s.a.w.w.) akazungumza naye kuhusu huku kunyimwa jihadi na kulalamika kwa maneno haya: “Tunawapatia waume zetu mahitaji yote ya maisha, nao wanashiriki kwenye jihadi wakiwa kwenye amani ya kiakili, ambapo sisi wanawake tunanyimwa baraka hii kuu.”

Hapo ndipo Mtume (s.a.w.w.) aliwapelekea wanawake wote wa Madina ujumbe ufuatao kupitia kwake: “Kama mmenyimwa baraka hii kuu kutokana na sababu za kimaumbile na kijamii, mnaweza kujipatia baraka za jihadi kwa kuyatekeleza majukumu ya maisha ya ndoa.”

Kwenye uhusiano huu, vile vile aliitamka sentensi ya kihistoria ifuatayo: “(Mwanamke) kuyatekeleza majukumu ya maisha ya ndoa kwa jinsi itakikanavyo ni sawa na jihadi katika njia ya Allah.”

Hata hivyo wakati fulani, baadhi ya wanawake wazoefu walitoka nje ya mji wa Madina pamoja na Mujahidiin (ambao hasa walikuwa ni wana wao, kaka zao na ndugu zao) ili kwenda kuwasaidia, nao waliwasaidia Waislamu katika kupata ushindi kwa kuwapa maji wenye kiu, kufua nguo za mashujaa na kuyafunga majeraha ya wale waliojeruhiwa.

Ummi Aamir, ambaye jina lake hasa lilikuwa Nasibah, anasema: “Nilijiunga na vita ya Uhud ili kuwapatia maji mashujaa na niliona kwam- ba hewa yenye kunukia vizuri ya ushindi ilikuwa ikivuma kuwaelekea Waislamu. Lakini upesi baada ya hapo, meza zilipinduliwa upesi sana na wale Waislamu walioshindwa wakaanza kukimbia. Vile vile niliona kwam- ba maisha ya Mtume yalikuwa hatarini, na nilifikiria kwamba

ni jukumu langu kuyaokoa maisha yake japo iwe kwa gharama ya maisha yangu. Hivyo nilikiweka chini kiriba changu cha maji na kuanza kuyarudisha nyuma mashambulizi ya adui kwa upanga uliopata kufika mkononi mwan- gu. Wakati mwingine vile vile nilipiga mishale."

Kisha alilitaja jeraha alilolipata begani mwake, na akasema: "Kwenye wakati ambao watu wamewageuzia migongo yao maadui, huku wakiwa wanakimbia, macho ya Mtume yalimwangukia mtu mmoja aliyekuwa kwenye hali ya kukimbia na akamwambia: "Hivyo sasa unakimbia, itupe chini ngao yako." Alifanya hivyo nami nikaiokota ili niitumie. Ghafla nilimwona mtu aitwaye Ibn Qumi'ah akipiga ukelele na kusema: "Yuko wapi Muhammad?"

Alimtambua Mtume na akamkimbilia huku akiwa na upanga uliofutwa. Mas'ab na mimi tulimzuia dhidi ya kulitimiza lengo lake. Ili kunirudisha nyuma, alinipiga dhoruba begani mwangu. Ingawa mimi nami nilimpiga dharuba, lakini dharuba yake ilikuwa na athari kubwa kwangu, iliendelea kwa mwaka mzima ambapo kwa kuwa alikuwa kavaa deraya mbili dharuba yangu haikuwa na athari kwake. Ile dharuba niliyoipata begani mwangu ilikuwa kubwa mno. Mtume aliona kwamba damu ilikuwa ikichuruzika kwa wingi kutoka jerahani mwangu. Mara moja alimwita mmoja wa wanangu akamwomba alifunge kitambaa jeraha langu! mwanangu alifanya hivyo na nikaenda kupigana tena.

Wakati ule nilifahamu ya kwamba, mmoja wa wanangu alikuwa kajeruhiwa. Mara moja niliokota vipande vya nguo nilivyokuja navyo kwa ajili ya kufungia majeraha ya watu waliojeruhiwa ikiwa ni pamoja na lile jeraha la mwanangu. Hata hivyo, kwa kuwa maisha ya Mtume yalikuwa hatarini basi kila mara nilikuwa nikimgeukia mwanangu na kumwambia: "Mwanangu! Amka na upigane."

Mtume alishangazwa mno kuuona uhodari na ushujaa wa mwanamke huyu ajitoleaye mhanga. Hivyo basi, alipomwona yule mtu aliyempiga dharuba mwanawe mara moja alimsoza akimwonyesha yule mwanamke na kuse- ma: "Huyu ndiye mtu aliyempiga dharuba mwanao."

Mama yule aliyekuwa akirukaruka kumzunguka Mtume (s.a.w.w.) kama vile arukavyo nondo kando kando ya mshumaa, mara moja alimshambulia mtu yule kama simba mwenye ghadhabu na akampiga dharuba kwenye shavu la mguu wake iliyombwaga chini. Wakati huu kule kushangaa kwa Mtume juu ya ushujaa wa mwanamke yule kuliongezeka zaidi na alicheka kutokana na jambo hili mpaka meno yake ya nyuma zaidi (magego) yakaonekana na kisha akamwambia yule mwanamke: "Umelipiza kisasi cha shambulio aliloshambuliwa mwanao."

Kwenye siku iliyofuatia, Mtume alipoviunda vikundi vidogo vidogo vya jeshi lake kutembea kuelekea Hamraa'ul Asad, Nasibah alitaka kwenda na jeshi lile, lakini lile jeraha kubwa alilotiwa halikumruhusu kufanya hivyo. Baada ya kurejea kutoka Hamraa'ul Asad, Mtume (s.a.w.w.) alimtuma mtu mmoja kwenda nyumbani kwa Nasibah kwenda kumtazama na alifurahi sana kusikia kwamba hali yake ilikuwa nzuri.

Ikiwa ni zawadi kwa kujitolea mhanga kwake kote, Bibi huyu alimwomba Mtume (s.a.w.w.) kumwombea kwa Allah ili aweze kuruhusiwa katika kumhudumia Mtume (s.a.w.w.) huko Peponi. Mtume (s.a.w.w.)

alimwombea na akasema: “Ee Mola Wangu! Wafanye kuwa masahaba zangu huko Peponi.”37

Jinsi Bibi huyu alivyopigana, ilikuwa yenye kupendeza sana kwa Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba alisema kuhusiana naye: “Leo cheo cha Nasibah bint Ka’ab ni bora kuliko kile cha watu fulani na fulani.”

Ibn Abil Hadid anasema: “Msimuliaji wa Hadith hii hakuwa mwaminifu kwa Mtume, kwa sababu hakuwataja dhahiri wale watu wawili ambao Mtume aliwataja kwa majina kwenye tukio hili.”38

Hata hivyo, nafikiri kwamba maneno fulani na fulani ni watu wale wale waliojipatia nafasi kubwa miongoni mwa Waislamu baada ya kufariki Mtume, na msimuliaji hakuwataja kwa wazi kwa sababu ya heshima na woga utokanao na nafasi zao.

Alama Za Matukio Kule Uhud

Maisha ya Mtume yaliokolewa kutoka kwenye hatari halisi kwa njia ya kujitolea mhanga ya watu wachache. Kwa bahati wengi wa maadui wali– jua kwamba Mtume alikuwa ameuawa na walikuwa wakiitafuta maiti yake miongoni mwa wale mashahidi. Na kuhusu wale wachache miongoni mwa maadui ambao walikuwa wakitambua kuapo kwake hai, mashambulizi yao yalikuwa yakirudishwa nyuma na Sayyidna Ali (a.s.), Abu Duj?nah na wengineo.

Wakati ule iliamuliwa ya kwamba taarifa za kifo cha Mtume (s.a.w.w.) zisingeweza kukataliwa na watu wakaziamini, hivyo Mtume aende kwenye lile bonde pamoja na masahaba zake. Alipokuwa njiani akielekea kwenye lile bonde alitumbukia kwenye shimo lililochimbwa na Abu Aamir kwa ajili ya Waislamu. Sayyidna Ali (a.s.) akamshika mkono upesi sana na kumtoa shimoni mle. Mtu wa kwanza kumtambua Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ni Ka’ab bin M?lik. Aliyaona macho ya Mtume (s.a.w.w.) yaking’ara kutoka chini ya kofia yake ya chuma na kupiga ukelele mara moja: “Enyi Waislamu! Mtume yuko hapa! Yu hai! Allah amemwokoa kutokana na madhara ya maadui.”

Kutokana na kwamba kutangazwa kwa taarifa za Mtume kuwa hai kungeweza kuzaa mashambulizi mapya kutoka kwa maadui, Mtume alimshauri Ka’ab kulifanya jambo hili kuwa siri. Hivyo akanyamaza hadi Mtume alipowasili kwenye bonde.

Wakati huo huo Waislamu waliokuwa jirani na sehemu ile walifurahia sana kumwona Mtume (s.a.w.w.) akiwa hai na wakaona aibu walipokuwa mbele yake. Abu Ubaydah Jarraah alizing’oa pete mbili za kofia ya chuma zilizodidimia usoni mwa Mtume (s.a.w.w.) ambapo Sayyidna Ali (a.s.) aliijaza maji ngao yake ili kumwezesha Mtume (s.a.w.w.) kuosha uso wake. Alipokuwa akiuosha uso wake (Mtume s.a.w.w) aliyatamka maneno haya: “Ghadhabu ya Allah imekuwa kali zaidi juu ya watu walioupaka damu uso wa Mtume wao.”

Wenye Kufuata Maslahi Miongoni Mwa Maadui

Waislamu walipokabiliwa na kushindwa kubaya mno pale Uhud, maadui waliinyakua fursa hii na wakaanzisha namna ya mbinu dhidi ya maoni ya Kiislamu ya Upweke wa Allah ambazo zikawa na athari za haraka mno miongoni mwa watu wajinga. Mwandishi wa zama zetu hizi anasema hivi: "Hakuna nafasi ifaayo zaidi kwa kuziathiri itikadi na fikara za watu kuliko wakati ule wanapokabiliwa na kushindwa, msiba, huzuni na dhiki. Wakati wa taabu kali nyoyo za watu wanaotaabika huwa dhaifu mno na zisizotu- lia kiasi kwamba busara zao hupoteza uwezo wa kuamua na kuyatathmini mambo, na ni katika wakati huu kwamba propaganda zenye uovu huziathiri fikara za watu walioshindwa."

Abu Sufyani, Ikrimah na wengineo waliokuwa wakiyashika masanamu makubwa mikononi mwao na walikuwa wakijihisi kuwa na shangwe, wali- itumia fursa hii kikamilifu na wakapiga kelele wakisema: "Naatukuzwe Hubal! Naatukuzwe Hubal." (Hubal lilikuwa ni jina la sanamu). Kwa kusema hivi walitaka kuwaambia Waislamu kwamba ushindi wao ulitokana na kuyaabudu kwao masanamu na kama angalikuwako mungu yeyote mwingine, na ibada ya Allah Mmoja tu ingalikuwa ndiyo dini ya kweli, basi Waislamu wangalishinda.
Mtume (s.a.w.w.) alitambua kwamba maadui walikuwa wakihubiri mambo yaliyo hatari sana katika nyakati hizo zilizo nyeti na walikuwa wakijinu- faisha kikamilifu kutokana na fursa waliyoipata wakati ule. Hivyo basi, alizisahau taabu zake zote na upesi sana akamwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) na Waislamu wengine kujibu tangazo hili la ibada ya masanamu kwa maneno haya: "Allah Yu Mkubwa na Mwenye nguvu zote." (Yaani kushindwa huku tulikokupata hakutokani na ule ukweli wetu wa kumwabudu Allah bali ni matokeo ya baadhi ya watu kuziasi amri za kamanda).

Hata hivyo, Abu Sufyan hakukoma kuzitangaza fikra zake zenye sumu, na akasema: "Tunalo sanamu kama vile Uzza ambapo ninyi hamna mfano wake." Mtume akaitumia nafasi hii na akawaamrisha Waislamu wajibu wakisema: "Allah Yu Mola wetu, nanyi hamna mola kama Yeye." (Yaani kama mwalitegemea sanamu lisilo chochote ila kipande cha jiwe au mti, sisi twamtegemea Allah Aliye Mkuu na Mwenye nguvu zote).

Watangazaji wa ibada ya masanamu wakasema kwa mara ya tatu: "Siku hii ni siku ya kulipizia kisasi Siku ya Badr." kwa dai hili Waislamu walijibu kufuatana na amri za Mtume (s.a.w.w.), wakisema: "Hizi siku mbili hazilingani, kwa sababu ndugu zetu waliouawa wako Peponi, ambapo wale wenu wako Motoni!"

Abu Sufyan alighadhibishwa mno na majibu haya makali yaliyokuwa yak- ija kutoka makooni mwa mamia ya Waislamu. Hivyo basi, baada ya kusema: "Tutakutana tena mwaka ujao" alitoka ule uwanja wa vita na kuamua kurudi Makka.[39]

Waislamu ambao miongoni mwao watu sabini waliuawa na wengi wao wakajeruhiwa, hata hivyo waliwajibika kutekeleza wajibu wa ki-Mungu (kusali sala ya Adhuhuri na ya Alasiri). Kutokana na udhaifu uliokithiri, Mtume (s.a.w.w.) alisali sala ya jamaa akiwa amekaa, na kisha akafanya kafani (kuvika sanda

) na mazishi ya mashahidi.

Mwisho Wa Vita

Miali ya vita ilizimishwa na yale makundi mawili yalitengana. Idadi ya wale waliojeruhiwa katika upande wa Waislamu ilikuwa mara tatu ya wale wa Waquraish. Ilikuwa muhimu kwao kulitimiza jukumu la kidini (kusali) na kuwazika wapenzi wao mapema iwezekanavyo.

Kabla ya Waislamu kuzizika maiti zao, wanawake wa Kiquraishi ambao waliuona uwanja wa vita ukiwa huru kutokana na aina zote za matendo ya kijinai, waliamua kuyatenda majinai makubwa mno baada ya ule ushindi, tena majinai yasiyo na kifani katika historia ya mwanadamu.

Hawakutosheka na ule ushindi wao wa dhahiri, bali ili kulipiza zaidi kisasi walivikata viungo, masikio, na pua za Waislamu waliokuwa wamelala chini wakiwa wameshakufa, na hivyo kuliweka doa la aibu kubwa juu ya tabia zao. Kwenye mataifa yote ya ulimwengu, maiti za maadui zisizo na msaada wowote na zisizolindwa, hupewa heshima. Hata hivyo, mkewe Abu Sufyan alitengeneza kidani na heleni za viungo vya Waislamu. Vile vile alilipasua tumbo la yule afisa mtiifu wa Uislamu, Hamzah, na kulitoa ini lake! Alijaribu kwa kadiri ya uwezo wake wote kulitafuna na kulila, lakini alishindwa!

Kitendo chake hiki kilikuwa cha aibu sana na chenye kuchukiza kiasi kwamba hata Abu Sufyan alisema: “Ninakikana kitendo hiki nami sikuamrisha kwamba kifanywe. Hata hivyo, wala mimi sichukizwi sana na jambo hili.”

Kutokana na kitendo hiki kichafu, Hind alifahamika miongoni mwa Waislamu kwa jina la ‘Hind mla ini’ na baadaye wanawe nao walifahamika kwa jina la ‘wana wa mwanamke mla ini.’

Waislamu waliwasili kwenye uwanja wa vita wakifuatana na Mtume (s.a.w.w.) ili kuzizika maiti zao. Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yaliangukia kwenye maiti ya Hamza naye alichukizwa mno kuiona hali yake ya kuhuzunisha. Dhoruba ya ghadhabu iliibuka akilini kwake na akasema: “Hasira na ghadhabu ninayoihisi nafsini mwangu hivi sasa haina kifani maishani mwangu.”

Wanahistoria na wafasiri wa Qur’ani wanaandika kwa makubaliano ya pamoja kwamba Waislamu waliweka ahadi neno lao (na wakati mwingine walimjumlisha Mtume s.a.w.w miongoni mwao) kwamba, kama wakipata mamlaka juu ya waabudu masanamu watawatendea maiti wao namna ile ile na watakata viungo vya maiti zao thelathini kwa kila Mwislamu mmoja. Mara tu baada ya nia yao ya kufanya hivyo, Aya ifuatayo ilifunuliwa:

“Na kama mkitaka kulipiza kisasi, basi fanyeni sawa na vile mlivyoonewa. Lakini kama mkisubiri, hakika itakuwa bora kwenu.” (*Surah al-Nahl*, 16:126).

Kwa njia ya Aya hii, ambayo yenyewe ni msingi wa uadilifu wa Kiislamu, kwa mara nyingine tena Uislamu umedhihirisha mwelekeo wake wa kiroho na kihisia na ukathibitisha ya kwamba Dini hii Tukufu

(Uislamu) si dini ya kulipiza kisasi. Haipuuzi misingi ya uadilifu na upole hata kwenye wakati mgumu mno, wakati mtu anapozidiwa nguvu na ghadhabu; na huutekeleza uadilifu kwenye matukio yote.

Safiyah dada yake Hamzah, alishikilia kutaka kuiona maiti ya kaka yake lakini, kama alivyoamrisha Mtume (s.a.w.w.), mtoto wake Zubayr alimzuia asiikaribie. Alimwambia mwanawe: "Ninafahamu kwamba wamevikatakata viungo vya mwili wake. Ninaapa kwa jina la Allah kwamba kama nikimkaribia sitadhihirisha kukereka kwangu na nitauvumilia msiba huu katika njia ya Allah." Bibi huyu aliyefunzwa aliikaribia ile maiti ya kaka yake kwa utulivu ustahilio heshima, akamwombea dua, akam– wombea wokovu na akarejea.

Bila shaka nguvu ya imani ndio nguvu iliyo kuu zaidi. Inadhibiti ghadhabu kali zaidi na shinikizo na inatoa heshima na utulivu kwa mtu aliyeathirika. Jambo hili lenyewe ni maudhui tofauti iliyojadiliwa na wanachuoni kuhu– siana na Utume na misingi ya imani.

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) aliwasalia wale mashahidi wa Uhud na kisha akawazika mmoja mmoja au wawili wawili. Aliamrisha hasa kwamba 'Amr bin Jumuh na Abdullah bin 'Amr wanaweza kuzikwa kwenye kaburi moja, kwa kuwa walikuwa marafiki walipokuwa hai, na ingalikuwa bora kama wangalibakia pamoja vilevile baada ya kifo.[40]

Neno La Mwisho La Sa'ad Bin Rabi'

Sa'ad bin Rabi' alikuwa mmoja wa wafuasi waaminifu wa Mtume (s.a.w.w.). Moyo wake ulikuwa umejaa imani na utiifu. Alipoanguka chini baada ya kupata majeraha kumi na mawili, mtu mmoja alipita karibu naye na akasema: "Wanasema kwamba Muhammad ameuwawa."

Sa'ad akamwambia mtu yule: "Hata kama Muhammad kauwawa Mola wa Muhammad Yu hai, nasi tunafanya jihadi ili kuieneza itikadi ya Upweke wa Allah."

Wakati miali ya vita ilipozimika, Mtume (s.a.w.w.) alimfikiria Sa'ad bin Rabi' na akasema: "Ni nani awezaye kunipatia taarifa juu ya Sa'ad." Zayd bin Thabit alilichukua jukumu la kuleta taarifa sahihi kwa ajili ya Mtume (s.a.w.w.) kuhusu Sa'ad kama yu hai au kauwawa. Alimkuta Sa'ad akiwa miongoni mwa wale waliolala na akamwambia: "Mtume amenituma ili nithibitishe juu ya hali yako na nimpelekee taarifa sahihi juu yako."

Sa'ad akamjibu akasema: "Zifikishe salam zangu kwa Mtume na mwambie kwamba si zaidi ya muda kidogo tu wa maisha ya Sa'ad uliosalia na Ewe Rasuli wa Allah! Allah na Akulipe malipo yaliyo mema zaidi yamstahikiyo Mtume." Vile vile aliongeza kusema:
"Zifikishe salam zangu kwa Ansar na kwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) na waambie kwamba, kama Mtume akipatwa na dhara lolote lile wakati wao wakiwa hai, hatawapozwa na Allah." Yule mtu aliyetumwa na Mtume (s.a.w.w.) alikuwa bado hajaondoka pale alipo Sa'ad wakati yeye Sa'ad alipokata roho.[41]

Huba ya mwanadamu juu na nafsi yake ina nguvu zaidi kiasi kwamba katu haisahau nafsi yake na hukitoa kila kitu kilicho chake kwa ajili ya kuihifadhi. Hata hivyo, nguvu ya itikadi na huba ya lengo na maslahi ya mtu katika fikara zake, ni kitu chenye nguvu zaidi, kwa sababu kama ilivyoelezwa dhahiri kwenye historia, huyu askari shujaa alijisahau mwenyewe katika wakati ule mgumu zaidi alipokuwa hayupo mbali kutoka kwenye kifo na alimkumbuka Mtume (s.a.w.w.), ambaye ulinzi wake ulikuwa njia kuu ya kulifikia lengo lake. Na ujumbe pekee alioupeleka kupitia kwa Zayd bin Thabit ulikuwa kwamba masahaba wa Mtume wasiwe wazembe wa usalama na ulinzi wake japo kwa kitambo kidogo tu.

Mtume (S.A.W.W.) Arejea Madina

Jua linasogea kuelekea magharibi na linaitupia miyonzi yake ya dhahabu kwenye ule upande wa pili wa nusu ya duinia. Sasa Uhud imetulia na kunyamaza kabisa.

Waislamu ambao baadhi ya wenzao wameuawa na wengine wamejeruhiwa, sasa wanalazimika kurejea majumbani mwao ili kwenda kuipata tena nguvu na kuvifunga vidonda vya wale waliojeruhiwa. Yule kamanda mkuu aliwaamrisha watu wake kuondoka na kuelekea madina. Mtume (s.a.w.w.) pamoja na Muhajiriin na Ansar baadae waliwasili mjini Madina. Mji ule ule ambao baadhi ya nyumba zake vilisikika vilio vya mama wa watoto na vya wake waliofiwa, waliowapoteza wana na waume zao.

Mtume (s.a.w.w.) alifika kwenye nyumba ya Bani Abdul Ashhal. Vilio vya wanawake wao vilimhuzunisha. Machozi yakaanza kumtiririka machoni mwake na akasema kwa sauti ndogo: “Ninapatwa na maumivu makali kwamba hakuna amliliaye Hamza.”[42]

Sa’ad bin Mu’aaz na wengineo walipotambua alichokitamani Mtume (s.a.w.w.), waliwaomba baadhi ya wanawake kufanya maombolezo kwa ajili ya Hamza, yule askari mwaminifu wa Uislamu. Mtume (s.a.w.w.) alipotambua hivyo aliwaombea wale wanawake na akasema: “Daima nimekuwa nikiufaidi msaada wa kiroho na kidunia wa Ansar.” Kisha aliwaomba wale wanawake kurudi majumbani mwao.

Kumbukumbu Zenye Kusisimua Za Mwanamke Mwaminifu

Maisha ya kujitolea mhanga ya wanawake kwenye kipindi cha awali cha Uislamu ni jambo la kushangaza na kutia moyo. Wakati tunaposema kwamba jambo la kushangaza, ni kwa sababu ni kwa nadra sana tunawaona wanawake walio mfano wao kwenye historia ya kisasa.

Siku hizi, kaulimbiu za ujasiri na ushujaa hutoka kwenye makoo ya wanawake wa ulimwengu huu na wanadai kuwa na nguvu na uthabiti utoshelezao kuyakabili matukio ya kutetemesha ya zama hizi, lakini hawawezi kuwa sawa na wale wanawake waumini na wenye kujitolea mhanga wa siku za awali za Uislamu. Nguvu na ufanisi wa wanawake wale ilikuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya imani zao katika hukumu ya Allah na mategemeo yao juu ya malipo ya huko Akhera.

Bibi mmoja wa kabila la Bani Din?r, aliyempoteza mumewe, baba yake na kaka yake alikuwa ameketi

miongoni mwa wanawake wengine na kulia huku akitiririkwa na machozi, na wale wanawake wengine walikuwa wakiomboleza. Mara ghafla Mtume (s.a.w.w.) alipita karibu na kile kikun- di cha wanawake. Huyu mwanamke aliyefiwa aliwauliza watu waliokuwa karibu naye kuhusu Mtume (s.a.w.w.). Wote wakamjibu: "Shukurani zimwendee Allah, yeye Mtume yu mzima kabisa."
Yule mwanamke akasema: "Mimi ninapenda kumwona kwa karibu." Mahali alipokuwa kasima- ma Mtume (s.a.w.w.) hapakuwa mbali. Hivyo wakamsoza kidole Mtume (s.a.w.w.). Yule mwanamke alipouona uso wa Mtume (s.a.w.w.), upesi sana aliisahau misiba yake yote na akalisema jambo litokalo kwenye kiini cha moyo wake, lililozaa mapinduzi akilini mwa wale wote waliokuwapo pale.

Alisema: "Ewe Mtume wa Allah! Mambo yote yasiyopendeza na misiba huwa rahisi katika njia yako." (Yaani, kama wewe uko hai, tunachukulia kila msiba utukumbao kuwa jambo dogo mno, na tunalibeua).

Nausifiwe uimara huu na isifiwe imani hii ambayo humuweka mtu salama kutokana na kutokutengemaa kama vile nanga iwekavyo jahazi katika hali ya usalama kutokana na mawimbi inaposafiri baharini.43

Mfano Mwingine Wa Mwanamke Aliyejitolea Mhanga

Katika kurasa zilizotangulia tumemtaja kwa kifupi 'Amr bin Jumuh. Ingawa bwana huyu alikuwa mlemavu, na haikuwa wajibu juu yake kufanya jihadi, alishikilia kushiriki, na baada ya kuruhusiwa na Mtume (s.a.w.w.) alijiunga na mujahidiin (askari wa Uislamu) watanguliao mbele. Sio tu kwamba alijiunga na safu za Mujahidiin, bali mwanawe Khallad na shemeji yake Abdullah bin Amr nae alishiriki kwenye hii jihadi takatifu na wote walikufa kishahidi.

Mkewe Hind bint Amr bin Hazm aliyekuwa shangazi yake Jabir bin Abdullah Ansar, alikuja pale Uhud. Alizikusanya maiti za mashahidi na wapenzi wake kutoka kwenye uwanja wa vita, akazipakia kwenye ngamia na akaondoka kwenda Madina.

Tetesi zilienea mle mjini Madina kwamba Mtume (s.a.w.w.) ameuawa. Wanawake walitoka kwenda Uhud ili kwenda kupata taarifa sahihi juu ya Mtume (s.a.w.w.). Akiwa njiani, Hind alikutana na wakeze Mtume (s.a.w.w.) waliomwuliza juu ya hali ya Mtume (s.a.w.w.).

Ingawa alikuwa kachukua maiti za mumewe, kaka yake na mwanawe katika ngamia, ali- waambia kwa utulivu kamili, kana kwamba hakuna msiba wowote uliomkumba: "Ninayo taarifa ya furaha kwa ajili yenu. Mtume yu hai na unapoifikiria baraka hii, misiba yote huwa kitu kidogo sana. Pili, Allah amewarudisha makafiri wakiwa wamejawa na hasira na ghadhabu."44

Kisha aliulizwa kuhusu zile maiti alizozichukua kwenye ngamia. Alijibu: "Ni ndugu zangu. Mmoja wao ni mume wangu, mwingine ni mwanangu, na wa tatu ni kaka yangu. Ninawapeleka Madina nikawazike huko."

Hapa tunaona kwenye historia ya Uislamu moja ya maelezo bora zaidi ya imani (yaani kule kuifikiria misiba yote kuwa rahisi, na kuzivumilia huzuni na matatizo kwa ajili ya kulifikia lengo la kiroho). Itikadi za

kimaada haziwezi kuwafunza wanaume na wanawake kujitolea mhanga kwa kiwango hiki. Watu hawa wanapigana kwa ajili ya kulifikia lengo la kiroho na wala si kwa ajili ya faida za kidunia au kwa kujipatia vyeo.

Sehemu ya baadae ya kisa hiki ni yenye kustaajabisha zaidi na haiafikiani hata kidogo na kipimo cha kimaada na misingi iliyowekwa na walimwen– gu kwa ajili ya uchanganuzi wa matatizo ya kihistoria. Ni wale watu wa Mungu tu na wale wenye itikadi madhubuti juu ya Allah na msaada wake wawezao kuichanganua hadithi ifuatayo na wawezao kuichukulia kuwa ni kweli kabisa.
Yule mama (Hind) alikuwa kashika hatamu ya ngamia mikononi mwake na alikuwa akimwelekeza mjini Madina. Hata hivyo, yule ngamia alikuwa akisogea kwa taabu sana. Mmoja wa wakeze Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Kwa hakika mzigo ulioko juu ya ngamia huyu ni mzito sana” Hind akajibu: “Ngamia huyu yu mwenye nguvu mno naye anao uwezo wa kuchukua mzigo wa ngamia wawili na bila shaka iko sababu nyingine inayomfanya afanye hivi, kwa sababu kila ninapomgeuzia Uhud anatembea kwa urahisi sana, lakini kila nikimgeuzia Madina huwa anasogea kwa shida au anapiga magoti.

Hind akaamua kurudi Uhud na kumwarifu Mtume (s.a.w.w.) jambo hili. Hivyo akaja Uhud pamoja na yule ngamia na zile maiti na akamwarifu Mtume (s.a.w.w.) juu ya hali ya yule ngamia. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Je, mumeo amemwomba nini Allah katika du’a yake pale alipokuwa akienda vitani?” Hind akajibu: “Amesema: “Ewe Mola wangu! Usinifanye nirejee nyumbani kwangu.” Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Sababu ya kukataa kwa ngamia kwenda Madina imedhihirika. Du’a ya mumeo imetakabaliwa. Allah hapendi kwamba maiti hii iende nyumbani kwa Amr. Ni muhimu kwamba uzizike maiti zote tatu kweye hii ardhi ya Uhud nawe huna budi kutambua kwamba watu hawa watatu watabakia kuwa pamoja huko kwenye ulimwengu mwingine pia.” Hind akiwa anachuruzikwa na machozi kutoka machoni mwake, alimwomba Mtume amwombee kwa Allah ili naye aweze kuwa pamoja nao.[45]

Mtume (s.a.w.w.) alifika nyumbani kwake. Macho ya binti wake mpenzi Fatimah Zahrah yaliangukia kwenye ule uso wake uliojeruhiwa na akaanza kutiririkwa na machozi machoni mwake. Mtume (s.a.w.w.) alimpa binti yake upanga wake ili ausafishe.

Ali bin Isa Arbali mwanahadithi na mwanahistoria wa karne ya saba Hijiriya anaandika hivi: “Binti yake Mtume alileta maji ili kuisafisha damu kutoka usoni mwa baba yake.

Amiri wa Waumini (a.s.) alimwagia maji na Zahrah akaisafisha ile damu kutoka pande zote, lakini kwa vile lile jeraha mle usoni lilichimbika sana, damu haikukoma kutoka. Mwishowe kipande cha mkeka kilichomwa na majivu yake yakapakwa kwenye kile kidonda na hapo ile damu ikakoma kutiririka kutoka mle kwenye jeraha la usoni mwake[46]

Ni Lazima Adui Afuatiliwe

Usiku ambao Waislamu walipumzika majumbani mwao mjini Madina baada ya tukio la Uhud, ulikuwa usiku nyeti mno. Wanafiki, Wayahudi na wafuasi wa Abdallah bin Ubayy walikuwa na shangwe kutokana

na yale yaliyotokea kule Uhud. Vilio na maombolezo ya wale waliofiwa yaliweza kusikika kutoka kwenye nyumba nyingi. Zaidi ya yote hayo, ilikuwako hatari kwamba wanafiki na Wayahudi wangaliweza kuasi dhidi ya Waislamu, au kwa uchache tu wangaliweza kuuharibu ule umoja na utulivu wa kisiasa wa yale makao makuu ya Uislamu kwa kujenga tofauti na mifarakano miongoni mwa wakazi wake.

Uovu unaofanywa na tofauti za ndani ni mkubwa kuliko ule ufanywao na mashambulizi ya maadui wa nje. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kwamba Mtume (s.a.w.w.) awaonye maadui wa ndani na kuwafanya waelewe kwamba nguvu ya Uislamu haiwezi kudhoofishwa kwa njia ya machafuko na ghasia, na kila kitendo cha propaganda chenye kuutishia msingi wa Uislamu kitakomeshwa tangu mwanzoni mwake kabisa kwa nguvu yote.

Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa na Allah kumuandama yule adui katika siku iliyofuatia usiku ule. Hivyo, alimteuwa mtu kutangaza katika sehemu zote za mji maneno haya: “Wale watu waliokuwa Uhud jana wajitayarishe kum– fuatilia adui kesho. Hata hivyo, wale wasioshiriki kwenye vita ile hawana haki ya kuungana nasi kwenye jihadi hii.”[47]
Hakuna shaka kwamba sharti hili liliwekwa kwa lengo zuri tu, lisiloweza kufichikana kwa mtu mwenye fikira za kisiasa; kwanza sharti hili ni aina ya shambulio kwa wale watu walioshindwa kushiriki kwenye Vita vya Uhud. Kwa hakika lilikuwa ni kukana mashindano na kundi lile ambalo halistahili ulinzi na kushiriki katika vita. Pili, ilikuwa ni adhabu kwa wale walioshiriki katika vita vya Uhud. Kwa kuwa Uislamu umepata pigo hili kutokana na utovu wao wa nidhamu, hivyo ilikuwa muhimu kwamba wafanye masahihisho kwa kushindwa huku ili kwamba hapo baadae wasionyeshe tena utovu wa nidhamu.

Tangazo lililotangazwa na yule mpiga mbiu wa Mtume (s.a.w.w.) lilifika masikioni mwa mtu mmoja wa kabila la Bani Ashhal, alipokuwa amelala pamoja na ndugu yake huku mwili umejeruhiwa.

Tangazo hili liliwa– tetemesha wote wawili kiasi kwamba, ingawa wote wawili hawakuwa na usafiri ila mnyama mmoja wa kupanda, na vile vile kuondoka kwao kulikuwa kwa taabu kutokana na sababu fulani fulani, waliambiana: “Si sahihi hata kidogo kwamba Mtume aende kwenye jihadi nasi tubakie nyuma.” Ingawa iliwalazimu ndugu hawa kuifanya safari hii kwa kupanda yule mnyama kwa kubadilishana, walifaulu kujiunga na askari wa Uislamu.[48]

Mtume (S.A.W.W) Aenda Hadi Hamraa’ul Asad

Mtume (s.a.w.w.) alimteuwa Ibn Ummi Maktum kuwa mwakilishi wake mjini Madina, na akaenda akapiga kambi Hamraa’ul Asaad mahali palipo umbali wa maili nane (kilometa kumi na tatu hivi) kutoka Madina. Ma’abad bin Khuzaa’, chifu wa kabila la Khuzaa’ah, ingawa alikuwa mwenye kuabudu masanamu, alionyesha huruma kwa Mtume (s.a.w). Watu wa kabila la Khuzaa’ wakiwemo Waislamu na wasio Waislamu, daima wamekuwa wakiwasaidia Waislamu.

Ili kumhudumia Mtume (s.a.w.w.) Ma’abad alikwenda kutoka pale Hamraa–ul Asad hadi Rawhah, makao makuu ya jeshi la Waquraishi na akakutana na Abu Sufyan. Aligundua kwamba Abu Sufyan alidhamiria

kurudi Madina na kuiharibu ile nguvu ya Waislamu iliyobakia.

Ma'abad akamzuia asifanye hivyo na akasema: "Ewe Abu Sufyan! Jihadhari na Muhammad, ambaye hivi sasa yuko Hamraa-ul Asad. Ametoka Madina na jeshi kubwa, na wale wasioshiriki kwenye vita jana leo wako pamoja naye pia. Nimeziona nyuso zilizogeuka kutokana na ghadhabu na katu sijapata kuziona nyuso kama hizo maishani mwangu mwote. Wanasikitika mno kwa utovu wa nid- hamu uliotokea jana." Aliielezea kwa maneno mengi mno ile nguvu ya Waislamu na moyo wao wa juu kiasi kwamba Abu Sufyan aliitupilia mbali ile dhamira yake.

Mtume (s.a.w.w.) pamoja na masahaba zake walikaa hapo Hamr?-ul Asad katika sehemu ya kwanza ya usiku, na akaamrisha kwamba uwashwe moto kwenye sehemu mbalimbali mle jangwani ili kwamba adui adhanie kwam- ba nguvu ya Waislamu ilikuwa kubwa kuliko ile waliyoiona kule Uhud. Safwaan Umayyah alimwambia Abu Sufyan hivi: "Waislamu wana hasira na wamekasirika. Ni bora kwamba tutosheke na kile tulichokipata tayari na turejee Madina.49

Muumini Wa Kweli Hadanganywi Mara Mbili

Sentensi hiyo hapo juu ni marudio ya maelezo ya Mtume (s.a.w.w.) aliyesema: "Muumini wa kweli haumwi mara mbili kwenye shimo moja." Abu Azza Jumahi alipomwomba Mtume (s.a.w.w.) katika vita vya Badr amwachie huru, Mtume (s.a.w.w.) alimwachia huru, naye akamwahidi kwamba hatajiunga na wenye kuabudu masanamu katika matendo yao dhidi ya Uislamu. Hata hivyo, aliivunja ahadi yake kwa kushiriki katika Vita ya Uhud dhidi ya Uislamu, na hatimaye alipokuwa akirejea kutoka Hamraa'ul Asad, Waislamu wakamteka tena.
Mara hii, vile vile alimwomba Mtume (s.a.w.w.) amsamehe na amwachilie. Hata hivyo Mtume (s.a.w.w.) hakulisikiliza ombi lake na kwa kuitamka sentensi hiyo hapo juu (yaani ile isemayo 'Muumini wa kweli haumwi mara mbili kwenye shimo moja) aliamrisha anyongwe. Kwa haya, ule msiba wa Uhud ambao ulikuwa ni wenye mafunzo kamili ulimalizikia.50

1. Maghaazil-Waqidi, Juzuu 1, uk. 184-190; Tabaqaat, Juzuu 2, uk. 31-34; na Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 101.
2. Wafasiri wa Qur'ani na wanahistoria kama vile Ali bin Ibrahim, Shaykh Tabrasi, (A'laamul wara') na Ibn Hisham, wanatofautiana juu ya suala la idadi ya askari. Hata hivyo, idadi hiyo tuliyoitaja hapo juu yaelekea kuwa ndio ya kweli.
3. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 203-204, na baadhi ya wanahistoria wanaamini kwamba yule mjumbe aliileta ile barua mjini Madina Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa msikitini na Abi bin Ka'ab alimsomea.
4. Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 111.
5. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 211.
6. Bihaarul Anwaar, Juzuu 2, uk. 125.
7. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 214; na Tabaqaatul-Kubra, Juzuu 2, uk. 38.
8. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 65.
9. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 9
10. Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 57.
11. Usudul Ghabah, Juzuu 2, uk. 59; na Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 57.
12. Maghaazil-Waaqid, Juzuu 1, uk. 221-222.
13. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk 66.

14. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 68-69.
15. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 12.
16. Hakusudii kwamba waisilamu walikuwa wakiwatusi watu pale, bali ina- maana kuwa ile hali halisi iliyokuwa dhidi ya adui kwake yeye adui aliichukulia kuwa ni matusi, ukizingatia kuwa adui alikuwa akijiona ni jeshi lenye nguvu na heshima katika Rasi ya Uarabu, hivyo mashujaa wake wanapogaragazwa kwa namna ile ni sawa na tusi kwao - Mhariri
17. Taarifa ya washika bendera tisa waliouawa na Sayyidna Ali (a.s.) imenukuli- wa mwenye Bihaarul Anwaar, Juzuu 2, uk. 51.
18. Khisaal, Juzuu 2, uk. 121. 220
19. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 68; na Tarikhut-Tabari, Juzuu 2, uk. 194.
20. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 83.
21. Sisi bado tuna shaka na kauli ya Ibnu Hishamu ifidishayo kuwa Anas alifia viwanja vile, pale aliposema: "Anas alipata majeraha makubwa kwenye vita hivi na hakuna aliyeweza kuitambua maiti yake ila dada yake tu." Kwa sababu yanapingana na masimulizi ya Anas mwenyewe, hivyo tunalazimika kujiuliza: Je Anas alisimulia yale masimulizi yake pale uwanjani vitani au baadaye? Na kama ni baadaye basi aliwezaje kusimulia wakati alikuwa kishakufa? Na kama alisimulia pale vitani basi nalo akili haikubali kwani hali halisi ya kivita haikuruhusu kuanza kusimulia hayo pale, na hasa ukizingatia hekaheka yake pale. Na zaidi ya hapo ni kuwa simulizi zake zaonyesha kuwa yeye Anasi alikuwa akisimulia mambo yaliyotokea vitani, hivyo ni lazima itakuwa alisimulia baada ya vita - Mhariri.
22. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 109.
23. Ibn Hadid, Sharhun- Nahjul Balaghah, Juzuu 15, uk. 23-24.
24. Ruba'iyat ni yale meno (manne kwa idadi) ambayo yako kati ya meno ya mbele na meno ya kukatia.
25. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 84; na Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 244.
26. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 107.
27. Ibn Abi Hadid, Sharhun-Nahjul- Balaghah, Juzuu 5, uk. 21.
28. Tarikhul Kamil, Juzuu 2, uk. 107.
29. Vile vitabu sita vya Hadith vilivyo sahihi miongoni mwa Ahlil Sunna.
30. Ibn Abil Hadid, Sharhun-Nahjul Balaghah, Juzuu 14, uk. 251
31. Khasaal, Juzuu 2, uk. 15.
32. Siiratu Ibn Hishamu, Juzuu 2, uk. 14.
33. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 18.
34. Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 84 na kuendelea.
35. Nasikhut-Tawaarikh, juzuu 1, uk. 357.
36. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 69-72.
37. Mlolongo wa huduma za mwanamke huyu aliyejitolea mhanga haukumal- izikia hapa. Baadae alishiriki pamoja na mwanawe kwenye kampeni dhidi ya Musaylimah Kadhab (Mdanganyifu) na akapoteza mkono kwenye vita vile.
38. Abil Hadid, Sharhun-Nahjul Balaghah, Juzuu 14, uk. 265-267.
39. Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 44-45.
40. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 498; Bihaarul Anwaar, Juzuu 20, uk. 131.
41. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 95.
42. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 99.
43. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 99.
44. Kufuatana na ilivyonakiliwa na Ibn Abil Hadid, Hind aliisoma Aya ya Qur'ani isemayo:
"Na Allah amewarudisha waliokufuru na ghadhabu yao; hawakupata faida yoyote; na Allah amewatoshea waumini katika mapigano; na Allah Yu Mwenye uwezo, Mwenye nguvu."(Surah al-Ahzaab, 33:25). Kisha anasema: "Hakika ameitaja maana ya sehemu ya kwanza ya Aya, kwa sababu Aya hii ilifunuliwa wakati wa Vita vya Handaq (Ahzaab), iliyopiganwa baada ya Vita vya Uhud." (Sharhun- Nahjul Balaghah, Juzuu 14, uk. 262).
45. Maghaazil-Waaqidi, Juzuu 1, uk. 265.
46. Kashful Ghummah, uk. 54.
47. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 101.

48. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 101.
49. Tabaqaatul Kubra, Juzuu 2, uk 49.
50. Siiratu Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 104.

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii

30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. As-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano

69. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa–u–llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al–Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al – Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al–Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an–Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna

108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe –Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe – Sehemu ya Tatu
111. Ujumbe – Sehemu ya Nne
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
113. Shiya N'abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas–ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili

Back Cover

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu zilizochakaa.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikra zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema:

“Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao.

Kwa juhudi nyingi niliyapitia matendo yao na nilizifikiria fikra na maten- do yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu, na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taar- ifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda his- toria kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.
Miongoni mwa hawa watu wakuu, hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivy- ofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote - wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [15]
Katika mtandao: www.ibn-tv.com [16]

URL del envío: https://www.al-islam.org/es/ujumbe-sehemu-ya-pili-jafar-subhani#comment-0

Enlaces
[1] https://www.al-islam.org/es/person/jafar-subhani
[2] https://www.al-islam.org/es/organization/al-itrah-foundation-0
[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/25243
[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/25243
[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/25243
[6] https://www.al-islam.org/es/person/dhikiri-u-m-kiondo
[7] https://www.al-islam.org/es/tags/quran
[8] https://www.al-islam.org/es/tags/history
[9] https://www.al-islam.org/es/tags/miraj
[10] https://www.al-islam.org/es/tags/battles
[11] https://www.al-islam.org/es/tags/quraysh
[12] https://www.al-islam.org/es/person/bwana-abu-talib

[13] https://www.al-islam.org/es/person/prophet-muhammad

[14] https://www.al-islam.org/es/person/imam-ali

[15] mailto:alitrah@raha.com

[16] http://www.ibn-tv.com